

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Pili – Tarehe 13 Mei, 2015

(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu!

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa, maswali tunaanza na ofisi ya Waziri Mkuu, anayeuliza swali la kwanza ni Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, kwa niaba yake Mheshimiwa Likokola!

Na. 11

Fedha za Mfuko wa JK kwa Wajasiriamali Wadogo

MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA (K.n.y. MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE) aliuliza:-

Mfuko wa Wajasiriamali wadogowadogo maarufu kama mabilioni ya JK uliwavuta wengi sana lakini masharti ya kupata fedha hizo yamekuwa magumu:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kufanya mpango huo uwe endelevu kwa lengo la kuwanufaisha wanyonge?
- (b) Je, ni wananchi wangapi wa Mkoa wa Kigoma wamenufaika na mpango huo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Serikali ilianzisha mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza ajira kwa kutoa mikopo yenye masharti nafuu. Lengo la mpango huu ni kuwawezesha wananchi mijini na vijijini kupata mikopo ya kuanzisha au kuendeleza shughuli za kiuchumi ili kuongeza ajira na kipato.

Masharti ya kupata mikopo hii si magumu sana ikilingalishwa na ile inayotolewa na mabenki, kwa sababu riba inayotozwa kwa mikopo hii ni asilimia 10, ikilinganishwa na riba inayotozwa na mabenki mengine, ambayo ni zaidi ya asilimia 20. Aidha, wananchi wanaopewa

mikopo kutokana na Mfuko huu, hawahitajiki kuwa na dhamana kama zile zinazotakiwa na mabenki.

Mheshimiwa Spika, ili kufanya mpango huu uwe endelevu, Serikali imepanga kufanya tathmini ya kina katika mwaka ujao wa fedha, tathmini inatarajiwa kufanyika katika maeneo yaliyopata mikopo hiyo kwa lengo la kubaini vikundi na wajasiriamali walionufaika, shughuli wanazozifanya, maendeleo ya shughuli hizo na changamoto zilizojitokeza.

Mheshimiwa Spika, aidha, matokeo ya tathmini hiyo, yataiwezesha Serikali kuendeleza mpango huu kwa njia bora zaidi ikiwemo kuandaa utaratibu mzuri zaidi wa utoaji wa mikopo hii, utakaosimamiwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

(b) Mheshimiwa Spika, kupitia mpango huu, Mkoa wa Kigoma ulipata mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 946.49, ambayo iliwanufaisha wajasiriamali 1,407. Kati ya wajasiriamali hao 553 wanatoka Kigoma Mjini, 827 wanatoka Kasuru, 207 wanatoka Kigoma Vijijini na 20 wanatoka Kibondo.

MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, Serikali haioni kwamba wananchi wengi mpaka sasa hawajawezeshwa kiuchumi, kwa sababu Baraza la Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi halina Kamati kuanzia ngazi ya Taifa mpaka ngazi ya vijiji na kwa maana hiyo kuwakosesha wananchi fursa. Je, Serikali itaweka msukumo katika kuunda Kamati za Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi, tangu ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya, Kata, Vijiji na mpaka ngazi ya familia?

Swali la pili, kwa nini Serikali haitumii benki ambazo zina matawi mengi mpaka vijijini. Kwa mfano, benki ya Posta na je, Serikali itakuwa tayari sasa hivi kutumia Benki ya Posta kwa ajili ya kuwakopesha wananchi wengi kwa sababu benki hii ni ya Serikali, lakini ina matawi mengi hadi vijijini?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza natambua kabisa hoja ya Mheshimiwa Likokola, maana mimi mwenyewe nimefanya ziara katika mikoa na wilaya. Udhafu niliouona ni huo kwamba, Baraza mahali pengi bado halijajulikana.

Kwa maelekezo niliyotoa nilipoingia hapa ofisini ni Baraza kutembea mikoani na wameanza. Nilivyowaeleza katika majibu yangu ni kwamba tunataka sasa kufanya mikopo hii iwe endelevu. Kwa hiyo, Baraza hili tunataka lishuke hadi ngazi ya familia kama anavyosema. Kwa hiyo, tunachotaka kukifanya sasa ni kuhakikisha kwamba mikoa kwanza ina watu wanaitwa *focal points* na wilaya zina watu wanaitwa *focal points* kushuka mpaka kwenye familia, ili wale walengwa waweze kujua, vinginevyo inakuwa vigumu mlengwa mwenyewe kama hajui Baraza linafanya kazi gani, akapate mikopo hii. Kwa hiyo, hoja ya Mheshimiwa Likokola ni ya msingi kabisa na ndiyo tunayoifanyia kazi kwa ajili ya kulifanya Baraza hili na mikopo hii iwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki ya Posta ni kwamba, tulipoanza tulichukua mabenki ya NMB, CRDB, tulitumia hata taasisi zingine, kama *Pride*, Dunduliza, ilikuwa ni mwanzo tu, wengine walifanya vizuri, wengine hawakufanya vizuri.

Kwa hiyo, sasa ushauri alioutoa kutumia Benki ya Posta ambayo ina matawi hadi huko kwenye wilaya, huu ni mzuri na ndiyo maana nimesema tunafanya tathmini upya katika mwaka

huu tuhakikishe kwamba tunatumia mtandao unaowafikia wakulima na wananchi wote ambao wako chini kabisa kuliko kuishia mikoani au makao makuu.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia fursa hii. Kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema ni kwamba Baraza hili la uwezeshaji halijajulikana na Baraza hili ni la muda mrefu sana na ndiyo sababu kumekuwa na malalamiko makubwa, kwamba hata marejesho hayafiki kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi, mikopo hii inatolewa kiitikadi. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri atueleze, wana mkakati gani kuhakikisha kwamba walengwa wote bila kujali itikadi za vyama wanapata mikopo hii, kwa sababu tumezunguka vijijini tunakuta matafizo hayo? Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwa nini inafanyika hivyo na je, mna mkakati gani kuhakikisha Watanzania wote wa hali ya chini wanafaidika na Mfuko huu?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Spika, lengo letu sisi ni kuhakikisha kwamba Mifuko hii ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, ambayo kwa kweli ni mingi, kwanza tunahitaji wawe na elimu, iko mingi zaidi ya 10, lakini walio wengi bado hawajaijua na mingine iko kwenye sekta mbalimbali na siwezi kuitaja hapa sasa hivi. Kwanza tunataka wajue ni Mifuko gani na iko wapi na masharti yake yakoje.

Sasa kuhusu suala la utoaji, nimesema tutafanya tathmini kujua nani kapata mkopo, yuko wapi, ikiwa ni pamoja na kufanya uhakiki na ukaguzi kuhusu marejesho ya mikopo hii. Maana ukikopa ukarejesha inakuwa endelevu ndiyo na wengine wakope.

Mheshimiwa Spika, suala la itikadi sina hakika kabisa kwamba hayo yalikuwa ni masharti, kwa sababu masharti ya kukopa hakuna mahali ambao tumesema yaendane na itikadi ama ya chama cha aina yoyote. Sisi walengwa ni wale, tuseme kwa kifupi tu, walala hoi! Maana ndiyo Mheshimiwa Rais alivyosema, tuwalenge wale wajasiriamali wadogo, *whether* ni wa chama hiki au kile, bila kujali itikadi.

Na. 12

Maendeleo katika Wilaya ya Tarime

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE aliuliza:-

Wilaya ya Tarime imepiga hatua kubwa kimaendeleo katika kipindi cha kuanzia mwaka 2010 – 2015:-

(a) Je, ni mambo yapi ya maendeleo yaliyopatikana katika kipindi hiki?

(b) Je, kwa nini ujenzi wa daraja la Kyoruba ambalo Serikali iliahidi kulijenga haujafanyika?

(c) Je, Serikali inasema nini juu ya ahadi ya Mheshimiwa Rais kuhusu ujenzi wa barabara ya Nyamwanga toka Tarime Mjini hadi Mto Mara kwa kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2010 hadi 2015, Wilaya ya Tarime imepata mafaniko makubwa katika sekta ya barabara, afya, elimu, maji, kilimo, utawala na kadhalika.

(b) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ilifanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa daraja la Kyoruba uliobaini gharama za ujenzi wa daraja hilo kuwa ni shilingi bilioni 1.5, katika mwaka wa fedha 2014/2015. Katika mwaka huo Wizara ya Fedha ilipelekea Halmashauri shilingi milioni 50 tu na kutokana na ufinyu wa bajeti Halmashauri ilishindwa kutangaza zabuni hiyo. Aidha, Halmashauri ilishauriwa kuweka suala hili kwenye mpango wake wa bajeti.

(c) Mheshimiwa Spika, barabara ya Tarime-Nyamwaga hadi Mto Mara hadi Mugumu hadi Natta Mbiso, yenye kilometa 123.97 ipo chini ya Wakala wa Barabara wa Mkoa wa Mara, yaani TANROADS, barabara hii hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha 2013/2014, ilikuwa na kilometa 5.53 za lami nyepesi zilizojengwa kutoka Tarime hadi Rebu. Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, zimetengwa shilingi 2,131,300,000/= kwa ajili ya ujenzi wa kilometa mbili na tayari Mkandarasi amekwishapatikana wa kutekeleza kazi hiyo.

Aidha, katika bajeti ya mwaka 2015/2016, imeombewa shilingi bilioni nne kupitia katika bajeti ya maendeleo ili kuendeleza ujenzi wa lami kilometa nne.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa hili daraja gharama yake ya kulijenga ni shilingi bilioni moja na milioni mia tano na kwa kuwa uwezo wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, kutokana na vyanzo vyake vya ndani ni shilingi milioni 50, ambayo imetengwa kulijenga hili daraja na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, nilishawahi kumuuliza hili swali akaniambia kwamba tuandike barua ya kuomba TAMISEMI isaidie kujenga hili daraja na hiyo barua niliipeleka kwake mimi mwenyewe. Sasa unawashauri nini wananchi wa Tarime kuhusu ujenzi wa daraja hili?

Swali la pili, hii barabara ina kilometa 124 na ujenzi wake huwa kwa mwaka ni kilometa tano tu. Mheshimiwa Waziri haoni kwamba itachukua miaka 25 kuikamilisha hii barabara na ananishauri nini na niwaambie nini wananchi wa Tarime?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza swali limeuliza mambo ambayo yamefanyika katika Halmashauri hii na katika Wilaya hii na katika Jimbo lake la Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, sipati tatizo, kwa sababu nimekwenda katika Wilaya yake, nimekwenda katika Halmashauri yake na nimeona kazi kubwa zilizofanywa pale. Nimekuta huyu Mbunge amegawa vitabu katika shule za msingi zote na shule za sekondari zote, kwa maana yake yeye ni *producer* anatoa vitabu. Kwa hiyo, *I have got no problem* kuelewa, ndiyo swali la kwanza alilouliza, watu wasije wakafikiri nam-*patronize*, swali la kwanza alilouliza ni hilo. Amefanya kazi kubwa, amefanya mambo mengi, hii *Constituency Development Catalyst Fund*

amei-disburse, ameipeleka katika maendeleo ya zahanati, ameipeleka katika maabara na vitu vingine. Kwa hiyo, nampongeza sana kwa kazi nzuri anayofanya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hii barabara anayoisema, amekuja ofsini, wakati alipokuja hapa alipozungumza na mimi, fedha zilizotakiwa kulipwa hapa, zilikuwa milioni 350, Halmashauri hii imetengewa shilingi milioni 750, ambazo zinakwenda kule kwa ajili ya *periodic maintenance* na mambo mengine madogo madogo, *sports improvement*, ambazo haziwezi kufanya kazi hii inayozungumza hapa. Nikawaagiza watu wetu, waende kule wakafanye usanifu ili wajue gharama halisi. Wamekuja kule wakaniambia hivi, hii barabara kama unataka ifanyike na hilo daraja lijengwe analolizungumza, *1.5 billion shillings*.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri hii kama nilivyokwambia, imetengewa shilingi milioni 700, kwanza wamepelekewa, hapa wamepelekewa milioni 152, bado milioni 615 tu, haziwezi kufanya kazi hiyo. Kwa maneno mengine hapa, sasa unatakiwa sasa uanze kufikiria njia zingine za kusaidia katika jambo hili, ili daraja hili liweze kuondoka pale. Tutasukuma hizi fedha, tuna habari kwamba kuna bilioni 14 ambazo zinatakiwa kwenda katika Halmashauri, tutaona kiasi gani kinaweza kutoka kwa ajili ya kupeleka katika lile daraja analozungumza Mheshimiwa Chacha Nyangwine.

Hii barabara nyingine anayoniuliza hapa, *to be honest and frank*, najibu hii barabara kwa sababu tu unanitaka nijibu, lakini barabara hii haiko chini ya Halmashauri, barabara hii iko chini ya TANROADS na wao ndiyo wanatakiwa kujibu, lakini habari nilizonazo kwa sababu mimi ni mwakilishi wa Serikali, barabara hii kwa mara ya kwanza wametenga bilioni mbili na bilioni nne. Kwa hiyo, sasa itakuwakuwaje, itakwendakwendaje, nitalipeleka jambo hili kwa Waziri wa Ujenzi, kumwambia Mheshimiwa Nyangwine anakuuliza hivi itakuwakuwaje, atafanyafanyaje na mambo mengine.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuuliza swlai dogo la nyongeza; kwa kuwa Serikali imefanya kazi nzuri sana, kutekeleza ahadi za Rais, hasa za ujenzi wa barabara, imebakiza ahadi chache sana, ikiwemo barabara ya Singida Mjini kwenda Ilongero, kujengwa kwa kiwango cha lami aliahidi wakati anaomba kura. Je, Serikali itasema nini kwa barabara hii iliyobakia wakati muda huu mdogo umebaki?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, sina hakika sana na hii barabara anayozungumza, lakini nataka nikwambie kwamba Manispaa ya Singida, iko katika hii miji ya kimkakati, ambako kuna mambo mengi sana tunafanya kupitia *World Bank*, mpaka kusomba takataka kule na mambo mengine. Tutacheki huu mji kwa maana ya manispaa uko katika mpango huo.

Kwa hiyo, nina hakika kwamba tutakapoiangalia barabara hiyo, kwa maana mpaka niisome, nijue barabara hiyo anayoisema iko kwenye huo mpango, asije akanibania hapo, halafu nitawasiliana na yeye, lakini Singida ni moja ya maeneo ambayo tunayafanyia kazi.

SPIKA: Ahsante. Naomba tuendeleo na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Amina Abdallah Amour atauliza swali linalofuata!

Na. 13

Udhibiti na Mikakati ya Kupunguza Ajali

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR aliuliza:-

Ni jukumu la Serikali kupitia vyombo vya barabarani kuhakikisha usalama barabarani:-

(a) Je, ni kampuni ngapi za mabasi zilizosababisha ajali na kuchukuliwa hatua?

(b) Kwa kuwa ajali zinaongezeka kila mwaka, je, Serikali ina mikakati gani ya kupunguza ajali hizo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Amour, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua madhubuti dhidi ya Kampuni za Usafirishaji zinazokithiri katika kusababisha ajali barabarani. Kwa mfano, mwaka 2014, makampuni 26 yenye jumla ya vyombo vya usafiri 98 yalifungwa kutoa huduma hapa nchini kwa kipindi cha kati ya mwezi mmoja hadi miezi sita kutegemeana na kiwango cha kasoro zilizobainika katika kampuni husika.

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na matukio ya ajali za mara kwa mara barabarani, takwimu zinaonesha kupungua kwa ajali nchini. Mwaka 2014 zilitokea ajali 14,000, zilizosababisha vifo vya 3,760 na kujeruhi 14,530, ukilinganisha na ajali 23,842 ambazo zilisababisha vifo vya watu 4,002 na majeruhi 20,689 mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mikakati mbalimbali kupambana na wimbi la ajali kama ifuatavyo:-

(i) Usimamizi wa mifumo ya sheria kudhibiti makosa hatarishi kama vile ulevi, mwendo kasi, ubovu wa vyombo vya moto na utendaji mbovu wa Askari wa Usalama Barabarani;

(ii) Utoaji wa elimu kwa umma kwa njia ya vyombo vya habari, mashuleni na kwenye mitandao ya kijamii; na

(iii) Serikali iko mbioni kutekeleza matumizi ya kifumo mipya ya udhibiti wa makosa ya usalama barabarani ikiwemo mfumo wa nukta katika leseni za udereva, mfumo wa kufuatilia mwenendo wa magari barabarani (*car tracking system*), mfumo wa kulipia faini kwa njia za elektroniki, mfumo wa ukaguzi wa lazima wa magari na mafunzo ya lazima kwa madereva wa magari makubwa hasa ya mizigo na madereva wa magari ya abiria.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Waziri amesema kuwa makampuni 26 yamefungwa kwa ajili ya ajali na kufungwa kwao ni kati ya mwezi mmoja hadi miezi sita na bado ajali zinaendelea kwa wingi sana. Je, Mheshimiwa Waziri haoni mwezi mmoja hadi miezi sita ni kidogo na badala yake iwe mwaka mmoja hadi miaka miwili?

Mheshimiwa Spika, swali lingine; kwa kuwa kuanzia Januari mwaka huu ajali nyingi zimetokea na kusababisha vifo vingi na ninyi Serikali mnasema mna mkakati madhubuti wa kupambana na ajali hizi, je, mikakati hiyo itaanza lini kufanya kazi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nimpungeze Mheshimiwa Amina kwa kuwa na uchungu wa kupoteza Watanzania wenzetu na wale ambao wanapata ulemavu wa kudumu. Sote tukiwa na uchungu nina hakika ajali zitapungua.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la kufungia zaidi ya mwezi mmoja kwa maana ya mwaka au miaka miwili tunalichukua, kwa sababu hili ni suala la kikanuni na iwapo watu wengi watakuwa na mawazo haya, basi hili linaweza likawa sehemu ya sheria tunazozisimamia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikakati, kama nilivyosema ni kweli kwamba katika miezi hii ya kuanzia mwezi wa Tatu mpaka mwezi wa Nne tulipata ajali nyingi sana na sina budi niungane na familia ambazo zilipoteza jamii zao, lakini kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu jana, ni kwamba mambo haya tunayafanyia utafiti kwa nini yametokea na yanatokea vile ilivyo.

Mheshimiwa Spika, mikakati yetu ilitakiwa ianze mwezi wa Nne mwaka huu na kuna baadhi ya vipengele tayari vilikuwa vianze, lakini mgomo wa madereva uliotokea bado tunaendelea kujadiliana, halafu ikiwezekana tutaianza moja kwa moja na kuna baadhi inahitaji fedha ambazo bado hazijapatikana.

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ongezeko la Awamu ya Nne ya Serikali yetu kujenga barabara nyingi za lami kwa kiwango ambacho kinapendezesha nchi yetu limesababisha kuwepo kwa ajali nyingi na kwamba barabara hizo mara nyingi zimejengwa zikiwa ama ni nyembamba ama hazina ubora unaostahili. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza ama kuzipanua barabara hizi ambazo nyingi zimekuwa nyembamba na huwa zinasababisha ajali ya magari kugongana uso kwa uso?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba baadhi ya barabara zinajengwa nyembamba na nyingine pia zinakosa uimara unaohitajika. Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi naiona inapanua sehemu za barabara. Hata mfano, barabara hii ambayo inatoka Morogoro kuja Dodoma naona inapanuliwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo tatizo letu kubwa si barabara kwa maana ya wembamba wake. *In fact* tatizo ambalo linasababisha ajali nyingi ni uamuzi wa madereva, wapi nifanye nini na wapi niache kufanya nini. Hili tukilisimamia, ambalo hasa ni la usimamizi wa sheria na elimu nina hakika tunaweza tukapunguza ajali.

SPIKA: Kutokana na muda tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Moses Machali!

Na. 14

Ujenzi wa Nyumba za Askari Polisi na Magereza – Kasulu

MHE. MOSES J. MACHALI aliuliza:-

Maisha ya Askari Polisi na Magereza katika suala la nyumba ni duni ni sana Wilayani Kasulu.

Je, ni lini Serikali itatenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za askari hao kaa ilivyo katika Wilaya nyingine?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyowahi kujibu maswali kadhaa ndani ya Bunge lako Tukufu kuhusu uhaba wa nyumba za Askari Polisi na Magereza hapa nchini, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa nyumba za Askari Polisi na Magereza katika Wilaya ya Kasulu kama ilivyo kwenye Wilaya nyingine haziko katika hali za kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, mahitaji halisi ya nyumba za Askari Polisi na Magereza nchi nzima ni makubwa sana kulinganisha na uwezo wa Serikali na kufanikisha ujenzi wa nyumba hizo kwa wakati mmoja ni vigumu. Serikali itaendelea kujenga nyumba za Askari Polisi na Magereza kwa kadiri bajeti itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jeshi la Polisi Serikali inatarajia kupata mkopo nafuu kutoka Serikali ya China utakaofanikisha ujenzi wa nyumba 4,136 nchi nzima ikiwemo Kasulu. Aidha, kupitia dhana ya mashirikiano na sekta ya umma na binafsi (PPP) Jeshi la Polisi chini ya Shirika lake la Uchumi litajenga nyumba kwa kuanzia 350 eneo la Oysterbay na kuendelea nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza limekuwa likifanya ukarabati wa majengo ambayo ujenzi wake haujakamilika na kujenga makazi mapya kwa kutumia vifaa vya ujenzi vinavyopatikana maeneo husika na ambavyo havizalishwi viwandani kwa nia ya kupunguza tatizo hili na pia gharama za ujenzi.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa nimuulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa mujibu wa majibu ambayo nimepata hapa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba, hizo nyumba 4,136 nchi nzima sio na maneno ambayo yameongezwa ikiwemo Kasulu hayapo katika majibu yangu. Sasa...

SPIKA: Majibu au katika swali...

MHE. MOSES J. MACHALI: Naam!

SPIKA: Hayapo kwenye nini?

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika hayapo kwenye majibu yangu hapa...

SPIKA: Ahaa!

MHE. MOSES J. MACHALI: Maneno mengine kwamba nchi nzima ikiwemo Kasulu wakati anasoma.

SPIKA: Nakala ya majibu aliyokupa.

MHE. MOSES J. MACHALI: Katika nakala ya majibu ambayo amenipatia.

SPIKA: Okay, endelea basi.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, sasa kwanza hii ni dosari maneno mengine yameongezwa hapa. Swala la kwanza, Mheshimiwa Waziri atakumbuka amefanya ziara Kasulu namshukuru vizuri, amekwenda Magereza, amekwenda Polisi, ameona nyumba za askari hali ni mbaya. Kwanza kuna nyumba zipatazo 11 za Askari Polisi, Magereza wana nyumba chache pia vile vile.

Mheshimiwa Spika, Askari Polisi waliopo katika Wilaya ya Kasulu ni takriban askari 200, nyumba 11. Mheshimiwa Waziri naomba anieleze na alieleze Bunge, je, katika hizi nyumba 4,136 Wilaya ya Kasulu itapata nyumba ngapi za Askari Polisi? Pia bila kuwasahau Magereza kama ambavyo uliona na nimetumia juhudi zangu kwa kutumia Mfuko wa Jimbo, kidogo nimekuwa nawachangia wanajenga kidogo kidogo. Naomba nijue ni nyumba ngapi.

Swali la pili; zipo taarifa kwamba eneo hili ambalo linatajwa ni eneo la Kituo cha Polisi Oysterbay linatajwa kwamba limeuzwa, sasa ninyi mnatumia mlango ambapo mnasema kwamba PPP. Naomba kauli ya Serikali, je, ni kweli kwamba eneo hili limeuzwa ili kusudi iweze kujengwa *shopping mall* halafu leo mnatambia kwamba mnajenga nyumba 350. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na suala hili?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kabla sijasema chochote, naomba nimpongeze Mheshimiwa Machali. Wakati natayarisha majibu haya ambayo nimempatia niligundua kwamba Mheshimiwa Machali alichangia milioni tano katika ujenzi wa nyumba za Magereza pale Kasulu. Mheshimiwa unakwenda ndipo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kuhusu nyongeza ya kusema ikiwemo Kasulu, nchi nzima haiwezi ikaitoa Kasulu. Kwa hiyo, hata kama sikuliandika sidhani kama ni makosa kama nchi nzima nikamtajia Kasulu kama sehemu ya nchi hii. Sasa katika nyumba 4,136 anauliza Kasulu itapata ngapi. Mgao bado haujafanyika na utakapofanyika namhakikishia kwamba nitampa taarifa hizi.

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusu Oysterbay. Oysterbay haijauzwa na haitauzwa. Oysterbay katika kutafuta *solutions* nje ya bajeti ya kupata nyumba kwa ajili ya askari anaowatetea, tukaingia ubia na mtu ambaye atafanya eneo la biashara Oysterbay na katika makubaliano hayo atajenga hizi nyumba 350 za askari. Hivi sasa ameanza kufanya kazi hiyo ya kujenga nyumba 350 na ataendelea kujenga maeneo ya biashara ambayo nayo Serikali haitafaidika tu na nyumba lakini itafaidika na ujenzi huu na biashara itakayofanyika.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Hii hadithi ya ujenzi wa nyumba za Polisi ni ya muda mrefu sana na ukweli ni kwamba askari wetu hasa Wilayani wanadhaliika mno. Pale Rombo wanaishi katika mabanzi ambayo kunguni, sungusungu wanawasumbua sana. Ni kwa nini Serikali, kwa sababu ya mazoea ya kuwaomba wananchi kuchangia katika maeneo mengi ujenzi wa Zahanati na mambo mengine, usiwepo msukumo wa Serikali kuwashauri wananchi kusaidia ujenzi wa hizi nyumba za askari kwa sababu ulinzi ni kitu cha muhimu sana katika nchi yetu?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Selasini anauliza aonekane lakini jibu la jambo hili analo. Mheshimiwa Selasini kule amejenga Vituo vya Polisi na amenialika nikavifungue vingi sana. Nyumba za Polisi si tofauti na Vituo vya Polisi. Mheshimiwa Selasini saidia kutoa haya majibu kwa wenzako ili Tanzania na askari wetu waweze kupata nyumba zinazohitajika.

SPIKA: Haya, tuendeleo, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, alitaka aseme hivyo. Mheshimiwa Obama Ntabaliba swali linalofuata. Mheshimiwa Machangu swali hilo!

Na. 15

Wakulima wa Kahawa Manyovu na Kalinzi

MHE. BETTY E. MACHANGU (K.n.y. MHE. ALBERT O. NTABALIBA) aliuliza:-

Wakulima wa kahawa wa Manyovu na Kalinzi walidhulumiwa kahawa yao kwa kutolipwa na Kalinzi *Organic*; Serikali kupitia Wizara husika iliahidi kufuatilia malipo hayo kwa wakulima:-

Je, ni lini sasa malipo hayo yatafanyika kwa wakulima hao wa kahawa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Jimbo la Manyovu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, msimu wa mwaka 2011/2012, vikundi vya wakulima wa kahawa vya Kalinzi *Organic Coffee* na Kalinzi *Coffee Farmers (KACOFA)* vilipeleka kahawa kwa ajili ya ukoboaji katika Kiwanda cha Kukoboa Kahawa cha Tanganyika *Coffee Curing Company Limited (TCCCO)* yenye thamani ya dola za Kimarekani elfu sabini na nne mia tatu tisini na saba nukta mbili nne na mia tano sitini na nne elfu mia saba tisini na nne nukta tisa moja sawia.

Hata hivyo wakati wa kupeleka kahawa hiyo mnadani na wakati wa mauzo kampuni ya TCCCO ilifanya makosa ya kuitambulisha kahawa ya Kalinzi *Organic* kama kahawa ya KACOFA, hivyo Bodi ya Kahawa kufanya malipo kwa kikundi cha KACOFA badala ya Kalinzi *Organic*.

Mheshimiwa Spika, kufuatia malalamiko ya kikundi cha Kalinzi *Organic* kutolipwa fedha zao, Wizara iliingilia kati suala hilo kwa kuzikutanisha pande zote zinazohusika na mgogoro huo (Kalinzi *Organic*, Kalinzi *Coffee Farmers*, Kiwanda cha TCCCO Limited na Bodi ya Kahawa ili kulipatia ufumbuzi suala hilo.

Mheshimiwa Spika, kupitia vikao vya usuluhishi Kiwanda cha TCCCO kilikiri kufanya makosa ya kuchanganya majina kwenye nyaraka za malipo. Kimsingi kikundi cha KACOFA kilikubali kurejesha fedha za Kalinzi *Organic Coffee*. Hata hivyo, suala hilo limechukua muda mrefu kutokana na viongozi wa KACOFA kutotekeleza makubaliano ya vikao vya usuluhishi.

Mheshimiwa Spika, baada ya viongozi wa KACOFA kukaidi kutekeleza makubaliano hayo, Wizara iliagiza Bodi ya Kahawa na Kiwanda cha TCCCO kuunda timu ya uchunguzi ili kubaini ukweli wa malipo ya dola za Kimarekani 74,397.24 walizolipwa KACOFA kimakosa kama wakulima wa KACOFA walilipwa fedha hizo au viongozi wa KACOFA ndio walionufaika na fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya timu hiyo kufanya uchunguzi ilibainika kuwa fedha walizolipwa KACOFA hazikulipwa kwa wakulima wa Kahawa bali viongozi wa KACOFA waligawana fedha hizo. Hivyo kwa mazingira hayo imekuwa vigumu kwa Wizara na Bodi ya Kahawa kukata fedha za KACOFA zilizopelekwa mnadani katika misimu iliyofuata ili kuwalipa Kalinzi *Organic* kwani kufanya hivyo ingekuwa ni kuwaadhibu wakulima wa KACOFA ambao hawana hatia.

Mheshimiwa Spika, katika hali hiyo Wizara imeagiza kiwanda cha TCCCO kwa kuwa ndio waliosababisha tatizo hilo kulipa deni la wakulima wa Kalinzi kiasi cha dola za Kimarekani 74,397.24. Sanjari na hatua hiyo Wizara kupitia Mrajisi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika inachukua hatua dhidi ya viongozi wa KACOFA waliohusika ili warudishe fedha hizo na kinyume chake hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika, duniani kote kahawa bado inaendelea kupendwa kunywewa na inavyoonekana kwa Tanzania kuhudumia kahawa kumekuwa kwa ghali sana kiasi ambacho wakulima wamekata tamaa kwa sababu ya yale madawa ya kuhudumia kahawa yamekuwa ni ghali sana na Serikali inaelekea kwamba haina tena *interest* ya kuwekeza kwenye kahawa. Naomba Serikali itueleze ni kweli kwamba wanaona kwamba kahawa haina tena faida?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika mdororo wa uchumi uliotokea miaka mitatu minne iliyopita wakulima wa pamba walikuwa *compensated* na Serikali kwa kile walichopoteza na hata ng'ombe waliokufa Ngorongoro na wenyewe walipata dhamana hiyo, lakini wakulima na Chama cha Kahawa cha *KNCU* tulipata mdororo huo huo na wakulima wale hawakulipwa hata senti tano. Naomba kauli ya Serikali.

SPIKA: Ahsante, swali la mwenzako hukulitendea haki hata kidogo. Haya! Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba Serikali imeacha kujali wakulima wa kahawa na kwa maana hiyo kwamba haiwahudumii. Naomba nimfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali bado inaendelea kutoa ruzuku katika uzalishaji wa miche ya kahawa kwa wakulima na kule pia upande wa Kaskazini Kilimanjaro kuna Kituo cha Lyamungo ambacho pia kinazalisha miche bora sana na kwa bei ambayo kimsingi ina ruzuku ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia tunatengeneza hivi vituo vya kukoboa kahawa (*Central Pulper Units*) ambazo kimsingi pia Serikali inavi-*subsidize* vituo hivi vya kukobolea kahawa ili wananchi hawa pia wasiendeleo kuona kwamba kuzalisha kahawa ni adhabu zaidi.

Mheshimiwa Spika, vilevile kodi ya kahawa zilikuwa karibu nane, miaka minne iliyopita kwenye kahawa kulikuwa na kodi zaidi ya nane, lakini kodi hizo zilipungua na sasa hivi kuna kodi karibu nne ambazo kimsingi ni kodi za kisheria ambazo lazima zilipwe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali imekuwa wakati wote inaangalia uwezekano wa kuinua uzalishaji wa zao la kahawa ili wananchi hawa waweze kufaidika. Mpaka sasa tunazalisha karibu wastani wa tani 42,000 kwa mwaka na kwa mipango iliyopo tunataka kufika angalau tani 60,000 za uzalishaji wa kahawa kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu *KNCU* kutopewa pesa. Serikali ilitangaza taratibu za wale ambao walinunua kahawa na kwa sababu ya mdororo wa uchumi wakaathirika, taratibu zilitangazwa ili waweze kuwa *compensated*. Wale ambao walifuata masharti yale walikuwa *compensated*. Sasa inawezekana *KNCU* hawakufuata yale masharti au namna gani, lakini kimsingi zoezi lile lilishakwisha na lilishafungwa.

SPIKA: Hukusimama kabla! Tuendeleo na swali linalofuata, Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, kwa niaba yake Mheshimiwa Mwatuka!

Na. 16

Mikopo Nafuu kwa Watanzania Waliojajiri Katika Sekta ya Kilimo

MHE. CLARA D. MWATUKA (K.n.y. MHE. ASAA OTHMAN HAMAD) aliuliza:

Idadi kubwa ya Watanzania wamejiajiri kwenye sekta ya Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa upatikanaji wa mikopo nafuu kutoka Taasisi za Fedha ili kuendeleza kilimo chenye tija?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa mikopo na mitaji kwa wakulima ni mhimili muhimu katika maendeleo ya kilimo nchini. Hata hivyo, upatikanaji wa mikopo nafuu kwa wakulima hususan wakulima wadogo unakabiliwa na changamoto mbalimbali kutokana na sekta ya kilimo kukabiliwa na majanga mbalimbali yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo ukame, mafuriko, milipuko ya wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea. Aidha, upatikanaji wa mikopo kwa wakulima wadogo unakabiliwa na changamoto ya kukosa hati miliki za mashamba zinazoweza kutumika kama dhamana (*Collateral*) na riba kubwa isiyoendana na msimu wa uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo, Serikali inachukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto hizo ikiwemo kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo (*The Tanzania Agricultural Development Bank – TADB*) ambayo inatoa mikopo nafuu kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, Mpango Mkakati wa Benki ni kufanya kazi kwa karibu sana na Benki za wananchi (*Community Banks*) pamoja na benki za ushirika (*Cooperatives Banks*). Aidha, Benki hiyo itaingia mikataba (*sub – contract*) na Benki nyingine za biashara pale ambapo hakuna Benki za Wananchi na Benki za Ushirika ili kuhakikisha inawafikia wakulima wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kupanua wigo wa utoaji wa mikopo kupitia Mfuko wa Pembejeo (*Agriculture Input Trust Fund*) ambao unalenga kukopesha wakulima pembejeo na zana za kilimo kwa gharama nafuu. Aidha, Serikali itaendelea kuhamasisha mabanki ya biashara kukubali hati za kimila (*Certificate of Customary Right of Occupancy – CCRO*) zinazotolewa kwa wakulima wanaomiliki ardhi ili waweze kupata mikopo kutoka kwenye benki kwa wale wanaokusudia kufanya hivyo ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo kwa wakulima nchini.

SPIKA: Mheshimiwa Clara Mwatuka, swali la nyongeza!

MHE. CLARA DIANA MWATUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuongeza maswali madogo kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, baadhi ya wakulima walio wengi hawana elimu au uelewa wa jinsi gani wanaweza kupata mikopo. Je, sasa Serikali ipo tayari kutoa elimu kwa ajili ya wakulima hawa ili waweze kunufaika na mikopo hiyo?

Pili, baadhi ya wakulima mashamba yao ni madogo ambayo hayana hati ya ardhi au hati ya kimila na baadhi yao wanategemea kilimo cha bustani za mboga na bustani za mboga zinahitaji gharama kubwa kwa mfano pembejeo, madawa na mbegu zenyewe, gharama kubwa ambazo wangehitaji kupata hiyo mikopo. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha wakulima hawa ili wapate hiyo mikopo?

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, elimu imekuwa inatolewa kwa wananchi na kwa kweli itashangaza sana kama kuna Mtanzania leo ambaye hajui kwamba zipo taasisi zinazotoa mikopo kwa wakulima au wafanyabiashara au makundi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lakini kama hilo ni tatizo, Mheshimiwa Mbunge pia naye ni Diwani katika nafasi yake, anaweza pia kutumia Halmashauri zetu na kwa sababu sisi ni wawakilishi wa wananchi kule chini, tukatumia fursa zetu na nafasi zetu tulizonazo ili kuwaelimisha wananchi hawa waweze kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye Halmashauri zetu kuna Mifuko midogo kwa wanawake na vijana ambayo pamoja na kwamba upatikanaji wake wa fedha unawezekana usiwe mzuri lakini pesa huwa zinatolewa pale zinapopatikana na hili kama Waheshimiwa Wabunge tungelisimamia vizuri, nadhani wananchi wetu pia wangependa kupata mikopo ya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni sawasawa tu na swali hili la pili ambalo anasema kwamba kuna wakulima wadogo ambao inawezekana hawana ardhi ya kutosha, lakini wangependa kulima bustani.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa mikopo upo katika namna mbalimbali na ndiyo sababu pia tunawahamasisha wananchi ili wajiunge kwenye vikundi vya ushirika ambapo wakiwa pamoja ni rahisi ukichangia kidogo ukapata mikopo na kuendeleza kilimo chako.

Kwa hiyo, nawaomba wananchi wengi waendele kujiunga kwenye vikundi vya ukopeshaji wa ushirika ambapo kupata mikopo inaweza kuwa ni rahisi zaidi kuliko kama akisimama peke yake.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Zaidi ya 80% ya Watanzania ni wakulima na mpaka leo tunasema uti wa mgongo wa nchi yetu ni kilimo. Sasa tumekuwa tukisisitiza kwamba wananchi wajitahidi kupata hati za kimila za maeneo yao wanayoyamiliki na lengo kubwa likiwa ni ili kuwawezesha kupata mikopo waweze kujiinua katika kilimo chao.

Je, ni lini Serikali itaweka utaratibu mzuri ili Benki za Biashara zikubali hati za kimila na kuwapatia wakulima mikopo ili waweze kuinua kilimo chao na kuongeza kipato cha Watanzania hawa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba lipo tatizo kimsingi la matumizi ya hati za kimila katika baadhi ya maeneo na hivyo kufanya mabenki au taasisi za kifedha kutozikubali moja kwa moja ingawa pia ni ukweli kwamba zipo baadhi ya benki ambazo zimeanza kukubali hati za kimila na hivyo kuwakopesha wananchi mikopo.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo ni kwamba kama umekopa mwenye hati ya kimila katika eneo 'X' na ikitokea mtu aliyekopa akashindwa kulipa, masharti yanataka mnunuzi atoke katika eneo lilelile. Sasa mabenki mengi katika utaratibu huo yamesita.

Mheshimiwa Spika, sasa tumeanza kufanya mazungumzao na wenzetu wa Wizara ya Ardhi ili tupitie hati upya ili tuondoe vile vipengele upya ambavyo vina kikwazo kwa taasisi za

fedha ili zikirekebishwa basi zitumike vizuri zaidi na mabanki au taasisi za fedha zisione kwamba ni kikwazo kutoa mikopo kwa wananchi ambao watakuwa na hati miliki za kimila.

SPIKA: Maelezo ya nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi!

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili kuongezea majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kutoka Wizara ya Kilimo.

Kwanza kabisa nzipongeze benki zote ambazo zimekuwa zikitoa mikopo kupitia hati za kimila, NMB wamekuwa wakifanya hivyo kwa baadhi ya sehemu, CRDB wamekuwa wakifanya hivyo, lakini vile vile kupitia SACCOS mbalimbali na nipongeze zaidi benki hizi katika Wilaya ya Mbozi lakini vile vile Namtumbo, Manyoni, Bariadi na Babati.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la utoaji wa hati za kimila, suala hili lipo chini ya Halmashauri za Wilaya, ni jukumu lao kupitia sheria ya vijiji namba tano ya ardhi, ndiyo waliyokasimiwa mamlaka ya usimamizi wa masuala mazima ya ardhi.

Vile vile ukiangalia suala hili mwenye jukumu kubwa la kwenda kuomba hati za kimila ni mwananchi mwenyewe na Wizara, lakini na Wizara lakini vilevile kushirikiana na TAMISEMI tumekuwa tukihamasisha na elimu imekuwa ikitolewa kwa watendaji wa Halmashauri kupitia Kamati za PLAM kuhakikisha kwamba wanatoa hati za kimila.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ambayo imekuwa ikipatikana kama ambavyo Mheshimiwa Zamboni amekuwa akieleza, unakuta katika hati moja ya masharti ni lazima atakayekuja kununua ikipigwa mnada lazima awe ni mkazi wa eneo husika. Kwa hiyo, ukiangalia kwa benki kwa kweli haziko tayari ku-*take risk* kwenye suala hilo na sisi kama Wizara tumeliona na tunalifanyia kazi kupitia marekebisho mbalimbali ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji, tunaangalia ni kwa namna gani tunalifanyia kazi suala hili ili kuondoa kikwazo hiki.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ambayo imekuwa ikitupata, ni lazima ili hati za kimila zitolewe kuwe na cheti cha usajili wa ardhi ya Kijiji. Vipo vijiji vingine vimekuwa vina migogoro ya mipaka na inapokuwa kuna changamoto hii, zoezi zima la utoaji wa hati za kimila inabidi lisimame mpaka hapo mgogoro huu utakapokuwa *resolved*.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa Halmashauri mbalimbali, ziendelee kutoa hati hizi maana yake ukiangalia hadi sasa ni Wilaya 67 tu ndiyo ambazo zimetoa hati za kimila.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Ahsante, maelezo yanatosha. Tunakwenda Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed atauliza swali hilo, kwa niaba yake Mheshimiwa Amina Mwidau atauliza swali hilo!

Na. 17

Serikali Kuanzisha Uvuvi Bahari Kuu

MHE. AMINA M. MWIDAU (K.n.y. MHE. RUKIA KASSIM AHMED) aliuliza:

Wavuvi wetu nchini hawana uwezo wa kuvua katika Bahari Kuu kutokana na ukosefu wa Teknolojia, zana na vyombo vya kuvulia vinavyohimili dhoruba ya Bahari Kuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha uvuvi wa Bahari Kuu?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu katika kuwasaidia wavuvi wadogo kushiriki kuvua samaki imefanya yafuatayo:-

(i) Mamlaka hiyo kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (*TAFIRI*) imeweka vifaa vya kuvutia Samaki (*Fishing Aggregate Devices (FADs)*) katika maeneo ya karibu na kisiwa cha Latham ili kurahisisha upatikanaji wa samaki.

(ii) Mamlaka pia imetoa ufadhili wa mafunzo ya uvuvi wa Bahari Kuu kwa wavuvi 100 (50 kutoka Serikali ya Tanzania Bara na 50 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar) kwa miaka ya fedha 2013/2014 na 2014/2015.

(iii) Kwa kushirikiana na *TAFIRI*, Mamlaka imeingia makubaliano ya kufanya utafiti wa maeneo ya uvuvi (*Potential Fishing Zones*) ambayo yatarahisisha uvuvi na kupunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu pamoja na Taasisi nyingine zinazojihusisha na uvuvi zitaendelea kuwasaidia wavuvi ili waweze kunufaika na fursa za kufanya uvuvi endelevu katika bahari, maziwa na mito hapa nchini.

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa, hali za kiuchumi za wavuvi wengi hasa katika ukanda wa Pwani ni duni sana na kutokana na vifaa duni wanavyotumia na soko lisilo na uhakika na katika ukanda wa Pwani Tanga kuanzia Mkinga mpaka Bagamoyo kuna kiwanda kimoja tu cha Samaki.

Je, hamwoni kuwa sasa hivi ni wakati muafaka wa kujenga kiwanda kingine kikubwa katika ukanda huo ambacho kinaweza kuwasaidia wavuvi hao ili kupata soko la uhakika na kuwa na vifaa bora vya uvuvi?

Swali la pili, katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri ameelezea kuwa mamlaka ya kusimamia uvuvi wa Bahari Kuu unashirikiana na *TAFIRI* umeweka vifaa vya kuvutia samaki katika maeneo ya karibu na Kisiwa cha Latham. Anaonaje sasa wakawasaidia wavuvi wa Pangani hususani katika Kijiji cha Mkwaja, kuna fungu la Buyuni ambalo *TANAPA* wamelichukua kama kivutio cha utalii. Wavuvi hawapati nafasi ya kwenda kuvua, wanapigwa na kunyanyaswa na wanalishwa samaki wabichi.

Je, kwa mfano huu aliouonyesha hapa wa kuweka vifaa vya kuvutia samaki, je, wanawasaidiaje wavuvi ili waweze kujikwamua na wasipate matatizo hayo?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mwidau, hotuba! Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba zana za wavuvi wadogo ni duni na ndiyo maana tuna mkakati mzima wa kusaidia wavuvi wadogo wadogo kwa kuwapa ruzuku na tumeanza na zaidi ya shilingi bilioni mbili katika mwaka wa fedha 2014/2015 kwa ajili ya kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo kupata zana ambazo zinaweza kusaidia katika uvuvi wa Bahari Kuu na katika maeneo mengine kandokando ya bahari, maziwa na mito.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kuchakata mazao ya samaki, ni kweli lakini kwanza tuna utaratibu wa kutaka kujenga bandari kuu kwa ajili ya uvuvi mkubwa ambapo meli kubwa zitakuwa zinawekeza pale ili tuweze kupata mazao zaidi ya samaki kwa kuwa na bandari hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wavuvi wadogo wadogo wa Pangani, naomba nipate nafasi ili nizungumze na Mheshimiwa Mbunge na niende huko ili niangalie hicho kilichotolewa na TANAPA ili tuangalie uwezekano wa kusaidiana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante. Kutokana na muda tunakwenda sasa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Dalali Peter Kafumu, kwa niaba yake Mheshimiwa Murtaza Mangungu.

Na. 18

Askari Waliopigana Vita vya Kagera

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU (K.n.y. MHE. DKT. DALALI P. KAFUMU) aliuliza:-

Mwaka 1978 Askari wengi wakiwemo Askari kutoka JWTZ, JKT, Jeshi la Mgambo, Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza walishiriki Vita vya Kagera ili kumwondoa Nduli Idd Amin. Mwaka 1979 baada ya ushindi Askari hao walilipwa mafao ambayo hayakutosheleza kutokana na kazi waliyoifanya na baada ya Uganda kuilipa fidia Tanzania, Serikali iliwaorodhesha tena Askari hawa ili walipwe, lakini hawajalipwa mpaka sasa:-

Je, ni lini Serikali itawalipa Askari hawa ambao sasa ni wastaafu waliopigania nchi yetu kwa uaminifu na uadilifu?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalali Peter Kafumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika vita ya Kagera JWTZ kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama walipigana bega kwa bega na hatimaye kushinda vita. Baada ya vita wapiganaji walitunukiwa nishani mbalimbali kama vile Nishani ya Kagera kwa wale waliokwenda mstari wa mbele na Nishani ya Vita kwa wale waliobaki nchini kulinda vituo muhimu, wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Spika, katika vita hiyo wapo wanajeshi waliopoteza maisha, kujeruhiwa na wapo waliorudi salama. Wote hao au familia zao wamelipwa fedha stahiki kulingana na viwango vya wakati huo. Aidha, Serikali inaendelea kuwajali na kuwathamini mashujaa wetu hao na kuwaona watu muhimu sana katika historia ya Taifa hili na kila tarehe 25 Julai ya kila

mwaka huwa tunaadhimisha Siku Maalum ya Mashujaa kwa kuwakumbuka wapiganaji wetu waliojitoa maisha yao katika kulilinda Taifa letu. Pia, wapiganaji waliopata ulemavu wakati wa vita hivyo wanaendelea kulipwa pensheni ya ulemavu hadi sasa.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Napenda nimuulize Mheshimiwa Waziri maswali mawili ya nyongeza. Wapo ambao wamelipwa fidia na kama Serikali ilivyoahidi kwamba inafanya utaratibu huu utakwisha lini kwa sababu sasa hivi ni zaidi ya miaka 37 tangu hilo jambo lihadiwe na Serikali. Kwa hiyo, ahadi ya Serikali ni lini watafidiwa pesa hiyo ya nyongeza ili kujikimu na kusaidia familia zao kwa sababu sasa hivi wengi ni wazee sana wanahitaji kusaidia familia zao ili waache urithi wa maisha yanayoendelea? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, katika mchakato huu wengi walichukuliwa, wakapelekwa kule na waliopoteza maisha na kuumia wengine mpaka leo hawajapata fidia hizi. Je, pale ambapo taratibu zitakuwa zimekamilika kwa maana ya kuwasilisha vilelezo, Serikali ipo tayari kuwalipa wananchi hawa?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba utaratibu wa kuwalipa waliopigana katika vita ya Kagera ulishakamilika na kwa wakati huo kwa viwango vilivyokuwepo wakati huo stahili zilitolewa kwa wahusika wote. Sasa sina uhakika ile ahadi ya utaratibu wa nyongeza imetoka wapi, lakini ninachoweza kusema ni kwamba nyongeza tunayoizungumzia ni nyongeza ya jumla yaani nyongeza ya pensheni kwa Askari wote pamoja na nyongeza ya stahili za malipo ya ulemavu. Kwa hiyo, hiyo ndiyo inayofanyiwa kazi na Serikali ili iweze kupatikana kwa wastaafu wote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la fidia ya kuumia, ninachoweza kusema ni kwamba, kila mwanajeshi anastahili kupata fidia akiumia kazini. Kwa hiyo, kama kuna ambao hawajapata mpaka sasa na wana ushahidi na vilelezo vya kutosha, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hao wanastahili hivyo waleta vilelezo vyao tutahakikisha kwamba wanalipwa stahili zao.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na swali la mwisho, Mheshimiwa Rachel Mashishanga!

Na. 19

Uonevu Unaofanywa na Kikosi cha Jeshi cha 516KJ

MHE. RACHEL R. MASHISHANGA aliuliza:-

Kumekuwepo na uonevu mkubwa unaofanywa na kikosi cha Jeshi cha 516 KJ kilichopo Kata ya Kizumbi, Manispaa ya Shinyanga kwa kuwapiga wananchi, kushikilia mifugo na kisha kuwatoza faini ya sh. 10,000/= kwa kila mfugo:-

Je, ni lini Serikali itatuma kitengo cha kukagua mipaka katika eneo hilo la Jeshi ili wananchi wasibughudhiwe na waendeleo kufanya shughuli zao kama ilivyokuwa hapo awali?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rachel Mashishanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la Kikosi cha 516 KJ kilichopo Kata ya Kizumbi, Shinyanga limepimwa mwezi Julai, 2005, ramani yake ilithibitishwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, tarehe 8 Oktoba, 2005 na kusajiliwa kwa *Plan No. 41251*. Serikali za Vijiji na wananchi wanaozunguka eneo hilo wanaijua mipaka ya eneo la Jeshi iliyowekwa baada ya upimaji kukamilika.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 2011, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliunda Tume ya Kufuatilia Migogoro kwenye maeneo ya Jeshi na kubaini kuwa kuna wananchi wengi katika Kata ya Kizumbi wanaingiza mifugo katika maeneo ya Jeshi kutafuta malisho. Uongozi wa Kikosi cha 516 KJ una wajibu wa kulinda eneo hilo ili litumike kwa shughuli za kijeshi zenye manufaa kwa ulinzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa rai kwa mara nyingine tena kuwataka wananchi kuheshimu mipaka ya maeneo ya Jeshi kote nchini ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima.

MHE. RACHEL R. MASHISHANGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kabla sijauliza maswali yangu mawili ya nyongeza naliomba Jeshi pia liheshimu mipaka yote ili kuepusha migogoro isiyokuwa ya lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi hili linazungukwa na barabara moja hivi ambayo inatumiwa na wanavijiji wanaotoka katika vijiji vya Ikoma, Mwamnyepele na Igumna. Wanavijiji hawa wamekuwa wakinyanyaswa na kupigwa wanapopita katika eneo hilo, lakini zaidi wanalazimishwa kula vinyesi vya ng'ombe. Naomba Serikali itamke hapa ni lini tabia hii itakomeshwa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Tatizo hili limekuwa ni kubwa sana na sugu kwa sababu maeneo mengi kwa mfano, hata Kunduchi na Arumeru wamekuwa na migogoro hii baina ya Jeshi na wananchi. Ni kwa nini Serikali isijikite katika kutoa elimu kwa wananchi ambao wanazunguka maeneo haya ya Jeshi? *(Makofi)*

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rachel Mashishanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninataka nimhakikishie kwamba, Jeshi linaheshimu mipaka. Hakuna sababu hata moja ya Jeshi kutoka nje ya mipaka yake kwenda kufuata raia walipo na kuwanyanyasa.

Kwa hiyo, mara nyingi kunapokuwa na migogoro utakuta ni raia wanaingia katika maeneo ya Jeshi kwa sababu Jeshi lilikamata maeneo hayo siku nyingi wakati ardhi ilikuwa haina thamani kama ilivyo sasa na ndiyo maana matatizo haya yanatokea. Hata hivyo, tunaendelea kusisitiza kwamba, mipaka itawekwa na kila upande; Jeshi kwa maana hiyo na upande mwingine wa wananchi wakiheshimu mipaka hiyo, tutaweza kuondoa tatizo hili linalojitokeza mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hili swali kwamba wananchi wanaopita barabarani wananyanyaswa na kuteswa, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, si utaratibu wa Jeshi kufanya vitendo kama hivi. Kama yanatokea haya ni mambo ambayo yanafanywa na mtu mmoja mmoja, tungependa kupata taarifa zake ili Jeshi liweze kuchukua hatua stahili. Utaratibu wa kuhakikisha kwamba, mipaka inafuatwa upo, lakini si kwa vitendo kama hivi. Kwa hiyo, kama haya yanatokea tungependa kupata majina hayo na ushahidi huo ili hatua stahili zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kuhusu ni lini migogoro hii itakomeshwa na elimu itatolewa kwa wananchi. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba, tuliunda Tume Maalum ya Wizara, ikatembelea maeneo yote yenye migogoro. Madhumuni yalikuwa kwanza, ni kuhakikisha mipaka inahuishwa katika maeneo ambayo kulikuwa kuna matatizo ya mipaka ili pande zote mbili zijue mipaka yake, lakini baada ya hapo wananchi walielimishwa ili wasiweze kuingia maeneo ya Jeshi. Kuna maeneo ambayo hata Jeshi liliyasamehe kwa sababu wananchi walikuwa wameshajenga.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunachoweza kusema ni kwamba, elimu hii itaendelea na katika bajeti yangu ya mwaka huu tutaeleza ni hatua gani tumechukua mpaka sasa kuhusu migogoro ya ardhi kati ya Jeshi na wananchi.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, majina ya wageni leo sijayapata. Kwa hiyo, ningependa kutoa ufafanuzi wa kitu kimoja maana hapa nakuta wengine wananiandikia barua sijui walifanyaje.

Tunajadili Ofisi ya Waziri Mkuu kwa siku tano na majina tunafuata ya wale walioomba kuchangia Ofisi hii ya Waziri Mkuu kama *priority* namba moja. Kwa mujibu wa Kanuni hii sifanyi peke yangu, nimeviruhusu Vyama kupanga nani waongee, maana sisi kule ofisini tunapanga *ratio* (uwiano) ambao uko kwenye Kanuni.

Kwa hiyo, uwiano ule nawapelekea viongozi wenu wa Vyama wananisaidia kusema kwamba, leo fulani na fulani watachangia. Ndiyo hivyo, kwa hiyo, naomba msiseme tulianza, tulipeleka, tukafanya nini, aah, utaratibu ni mzuri tu.

Kwa hiyo, ndiyo hivyo, vyama vyenu vinaweza kuwabadilisha. Mimi nafuata orodha, lakini nimevishirikisha Vyama kwa mujibu wa Kanuni. Wananipa majina yale yanayotosha kuchangia siku hiyo, *priorities* zao wanatoa wenyewe. Kwa hiyo, naomba msikonde kwa kunung'unika kila saa, mtakonda kweli! (*Kicheko*)

Haya tundaendelea, Katibu!

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2015/2016 – Ofisi ya Waziri Mkuu na TAMISEMI

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ninachosema ni kwamba, tujitahidi kuwepo Bungeni. Kwa sasa hivi sijui kama nitakaowaita wapo, maana majina nimepewa na Vyama na *I believe* wapo. Wachangiaji wa asubuhi watakuwa Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami, Mheshimiwa Said Nkumba na Mheshimiwa Abulkarim Shah, halafu nitaendelea kuwataja wengine.

MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba, naunga mkono Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Pia niseme kwamba, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini nawapongeza sana Mawaziri walioko katika Ofisi ya Waziri Mkuu; Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Joshua Mwanri. Wamekuwa wepesi sana kusikiliza hoja za Wabunge hasa katika Halmashauri zetu na katika maeneo yetu ambayo tunayawakilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Kassim Majaliwa naye amekuwa mwepesi sana linapokuja suala la elimu. Kwa namna ya pekee nimshukuru sana Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama kwa wepesi wake linapokuja suala la maafa. Ni majuzi tu Jimboni kwangu wananchi karibu 3,000 walikuwa hawana mahali pa kuishi, hawana chakula, nilikwenda ofisini kwa Waziri Mheshimiwa Mhagama, ndani ya saa 48 chakula kikawa kimefika Moshi na wananchi wale wanashukuru sana. Nimshukuru sana Mheshimiwa Mhagama na niseme kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu ana wasaidizi wazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana alisimama ndugu na rafiki yangu hapa akaitukana Serikali ya Chama changu akaiita Serikali ambayo imechoka. Mimi ni Mchumi ukiniambia kitu kimechoka huwa nakwenda kwenye takwimu. Katika takwimu nilizokwenda kuangalia, niligundua kwamba, Serikali hii ambayo inaitwa imechoka ni Serikali ambayo imejenga kilometa za lami 3,884 ndani ya miaka 10 na barabara hizi zimejengwa Tanzania nzima hata katika Majimbo ya hawa watani zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata Mheshimiwa Rais alipokuja kule Kilimanjaro kufungua Barabara ya Hai, Kiongozi wa Upinzani Bungeni alimsifu na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo Serikali hii imefanya. Pia alipokwenda kule kwa kaka yangu Selasini, Mheshimiwa Selasini alimsifu sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kujenga barabara ya Rombo. Naongea takwimu, sipendi kuongea maneno ya kumkashifu mtu, lakini unaposema Serikali haijafanya lolote na imechoka, napata shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wale walioko Moshi kilometa 3,884 ni sawa na kutoka Moshi mpaka Dar es Salaam mara sita, hizo ndiyo zimejengwa na Serikali hii ambayo leo inaitwa imechoka. Nasikitika sana!

Mheshimiwa Spika, Serikali hii pia imejenga madaraja makubwa ambayo hakuna mtu alidhani kwamba, yangeweza yakajengwa ndani ya muda wetu huu ambao tunaishi. Madaraja yamejengwa makubwa kabisa na mengine yako njiani yanajengwa. Kwa mfano, Kigamboni, Malagarasi kule, Kilombero, ni madaraja makubwa ambayo wananchi wa Tanzania wanakumbuka shida waliyokuwa wanapata kwa kutumia mitumbwi kupita katika ile mito, leo hii wanapita juu ya madaraja ambayo Serikali hii imejenga.

Mheshimiwa Spika, ukija kwenye umeme mpango wetu wa maendeleo unasema kwamba, ifikapo mwaka huu wa 2015 asilimia 30 ya Watanzania wangukuwa wamepata umeme. Tumefika mwaka 2015 asilimia 36 na siyo 30 ya Watanzania wanapata umeme. Hiyo ndiyo Serikali ambayo tunaiita imechoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye elimu wakati Rais Kikwete anaingia Ikulu wanafunzi wa Tanzania waliokuwa *form one* mpaka *form four* walikuwa 524,000 leo hii wako 1,700,000. Ameongeza kwa asilimia 225, unasimama hapa unasema kwamba, Serikali imechoka. Walimu wa Sekondari walikuwa elfu ishirini na ushee, leo hii wako 80,000, unasema kwamba, Serikali imechoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vyumba vya madarasa vimeongezeka kutoka 5,700 na ushee mpaka 49,000 unasema Serikali hii imechoka. Maabara zimeongezeka kwa asilimia 2,300 ndani ya miaka kumi. Vyuo Vikuu vilikuwa 23, leo viko 49 unasema Serikali imechoka, lakini hata udahili wa vyuo vikuu walikuwa wanafunzi 40,000, leo wako 204,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Hatuwezi kukaa hapa tukashuhudia Serikali yetu inatukanwa, Rais wetu anaambiwa amechoka, Serikali

yake imechoka, sisi tukakaa kimya. Ni lazima tupaze sauti zetu tuseme kwamba, jambo hilo siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba kuna Serikali ambayo inaweza ikamaliza shida zote na sisemi hapa kwamba Serikali ya CCM imemaliza shida zote, hakuna Serikali duniani ambayo shida zote zimekwisha. Hata Amerika na Uingereza ambako wanatufundisha demokrasia hata kule kwao shida zipo, lakini kinachoangaliwa ni ile dhamira thabiti ya Serikali kuhakikisha kwamba, matatizo ya nchi yanatatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba, Watanzania ambao wameyaona haya yote ambayo Mheshimiwa Kikwete ameyafanya kwa miaka 10 watakirudisha tena Chama cha Mapinduzi pale Magogoni, mwezi wa Kumi mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba Serikali haiwezi kumaliza kila kitu na kazi yetu kama Wabunge kwa kweli ni kuisimamia Serikali na kuishauri iboreshe wapi ambapo labda hapajakaa vizuri. Nataka niseme moja, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameongea vizuri kuhusu utalii, kwa kusema Sekta ya Utalii ndiyo ambayo imeingiza nchi hii mapato ya kigeni kuliko sekta nyingine yoyote. Hata hivyo, nataka niweke wazi hapa kwamba, hakuna kivutio kimoja cha utalii Tanzania kinachoingiza fedha kama Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, Mlima Kilimanjaro wenyewe unaiingiza TANAPA asilimia 38 mpaka 40 ya mapato yake yote, lakini wakati Watanzania wenzetu kila mahali ambapo wanaiingiza nchi fedha wanapata asilimia kidogo kwa ajili ya wale watu ambao wanazunguka lile eneo, Mlima Kilimanjaro zipo Halmashauri sita; nne za Kilimanjaro na mbili za Arusha ambazo ndiyo walezi wa Mlima Kilimanjaro, hatupati chochote.

Mheshimiwa Spika, ukitaka kujenga shule pale Vunjo, Moshi Vijijini au Longido inabidi uende Arusha kuomba kule TANAPA Makao Makuu wakupatie shilingi milioni 10 za kujenga shule. Nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu yeye ndiye msimamizi wa Wizara zote kwamba, suala hili la mapato ya Mlima Kilimanjaro, kwa kweli asilimia kidogo igawanywe kama vile ambavyo kwenye migodi asilimia zinagawanywa kusaidia zile Halmashauri ambazo zinazunguka migodi ile. Hilo kwa kweli litasaidia zaidi wananchi ambao wanachunga milima hii na wanazima moto ili waweze kuwa na moyo zaidi. Wakiwa na moyo zaidi ni kwamba, mapato ya utalii yataongezeka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niongee kidogo kuhusu suala la TAMISEMI ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kwamba, kipindi hiki kuna Mikoa imeundwa, Wilaya na Kata zimeundwa na Vijiji vimetangazwa.

Sasa pale Moshi tuna tatizo, Manispaa ya Moshi wanataka kuongezeka wawe Jiji na wanafikiria kwamba, wachukue ardhi ya Moshi Vijijini. Mheshimiwa Rais alikuja pale Moshi wakamwomba, akawaambia ongeeni na Moshi Vijijini, hamwezi kuniambia mimi kama Rais nisaini tu kwamba, ardhi ya Moshi Vijijini iondoke ije Manispaa.

Mheshimiwa Spika, alikuja Mheshimiwa Magufuli wakati huo akiwa Waziri wa Ardhi naye vile vile akawajibu hivyo hivyo. Sasa hivi wananchi wa Old Moshi wana wasiwasi na mashamba yao yaliyoko Mandaka Mnono, Sango na Saningo, hawajui hatima yake kwa sababu pale mjini wanaambiwa kwamba, mashamba yao yatachukuliwa wakati wowote na wale wananchi watapewa kila heka shilingi 500,000/= halafu Manispaa ikiyapima yale mashamba watauzi vile viwanja kwa shilingi milioni 20.

Mheshimiwa Spika, sasa mwenye ardhi unampa shilingi 500,000/=, halafu unapima tu viwanja unauzia watu wengine kwa shilingi milioni 20! Nadhani jambo hili halijakaa vizuri.

Namuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na hasa Mheshimiwa Hawa Ghasia, ajaribu kwa kweli kuweka wazi hiyo hali ikoje. Je, kuna uwezekano mji ukapanuka kwenda vijijini kwa kulazimisha tu kwamba, wanakwenda vijijini pale kwenda kuchukua ardhi bila ruhusa au makubaliano na wenye ardhi! Naomba hilo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hili suala la uwezeshaji. Nakiri kutambua kazi kubwa ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo inahusika na Uwekezaji, lakini kwenye Uwezeshaji napata tabu sana. Sioni jinsi ambavyo Uwezeshaji pale unasaidia katika Wilaya na Kata zetu na hasa vijana. Kwa mfano; Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza kabisa hapa kwamba, vijana wa Tanzania ni milioni 16.2, lakini fedha ambayo imetengwa kusaidia vijana kwenye SACCOS ni shilingi bilioni tano.

Mheshimiwa Spika, sasa huwezi kusema shilingi bilioni tano ambayo imekopeshwa vijana ambao ni milioni 16.2 inaweza ikakidhi mahitaji ya vijana ya mitaji. Nataka niseme kwamba, upo umuhimu wa Serikali kuangalia eneo hili la uwezeshaji ili kweli watu wa kule vijijini waone kwamba, eneo hili la uwezeshaji linafanya kazi kwa maana ya mitaji na fedha ambazo wanazihitaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nataka niongee kuhusu suala la SACCOS za Walimu. Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake ameonsha jinsi ambavyo Serikali inawatia moyo watu kuwa na SACCOS mbalimbali. Sasa katika nchi hii SACCOS za Walimu zimeanzishwa kwa Walimu kukubali kukatwa fedha kwenye mishahara yao ili ziingie kwenye SACCOS, halafu kutoka kwenye SACCOS waweze kukopa.

Mheshimiwa Spika, sasa kuanzia mwezi wa Saba mwaka jana kumekuwa na matatizo kidogo kuhusu zile fedha kwa sababu badala ya kutoka Hazina kwenda kwenye Mifuko ile ya SACCOS, Serikali imeamua kushikilia zile fedha na kuamua kuzipeleka moja kwa moja kwenye zile SACCOS.

Mheshimiwa Spika, tatizo ni kwamba, baadhi ya Maafisa pale Hazina wanataka tena zile fedha za Walimu ambazo wamekubali wakatwe kwenye mishahara yao na wameshalipia kodi, wanataka tena kukata asilimia mbili ya zile fedha ndiyo ziende katika zile SACCOS za Walimu.

Mheshimiwa Spika, jambo hili limetupa wakati mgumu kidogo na mimi mwenyewe nashukuru nimekwenda pale Hazina nimepata msaada mkubwa wa Naibu Katibu Mkuu, lakini naomba jambo hili liondoke na lisiwe suala la utashi wa mtu. Jambo hili liwe kwamba ni fedha ya Walimu imekatwa inakwenda kwenye SACCOS ya Walimu na kusiwepo na mtu yeyote ambaye anaweza akakata asilimia yoyote kwa sababu watu hawa wameshalipa kodi.

Mheshimiwa Spika, nimeona niyaseme hayo, lakini nataka niseme kwamba, sisi kama Watanzania kwa kweli tuwe mstari wa mbele kuitetea nchi yetu, tusiwe watu wa kulalamika tu kuipinga Serikali kwa kila kitu ambacho kinafanyika. Linapotokea tatizo lolote kwa mfano; mvua imenyeshwa badala ya kusema tufanyaje kama nchi tunaanza kuinyoshea Serikali vidole na kusema imechoka na wakati mvua imenyeshwa.

Wenzetu wa pale Nepal tetemeko limetokea, watu wote wameungana chini ya Waziri Mkuu wanatatua tatizo lile bila kujali itikadi. Sisi hapa kwetu likitokea tatizo hata kama ni la

Mungu, liwe tetemeko au chochote hata mafuriko, vidole vyote ni kwa Serikali, lakini Serikali ikifanya vizuri hakuna ambaye anaisifu Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwaombe sana wenzangu kwamba, wakiendelea hivi hata hiyo Ikulu wakiipata (japokuwa siamini kwamba wataipata), itakuwa shida kweli, kama hawatambui mchango ambao wamefanya wenzao.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba kuiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Said Nkumba, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdulkarim Shah na atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid.

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini naomba vile vile kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wa Nchi katika ofisi yake kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya kuendeleza utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpongeza sana Ndugu yangu aliyemaliza sasa hivi kwa takwimu sahihi ambazo amewapa wenzetu. Hata hivyo, nataka kusema ukiona watu wanaungana kwenye vita maana yake wao ndiyo dhaifu, wameshindwa. Sasa nashangaa unapokiambia Chama cha Mapinduzi na Serikali yake kimechoka wakati wewe ndiyo unatafuta nguvu za kuunganisha kupambana na Chama cha Mapinduzi. Udhaifu ulionao ndiyo unakufanya uunganishe nguvu kupambana na Chama ambacho ni imara. *(Makofi)*

Sasa niwasihi tu, ni hesabu rahisi huwezi kwenda Ikulu kama hujashinda Serikali za Mitaa. Sisi tumeshinda karibu 75%. Kwa hiyo, naomba mwendeele kuendelea kukaa katika hali ya kuvuta taswira za kuendelea kukaa kwenye upinzani miaka kumi, ishirini ijayo. Bado sana, mnaendelea kujifunza, maana yake hata haya mafanikio na hatuwezi kukabidhi nchi, kwa mtu ambaye hajui maendeleo yamefanyika namna gani kutoka uhuru mpaka leo kwa sababu hata ile mipango ya maendeleo ya kipindi kijacho ataipangaje kama hujui haya maendeleo yaliyopatikana kutoka uhuru mpaka sasa, yale maendeleo mengine utayapangaje. Kwa hiyo, bado nyie hamiwezi na mtakapokuwa mtaacha haya maneno mnayoyazungumza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kwanza kuendelea kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kuifanya. Tumefanya kazi nzuri ya kupeleka umeme vijijini, tumefanya kazi nzuri ya miradi ya maji, tumefanya kazi nzuri ambayo tunaendelea nayo ya utengenezaji wa barabara, lakini kwenye mawasiliano tunaelekea sasa vijijini na niwaombe sana pale Sikonge tuendeleze jitihada za kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo mmetuahidi hasa maeneo ya Tarafa ya Kiwele kule Kitunda na Kipili, mtimize. Hata hivyo, kazi nzuri inaonekana kwa kweli kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata fursa ya kutumia fursa hii ya mawasiliano katika maeneo mengi ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, pia naomba kuendelea kusema kwamba, ili tuwakomboe Watanzania, nataka kuzungumza jambo moja tu hapa, jambo la ardhi. Ili tuwakomboe Watanzania ni vizuri tukajielekeza katika kuitumia Hazina hii kubwa ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu katika kuwasaidia Watanzania maskini.

Mheshimiwa Spika, niombe sana Serikali kama tulivyoamua kujenga sekondari, kama tulivyoamua kwenye suala la maabara, tukihakikisha kwamba tunaweza kuhakikisha kwamba,

suala la ardhi ambalo ndilo lina migogoro mingi, ni vizuri Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi ikaamua kwa dhati kabisa kuhakikisha kwamba tunaweze kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, ufumbuzi wangu hapa ninaousema ni kwamba, ni lazima tuhakikishe sasa ardhi ya Watanzania inapimwa yote ili Watanzania wasiendelee kubaki tena na migogoro. Watanzania wakishapimiwa ardhi yao, wafugaji watakuwa na ardhi yao, wakulima watakuwa na ardhi yao, wachimbaji wa madini watakuwa na ardhi yao na hili jambo litawasaidia Watanzania waweze kuondokana na matatizo ya migogoro ya ardhi ambayo wanayo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, niishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika kuhakikisha kwamba Mkoa wa Tabora sasa unaweza kupata maji kutoka Ziwa Victoria siyo kwa Wilaya chache tu, ni kwa Wilaya zote za Mkoa wa Tabora, Wilaya za Sikonge na Urambo zilikuwa zimeachwa lakini nimepata taarifa kwamba Wilaya ya Sikonge na Wilaya ya Urambo na zenyewe zinaingia katika utaratibu wa kuletewa maji kutoka Ziwa Victoria. Niishukuru sana Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niombe nimalizie kwa haya maelezo ambayo yamekuwa ni ya kejeli kubwa kwa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. Kwanza suala la kuiambia Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete anayo nia ya kuendeleza utawala wake baada ya Oktoba, haya ni maelezo ambayo sijui yanatoka wapi, kwa sababu mmemsikia Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kila siku akisema kuwa anayo nia thabiti ya kukabidhi madaraka baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba.

Mheshimiwa Spika, sasa ni hofu tu, hofu ya Wapinzani wanahofia kwamba uchaguzi ufanyike ama hautafanyika hawajajiandaa. Nataka kusema tu kwamba, wajandae uchaguzi utafanyika Oktoba na uchaguzi utakapofanyika tuna uhakika Serikali ya Chama cha Mapinduzi itaendelea kushinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile unapomwambia mwenzako kuwa amechoka, nina mambo mawili hapa nataka kusema, sisi hatujachoka na hatujachoka kwa sababu...

(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakimrushia maneno msemaji pasipo utaratibu)

MHE. SAIDI J. NKUMBA: Eee! Serikali ya CCM na mimi ndiyo Mbunge wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kama hujaelewa. Kwa hiyo, nataka kusema hata ule muungano wa kwao, maana muungano ndiyo unaoleta tafsiri, muungano wa kwao unaitwa UKAWA. Sasa UKAWA ni Umoja wa Katiba ya Wananchi, mnaendaje na Umoja wa Katiba ya Wananchi...

WABUNGE FULANI: Watoto.

MHE. SAIDI J. NKUMBA: Hapana. Ninachotaka kusema ni kwamba, Umoja huu walikuja wakakutania tu hapa Bungeni, yaani hawakuwa na maandalizi huko wamekuja wamekutana tu hapa Bungeni na baada ya kukutana hapa Bungeni, wameunda huu Umoja wa Katiba ya Wananchi. Hawawezi kuwa na Umoja wa Katiba ya Wananchi, umoja huo ndiyo wakautumia kwenda kuwaomba kura kwa Sera ambazo zimeparaganyika. Kwa hiyo, nawaomba sana wananchi waelewe huko, mnapoambiwa Umoja wa Katiba ya Wananchi, hauwezi kuwa ni ajenda katika suala zima la uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, niwaombe vile vile maana wanaweza wakawa wanatuambia sisi mmechoka mmechoka na mambo mengine wanajitukana wao wenyewe, hebu mchukue Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, mchukue Katibu Mkuu wa CHADEMA,

mchukue na Katibu Mkuu wa CUF, wape hawa wakimbie kilometa tano ni nani ataonekana amechoka? (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni mambo wanaweza wakawa wanazunguza wanajitukana wao mwenyewe bila ya kuelewa, wanawatukana viongozi weo. Wape hawa wakimbie kilometa tano nani atakuwa amechoka? Kwa hiyo, nataka kuendelea kusema kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi bado iko imara na Watanzania wanaelewa na ni msingi ambao kwa kweli Watanzania wanajiandaa kuendelea kukichagua Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, nakushukuru sana na naendelea kuunga mkono hoja. Ahsanteni sana. (Makofi)

SPIKA: Kama mngekuwa bado mpo, tungeanzisha ile inaitwa *VIP race*, hapo ndiyo tungepima wachovu wako wapi. (Kicheko)

Sasa nimwite Mheshimiwa Abdallakarim Shah halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid, halafu Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza!

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, lakini kwa jina naitwa Abdulkarim Shah siyo Abdallakarim na kama wameandika hivyo wamekosea. Kwanza kabisa...

SPIKA: Nimekosea mimi.

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia. La kwanza nami kama kiumbe nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa fursa hii na afya njema ya kuweza kusimama hapa na kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Hotuba ya mwisho katika Bunge la Bajeti katika kipindi hiki cha miaka mitano ambayo tunamalizia miaka hii mitano kwa awamu hii.

Mheshimiwa Spika, pili, leo kila mmoja na mambo yake, kwangu leo itakuwa ni kushukuru. Kama nitawaudhi wengine nitaomba tusameheane. Kwa hiyo, kwanza naomba sana niwashukuru leo kupitia fursa hii kuwashukuru wanachama wenzangu wote na wananchi wa Mafia, Wazee, Mashehe, Walimu wa Madrasa, Maimau wa Misikiti, Viongozi wote wa Dini waliokuwa katika Wilaya ya Mafia na nje ya Mafia ambao kwa mara nyingine walikuwa wakiniombnea kila wakati dua katika kufanikisha haya ambayo tulikuwa tunategemea kuyafanya na kuyatimiza katika Wilaya yetu ya Mafia, nimeweza kuyafanya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, yeye na familia yake kwa maana ya Mama Salma kwa kuweza kuhakikisha kwamba mambo mengi yamefanyika Mafia na wao walikuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kwamba, yale tuliyoyasema yametimia. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais na Mwenyezi Mungu atakuongoza katika maisha yako haya ya uraiani baadaye mambo ya heri na wewe utakuwa ni kioo kwa jamii katika nchi yetu na dunia nzima, wewe na kizazi chako kwa maana ya familia yako. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Pia niwashukuru Mawaziri wote, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, bila kuwasahau viongozi wangu wa Chama kuanzia ngazi za Mashina, Matawi, Kata, Wilaya, Mkoa mpaka Taifa kwa maana ya Taifa Mheshimiwa Mwenyekiti na Katibu Mkuu, sekretarieti yote na viongozi wote waliokuwa wananjua kupitia Chama.

Mheshimiwa Spika, nisimsahau upande wa Serikali Mheshimiwa Mkuu wangu wa Wilaya na Wakuu wa Wilaya wote waliokuwepo katika Wilaya ya Mafia katika kipindi changu cha

Uongozi wa miaka hii mitano. Pia namshukuru sana Mkuu wa Mkoa aliyekuwepo, lakini pia namshukuru Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, Mkuu wa Mkoa aliyekuwepo, tulifanya kazi vizuri, lakini pia namshukuru yeye tena kama Kamanda wangu, Skauti Mkuu na kuweza kunipa imani ya kunichagua kuwa Kamishna Mkuu na Mtendaji Mkuu wa Skauti hapa nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana kuwashukuru viongozi wote wa Serikali kwa jinsi walivyoweza kufanikisha miradi na kero kwa kuzipunguza kwa kiwango kikubwa kabisa katika Wilaya yetu. Kwa hiyo, ndugu zangu, familia yangu, rafiki zangu na wote walionisaidia katika kufanikisha yote yale ambayo tumeyatimiza, nashukuru. Mashirika ya aina mbalimbali, lakini naomba kwa pekee niishukuru Taasisi yangu ambayo tuko pamoja katika kuhakikisha miradi mingi tunaifanya pale Mafia kwa kushirikiana na Serikali, Taasisi ya *MIDEF*; Mwenyekiti, Katibu na Wajumbe wote wa *MIDEF* naomba kuwashukuru sana tumeweza kufanya mambo mengi katika kupunguza kero kwa maana ya kuisaidia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nawashukuruni Waheshimiwa Wabunge wote...

MBUNGE FULANI: Unaaga kumbe unaondoka.

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH: Siagi Bwana naendelea we vipi?

Nawashukuruni Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuniamini na kunichagua kwa kushika nafasi mbalimbali ndani ya nchi na nje ya nchi kwa kuwakilisha Kimataifa. Pia nawashukuru sana Waheshimiwa majirani zangu mmenisaidia mambo mengi katika kunipa ushauri mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa shukrani hizo na wote wale ambao sikujaliwa kuwasema humu kwa sababu ni wengi sana, siwezi kuwatamka, naomba wote waliogusa katika kunisaidia, katika kufanikisha lolote lile katika Wilaya ya Mafia, nawaombea *Yarab* Mwenyezi Mungu awape kila la heri hapa duniani na ahera waendapo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana baada ya kushukuru hivyo, tumefanya mengi, sitaki kuingia hawa wanaosema sisi tumechoka, haya ni maneno tu acha waseme, lakini nataka kusema kuwa Mafia mambo mengi tuliyokuwa tumeyahidi mimi na Viongozi wangu kwa maana ya Chama na Serikali tumeyatimiza yote kwa asilimia mia moja. Serikali yangu naishukuru sana, wananchi wangu nawashukuru sana. Kwa hiyo, yapo mambo ya kumaliza, sasa haya ya kumaliza, ndiyo naamini katika kipindi hiki cha mwezi mmoja naamini kabisa tutaweza kuyamalizia.

Kwa mfano, kuna mradi wa maji ya Jibondo Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru sana, Waziri wa Maji, Profesa Maghembe na Katibu Mkuu na wataalam wote na Wakurugenzi wako wa Maji Vijijini na Mijini nawashukuru sana kwa kuweza kufanikisha, kunipatia fedha na kupeleka maji katika Kisiwa cha Jibondo. Hakika mmemwosha uso Mheshimiwa Rais, mmetupamba na kutupa manukato mimi na Mheshimiwa Rais kwa jamii ile ya wananchi wa Mafia. Hakika Mwenyezi Mungu kwa heri hii mnayoifanya Mwenyezi Mungu atawalipeni heri na nyie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakika ndugu zangu wa Jibondo maji yanakuja na keshokutwa tunakwenda kupokea mabomba ya kuweza kuvusha maji kuleta katika kisiwa cha Jibondo.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri Mkuu, sisi watu wa Visiwani linapotokea kero, basi huwa tunaadhibika mara mbili yake ya watu wanaokaa Bara kwa sababu huku njia za gari ni rahisi kufika. Sisi kwetu tuna tatizo la *X-ray* tumejitahidi kutafuta wafadhili sisi *MIDEF* tumesema tutajenga, lakini jana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya alisema kwamba tayari Serikali italeti *X-ray* na *Ultra Sound* katika hospitali zote za Wilaya. Tunaomba

Mafia mtupe kipaumbele, hivi sasa mtu akivunjika mkono, tunamsafirisha kuja Dar es Salaam na inakuwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, yule ambaye hana uwezo anapita baharini na anapata dhiki kubwa sana ya kuweza kufika. Kwa hiyo, tunaomba sana katika ufungaji wa hizi mashine Mafia tupewe kipaumbele, jamani tuko Visiwani, tunateseka na tunaumia sana.

Mheshimiwa Spika, la pili wananchi wa shamba la Utumaini, nakwambieni Mheshimiwa Waziri siku 90 zimepita, sasa hivi Serikali iko katika mchakato wa kuhakikisha shamba hilo linatwaliwa na Serikali na kuwapa wananchi. Wasije watu na kughiribu na kusema yale ni maneno ya kihuni, tutaona nguvu ya huyo Mwekezaji feki na Serikali ipi ina nguvu. Nawahakikishieni wananchi wa Utumaini kuwa shamba lile tatalichukua na wananchi mtaweza kuishi maisha ya raha, mustarehe mahali pale mlipo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, Mheshimiwa Waziri Mkuu tunajua kwamba kuna Wizara nyingi, lakini nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi atuhimizie lile tishari liweze kufungwa mapema pale ili vyombo vyetu viweze kufunga na kutia nanga katika Bandari ya Kilindoni bila ya matatizo yoyote.

Mheshimiwa Spika, tunalihitaji lile tishari lifike haraka lakini pia ahadi waliyosema viongozi wa Mamlaka ya Bandari ukarabati wa Bandari ya Nyamisati, naomba zile pesa sasa zifanye kazi, ikarabatiwe hii bandari ya Nyamisati, wananchi wa Mafia na wananchi wa maeneo ya Visiwa vya Rufiji maeneo ya *Delta*, tuweze kusafiri kwa njia nzuri bila ya kupata dhiki.

Mheshimiwa Spika, lingine naleta ombi, nimejaribu kuomba lakini leo naleta ombi rasmi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu amwombe Mheshimiwa Magufuli, ile meli iliyokuwa ikisafiri inayotaka kufanya safari za Bagamoyo - Dar es Salaam, kwa kipindi hiki watulettee na sisi Mafia tuweze kupata usafiri mzuri, itaweza kusaidia na itaweza kuleta tija kwa wananchi wa Mafia na wa Dar es Salaam wale watakaokuwa wanasafiri kati ya Dar es Salaam na Mafia, ile meli itatusaidia sana na nasema italipa na itaweza kuleta tija na nyinyi wenyewe mtaona hali itakavyokuwa kuwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo naomba sana muweze kuliangalia sana. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu akae na Mawaziri wenzake aweze kuhakikisha kuwa ile meli inakuja Mafia ili tuweze kupata usafiri.

Mheshimiwa Spika, lingine naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu keshokutwa tunakwenda kuzindua barabara ile inayotoka Kilindoni kwenda Utende ya Kilometa 14 na mita 300, nakuomba sana kipande kile kilichobaki cha kilometa 45, hebu itolewe kauli kwamba je, mwaka huu ile barabara tutaweza kuijenga kwa sababu wananchi hivi sasa tunavyoongea mvua ni nyingi sana, barabara ile ya udongo imekatika wananchi wanapata adhabu.

Mheshimiwa Spika, sasa tukianza ujenzi wa hii barabara ya lami kuelekea Kaskazini, tayari Mafia tutakuwa tumekamilisha dhiki zote na *Inshallah* mengine yatakayokuja tutaweza kuyamudu na kuweza kuyafuatilia kidogo kidogo na kuweza kupunguza au kuondoa kero zote.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe na kuwashukuru Watumishi wote wa Bunge na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

SPIKA: Nilisema namwita Mheshimiwa Hamad Rashid, atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta halafu Mheshimiwa Eugene Mwaiposa!

MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii asubuhi ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Pili, niwapongeze Mawaziri, Waziri Mkuu mwenyewe na Mawaziri wake kwa kazi nzuri waliyofanya, lakini tatu niseme kuwa huu ni mwaka wa uchaguzi na mwaka wa uchaguzi una mambo mengi, lakini kubwa la kwanza niombe Tume za Uchaguzi zote zijitahidi kadiri ya uwezo wake kuwa wazi, kushirikisha na kuhakikisha kila raia anapata haki yake ya kupiga kura bila ya usumbufu wowote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nalisema hilo kwa sababu uchaguzi ni sehemu ya kichocheo cha uvunjifu wa amani, kama hamkulisimamia vizuri suala la uchaguzi, amani inaweza kutoweka katika nchi. Kwa hiyo naomba sana Taasisi hizi za Tume, lakini vile vile na Taasisi zingine zijitahidi sana kusimamia uchaguzi ili uwe huru, haki na wazi na kila mmoja apate haki yake kwa vile alivyojitahidi na atakavyochaguliwa na wananchi. Hili ni ombi langu la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, kupitia hotuba ya Waziri Mkuu ina mambo mengi, ningeomba niyaseme mambo matatu ya kwanza. Kwanza ni suala la wewe mwenyewe ulisimamia katika Bunge hili tukaanzisha *Budget Commitee* na bahati nzuri tumeanzisha Sheria na Sheria hiyo sasa tutakuwa na *Budget Committee* na tutakuwa na Sekretarieti ya *Budget Committee* yenyewe.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo tumejifunza katika kipindi hiki ni nidhamu ya kusimamia *budget*. Nidhamu haijawa nzuri hata kidogo na hili lazima kwa kweli Serikali ijipange sana. Nidhamu ya bajeti bado haijawa nzuri hata kidogo. Fedha zilizopitishwa na Bunge hili na ambazo zimekwenda katika Wizara mbalimbali hasa katika Halmashauri huku chini ni cache ama kidogo sana, haziwezi kuzidi asilimia 40.

Mheshimiwa Spika, sasa hii siyo hali nzuri hata kidogo. Vile vile usimamizi wa matumizi yenyewe. Ukienda kuangalia *re-allocations* au matumizi nje ya *budget* yanazidi hata matumizi ambayo yamepitishwa katika bajeti. Hiyo siyo hali nzuri hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba sana nakushukuru kwa kuanzisha hii *Budget Committee*, kupitisha sheria yenyewe, ili sasa Serikali irudi katika utaratibu wa kusimamia *proper budgeting system* ili angalau watu waone matunda ya bajeti yenyewe. Vinginevyo tutakuja hapa ndani tunazungumza, tunaondoka, lakini matumizi na mwendelezo wa bajeti yenyewe hayaonekani. Hili ni jambo langu la pili.

Mheshimiwa Spika, la tatu, karibuni mtapata jambo moja la kujifunza kwamba, kuna matatizo makubwa katika nchi kumbe yanashughulikiwa lakini hayajashughulikiwa kikamilifu. Nayo ni matatizo ya maji safi na salama. Nilivyofuatilia takwimu nikakuta maji safi na salama ni asilimia kama 26 mpaka 30. Maji safi ni asilimia kama 53 mpaka 60 hayazidi. Hii sio hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanahitaji kunywa maji safi na salama. Napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Maghembe, ameliona hili, wakaanzisha na kituo cha kufanya utafiti na kadhalika lakini bado juhudi zinahitajika. Hivi sasa tunapozungumza taarifa za Wizara zenyewe, Mkoa wa Shinyanga, Mara, Rukwa, Arusha, Moshi na sehemu ya Tanga maji wanayokunywa yana *fluoride* isiyopungua *millimeter* kwa lita moja. Hii ni sumu. Waziri mwenyewe ananiambia hii ni sumu. Ikizidi miezi sita mtu anayekunywa maji haya ama mgongo utakuwa umekatika kabisa, acha yale ya kuoza meno, lakini hata mgongo wenyewe utakuwa umekatika kabisa.

Mheshimiwa Spika, kuna visima mia moja na themanini na tisa vimechimbwa vina matatizo haya na kila kisima kina wastani wa lita milioni moja, visima hivi vimefungwa. Hii ni rasilimali ya nchi imekaa kwenye ardhi. Ningeomba Serikali kwa sababu teknolojia sasa

imepatikana za kuweza maji haya kuwa safi na yakatumika kwa wananchi na rasilimali kubwa ya fedha nyingi imewekwa pale, naomba Serikali ifanye mambo ya dharura ili teknolojia hii itumike, ili maji haya sasa yatumike! Haya ni maji asilimia 30 ya wananchi wa Tanzania wangeweza kuyatumia.

Mheshimiwa Spika, yamekaa bure, yamefungiwa hayatumiki kwa sababu ya matatizo. Teknolojia imepatikana ningeomba sana Serikali ilipe umuhimu wa juu kabisa jambo hili lishughulikiwe haraka, wananchi hawa wapate maji safi na salama. hili lilikuwa jambo langu la tatu.

Mheshimiwa Spika, la nne, ni suala la vijana. Ukiangalia takwimu ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu ametupa hapa, ya vijana kama milioni kumi na, lakini vijana ambao wamepata *training* ni vijana ishirini elfu, waliopata mafunzo ya ujasiriamali. Kwa takwimu za *Sub Sahara Africa, Informal Sector* ipo kama asilimia tisini. Kama huja-*deal* nayo hiyo bado tatizo la ajira katika nchi litakuwepo.

Sasa katika hili kuna matatizo matatu makubwa. La kwanza sekta binafsi haijapewa fursa nzuri ya kutosha. Kama sekta binafsi haijakua vijana hawawezi kupata ajira. Ukisoma takwimu zote zilizotolewa hizi, ushiriki wa sekta binafsi bado haujawa wazi hata kidogo. Andika barua kwenye Shirika lolote ama Wizara yoyote, ukipata majibu ni bahati yako na utakuwa umekwenda zaidi ya mara kumi na tano kupata jibu la barua moja. Hamuwezi kukuza sekta binafsi na hamuwezi kutatua tatizo la ajira kama sekta binafsi haijakua inavyopaswa.

Mheshimiwa Spika, katika hili, ni lazima Serikali ikae kitako na sekta binafsi, hata ule mkutano wao unaotakiwa kufanyika kila mwaka ambapo Rais ni Mwenyekiti na wenyewe haufanyiki kwa wakati. Hilo ni tatizo la msingi sana. Kwa hiyo, ningeomba hili suala la sekta binafsi na suala la ajira liende pamoja na liende sambamba na kuvilinda viwanda vyetu.

Mheshimiwa Spika, Viwanda vyetu vinahujumiwa vibaya sana. Kuna viwanda vinazalisha hapa nchini vimefungwa kwa sababu bidhaa zinazolingizwa hafifu kutoka nje ndizo zinapewa fursa zaidi na watu hawalipi kodi inayopaswa, viwanda vinafungwa hatuwezi kukuza ajira hata siku moja. Hayo mambo matatu lazima yaende pamoja;. Kushirikiana na sekta binafsi, kuhakikisha inalinda kabisa viwanda vyetu vya ndani na tatu kuhakikisha vijana hawa wanapata *proper training* ya kuweza kuingia katika ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, la nne kabisa wamelisema wenyewe la fedha. Bado sekta ya fedha pamoja na kukua kwake imekua Mijini zaidi. Hata hivi VICOBA na kadhalika ukitazama *interest rate* yake inayotolewa watu hawawezi kukopa na kuweza kujiendesha wenyewe. Kwa hivyo, kunahitaji kabisa riba idhibitiwe vya kutosha. Upo utaratibu unatumika sasa hivi watu hawatozi riba, chama cha EDC wameanzisha utaratibu wa VICOBA havitozi riba na wanaendelea vizuri tu.

Mheshimiwa Spika, tufanye utaratibu ambao kama Benki za Kiislamu hazitozi riba, kwa nini tusiziige tusitoze riba? Kwa sababu riba ni sehemu moja inayowaumiza wafanyabiashara hasa wafanyabiashara wadogo.

Mheshimiwa Spika, ningeomba kabisa tuiambie *central bank* ifanye *study* ya kutosha ione ni vipi inaweza kuliondoa tatizo la riba ambalo linawakwaza sana hasa wajasiriamali wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulisema ni suala la ndugu zetu hawa wanaohujumiwa sana, ndugu zetu *albino*. Serikali imejitahidi imefanya iliyoyafanya, lakini

bado hali haijawa nzuri. Nafikiri tunahitaji operesheni maalum ya kulishughulikia tatizo la vijana hawa wenzetu, ndugu zetu *albino* ili nao waishi kwa usalama na amani. Bado hali yao haijawa nzuri.

Mheshimiwa Spika, njia moja ya kufanya ni kwamba, ule utaratibu wa kuwa na Mahakama za haraka haraka kusikiliza kesi zao, basi angalau spidi iwe inaendelea vizuri zaidi na kuwe na uendelevu wa jambo lenyewe. Unaona kuna kasi fulani inatokea halafu moto unazimika hivi. Ule moto uwe unaendelea hausimami, nafikiri spidi yao ya kuhujumiwa itakuwa imepungua kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa bahati nzuri nimeamua kutokugombea ubunge. Kwa hiyo, nataka kuwaga rasmi. Toka 1977 kuwemo Bungeni, nafikiri nahitaji kupumzika katika shughuli hii na nitafute kazi nyingine inayofaa. Kazi inayofaa naomba Urais kupitia ADC Zanzibar. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba ndugu zangu wote kwanza waniombe dua, waniunge mkono, naenda kugombea Urais kupitia tiketi ya ADC Zanzibar tukijaliwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Humu ndani Marais wapo wengi. *(Kicheko)*

Waheshimiwa sasa tuendeleo! Nilisema nitamwita Mheshimiwa Conchesta, halafu atafuatia Mheshimiwa Eugene Mwaiposa, halafu Mheshimiwa Agripina na ajiandae Mheshimiwa Pauline Gekul!

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia mawazo yangu kidogo katika hoja hii iliyopo mbele yetu ya hotuba ya Waziri Mkuu pamoja na bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ambayo pia mimi ni Mwanakamati. Napenda pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha siku ya leo tangu kuingia katika Bunge na kutupa afya njema.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichangie kuhusu uwezo wa Halmashauri katika kutekeleza mambo yake. Halmashauri ni vyombo ambavyo vimeundwa ili viweze kusogeza huduma kwa wananchi. Halmashauri hizi zinatekeleza pia sera na mipango ya maendeleo ambayo inatoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, ukitazama mtiririko wa bajeti tangu mwaka 2013/2014, 2014/2015 utaona kwamba Halmashauri hizi kama tutakwenda katika staili hii zinakwenda kufa. Bajeti ya mwaka jana, nitaongelea bajeti ya maendeleo na tumeiongelea vizuri katika kitabu chetu ukurasa wa nane. Tumepitisha bajeti ya maendeleo bilioni mia sita sitini na pointi, lakini mpaka sasa hivi ni bilioni mia sitini tu, ndiyo iliyotolewa takriban asilimia 23.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri haziwezi kujiendesha, Halmashauri haziwezi kutoa huduma kwa wananchi kama Serikali Kuu itaendelea kuziumiza namna hii. Halmashauri hizi zinabeba mizigo mikubwa. Mwaka jana zililazimika kulipia uchaguzi wa Serikali za Mitaa kana kwamba Serikali Kuu ilikuwa haijui kama uchaguzi huu upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Halmashauri zimejikuta zinalazimishwa kuchangia ujenzi wa maabara. Hatujasema maabara zisijengwe, lakini Halmashauri zilikuwa hazikutenga bajeti kwa ajili ya jambo hili. Kwa hiyo, zimejikuta makusanyo yote ambayo yamekusanywa, ambayo

yangeweza kutekelezwa kutokana na mapato yao ya ndani, kutekeleza miradi yao iliyokuwa imepangwa kwenye bajeti, haikutekelezwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zinadai madeni mengi. Nitoe mfano Halmashauri ya Simiyu, inadai ushuru wa pamba. Sisi kama Kamati tumegundua kwamba, hakuna mawasiliano kati ya TAMISEMI na hizi Wizara za kisekta. Maana yake TAMISEMI inaweza ikapanga bajeti, Halmashauri zinapanga bajeti, ghafla anatoka Waziri wa kisekta huku naye anatoa amri yake. Atasema sasa msitoe ushuru wa hoteli, lakini Halmashauri zimeshaweka kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, anakuja naye Waziri mwingine wa Kilimo huku, anasema sasa kuanzia leo makusanyo yote ya cess ya pamba yatarudi kwenye Bodi. Matokeo yake bajeti inaharibika.

Naomba kuanzia sasa Serikali TAMISEMI ambayo ni Wizara ndiyo yenye watu, kwa sababu watu wapo katika Halmashauri! Kule ndiyo kuna watu, kule ndiyo kuna Idara mbalimbali, basi kuwepo na mawasiliano mazuri kati ya TAMISEMI na Wizara za kisekta ili kuondoa mkanganyiko huu wa kuharibu bajeti.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Simiyu peke yake unadai Bodi ya Pamba trilioni tano, milioni mia moja kumi na nane, mia tisa kumi na nane elfu, mia saba kumi na moja na senti sabini na sita na huo ni Mkoa mmoja. Sasa Halmashauri zitawezaje kutimiza mipango yao. Zitawezaje kulipa madeni?

Mheshimiwa Spika, tumegundua kwamba Halmashauri zinadaiwa na Wakandarasi, watoa huduma, ukienda kwenye Mkoa wetu Mkoa wa Kagera shule zilifungwa kwa sababu ya kukosa chakula, kwa sababu Serikali imeshindwa na Halmashauri zimeshindwa kulipia gharama ya wale wanaotoa huduma za vyakula katika mashule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo tukiliangalia kwa makini mtaona hizi Halmashauri, mlizinyang'anya vyanzo vingi vya mapato takribani 20, kwamba Serikali itarudisha ruzuku katika Halmashauri hizi. Kama inarudishwa inapelekwa kiduchu na dakika za mwisho. Ie *quarter* ya nne ndio wanapeleka fedha za maendeleo na fedha hizi tumegundua zinaliwa kwa sababu zinaletwa kama bakaa. Hazitengenezi kitu chochote.

Mheshimiwa Spika, ukifuatilia miradi, kwa mfano Halmashauri ya Njombe, tumekuta Mkoa wa Njombe kuna Halmashauri moja yaani wanabeba bakaa, kutoka mwaka 2013/2014. 2014/2015 na mpaka sasa hivi. Kwa hiyo, unaweza kugundua kwamba fedha nyingi zinapotea kwa mtindo wa bakaa. Tunaomba Serikali ipeleke pesa jinsi inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, tumesema katika kitabu chetu na napenda kuwaambia kwamba haya mawazo si mawazo ya Mwenyekiti, ni mawazo ya Wajumbe. Tume-*scrutinize* tukaona ni kwamba, ni kwa nini Serikali inaendelea kutenga bajeti wakati haina uwezo wa kutimiza bajeti hii. Heri mara mia moja, tutenge pesa zetu ambazo zipo katika uwezo wetu, tuzitumie tukijifunga mkanda kuliko kutegemea watu wa nje ambao pesa hazionekani. Miradi yote ya maendeleo imekwama, yaani huko kwenye Halmashauri ni kwamba Serikali ipo *static* kabisa.

Mheshimiwa Spika, nikimaliza hiyo, naomba niongelee barabara katika Halmashauri. Hii ni mara yangu ya pili naongelea jambo hili. Ni kwamba kila shilingi mia moja iliyo kwenye Mfuko wa barabara Halmashauri inapata shilingi 30 yaani 30 *percent*. Sasa wakati sheria hiyo inapitishwa, Halmashauri ilikuwa na barabara mtandao wa kilometa 56,000, lakini sasa hivi hata

ukisoma kitabu cha Waziri Mkuu, ukurasa wa 77 kimeeleza vizuri jinsi maeneo mapya ya utawala yalivyoongezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa utakuta Halmashauri hata barabara zimeongezeka. Zinakwenda mpaka kilometa laki moja na zaidi sasa hivi. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iangalie hiyo sheria ilivyo. Wakati mwingine tumeona kwamba inakuwa vigumu kuweza kuwapa Halmashauri fedha za barabara kwa sababu Waziri wa Ujenzi ndiyo mwenye sheria hiyo, labda yeye anaona angalie barabara zake, lakini na yeye hata barabara anazozitengeneza. Kwa mfano, napita kwenye ile barabara ya Biharamulo ile imeanza kuharibika na imefunguliwa mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, sasa hata hawa Wakandarasi wanatengeneza pamoja na kusifu barabara mnazozitengeneza si imara, hazina usimamizi! Kwa sababu hakuna usimamizi ndiyo maana tunasema kwamba, mmechoka. Mtu akikwambia umechoka, ni Serikali usikate tamaa, wala usilalamike nenda ukaifanyie Serikali yako *massage* ili kusudi uchovu utoke. Tuirekebishe hii Serikali ili kusudi mambo yaweze kufanyika yawe na usimamizi. Hakuna usimamizi mzuri hata ndani ya Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali izitazame Halmashauri hizi. Sekretarieti za Mikoa zinalalamika na hata tukiendelea kuwabana Mawaziri waliokaa pale wao siyo Hazina. Tutawasema Mawaziri wa TAMISEMI, tutawasema Wakuu wa Mikoa, tutawasema Wakurugenzi! Watafanyaje kazi wakati Serikali Kuu inakataa kutoa pesa hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba zitolewe fedha za NFRA. NFRA karibu Mikoa yote ya Kusini, Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Ruvuma, Mkoa wa Njombe zote zinadai mabilioni ya pesa kwa sababu NFRA hawajawalipa. Kwa hiyo, unakuta Halmashauri zinashindwa kabisa kabisa kuendesha shughuli zake na kweli Serikali ituambie kama inataka kuziua hizi Halmashauri za Mitaa iseme waziwazi.

Mheshimiwa Spika, pia katika bajeti, Serikali isitufanye tukae hapa, yaani ni kama tunafanya usanii. Tunapitisha pesa! Sisi katika TAMISEMI mwaka jana tumepitisha trilioni 4.7 na sasa hivi tunapitisha bajeti trilioni 5.5, lakini zitatoka wapi Hazipo! Kwa hiyo, hakuna sababu ya kufanya maringo tu na kujikweza hapa, kwamba hii Serikali itatekeleza mambo haya wakati bajeti hazitolewi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Eugene Mwaiposa atafuatiwa na Mheshimiwa Agripina Buyogera, wajiandae Mheshimiwa Pauline Gekul na Mheshimiwa Peter Msigwa!

MHE. EUGINE E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kwanza kabisa kushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Pia nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunjalia afya njema. Zaidi sana nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri, lakini na usimamizi mzuri wa kazi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kujikita zaidi kwenye suala la miundombinu. Miundombinu ni muhimu sana katika shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo yoyote. Ndiyo inayotegemewa sana kuharakisha maendeleo katika maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais amejitahidi sana kuunganisha Mikoa na Mikoa, Wilaya na Wilaya na barabara nyingi kwa kweli zimefanikiwa sana katika nyanja hizo. Pamoja na pongezi hizo, nizungumzie kusikitishwa kwangu na jinsi ambavyo Jiji la Dar-es-Salaam limeachwa bila ya kupewa kipaumbele katika suala la barabara.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar-es-Salaam ndiyo kioo cha nchi yetu ya Tanzania, lakini kusema ukweli hali ya barabara katika Jiji la Dar-es-Salaam hata ukienda pale centre kabisa pale Posta barabara ni mbovu.

Namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ajaribu sana na dhakikishe kwamba anatoa mwongozo wa kuhakikisha kwamba Jiji la Dar-es-Salaam linapewa kipaumbele kwa ajili ya barabara za Jiji lile.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kubwa sana kuona kwamba pale Mjini katikati karibu na Ikulu barabara ni mbovu. Tukiachia Manispaa ni kwamba haitaweza kushughulikia barabara zote za Jiji la Dar-es-Salaam. Ni lazima Serikali ihakikishe inakuja na mkakati mzuri wa kuangalia au kutoa kipaumbele cha barabara katika Jiji la Dar-es-Salaam. Nimpongeze pia Rais juzi nilimuona akiwa anatembelea maeneo mbalimbali ambayo yameathirika na mvua na maeneo ni mengi.

Mheshimiwa Spika, katika Jiji la Dar-es-Salaam bado mvua zinanyesha na barabara zimeharibika kwa kiwango kikubwa. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu asaidie jambo hili ili barabara zile ziweze kurudi katika hali yake. Ziko barabara nyingi ambazo ni mbovu, kwa mfano tu katika Jimbo la Ukonga, barabara zimeharibika sana, hata zile ambazo zilikuwa zinatengenezwa au zile ambazo zimetengenezwa siku za hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, barabara yetu ambayo hata Mheshimiwa Rais aliahidi ya Kitunda – Kivule - Msongola imeharibika vibaya mno, lakini pia kuna barabara ya Kitunda - Mwanagati, barabara ya Kampala *University* kuelekea Majohe, barabara ya Pugu – Majohe na hata Gongo la Mboto kuelekea Ulongoni. Hizi ni baadhi tu ya barabara ambazo zimeharibika sana na mawasiliano yanakuwa ni tatizo kubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, pia lipo daraja ambalo liliharibika mwaka jana kwenye zile mvua zilizokuwa zinanyesha mwezi wa Nne ambalo ni daraja linalounganisha Ukonga na Mongo la Ndege la Mto Msimbazi, daraja lile ni muhimu sana kwa vijana ambao wanavusha watu hasa kwa pikipiki lakini na magari yanayotoka Ukonga kuelekea Mongo la Ndege. Naomba sana barabara au daraja hili mhakikishe kwamba linapewa kipaumbele kwa sasa liweze sasa kuboresha mawasiliano katika maeneo haya mawili.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa pia nizungumzie suala la ajira kwa vijana. Suala hili katika nchi hii na katika nchi nyingine pia limekuwa ni tatizo kubwa kwa sababu vijana ni wengi kama hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ilivyosema kwamba ni asilimia 35. Hii ni nguvu kazi ya Taifa, lakini kumekuwepo na tatizo kubwa sana la ajira kwa vijana wetu na niseme tu kwamba Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu ameelezea kwenye hotuba yake, ni kweli kwamba upo lakini vijana wengi hawana ufahamu ni namna gani ambavyo fedha hizi zinaweza kupatikana kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, nataka tu niombe Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati wa kuja kuhitimisha awaeleze Watanzania utaratibu hasa ambao vijana wanatakiwa kuufuata ili waweze kupata fedha hizi. Vijana wengi hawana ufahamu kabisa na taratibu za kupata fedha hizo bado ni kitendawili kwa vijana hao.

Mheshimiwa Spika, niishukuru Serikali kwa kutoa agizo la kutenga ile asilimia tano kwa vijana na asilimia tano kwa wanawake. Kama jambo hili lingekuwa na usimamizi mzuri katika

Manispaa zetu lingeweza likasaidia sana vijana kupata ajira au kupata mikopo kutoka katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha ni kwamba, Halmashauri nyingi hazitengi fedha hizi na zile zinazotenga ni kwamba fedha hazina usimamizi mzuri; nyingine huishia tu mikononi au kwenye mifuko ya Watendaji au wasimamizi wengine wanaosimamia fedha hizo. Kwa hiyo, fedha hizi zinahitaji licha ya kwamba zinatengwa lakini zipate usimamizi mzuri.

Mheshimiwa Spika, katika Manispaa ya Wilaya ya Ilala miaka yote mitano fedha hizi zilikuwa hazijatengwa, nimesikia kwamba zinatengwa mwaka huu milioni mia moja kwa kila Jimbo, lakini miaka minne yote iliyopita, fedha hizi aidha zilikuwa zinatengwa lakini hazieleweki kwamba zilikuwa zinakwenda wapi na vijana wakiwa wanahaha wakiwa hawana ajira, wakiwa hawana fedha kwa ajili ya kufanya maendeleo yao wenyewe. Kwa hiyo, naomba sana uwekwe utaratibu mzuri wa kushughulikia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nizingumzie kuhusu Vyuo Vikuu, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Vyuo vingi Vikuu vimekuwa sasa vinasimama kabisa kwa shughuli zake za maendeleo. Shughuli za maendeleo hazifanyiki karibu Vyuo vyote vikuu vilivyopo nchini kwa sababu fedha za maendeleo hazipeleki kule, hii ni pamoja na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi. Mpaka tulipokuwa tunakaa kikao cha mwisho Chuo hiki kilikuwa hakijapata asilimia kubwa sana ya fedha, lakini hata ukichunguza nimeongea na Waheshimiwa wengine wanaowakilisha Vyuo Vikuu, nao pia Vyuo vyao havijapata fedha. Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu aje na utaratibu na atuambie ni lini fedha hizi zitapeleka katika Vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo nizingumzie tu pia migogoro inayotokea katika baadhi ya Vyuo Vikuu. Nina taarifa kwamba kuna Chuo cha Kampala *International University*, Chuo hiki kipo katika Kata ya Gombo la Mboti pale Ukonga. Chuo hiki kimekuwa na migogoro ya mara kwa mara, lakini migogoro hii imeshindwa kabisa kutatuliwa kwa sababu utawala wa pale hauko imara sana.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna wanafunzi ambao wamechanganyikiwa kabisa, wanafunzi wanaosoma *Pharmacy* na Udaktari, wanafunzi hao wengi wamemaliza pale, lakini wameshindwa kupata ajira kwa sababu Vyeti vyao havitambuliki. Inasemekana kwamba shule hii haijajisajili katika Baraza la Famasia, kwa hiyo wanafunzi pale waliomaliza na wanaoendelea wapo *frustrated* na muda si mrefu pale utaibuka mgogoro ambao kuuzima itakuwa ni kazi kubwa. Namwomba sana Waziri Mkuu ashughulikie jambo hili ili wanafunzi hawa ambao wamekwishamaliza hizi kozi katika chuo kile waweze kujua kwamba hatma yao itakuwa ni nini. Pale kuna shida sana ya uongozi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa kupata nafasi lakini naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Agripina Buyogera, atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa na Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya!

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri Mkuu ambayo ndiyo roho ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako naomba nianze kuwashukuru wafuatao, kwanza nianze na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Wabunge wote kwa heshima

kubwa mliyonipatia mwaka 2011 kwa kuniamini kuwa Kamishna wa Bunge. Naomba pia nimshukuru Waziri Mkuu kwa ushirikiano katika utendaji wangu kwa muda huu ambao nimekuwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana sana Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa uamuzi wake wa busara wa kuweza kutuunganisha Wabunge wote katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hatimaye kuzaliwa UKAWA ambalo ndiyo suluhisho la Watanzania. Bila kumsahau Mheshimiwa James Mbatia Mwenyekiti wa Chama changu cha NCCR-Mageuzi kwa miongozo yake na kwa kweli kunifikisha hapa. Kubwa zaidi niwashukuru sana Waheshimiwa wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini kwa kuniamini na kunipa ushirikiano wa hali ya juu kuliendeleza Jimbo letu la Kasulu Vijijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, naomba sasa nijikite kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naanza na ukurasa wa 13, Shughuli za Bunge. Katika shughuli za Bunge nimshukuru sana Katibu wa Bunge kwa utendaji wake mkuu, lakini naiomba Serikali kwa muda ambao nimekuwa Kamishna kwa niaba ya Wabunge, ishughulikie tatizo la *parking* ya magari ya Wabunge pale kwenye Ofisi Nogo za Bunge, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo kubwa sana tena ni aibu kwa Bunge, Mbunge unaingia ofisini unafika getini huwezi kupita, gari huna pa kupaki, unagombana Mbunge na *taxi driver*, unagombana Mbunge na bodaboda.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa Wabunge wako, ni aibu kwa mhimili mkubwa kama huu wa Bunge. Hainiingii akilini kwamba Serikali imeshindwa kulipatia Bunge kiwanja cha kujenga eneo la ofisi za Watendaji wa Bunge na *parking* ya magari kwa ajili ya Wabunge. Naomba Mheshimiwa Jenista Mhagama wewe ni msaidizi wa Ofisi ya Waziri Mkuu ulichukue suala hili na nakuamini sana ulifanyie kazi, ili tutakaporudi kwenye Bunge lijalo tusikutane na adha za kugombana na bodaboda na *taxi driver*. Naamini Serikali itanipa majibu ya lini watatupa kiwanja.

Mheshimiwa Spika, niendeleo na hotuba ya Waziri Mkuu. Ajira kwa vijana, Ajira kwa vijana imezungumzwa na Wabunge wengi, naomba nizungumze moja tu kwa ajili ya vijana waliopewa ajira na Halmashauri zetu ambao wamehitimu elimu ya Diploma, matokeo yake wameajiriwa na Halmashauri zetu kwenda kuwa Watendaji kwenye Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, leo hii Serikali inakataa kuwaingiza kwenye *payroll*, sasa wanajuliza elimu ya Diploma haikubaliki Tanzania? Kama haikubaliki kwa nini mnaruhusu iendeleo kutolewa kwenye Vyuho vyetu? Hilo naomba ufafanuzi na ikiwezekana wakiwemo na vijana walioajiriwa na Halmashauri yangu ya Wilaya ya Kasulu waingizwe kwenye *payroll* na kama haiwezekani tupewe majibu.

Mheshimiwa Spika, nimesema najikita kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nije ukurasa wa 53 kuhusu barabara, madaraja na vivuko. Naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa azma yake ambayo alikuwa amejitoa kutuahidi Watanzania tuishio Mkoa wa Kigoma kwamba Serikali ya Awamu ya Nne itahakikisha inaufungua Mkoa wa Kigoma kutuunganisha na mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, amejenga daraja la Malagarasi tunamshukuru sana kwa hilo, lakini napata kigugumizi ni nini kinafanyika kwenye Serikali yake kuhujumu mawazo mazuri ya kuufungua Mkoa wa Kigoma kwa kukwamisha ujenzi wa barabara ya lami ya Kidahwe-Nyakanazi. Nataka majibu ni kitu gani kinasababisha mdharau kauli na ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nije ukurasa wa 75 kwa Mheshimiwa Mzee wangu, kaka yangu Profesa Maghembe, kuhusu maji, kilio changu kipo pale pale, nitakuwa mnyimi wa fadhila bila kusema ahsante kwa kunipa miradi mikubwa mitatu Jimboni kwangu, lakini nataka leo mnipe majibu ni kwa nini miradi yote mitatu mikubwa ya maji ambayo ingewasaidia Watanzania wanaoishi Jimbo la Kasulu Vijijini leo yote ime-collapse, imekwama, hakuna mradi wa maji hata mmoja ndani ya miaka mitano ambao umekamilika, kuna nini?

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Kasangenzi, Nyarugusu, Rungwe Mpya na ahadi kila bajeti tunaleta, Kijiji cha Asante Nyerere, maisha yote hawajawahi kuchota maji kwenye bomba, halafu leo tukiongea wengine mnasema Serikali imefanya mambo mengi, imefanya makubwa, imeyafanya wapi, kwangu mbona siyaoni? Wanatakiwa wananchi wa kule na wao wachote maji.

Mnaposema Serikali imetekeleza mambo makubwa na mimi Mbunge wao nikisimama niseme ni sahihi na ndiyo maana nashukuru kwamba mlinipa miradi, ni kwanini haikamiliki au mmetupaka mafuta kwa mgongo wa chupa? Katika hili mnawaweka katika mazingira magumu watakaogombea mwaka huu kupitia CCM, ni afadhali mtangaze tu kwamba Buyogera anapita bila kupingwa! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nije TAMISEMI, niongee neno moja tu kwa sababu masuala mengi sana yapo Ofisi ya Waziri Mkuu. Naomba nikushukuru dada yangu Hawa Ghasia na Manabu Mawaziri wako, lakini niishukuru Wizara; Katibu Mkuu kwa kutekeleza kilio changu cha ujenzi wa barabara ya Makele - Kitanga ambayo barabara ile niliwaambia ndugu zangu ni barabara muhimu sana kwa Mkoa mzima wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, leo tunategemea barabara mmoja, lakini ukiitengeneza hii barabara ya Makele - Kitanga umeufungua kwa namna moja au nyingine Mkoa wa Kigoma, kwamba hata ikitokea tatizo lolote, daraja la Malagarasi pale ukakwama, unaweza ukapitia barabara ya Kitanga kwenda kutokea Kibondo. Ni barabara ambayo unaweza ukapitia Kitanga kwenda Burundi.

Mheshimiwa Spika, Warundi wote waliojaa Kambi ya Wakimbizi pale Nyarugusu wanapita barabara hiyo, kukitokea tatizo lolote la ujambazi hakuna Polisi anaweza kufika kule haraka iwezekanavyo kwa sababu barabara ni mbovu.

Mheshimiwa Spika, sasa mmenipa pesa nawashukuru katika ukurasa wa 18. Katika Wilaya ambazo zimepewa pesa za kutengeneza barabara ni pamoja na Kasulu ikiwemo hiyo barabara, lakini ninachoendelea kuomba kuna nini hapa katikati, mnaponipa miradi halafu hamuikamilishi kuna nini? Nahitaji majibu ni lini miradi hii inakamilishwa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, niingie kwenye migogoro ya ardhi, tumekuwa na migogoro ya ardhi kwa muda mrefu, naomba majibu na tumeunda Kamati humu. Kamati iliyokwenda, imefanya kazi, imetuletea majibu kwamba mipaka ya vijiji na hifadhi ni lazima ipitiwe upya, ambalo ni jambo rahisi sana kuweza kufanya migogoro ipungue kwa Watanzania wetu.

Mheshimiwa Spika, tangu nimeingia Bungeni nalia na Kagera Nkanda, mpaka leo kwenda kusogeza mpaka au kukagua ni nini kifanyike pale, matumizi bora ya ardhi ndiyo suluhisho la hili!

Sasa wajanja wachache hawa viongozi wetu, watendaji wengine wanakuwa na maslahi ya siri kwenye vijiji hivyo. Wanakwenda wanaongea na watu wa maliasili, wanawaambia sasa huu ni mpaka, hili ni eneo la hifadhi, kumbe kuna vitu wamegundua huko wanataka wajifiche kupitia maliasili kumbe wanataka wakachimbe madini.

Mheshimiwa Spika, naomba hili mliangalie vizuri. Mnapewa taarifa, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli nikushukuru sana katika hili kwa niaba ya wananchi wa Kasulu, Kagera Nkanda mwaka 2012 bila wewe tungekufa njaa, lakini uliweza kuagiza wananchi wakavune mahindi na nishukuru sana salamu zangu ufikishe kwa Mheshimiwa Rais mwenye nchi yake, kumpumzisha Danny Makanga, leo tumeletewa DC mwingine angalau ameweza kutangaza...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Kengele imelia

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nadhani nitakuwa nimeelewewa, ahsanteni sana.

SPIKA: Ahsante! sasa nimwite Mheshimiwa Pauline Gekul atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Msigwa!

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa maoni yangu katika bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ipo mbele yetu ili tuweze kuwatendea haki Watanzania ambao tunawawakilisha.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa jinsi ambavyo anatupa afya njema, najua ni kwa neema tu, hakuna mtu ambaye ana haki ya kusema kwamba yeye anastahili, lakini pia kusimama katika Bunge hili Tukufu pia ni kwa neema za Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuweka jambo moja vizuri ambalo limekuwa likisemwa sana na Wabunge wenzetu wa upande wa pili, kwamba uchovu wa Serikali wanaufananisha na afya. Ni dhahiri kwamba unaweza ukawa mchovu wa afya, lakini *upstairs* ukawa uko vizuri, lakini pia unaweza ukawa mlemavu *upstairs* ukawa uko vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza uchovu wa Serikali hatuzungumzii afya za Watendaji wa Serikali, bali tunazungumzia mipango mibovu, tunazungumzia jinsi ambavyo vipaumbele haviendi, tunazungumzia jinsi ambavyo bajeti mnazozitenga hamuishi nazo, hamtekelezi, hamtembei kwenye hizo bajeti, tunazungumzia jinsi ambavyo miradi ya maendeleo inasuasua, tunazungumzia jinsi ambavyo Hazina hawapeleki pesa kwenye taasisi ambazo Bunge tumezi-allocate hizo pesa. Kwa hiyo, wale wanaosema twendeni uwanjani tukapige riadha, nafikiri hawapo kwenye mlengo ambao unaeleweka kuhusu uchovu wa Serikali ambao tunazungumzia.

Mheshimiwa Spika, uchovu huo unadhihirishwa kwenye masuala ya maendeleo kupitia Wizara hii na Wizara ya TAMISEMI. Ukiwaona TAMISEMI hawa ndiyo Watanganyika, hawa ndiyo wanaoishi na Watanzania wote kwenye *grass root level*, huku chini kabisa Watanzania wa hali ya kawaida, ukiwaona wamekaa pale halafu wakawa wamepangiwa bajeti na Serikali, asilimia 28 tu ya miradi ya maendeleo ndiyo mnapeleka kwenye Halmashauri, ndiyo tunazungumzia uchovu huo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa bajeti unaoisha sasa hivi, hadi kufikia Machi, Wizara hii ya TAMISEMI, ya Tanganyika, ya Watanzania wamepelekewa 28% tu ya miradi ya maendeleo. Hivi hii Serikali tukisema mmechoka kwa nini mnaruka? Si mtulie tu! Mpokee vidonge hivi vya ukweli, bajeti yenu na vitabu vyenu hivi hapa vya Mheshimiwa Waziri Mkuu na vya TAMISEMI!

Mheshimiwa Spika, lakini hilo kama halitoshi, Mikoa wamepelekewa 17%! Hii Mikoa ndiyo wana Hospitali zetu za Rufaa! Hawa Mikoa ndiyo wanajenga ofisi mbalimbali za Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, 17% tu ndiyo imeenda! Halafu tukisema Serikali imechoka, watu wanaruka hawataki kukaa kwenye viti, mnataka tuwaambie nini wakati fedha hazipelekiwi?

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu ya TAMISEMI, *ni-declare interest*, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI; Mheshimiwa Spika tukakuandikia wewe Ofisi yako kama Wanakamati, Hazina waje! Waziri wa Fedha aje atujibu kwa nini hapeleki fedha TAMISEMI? Mheshimiwa Spika tunataka tufunge magoli Wabunge wako, ofisi yako mnakimbia na magoli na mpira, hamtaki tukutane na Waziri wa Fedha atueleze kwa nini hapeleki fedha. Halafu tukisema Serikali imechoka mnaona watu tunafanya mzaha katika masuala ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tu tukawekana sawa, hivi kama Wabunge wanataka kukutana na Hazina tuhoji kwa nini TAMISEMI hawatendewi haki halafu Ofisi yako inasema mtakaa kikao cha Kamati ya Uongozi na mpaka leo tunajadili bajeti hii, Kamati ya TAMISEMI hatukujibiwa kwa nini Hazina hawapeleki fedha TAMISEMI! Mheshimiwa Spika unataka kutuambia nini? Maana yake unadhoofisha Bunge lako hili. Ujumbe huu uko sawa kabisa kwamba, Wabunge tunataka kuisimamia Serikali na Ofisi yako pia itupe ushirikiano; kwa nini Hazina hawapeleki fedha kwa wananchi wetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, miradi mingi ya maendeleo inakwama kwa sababu Hazina hawatoi pesa. TAMISEMI wana mipango yao, Hazina hawawapelekei pesa. Mimi naona tunapoteza tu muda wa Watanzania, tunakaa ku-*budget* vitu ambavyo Serikali haitaki kutekeleza kabisa.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye jambo la pili. Kuna suala la Tume ya Taifa ya Uchaguzi, wamezungumzia kuhusu *Voters Apathy*. Tume hii inasema kwamba inategemea kutokuandikisha Watanzania wasiopungua milioni mbili na laki tisa katika zoezi zima hili la uandikishaji wananchi katika Daftari hili la Wapiga Kura.

Mheshimiwa Spika, kama Tume inathubutu kupanga haya, ni vizuri Mheshimiwa Waziri Mkuu pia akatuambia, hivi hii Tume imeshapanga kwamba hawa Watanzania watakuwa wamefariki au wameshapanga Watanzania hao milioni mbili na laki tisa hawatatoa ushirikiano? Ni jambo kubwa! Huu mwaka ni mwaka Mtakatifu sana. Ni mwaka wa Watanzania kukaa chini na kufikiria kwamba tulikotoka ni wapi, tunakwenda wapi na tunakwenda na watu gani watakaotuongoza katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, lakini msibeze umoja wa UKAWA kwa sababu Watanzania wanafahamu ni nini tunachokitaka. Tunahitaji mabadiliko ya kweli lakini mabadiliko haya yatafanyika kupitia uchaguzi wa Oktoba mwaka huu. Mimi ni-*caution* tu, ikitokea mkathubutu, wenzetu mlioko madarakani kuahirisha uchaguzi huu, mimi niwaambie tu Watanzania hawatathubutu kuwavumilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia niipongeze Serikali ya Tanzania kuwapokea wakimbizi hawa ambao wametoka kwenye nchi ya jirani ambao wanapinga mambo haya, hawa wakimbizi watasaidiana na Watanzania kuandamana kuelekea Ikulu kusema kwamba uchaguzi ufanyike. Hatuwezi tukaendelea kuvumilia Tume ya Taifa ya Uchaguzi hawapelekewi pesa, lakini pia, Tume inatoa takwimu ambazo kila mwaka zinatuchanganya! Ukisoma Hotuba ya Mheshimiwa Freeman Mbowe, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ameeleza takwimu za Tume zinavyojichanganya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi nizungumzie Tume, tena naomba Serikali mtupatie majibu, kila wakati tunapoenda kwenye mwaka wa uchaguzi mnacheza na wanafunzi wa vyuo vikuu. Hivi tunavyozungumza wanafunzi wote wanaokaa kwenye vyuo vikuu iwe ni Dar-es-Salaam, iwe ni Dodoma, hawajui hatima zao kama wanaweza wakapiga kura. Ndiyo maana mimi naweza nikaambatanisha na hili la *Voters Apathy* kwamba hata Tume inawezekana inafikiria hawa wanafunzi tunawandikisha vyuoni, wakati wa uchaguzi wanafunzi hawa wanakwenda majumbani, mnawafahamu hawa Watanzania wanatakiwa wapige kura, lakini hamsemi kwamba wakijiandikisha hamtafunga vyuo. Mnawachezea wanafunzi wa vyuo vikuu wanakosa haki zao za kupiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ituambie wanafunzi wa vyuo vikuu watapiga kura? Maana mnawaandikisha vyuoni, wakati wa uchaguzi mnawaondoa, nendeni majumbani tumefunga vyuo, mkicheza awamu hii hawa vijana wamechoka, kwanza hawana mikopo, hawaelewi hatma zao kwenye vyuo vikuu, mnawapa mikopo kwa upendeleo, wenye uwezo ndiyo wanapewa mikopo, wanahitaji kufanya maamuzi kwa ajili ya maisha yao ya elimu, pia wanahitaji kupiga kura waweke Serikali ambayo inawasikiliza. Nahitaji majibu ya kina wanafunzi hawa wa vyuo vikuu wanapigia kura wapi na wanaandikishwa wapi?

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi kwa mwaka huu ambao tunaelekea kwenye uchaguzi watakumbukwa kwa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, wakulima watawakumbuka kwa jinsi ambavyo mnachukua mazao yao halafu hamuwalipi, mnawalipa siku mnyotaka. Cess za mazao hamlipi, *NFRA* hawalipi hela za wakulima lakini pia hata Halmashauri wanazodai hizo cess hawalipwi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi mtakumbukwa kwa mauaji ya Watanzania. Ma-*Albino* wanalia hawajui hatima yao lakini pia hata wale waliouwawa kwenye Operesheni Tokomeza, hata baada ya Ripoti kupelekwa kwa Mheshimiwa Rais hawasemi hawa watu watalipwa kama vile Bunge tulivyoazimia! Watanzania watawakumbuka kwa jinsi ambavyo maisha yao yalitolewa na jinsi Serikali ilivyofanya uzembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, Watanzania watawakumbuka katika mwaka huu wa uchaguzi kwa vijana wengi kutokuwa na ajira, wamekaa na vyeti vyao wako majumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali hii ambayo inamalizia muda wake na UKAWA watachukua nchi hii, watakumbukwa kwa kutokujenga viwanda katika nchi hii na kutoa ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tano, Serikali hii itakumbukwa kwa Serikali kutegemea eti VICOBA! Waziri anasimama hapa anazungumza kuwawezesha wananchi, anazungumzia VICOBA! VICOBA hivi vimeanzishwa na wananchi baada ya kutokupata mikopo kwenye benki kwa ajili ya riba lakini leo Serikali mnajivunia VICOBA, watu wanadunduliza, mtakumbukwa!

Mheshimiwa Spika, sita, lakini katika nchi hii Serikali ya Chama cha Mapinduzi mtakumbukwa kwa kutokumaliza migogoro ya ardhi. Nchi nzima ni migogoro, vijiji havipimwi! Mimi nampongeza Naibu Waziri wa Ardhi, amesema asubuhi Wilaya 66 tu ndiyo vimeweza kubaini hiyo mipaka. Hivi kweli, miaka 50 ya uhuru mpaka leo vijiji havijapimwa, watu wanashindwa kupata hizo hati miliki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali hii mtakumbukwa kwa mengi ambayo mmeshindwa kutekeleza lakini zaidi mtakumbukwa kwa bajeti hewa! Mheshimiwa Waziri Mkuu unasema katika bajeti hii shilingi bilioni 350 ni miradi ya maendeleo, miradi haifanyiki, mnawachangisha wananchi ujenzi wa maabara. Tena mlisema wakati wa msimu wa kilimo hamtawachangisha, sasa hivi ni Sh.60,000, Sh.70,000 hata hazijulikani ni shilingi ngapi. Watanzania watawakumbuka kwa kuwachangisha wakati ninyi mnakusanya kodi zao hamuwapelekei maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, niwaombe Watanzania, wajitafakari. Hatuwezi tukalalamika miaka yote, wafanye maamuzi basi. Kwenye daftari la kujiandikisha wajiandikishe, mwezi wa Oktoba wajitokeze kupiga kura... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante. Namwita Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi lakini kwa maumivu makubwa napata tabu sana tunapokuwa na Wabunge ambao wanashindwa kutofautisha kati ya Serikali na Nchi. Kuna watu tunapoikosoa Serikali wanaona kwamba Serikali hii ya CCM ni Taifa. Naomba Wabunge tuelewe kwamba Serikali ya CCM sio Taifa. Serikali, nirudie tena, huwa zinakuja zinaondoka kama ambavyo Serikali hii itaondoka mwaka huu! Tunazungumzia maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani jana amezungumza vizuri na ametoa Hotuba ambayo inaleta mwelekeo kwa Taifa letu tunapokwenda kwenye Uchaguzi Mkuu. Nizungumze kabisa na mimi narudia, Serikali hii imechoka, tumezungumza miaka mitano na tutaendelea kusema hata kama ni uchungu ambao unawaumiza katika masikio yenu na mioyo yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha sana leo tunapozungumza, deni la Taifa lime-double ukilinganisha na sasa kutokea mwaka 2012. Mwaka 2012 kila Mtanzania alikuwa anadaiwa Sh.480,000/= leo nchi hii deni la Taifa limefika shilingi trilioni karibu 40 na kila Mtanzania anadaiwa Sh.856,000/=. Madeni haya makubwa hayaendani na maendeleo ya nchi hii. Tumezungumza matatizo makubwa tunayoyapata katika nchi hii ni kwa sababu nchi haina dira, nchi haina mwelekeo na Viongozi Wakuu tunasema wamechoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wazabuni katika nchi hii wanalidai Taifa. Wakandarasi katika nchi hii wanalidai Taifa. Mheshimiwa Mwigulu ni rafiki yangu, wewe tena ni Mchumi wa *First Class*, lakini mtu akisoma uchumi wa *Form IV (Economics)*, haiingii akilini kwamba Taifa hili katika kipindi cha mwaka mmoja mnafanya mambo makubwa ambayo hamna uwezo nayo. Kipindi cha mwaka mmoja tumeenda kwenye Katiba na Kura ya Maoni. Kipindi cha mwaka mmoja mmelitangazia Taifa kwamba tutakuwa na Uchaguzi Mkuu, tutakuwa na Vitambulisho vya Uraia. Tumefanya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, tunaenda kwenye Uchaguzi Mkuu, haya mambo yote yanahitaji pesa nyingi, hela mnazo? Tukiwauliza mmechoka, mnashindwa kujieleza hapa. Hata nchi wafadhili hazifanyi mambo makubwa kwa wakati mmoja kama haya. Tukisema nchi imepoteza dira, mnasema sisi wakorofi. Haya ni mambo ambayo tunayasema kulitakia Taifa letu mema, sio Serikali na tunapoikosa Serikali ndiyo uzalendo wenyewe, yaani hapa mimi ni mzalendo kuliko wewe uliyeko kwenye Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania mtambue kwamba Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi ni hatari kwa usalama wa Taifa. Usalama wa Taifa unaingia kwenye mgogoro kwa sababu Serikali hii inashindwa kupanga mambo yake. Unapokuwa una madeni ya nchi, hii ni *multiply effect* katika uchumi wa *Form IV* tu. Unapokuwa huwalipi wakandarasi, kule Iringa kwenye Mkoa wangu wakandarasi wanaidai Serikali zaidi ya shilingi bilioni nane, maana yake huyo mkandarasi anashindwa kulipa nondo, Mama-Ntilie anashindwa kulipa mchele, madhara yanashuka mpaka kule chini, mnasababisha mgogoro wa mawazo na fikra kwa Watanzania na hii ni hatari kwa usalama wa Taifa. Watu wamekosa ajira, hamna miongozo inayofaa, halafu tukiwaambia hapa mnapiga kelele.

Mheshimiwa Spika, lakini cha kushangaza viongozi wakuu wa Nchi hii mnasimama mnasema uwongo. Halafu mkisema uwongo mnakaa kimya, hamuombi radhi kwa wananchi. Mtuambie leo wananchi wanatusikiliza, aidha Usalama wa Taifa ume-*paralyse* katika nchi au viongozi tulionao wana matatizo. Haiwezekani Mheshimiwa Rais asimame *two weeks before* aseme kwamba Kura ya Maoni itakuwepo Aprili, 30. Anakuja Waziri Mkuu na yeye anasimama *two weeks before* kwenye vyombo vya habari, anasema Kura ya Maoni iko palepale. Mtuambie, Usalama wa Taifa ume-*paralyse*, hauleti habari au ni viongozi wadhaifu hawaleti habari? Haiwezekani mambo makubwa kama haya, viongozi wa Nchi, Taasisi ya Rais, Usalama wa Taifa unafanya kazi gani? Mimi siamini kwamba Usalama wa Taifa ume-*paralyse*, naamini kwamba viongozi ninyi wenyewe hamtaki kusikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtaalamu mmoja wa mambo ya uongozi anasema, "*a weak person is more dangerous than a wicked person*" yaani mtu dhaifu ni hatari zaidi kuliko mtu mhalifu kwa sababu mhalifu anapofanya uhalifu anatomia akili lakini ukimuweka mtu dhaifu kwenye *position* za kutoa maamuzi analeta madhara makubwa kwenye Taifa. Haya tunayozungumza ni ya msingi kwa ajili ya Usalama wa Taifa. Haiwezekani Kura ya Maoni haipo halafu mnakuja hapa hamtuombi radhi tuliowapa dhamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania niwaambie, adui namba moja wa Usalama wa Taifa wa nchi hii ili tuwe salama ni Chama cha Mapinduzi. Ili Taifa letu liwe salama ni lazima tukitoe Chama cha Mapinduzi. Hatuwezi kuwa na viongozi ambao wana ndimi mbili! Leo wanasema hivi, kesho wanasema hivi, kuanzia Bunge ka Katiba. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tulitoka humu ndani mkawa peke yenu, hata kupiga kura Mheshimiwa Tundu Lissu kasema hapa, mlshindwa! Mpaka ujanja ujanja, maarifa yalifanyika, 2/3 Zanzibar haikupatikana, mkatangazia umma! Leo Viongozi wa Dini wanagombana na ninyi tukisema hapa mnasema sisi ni wachonganishi. Huu ndiyo uzalendo tunaouzungumza hapa, tunalipenda Taifa hili kuliko Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Ndiyo maana tunasimama tunasema kwa ujasiri, naomba mnisikilize vizuri, najua dozi inaenda vizuri! *(Makofi/Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Inaingia.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, kura hazikupigwa, tukajitoa kwenye Bunge la Katiba, tukasema kura mpige wenyewe, tukajitoa mkakaa peke yenu lakini nayo mmeshindwa, peke yenu mmeshindwa, sisi tukiwa pembeni, sisi tunavuruga nini? Peke yenu sisi tuliondoka tukasema hatuhusiki, mmeshindwa! Tukisema ninyi hamna dira, wadhaifu, wapi tunakosea? Nani mzalendo, mnarukaruka hapa, mme-panic, why? Mje na majibu haya! Unakuwa na Kiongozi wa Nchi, Taasisi kubwa, Usalama wa Taifa unafanya kazi gani, anasema Kura ya Maoni iko palepale halafu haipo! Tukija hapa hamtoi majibu! Tunaomba tupate majibu Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni Serikali ya ajabu kabisa hii!

MBUNGE FULANI: Umesahau?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Sijasahau, tulia!

MBUNGE FULANI: Tulia awape dawa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, mwaka jana Mheshimiwa Mwigulu Mchemba nilikuuliza hapa, wazabuni wangu kule Iringa, wanalisha shule za *Iringa Girls*, Lugalo, Tosamaganga na wengi mmefaidika sana na Iringa yetu, leo kuna madeni makubwa. Uliahidi kwamba mwaka huu yatalipwa, hawajalipwa mpaka leo. Wameathirika, hawawezi kulisha familia zao, wana madeni benki, bajeti inakuja ileile mwaka hadi mwaka. Sasa tukisema hamna vision tufanyeje halafu mnasema sisi ni wachochezi!

Mheshimiwa Spika, ni wakati muafaka ndugu zangu mjue kwamba Taifa ni kubwa kuliko chama chenu! Taifa ni kubwa kuliko Serikali hii! Mnasema hamjachoka, ni muda gani ambao ninyi mmebadilisha Wabunge hapa na kwa bahati mbaya kama wewe ni Mbunge wa Chama cha Mapinduzi hujapata Uwaziri safari hii ndiyo basi tena huwezi kupata maana tumebadilisha kila siku; mmebadilisha mara ngapi? Mmechoka kila siku mnabadilisha mambo ni yaleyale, anakuja huyu ni yaleyale, anakuja huyu ni yaleyale, mmechoka mkubali. Muunganwa huwa anasimama anasema hili nimeshindwa, hili nimeweza. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu Watanzania, hususan kwenye Jimbo langu mpo kwenye kujiandikisha BVR ambapo tunaona kuna ujanjaujanja, taarifa haziendi sawasawa, niombe muendeleo kujiandikisha kwa wingi ili itakapofika mwaka huu mwishoni tarehe 25 tuweze kufanya maamuzi ya kihistoria. Kama ambavyo Mheshimiwa Kigwangalla amesema, akili ileile, mawazo yaleyale hayawezi kutatua matatizo. Nakumbuka mwaka 2012 nilisema *problems can not be solved by the same level of thinking that created them!* Haya mabadiliko, nasikitika tu Mheshimiwa Kigwangalla ameyagundua baada ya miaka mitano. Tumekuwa tukiongea toka tumeingia humu ndani kwamba Wizara hizi ni nyingi sana, ni mzigo kwa Serikali, Serikali inashindwa kubeba. Kweli niseme TAMISEMI wakati mwingine tunawabebesha mzigo mkubwa ni kwa sababu ya mipango mibaya; hawa ndio wana watu lakini hela haziendi! Watu wamekaa tu huko ofisini wanatoa maagizo lakini kule kwenye watu mambo hayaendi lakini mmekuja kugundua haya wakati muda unaisha. Niwaombe Watanzania ni wakati muafaka, tunahitaji mabadiliko muhimu katika nchi hii. Tunatakiwa mabadiliko ya msingi ili Taifa letu liweze kuhama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo uchaguzi wa Serikali za Mitaa na hili nimlaumu sana Mheshimiwa Hawa Ghasia, mnaenda kuwafukuza Wakurugenzi kwa makosa yenu. Kwa mfano, Iringa Mjini bajeti ilikuwa ya shilingi milioni 100, mmeleta shilingi milioni 40, halafu mnawalaumu Watendaji na nchi nzima hivyo, mnakuja mnawakuza hapa wamekosa nini? Kazi ni kwenu ninyi

wenyewe mmeshindwa kujipanga vizuri, mnakuja mnawafukuza Watendaji. Mnagombana na Walimu ambao zamani walikuwa maswahiba wenu, mnagombana na Viongozi wa Dini ambao waliamini Serikali hii, mnagombana mpaka na madereva, tunawaambia mmechoka! Ni wakati muafaka wa kukubali kwamba sasa mnahitaji mpumzike, ili watu wengine waendeleze kijiti hiki na kusema mmechoka sio vibaya, tunachozungumzia siyo *physical, we are talking up-stairs, the brain!* Unaweza ukawa na umbo kubwa, *brain* yako ni ndogo, mmechoka! *You can not think anymore, mmefika bar!* Tunaomba mkubaliane na hilo.

Mheshimiwa Spika, nirudie kusema...

MBUNGE FULANI: Umesahau?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, hatari kubwa ya Usalama wa Taifa wa Nchi hii ni Serikali ya Chama Cha Mapinduzi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, Mungu akubariki sana, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante Mchungaji kwa kunibariki. Mheshimiwa Injini Stella Manyanya. *(Kicheko)*

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika na Rais wetu wa Bunge la SADC, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili pia niweze kuchangia. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kushuhudia bajeti hii ya mwisho ya kipindi chetu cha 2010-2015.

Mheshimiwa Spika, nitoe pongezi kubwa sana kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kazi kubwa iliyofanyika katika kipindi hiki cha miaka 10 ya uongozi wake ikizingatiwa kwamba Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imefafanua sekta kwa sekta nini kimefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haraka mtu unaweza ukaona ni mambo madogo kwa sababu yako kwenye hiki kitabu kidogo lakini mimi ningeshauri Hotuba hii ifupishwe zaidi katika kuweka hizo takwimu na tuitoe kwenye magazeti kwa sababu watu wakiangalia Serikali ikinyamaza wanafikiri haifanyi kazi. Ni vema wananchi wajionee wenyewe, wasisikie tu kutoka katika midomo ambayo imeamua lazima ipotoshe ili iweze kuingia madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazungumza hayo nikiwa na uhalisia hasa katika maeneo yale nayoongoza na nitaomba mniwie radhi, nitachangia nikiwa kama kiongozi wa Serikali kwa upande mmoja lakini upande mwingine kama Mbunge. Mbunge ninapokuwa Mkoa wa Ruvuma, kiongozi wa Serikali kwa sababu hata hapa siulizi maswali, naambiwa ni kiongozi wa Serikali kwa hiyo lazima niitete na Serikali. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano katika Mkoa wa Rukwa, tunayo furaha sana na naipongeza sana kampuni ya Nakuruli, juzi tayari umeme umeshawashwa katika Wilaya ya Kalambo pale Matai na umeshafika mpaka Kasanga, nguzo zimeshafika mpaka Kirandu, zimesharudi mpaka Laela, mpaka vijijini, sasa tunataka maendeleo gani? Ya kusemwa yatasemwa lakini kwa sababu wanashauri tunayapokea lakini wakati huohuo sifa za msingi za Serikali yetu lazima ziwepo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia suala la ulinzi. Nimesikia kuna kubeza uwepo wa magari kwa ajili ya Polisi. Mimi nashukuru na naipongeza sana Serikali, Askari asipokuwa na vitendea kazi unamtuma na yeye aende kugeuka kuwa mwiba kwa wananchi. Kwa hiyo, ni

muhimu sana Jeshi la Polisi, Jeshi la Ulinzi kupewa vitendea kazi vya kutosha isije ikafikia mahali tunataka ku-*paralyze* system ya ulinzi halafu kila mtu akaanzisha vikundi vyake.

Mheshimiwa Spika, juzi ulitupa nafasi ya kwenda DRC, kule kuna vikundi vya kila aina vinaitwa Vimaimai, kuna Vimaimai Vita, Vimaimai Nyerere, kuna kila Kimaimai ili mradi tu kujitengenezea uhalali wa maisha yao ya kuporapora. Sasa huu mchezo unaanza kujitokeza katika nchi yetu, unasikia kikundi hiki wanasema leo tumeamua kugoma tunafunga barabara zote, unasikia wanakaa kikundi hiki leo tumeamua kugoma tunachoma barabara moto, haiwezekani kuendelea kuona nchi hii watu wanajichukulia hatua za kipuuzi mkononi ambazo zinaharibu mali ambazo hazihusiani na madai yao. Kama una madai yako ziko njia sahihi za kuwasilisha madai lakini siyo kuharibu mali ambazo tumezitaifuta miaka nenda rudi, tena kwa misaada ya wahisani pamoja na nguvu zetu sisi wenyewe eti kwa visingizio na wengine kwa kutimiza matakwa ya kisiasa, hapana, hapana, hapana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie kidogo suala la maji ambalo lilijitokeza jana. Kwa kweli mara nyingi mimi nashikiriana vizuri sana na Mheshimiwa Mbunge wangu Mzee Keissy, lakini katika hili naomba nilitolee ufafanuzi kwa sababu mimi nitakuwa nalijua zaidi. Kimsingi ni kwamba fedha hizo shilingi milioni 200 hazijaliwa kama inavyozungumzwa. Kulikuwa na mradi wa maji ambao ulitakiwa uende Kirando lakini utokee kwenye Mto baadaye Mheshimiwa aliposhauri tuchukue kwenye Ziwa ili vijiji vingi waweze kupata maji ndilo lililofanyika na kwa bahati ikawa baadhi ya vifaa vilishanunuliwa tayari. Kwa hiyo, nachoshauri Wizara iongeze kasi ya kuutekeleza mradi huu ili kumwezesha Mheshimiwa Mbunge kuona matokeo ya mradi huu. Bahati nzuri *feasibility studies* zimeshafanyika, kwa hiyo, naamini uendelezaji utakuwepo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maji kwani katika Mkoa aliouangalia wa kwangu ni mmojawapo na hasa pia kupitia maombi ya Mheshimiwa Mbunge Keissy ametusaidia sana na kuna miradi kumi na sita tayari imeshaanza kazi. Kwa hiyo, mimi naomba tuendeleo kufuatilia lakini tumtie moyo huyu mtu ambaye anateseka kwa ajili yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, sasa niongee kwa ajili ya Jimbo ambalo litaitwa Nyasa sasa, maana kule Nyasa sisi hatuna Mbunge sasa hivi Mwenyezi Mungu amrehemu marehemu Komba. Nimefanya ziara kule, nimepitia kwa wananchi, wana tatizo kubwa sana la maji na wananchi wa kule wao wanasema sisi tunachotaka mtupe mabomba tu, kuchimba mifereji, kuunganisha wao wenyewe wana uzoefu maana walishazoea hata kupitisha maji ya mifereji, tunaiita '*mikolulela*', kwa hiyo, wanahitaji mabomba tu. Mheshimiwa Waziri pamoja na kukutetea nipe shilingi milioni 50 tu au nipe mabomba, ukinipa *roll* kama 200 hivi utakuwa umewatendea haki. Tatizo lao kubwa ni kuona shule za msingi na sekondari zinapata maji. Watoto wa kike wanaenda shule wanashindwa kunawa, wanatoroka shule kwa sababu hakuna maji, wananchi wale wamegundua umuhimu wa maji naomba uwasaidie. Naomba sana bajeti izingatie suala la maji. Kwa hiyo, vijiji vyote naomba mkae mkao wa kupata maji naamini kabisa hatutanyimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Maliasili, mara ya mwisho nilienda katika kijiji cha Mitomoni na Mipotopoto wako jirani na hifadhi ya Lipalamba, kwa utaratibu huu ambao unaendelea wa kuangalia mipaka upya, naomba mipaka ipanuliwe kwa kiasi fulani. Hawa watu wako jirani na hifadhi lakini wanakosa mashamba na wanahitaji pia kuwa na *buffer zone*. Kwa hali hiyo, naomba katika maeneo ambayo mtaenda kuangalia, kijiji hiki cha Mitomoni na Mipotopoto naomba sana vipewe uzito na wasaidiwe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, nilitembelea pia vituo vya afya. Katika vituo vya afya baada ya kufuatilia kwa kina, kitu nilichogundua ni akina mama ambao ni viwanda vya kuangalia watu wanaoongea humu kwa nguvu zote na kwa furaha zote, viwanda hivi bado hatujavitendea haki ya kutosha. Zahanati nyingi katika bajeti haziangalii zaidi katika eneo la akina mama. Unakuta vitanda havina hata ile mipira lakini tukiamua sisi kujipanga katika bajeti zetu nina uhakika tunaweza tukatoa mipira kwa ajili ya vitanda vya kinamama lakini hata groves, hakuna sababu meneja mkuu anapoenda kujifungua abebe groves, ni shilingi ngapi? Mimi nadhani hatujafanya maamuzi katika Bunge hili na hapa hakuna kuisingizia Serikali gani wala chama gani, ni sisi wote tulioko humu kwa sababu bajeti haipiti kwa upande mmoja. Tunatakiwa kuona kwamba muda wa mwanamke kubeba groves, muda wa mwanamke kubeba mipira wa kujifungulia uwe mwisho. Wanawake waende hospitali kujifungua tayari vifaa vyote viko pale abakie kubeba maamuzi ya kufanya ile kazi kubwa ambayo wanaume hamuwezi kuifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo haya ambayo nimeyazungumza lakini nizidi tu kusisitiza kwamba lengo la kikao hiki ni kuona bajeti inapagwa vipi na bajeti ikipangwa vizuri wananchi watafaidika zaidi. Hata tukilumbana vipi bila kuweza kujaribu kusaidia ni maeneo yepi yaboreshwe haiwasaidii wananchi.

Mheshimiwa Spika, pengine nisisitize hili suala la uandikishaji, kwa uzoefu ulionekana hasa vijijini ni kwamba wale wataalam wanaoandikisha unakuta uzoefu wao ni mdogo. Kwa hiyo, wanachukua muda mrefu kidogo katika kumuandikisha mtu mmoja, kwa hali hiyo unakuta kuna wananchi wanakuwa hawajaandikishwa. Kwa mfano, kwenye Jimbo letu la Nyasa ambako sasa hivi wanaendelea na zoezi ni kwamba wananchi wengine katika baadhi ya maeneo hawajaandikishwa. Niombe sana Wizara na Tume ya Uchaguzi kuliona hilo kwa sababu wananchi wamehamasika sana kupenda kujiandikisha na kupigia kura viongozi wanaowaamini. Kwa hali hiyo, niombe angalau kuongeza muda hata kama ni wa siku moja moja lakini baada ya kubaini uhalisia wa maeneo yale, wangapi wameandikishwa, wangapi hawajaandikishwa ili kuona kwamba zoezi letu linaenda vizuri. Mimi nimewaambia watulie, wale ambao hawajaandikishwa waorodheshwe ili waweze kufikiriwa na naamini Serikali hii sikivu itafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, suala hili la wanafunzi ni muhimu kuliangalia kwa sababu sasa hivi wako vyuoni na wakati wa kupiga kura watakuwa kwenye maeneo yao. Kwa hali hiyo, mimi naomba tuliangalie *positively* namna gani tunaweza tukawa-*accommodate*. Kama watakuwa wameandikishwa sasa hivi, ni namna gani wanaweza kuhamu na vitambulisho vyao kuweza kwenda kupigia kura katika maeneo yao wakati huo muda ukifika ili mradi watu au kikundi cha watu kisiwatumie vibaya kwa kuamua kuwapeleka sehemu ambayo wanajua wataenda kuleta vurugu au kupiga kura kwa ajili ya mtu wanayesema kwamba huyu lazima tumng'oe kwa sababu huo utamaduni pia wakati mwingine unajitokeza. Ni wajibu wetu kwa pamoja kushirikiana na upande wa Kambi ya Upinzani pale tunapona upungufu kushauri na mimi nasema kwamba bajeti hii ni muhimu sana kwa wananchi kwa sababu ni ya mwisho lakini pia inayotoa dira ya namna gani Serikali itakayoanza awamu inayofuata itakuwa.

Kwa hiyo, iwe ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi, iwe ni Serikali yoyote ile itakayojitokeza Mwenyezi Mungu aepushe lakini iweze kuendelea kufanya shughuli zake bila kuona kwamba Watanzania wanapata matatizo. Kwa hiyo, hapa tusifanye kama vile tunataka kuikomoa Serikali fulani, tufanye kama nchi inataka kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ahsante kwa kunisikiliza. (Makofi)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Lusinde.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mungu sana kwa kunipa fursa ya kusimama katika Bunge lako Tukufu. Namshukuru kwa afya na vipawa vingi ambavyo ametukirimia.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri aliyoitoa, hotuba iliyodadavua mambo mengi sana, yaliyofanyika na ambayo yataendelea kufanyika. Ni ukweli usiofichika kwamba katika miaka mitano hatuna uwezo wa kumaliza matatizo yote na kama ingewezekana kulikuwa hakuna sababu ya kuwepo Bunge maana lingeshamaliza shughuli zote na ukumbi huu ungefungwa tungeendelea na mambo mengine. Kwa hiyo, kwa sababu ni nyingi na ni za siku zote ndiyo maana kila baada ya miaka mitano tunachaguliwa na watu wanachagua Serikali ili iweze kushika nafasi ya kushughulikia matatizo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza, mara nyingi sana huwa nasimama kumpongeza ndugu yangu Msigwa, lakini leo sijui nikulaumu wewe Mheshimiwa Spika ulivyomitaja mimi ukampanikisha Msigwa, akapaniki, akatoka nje ya mada akaanza kuzungumza mpaka povu linamtoka, siku nyingine usifanye hivyo. Mchungaji Msigwa anashangaa deni la Taifa kuongezeka, wakati hapa Wabunge wote tuna madeni, wote tumekopa, sasa unashangaaje deni la Taifa kuongezeka wakati katika maisha yetu hatujawahi kuwa na madeni kama sasa. Kuna Wabunge walikopa shilingi milioni 200, wengine shilingi milioni 150 akiwepo Msigwa, sasa leo mbona hashangai deni lake kuongezeka anashangaa la Taifa, unaweza kuona maajabu ambayo yako kwenye nchi hii. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini nikiliacha hilo, nataka nizungumzie kuhusu uchaguzi, ni jambo la aibu sana kwamba watu katika miaka mitano tumesema hapana, lakini leo tunataka kupata sifa eti kwamba uchaguzi mkuu ukifanyika mwezi wa kumi ionekane kuna mchango wa upinzani katika hilo. Ratiba ya uchaguzi inafahamika kila baada ya miaka mitano unafanyika isipokuwa tusiwaambie Watanzania vitu ambavyo hata sisi wenyewe tunavijua. Hivi leo unaposema ikisogezwa mbele hata nukta moja ya uchaguzi nchi italipuka? Unasema kweli, kwenye kumbukumbu zako unazo, hivi uchaguzi wa mwaka 2010 tulisogezwa mbele baada ya mgombea wa CHADEMA kufariki, nchi ililipuka? Msizungumze vitu ambavyo hamna kumbukumbu navyo nyie. Hawa watu wa namna gani hawa? Wanasema eti tukisogezwa mbele tu nukta moja moto utalipuka nyie Mungu? Mnajua Mungu kapanga nini kwenye Taifa hili? Mbona Rajab Jumbe alipokufa tulisogezwa mbele nchi haikulipuka na nyie wenyewe ndiyo mliopendekeza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo, nataka niseme tusiwashauri wananchi wakabaki wana-*pressure* kwamba ni lazima ufanyike tarehe hiyo, tarehe itapangwa lakini iko tarehe ya Mungu ambayo nayo atakapoisema tutaifuata. Kwa hiyo, nataka nikubaliane nanyi kwamba uchaguzi unafahamika, unafanyika kila baada ya miaka mitano na hiyo msitafute sifa kwamba mmeshinikiza nyie? Uchaguzi mbona unafahamika, kama kuna mambo tuyaelekeze tu Serikali irekebishe hiki, irekebishe hiki ili tuweze kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo moja nataka nilitolee mfano hapa, iko nchi moja ya Kifalme, Mfalme akaita Waziri Mkuu wa ile Serikali na Kiongozi wa Upinzani wa ile Serikali, akawauliza nyie mbona mnapingana sana hamfanyi kazi za wananchi? Mfalme akachoshwa na yale malumbano. Akamwambia yule wa Upinzani hebu omba kitu kimoja cha maana mimi nitakupa kama Mfalme wa nchi hii lakini mwenzako huyu nitampa viwili. Basi yule Bwana aliomba wiki ya kwenda kutafakari, akapewa wiki Kiongozi wa Upinzani katafakari. Ile wiki nzima aliimaliza kuitafakari kwa nini mwenzangu apewe viwili mimi nipewe kimoja. Hajajua hata cha kwenda kuomba ni nini, anajuliza kwa nini mwenzangu apewe viwili mimi nipewe kimoja. Wiki

ikaisha, akaenda kwa Mfalme, Mfalme akamuuliza umeshakipata akasema nimekipata Mfalme, najua wewe ni mtu mzuri utakachonifanyia mimi mwenzangu utamfanyia viwili, naomba ning'oe jicho moja ili mwenzake ang'olewe mawili, angali roho mbaya ya Upinzani yaani eti hana cha kuomba anaomba Mfalme amng'oe jicho moja ili Waziri Mkuu ang'olewe mawili kwa hiyo, yeye awe na nafuu. Jamani, upinzani gani huu tunataka kuujenga? Tujenge upinzani wa hoja, tujenge upinzani unaoeleweka nchi tunaipeleka wapi, tusijenge upinzani kwa kubishania tu, tunabishania vitu ambavyo havina msingi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nisimame kwenye Bunge hili niseme wakati umefika wa kuwaambia Watanzania ukweli na nyie Watanzania mtusikilize sana sumu haionjwi, kuwachagua UPAWA ni sawasawa na kuonja sumu. Miaka yote tunashindana na wagombea wanatoka kwenye vyama vyao, vyama vina sera, leo ukachague mgombea kutoka kwenye chama hakijasajiliwa, hakifahamiki kinaitwa UPAWA, ataongoza kwa sera gani? Kwa hiyo, lazima tukubaliane hapa, miaka yote tunashindana na wagombea wanatoka CHADEMA, NCCR Mageuzi, wanatoka wapi, mwaka huu kutoka UPAWA, chama hiki kimesajiliwa na nani, kina sera gani, kinataka kuleta maendeleo katika hoja ipi? Katika mwaka ambao hawa jamaa wamebugi ni mwaka huu.

MBUNGE FULANI: Wape!

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Nataka niwaambie, ukichanganya mayai yote kwenye kapu moja, ukampata mtu mwenye shabaha akipiga vizuri yamevunjika yote, safari hii tuwapige hawa.

MBUNGE FULANI: Sawaa. *(Makofi)*

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Tuwapige! Hamna kitu, wanakuja wakiwa hawana sera, wana umoja unaofahamika, walikuwa wanapinga Muungano wa Tanzania waliunganisha watu wawili, haya muungano wa UPAWA wameunganisha watu wangapi? Si wawili hivyo hivyo, hawa wanaiga kila kitu, hamna kitu wala msitishike na hawa, hawana hoja ya msingi ya kuja mbele. Walikuwa wanatafuta *kick* tu ya kuingia pamoja lakini siyo kwamba kuna hoja ya msingi wanayoismamia. Kwa hiyo, nataka niwaambie hatuna sababu ya kutetemeka, tunawasubiri kwa hamu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la uchovu, mimi nataka nikubaliane nanyi, mjue mmemjibu Tundu Lissu kwa kumkosea, ndugu zangu hivi Serikali inayofanya kazi ya kujenga barabara kama kilomita mlizotaja, Serikali inayofanya kazi ya kujenga zahanati nchi nzima, Serikali inayofanya kazi ya kukopesha wanafunzi kwa miaka mitano lazima ichoke ndiyo maana inatakiwa kufanyiwa *service* kwa kuchaguliwa nyingine ili ifanye kazi. Hivi gari la Tundu au Mbowe likitembea kilomita 5000 analitupa si anafanya *service* ili lipate nguvu ya kuendelea? Hawa wanatuambia nini hawa? Hapa tumekuja kuwaambia tumechoka, tumefanya kazi kwa miaka mitano, kazi kubwa, tunahitaji kuchaguliwa tena, tupewe tena miaka mingine mitano tufanye kazi kubwa, nyie endeleeni na hiyo ya kwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu anayeongoza nchi kwa sera, anayeongoza nchi kwa kusimamia mafuriko yake, njaa yake, shida yake, katika miaka mitano lazima achoke maana ana kazi, hawa kwa miaka mitano kazi yao ni kusema 'hapana' herufi sita, herufi sita tu. Muda wote wanatumia herufi sita tu kwa kusema 'hapana', sasa wataweza kuchoka hawa, hawawezi kuchoka kwa sababu hawana kazi wanayoifanya, wakisisimama humu wao ni 'hapana'. Hapa tunapitisha bajeti ya kupeleka maji mji wa Iringa wanasema 'hapana', tunajenga barabara kuelekea Hai wanasema hapana lakini sisi ambao tunafanya kazi hiyo kiukweli kweli ndiyo maana wanatuona tumechoka, tumechoka kwa sababu tumepambana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie wakati mwingine mkisema muwe mnasema kwa nidhamu, hata wazee wenu wengine wamechoka lakini ndiyo wanaoendesha chama hicho. Mzee Mtei amechoka lakini ndiyo *sterling* wa kuendesha chama chenu nyie, amefanya kazi kwenye Serikali na sehemu nyingine pia. Hivi kweli kuna mtu amechoka kama Dkt. Slaa mbona mnategemea kwenye Urais...

MBUNGE FULANI: Wanajitukana wenyewe.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mnajitukana wenyewe bila kujua. Ukimweka hapo Dkt. Slaa na wagombea wote wanaotajwa yeye ndiyo yuko taabani lakini bado hamtaki Profesa, mnataka mchovu aingie Ikulu, mnawafanya Watanzania wajinga, Ikulu siyo *ward* ya wagonjwa, Ikulu tunataka watu waende wafanya kazi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukubaliane hapa kwamba kama ni masuala ya uchovu pande zote zina watu wamechoka lakini wako waliotumikia nchi, kama Mzee Mtei namtaja kwa heshima ametumikia nchi hii. Kwa hiyo, huwezi kusimama tu na kusema mmechoka, mmechoka tumechoka kwa sababu tumefanya kazi. Timu iliyocheza dakika 90 ikapata ushindi wachezaji wake watakuwa wamechoka lakini wamepata ushindi kama ambao tutakaoupata sisi. Nyie sifuri, sasa kama sifuri utachoka nini, kila ukisimama unasema 'hapana', wenzako wanasema maji wewe unasema 'hapana' utachoka! Huwezi kuchoka! Ndiyo maana nataka niwasihi Watanzania kwamba CCM hatuhofii, sisi ni majembe, tutapambana na hawa na hakuna lolote watakalotufanya. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Desderius Mipata atafuatia na Mheshimiwa Sabreena Sungura.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii muhimu sana ili nami nitoe mchango wangu katika bajeti hii ya mwisho. Nimshukuru Mungu kwa kutujalia uzima na kutufanya tukamilishe miaka mitano hii tukiwa tunawatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi katika miaka mitano hii katika Jimbo langu wananchi wamenituma yafuatayo:-

La kwanza, Mheshimiwa Rais wetu alitoa ahadi ya kupeleka mawasiliano ya barabara kwenye Kata tatu zilizokuwa hazipitiki na ninavyosimama hapa ni shangwe, ni mambo mazuri tutakapokuwa tunafika katika uchaguzi unaosogea tutakuwa tunashangilia kila mahali kwamba utatuzi wa matatizo ya wananchi umefikia kiwango cha kuridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Wampembe ilikuwa inapita *Landcruiser* peke yake, leo hii ninavyozungumza barabara hiyo mabasi yanafika. Juhudi hii ni ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Ni lazima tushukuru na masikio ya Wabunge wote hapa, nimeisema sana hii barabara kumbe Serikali ilikuwa inasikia na chini ya Waziri Mkuu huyu pesa nyingi za kutosha zimepelekwa zaidi ya shilingi bilioni moja na milioni mia moja zimepelekwa kwa njia ya dharura na siyo kwa bajeti ya Halmashauri kwa sababu Halmashauri haina pesa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wanaosimamia Wizara hii, Katibu Mkuu Ndugu Sajin pamoja na Injiniya Kayanda kwa juhudi kubwa na kusikia kilio chetu. Bado barabara ya Nkanakala, tumeweza kupata pia shilingi milioni mia nane ambazo zimesaidia sana kubomoa ule mlima na sasa hivi kuna shilingi milioni mia nne

alinipa juzi. Jambo hili linawafaraji sana wananchi, wanasema kwa kweli Serikali hii imewatendea haki. Barabara hii nina hakika itapitika na basi zitaenda, wananchi wakae mkao wa kufaidi na kufanya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, iko barabara ya Namanye kwenda Ninde, barabara hii ilifungwa kabisa na wananchi wakasema kabisa wewe kama unataka kurudi Bungeni, kaipigania hii barabara. Nashukuru kuwaambia kwamba barabara hii nayo ilipata pesa chini ya Mfuko wa Dharura na itaanza kupitika hivi karibuni kwa kupata zaidi ya shilingi milioni 350. Kikwazo kilichokuwepo kimeondolewa. Ni lazima tushukuru, asiyesukuru ni kafiri.

Mheshimiwa Spika, lazima pia niseme yapo matatizo yanayotukabiri katika Jimbo langu ambapo ni tatizo la mtandao wa simu katika Kata ya Kala, Wampembe na Ninde, ni changamoto kubwa. Nimeona juhudi kubwa sana ya Mawaziri wetu na watendaji wote lakini dosari ninayoiona ni mfumo kwamba katika jukumu hili tumetegemea zaidi makampuni. Naishauri Serikali ibadilisha utaratibu huo wa kutegemea makampuni katika mambo ambayo yanapeleka huduma kwa wananchi. Tuweke utaratibu wa kuweka bajeti kama tunavyofanya kwenye Wizara nyingine ili tukisimama hapa na kutoa ahadi kama tulivyowaambia wananchi wa Kala, Ninde na Wampembe kwamba mawasiliano yanakuja kwa nyaraka nilizotoa hapa Bungeni na kwa maagizo na barua alizonipa Mheshimiwa Waziri lakini kesho yake unakuta hakuna kitu kilichokwishafanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba mipango ya *Viettel* iliyopo Mheshimiwa Waziri aisimamie vizuri ili ijibu ahadi tulizokwishawaambia wananchi kwani hawatatuelewa. *Viettel* na wenyewe wamekuja wanaenda maeneo ambayo hayana changamoto ya mawasiliano, wanaenda mijini wanaacha Wampembe, Ninde na Kala. Namshukuru Waziri Mkuu, namshukuru Mkuu wetu wa Mkoa, namshukuru vilevile Waziri amekuwa akiwahimiza. Sasa kama hawawezi kuwasikiliza viongozi wanawasikiliza akina nani? Mimi naomba muwaone hawa nao wasije wakatuingiza mkenge.

Mheshimiwa Spika, suala la maji. Katika Jimbo langu kuna tatizo la maji lakini lazima tukae hapa tushukuru. Tumezungumzia sana mradi wa Kawa, Bwawa la Kawa sasa limepata pesa na kazi inafanyika vizuri kwa kasi kubwa. Leo navyozungumza mtandao wa kupeleka maji Fyengerezya, Nkundi na Kalundi umeshajengwa na sasa wanajenga matanki. Changamoto iliyobaki ni kuhusu Wizara yenyewe kutengeneza chujio ili maji yaweze kufikia wananchi. Jambo hili tumelisema sana hapa lakini Serikali ya Chama cha Mapinduzi inasikiliza Wabunge wake. Leo hii nasema kuna mafanikio na wananchi wana matumaini makubwa katika hilo. Sasa nitawezaje kusema Serikali haijafanya kazi, nitakuwa mtu wa ajabu sana.

Mheshimiwa Spika, siyo hapo tu vilevile Chala kulikuwa na kilio cha maji, ameenda Mheshimiwa Maghembe, wakamlilia na wakasema usipoleta maji hapa Mbunge wako harudi. Leo hii maji Chala maji bwerere, Chala A, B,C maji mengi, tunasubiri tu muda wa mkandarasi wa matazamia uishe ili tuweze kuzindua ili tuweze kuzindua na kwa heshima kabisa tunaomba viongozi wakubwa waje kwa sababu ilikuwa ni shida kubwa katika Mji Mdogo wa Chala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tatizo la maji lipo katika vijiji kadhaa, naomba changamoto iliyopo ya kupeleka pesa ndiyo inayoturudisha nyuma. Kijiji cha Kisura kina shida na mradi wake umeshapitishwa, hela hamna. Kijiji cha King'ombe kuna mradi tumetumia zaidi ya shilingi milioni mia tano lakini kwa sasa hatujapata maji bado. Naomba Serikali imalizie shilingi milioni mia mbili iliyobaki ili maji yaweze kupatikana King'ombe. Vilevile katika mradi ule wa kupeleka maji Sale kupitia vijiji vitano vya njiani, vijiji vya Nkata, Ntemba, Ntunchi na Msilihofu uweze kupatiwa pesa ili wananchi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, lakini hatujatoka hivihivi, ni hatua kubwa. Tunazungumzia Chala tutapata maji, King'ombe nina uhakika tutapata maji, Kalundi tutapata maji, Nkundi tutapata maji, Fyengereza tutapata maji na Kisura tutapata maji, hatujatoka bure, ni kazi kubwa. Changamoto haziwezi kuisha siku moja, kazi kubwa imefanyika na tumefanya kazi. Ni lazima tuishukuru Serikali yetu na Chama chetu cha Mapinduzi kwa mipango mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni la muhimu sana ni suala la kilimo. Naomba nitoe ushauri, katika suala la kilimo tuone namna nzuri ya kuwasaidia wakulima. Miaka yote hii tumeenda vizuri sana lakini mwaka huu hasa tumewaacha wakulima kwa namna ambayo haijaridhisha sana. Tumetegemea taasisi binafsi, tumewategemea hawa watu makundi makundi kwamba labda watawasaidia tukaacha mfumo wetu wa kuwapatia wakulima pembejeo. Ule utaratibu ulikuwa mzuri sana, ulikuwa unatusaidia, ulikuwa na changamoto zake, sasa mlipouacha ndiyo tumeona cha moto wakulima. Wakulima hawakunufaika kabisa na mbolea wala mbegu kutoka kwa Serikali yao kwa mwaka huu hasa kwa Mkoa wa Rukwa. Naomba mbuni utaratibu mzuri zaidi kwa sababu kilimo ndicho kinabeba Watanzania walio wengi, ndicho kinachotoa ajira kubwa pamoja na juhudi kubwa inayofanyika katika mikopo mbalimbali ikiwepo matrekta na vitu vingine muone namna nzuri ya kuhudumia wakulima hasa wakulima wa chini wanaohangaika na pembejeo, itatusaidia sana kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho nishukuru, tunamaliza Bunge nikiwa nimefanya kazi vizuri kwenye Jimbo langu kwa kusaidiwa na viongozi mbalimbali akiwemo Mkurugenzi Mtendaji, Mkuu wangu wa Wilaya, Mwenyekiti wetu wa Halmashauri na Madiwani pamoja na watendaji wengine. Hata hivyo, hawa Madiwani posho zao kwa kweli ni hafifu na bajeti zinazokwenda kwenye Halmashauri zimekuwa shida sana. Wamekuwa wakati mwingine hawafikii malengo na tunawalaumu sana kwa sababu pesa hazifiki inavyotakiwa. Naishauri Serikali itafute mfumo mzuri wa kuipelekea Halmashauri pesa.

Mheshimiwa Spika, mfumo uliopo sasa unadhaliisha Halmashauri zetu za Wilaya kwa sababu mwaka hadi mwaka mwingine pesa zinazidi kupungua, bora hata kuacha vyanzo vya vilevile walivyokuwanavyo tulivyovifuta wakavikusanya wao wenyewe ingeweza kuleta heshima zaidi kwenye Halmashauri na wakatengeneza *autonomous* ya madaraka yao ya utendaji kazi na namna wanavyotawala eneo la Halmashauri husika. Ukimpa mtu uwezo wa kutawala halafu unamyima uwezo wa pesa sijaona kama tunawatendea heshima. Kwa hiyo, wakati mwingine tunazilaumu Halmashauri bila haki, tunatakiwa tuwape nguvu za utendaji kwa kuwapa vyanzo zaidi au pesa zaidi kwenye Halmashauri zetu ili Wakurugenzi hawa na Madiwani hawa waweze kufanya kazi zinazoonekana vizuri zaidi kwa watu. Hili mimi nimeliona kama ni dosari sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni posho ya Wenyenviti wa Serikali za Vijiji. Watu hawa wanafanya kazi vizuri sana na kwa kweli wamekuwa ni chachu wanasimamia kila mahali kazi hizi za kujitolea. Tuone namna ya kuwasaidia watu hawa ni muhimu sana katika utangamano wa nchi yetu.

Ndugu wananchi niwaambie, nchi yetu imetulia ni kwa sababu vitu hivi vimetengenezewa utaratibu maalum. Nchi nyingine hakuna utulivu wa namna hii na watu wanakimbia kutoka nchi zile wanakuja kwenye nchi yetu, kwa nini? Msidanganyike kirahisira, mtu anasimama hapa bila hata kufikiri vizuri anasema nchi itaharibika, nchi itawaka moto, vitu hivi mimi nasema siyo vya kuumua watu. Unaweza ukakuta unaumua watu ambao hawafikiri vizuri wakafuata maneno yako ukaleta shida katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Sabreena Sungura atafuatiwa na Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Selemani Zedi, hawa kwanza. Mheshimiwa Sabreena!

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia bajeti hii muhimu ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Idara zake.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kupongeza Hotuba ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ni hotuba nzuri, ni hotuba iliyotukuka na ni hotuba inayoitaka Serikali ijirekebishe kutokana na uzembe na uchovu ambao umefanyika kwa takribani miaka 53. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Wapinzani tunaposimama hapa na kuisema Serikali hatuichukii Serikali, tunataka Serikali itende. Kama kuna Wabunge wanafikiri Serikali inaharibu wanaendelea kuitetea, haiwaipendi Serikali bali wanaiharibia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana, ukiangalia fedha za ndani zilizotolewa na Hazina kwenye miradi ya maendeleo kwa Mkoa kwa Mkoa utasikitika, utasikitika zaidi ya kusikitika. Hawa Wabunge wanaotetea ujinga humu ndani *wallah* kama uko karibu unaweza ukawachapa makofi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kitabu hiki, Mkoa wa Katavi, bajeti ya maendeleo imeenda kwa asilimia kumi mpaka Machi, robo tatu, huo ni Mkoa wa Waziri Mkuu. Mkoa wa Simiyu asilimia 10, Mkoa wa Njombe asilimia 17, Mkoa wa Geita asilimia 10, Mkoa wa Arusha asilimia 15, Mkoa wa Pwani asilimia 14 na Dodoma asilimia 14. Ukija Mkoa wa Mara asilimia 10 ya fedha za ndani zimetolewa kutoka Hazina, Mkoa wa Shinyanga asilimia 13, Singida asilimia 10, Tabora asilimia 15, Kagera asilimia 15, hali hii inatia huzuni. Mkoa wa Kigoma asilimia 21 ya fedha za maendeleo kutoka Hazina ndiyo zimeenda halafu watu wanasimama hapa wanatetea ujinga wanasema Serikali imefanya, imefanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumesimama mara kadhaa tukiishauri Serikali kwamba kuna vyanzo vya mapato vingi ambapo fedha haikusanywi kama inavyotakiwa lakini Serikali haisikii. Sasa hii Serikali ni sikivu, Serikali chakavu au Serikali iliyodumaa! Tumeshauri hapa kuna bandari bubu tele katika ukanda wa Pwani, kuna bandari bubu tele Mkoa wa Tanga, watu wanashusha na kuondosha rasilimali za nchi Serikali ipo imelala, hii Serikali ashuke Mungu aje awaambie? Sisi ni Wabunge tunawaambia ili mjirekebishe mtende, kuna vyanzo vya fedha kule, mchukue hatua za makusudi kuhakikisha kwamba fedha ile inaingia Serikalini na miradi mbalimbali iendelee kutekelezwa katika maeneo mbalimbali lakini tunaonekana kwamba tunaichukia Serikali. Serikali ni lazima iwe sikivu. Sisi tunaomba Serikali ukweli ndiyo tunaitaka Serikali hii iendelee kufanya vizuri na ijirekebishe ili mustakabali wa Watanzania upatikane.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo katika Halmashauri zetu. Naomba ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI. Kuna udhaifu ambao unatokea katika Halmashauri mbalimbali nchini, Waheshimiwa Madiwani, Wenyeviti wa Halmashauri pamoja na watendaji wanafanya biashara. Halafu tunategemea mamlaka ya nidhamu ya watendaji wawe ni Waheshimiwa Madiwani, watu wanapiga *deal* pamoja, wanakula hela pamoja, nani atamfukuza mwenzake? Tunaiomba Serikali mamlaka ya nidhamu ya watendaji irudi TAMISEMI ili mtu akiharibu *point A* afukuzwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulienda Arusha tukakuta kuna Afisa Mipango wa pale ameuzwa viwanja vya shule, *public space* zote ameuzwa kawapa watu binafsi. Mtu yule tunamtafuta katika Manispaa ya Arusha tunaambiwa kapewa *transfer* kaenda Igunga. Tunamfuatilia Igunga tunaambiwa kaondoka kaenda Shinyanga. Tunam-*trace* Shinyanga tunaambiwa mwaka uliopita kama miezi mitatu ameacha kazi, hii nchi inapelekwaje? Mtu anaiba *point B* anahamishwa C anahamishwa D halafu anaacha kazi anaondoka, hakuna hatua za makusudi zinazochukuliwa. Ni muhimu sasa mamlaka haya yahame kutoka kwa Madiwani, TAMISEMI ishike hatamu ishughulikie watu ambao wanafilisi nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kuongelea ni pesa za vijana na wanawake. Kama hii Serikali ingekuwa sikivu na kutenga asilimia tano kwa ajili ya maendeleo ya vijana na asilimia tano kwa wanawake, nchi hii ingekuwa mbali. Hili suala si sualala utashi wa mtu ni suala la kisheria lakini sheria hii inavunjwa, Mikoa na Halmashauri pale inapojsikia kupeleka inapeleka, wengine wanapeleka kiasi kidogo sana na wengine hawapeleki kabisa. Kamati ikifika ndiyo watu ambao wamekataa kulipa ushuru wa madini na watu ambao wamekataa kulipa ushuru wa vitu vingine labda minara ya simu na kadhalika ndiyo wanaenda kuombwa zile hela wazitoe ili makundi haya muhimu ya vijana na wanawake yapelekewe. Hatulitendei haki Taifa hili kama hatutaangalia kada hii muhimu ya vijana na wanawake.

Mheshimiwa Spika, kwenye Kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu tumeona asilimia 35 ya nchi hii ni vijana takribani milioni 16 lakini waliopo kwenye sekta rasmi kwa maana ya walioajiriwa hawazidi milioni moja na kidogo na walioajiri wenyewe siyo zaidi ya milioni mbili. Tuna kundi la vijana takribani milioni 14 wako mtaani hawajui hatima yao ya maendeleo. Kwa hiyo, kama fedha hizi zingetolewa, zingewafaa sana hawa vijana.

Mheshimiwa Spika, vijana walioko vyo vikiu hawapati mikopo. Mimi nina mfano wa kijana mmoja kule kwetu ameenda chuoni kapewa mkopo nusu, mwaka wa kwanza, mwaka wa pili ameshindwa kuendelea na chuo ikabidi aache chuo. Anarudi mtaani akaamua aende chuo cha ualimu, anafika chuo cha ualimu anaambiwa *qualification* za kuingia chuoni hapa unatakiwa upitie jeshini, anarudi nyumbani anasema aende jeshini, anafika jeshini anaambiwa umri wako umezidi. Kijana yule yuko mtaani mpaka dakika hii. Vijana hao siyo mmoja ni zaidi ya vijana hata 1,000, 10,000, 20,000 na mamilioni. Sasa vijana hawa hatma yao nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunataka wakawe majambazi au tunataka waingie kwenye kitu gani? Tunawaingiza watoto wengi sasa hivi kwenye mafunzo kwa mujibu wa sheria lakini vijana wale wakitoka mafunzo ya jeshi wakifika mtaani hakuna cha msingi kinachofanyika. Ajira hakuna, ajira zilizopo zote zinatolewa kwa mjuano. Sasa ni lazima hii asilimia tano za vijana tuitoe ili makundi haya muhimu ya kijamii yaweze kufanya kazi na nchi iweze kupata maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani ameshauri kuna haja ya nchi yetu kuanzisha *Real Estate Regulatory Authority* kwa maana kwamba itashughulikia kodi zote za *real estate* hususani majengo makubwa yanayojengwa nchini kwetu na *apartment* mbalimbali. Ukienda katika Majiji makubwa kuna *apartment* zinazwa dola laki mbili, dola laki nne, dola laki tano, dola laki saba, wanapangisha kwa mwezi dola elfu tatu, dola elfu nne, dola elfu tano mpaka dola elfu kumi, Serikali inapata nini? Sisi tuko TAMISEMI mapato hayo hatuyaoni, Serikali inaambiwa inasema Serikali inafanya kazi, inafanya kazi gani? Yaani ushauri hamuwezi kuuchukua na kuutumia *simply because* unatoka kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani? Hii ni nchi yetu hatuwezi kuiendesha hivi, lazima Serikali isikie na lazima ifanyie kazi mambo mazuri yanayotoka kwa Wapinzani.

Mheshimiwa Spika, tulishauri kuhusu ununuzi wa samani. Kila mwaka Serikali imekuwa ikivunua vyombo mbalimbali vya matumizi ya ofisi kutoka nchi mbalimbali labda China, Uturuki na sehemu nyingine. Tukashauri tuna vyombo vya Magereza, tuna Jeshi wanaanda samani mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya ofisini. Kwa nini sasa Serikali isije na mkakati wa kununua vitu vile nchini badala ya kuagiza nje? Mheshimiwa Waziri aje atuambie ni kwa kiwango sasa suala hili la ununuzi wa samani, ni kwa kiasi gani imenunua hapa ndani ya nchi na kwa kiasi gani wameweza kuagiza kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda upande mwingine nisikitike sana kuhusiana na suala zima la fidia. Fidia imekuwa ni tatizo sugu. Katika Mkoa wa Kigoma hususani Manispaa ya Kigoma Ujiji, leo hii tunaongea hapa watu wa Kibirizi wamelipwa na TPA pesa pungufu kesi iko Mahakamani. Ukienda kwa upande wa watu wa Kahabwa na wenyewe wanalalamika, mtu ana nyumba ana mtoto, ana mke, ana kaburi na kadhalika, analipwa shilingi milioni mbili mpaka milioni tatu, kiwango kile ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia *trend* ya bajeti hii kwa utekelezaji wa asilimia hizi 10, 15, 12, hakuna fedha za kuwalipa wananchi. Sasa kwa nini msiwe na utaratibu wa kutowahamisha wananchi kwanza kabla hamjapata fedha? Kama Serikali inaona haina fedha, basi baadhi ya mambo muweze kuongea na wananchi vizuri, kwa sababu itaonekana wananchi wanazuia miradi lakini tu ni kwa sababu Serikali iliyoko madarakani imeshindwa kusimamia ukusanyaji wa fedha, imeshindwa kusimamia mapato ili wananchi walipwe fidia stahiki. Mji mzima wa Kigoma mpaka sasa hivi wanalalamika juu ya fidia mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alikuja Mheshimiwa Rais mwaka 2006 akasimamisha ujenzi katika mlima wa Mlote, wananchi wasijenge pale, lakini mpaka dakika hii miaka tisa, hakuna fidia wala fununu ya fidia. Mkoa ume-*declare* hauna uwezo wa kuwalipa wananchi wale, Manispaa imesema haina uwezo wa kuwalipa wananchi wale, TAMISEMI iko kimya, Wizara ya Maliasili na Utalii iko kimya, ya Mazingira iko kimya, wananchi wale mwaka wa tisa, Serikali iko kimya, tuiseme Serikali imedumaa, tuiseme Serikali chakavu! Toeni majibu kwenye mambo ya msingi, wananchi wanavumulia wanataka wasikie majibu. Sisi ni Wabunge, ni wawakilishi, kero za kule tunazileta hapa, kwa nini Serikali hamji na majibu! Huo siyo uchonganishi wa kuwachongea Wabunge? Serikali toeni majibu kwenye mambo ambayo ni ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kuliongelea, ni suala la ukusanyaji wa fedha. Ukiangalia katika sheria mbalimbali ambazo zinafanya ukusanyaji wa fedha uwe rahisi, hususan Sheria Ndogo, tumegundua katika Kamati yetu ya TAMISEMI, maeneo fedha hazikusanywi kutokana na ukosefu wa Sheria Ndogo. Hata hivyo, tukashauri Wizara waandae *uniform By Laws*, ambazo zitasaidia Halmashauri zote nchini ziweze kupata mapato na kuweza kujiendesha lakini mpaka dakika hii, tumeshauri karibia mwaka wa tatu, bado Wizara iko kimya, hatuoni suala lolote linaloendelea mbele.

Mheshimiwa Spika, lakini, la mwisho na la umuhimu wa kipekee, ni suala ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Pole, pole. Nimesema nitamuita Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Selemani Zedi, Mheshimiwa Meshack Opolukwa, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa. Hawa wote wataitwa. Mheshimiwa Mkimwa!

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni wajibu wangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na nguvu nami nikaweza kusimama katika Bunge lako hili na kuweza kuchangia hoja ya bajeti ya Waziri Mkuu iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nami pia ni Mjumbe wa Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, matatizo yaliyoko TAMISEMI tunayafahamu kwa undani. Pamoja na kuyafahamu matatizo haya, sisi kama wanakamati tulikuja na mapendekezo miaka miwili na nusu iliyopita kwamba tunaomba Halmashauri wafanye makusanyo na watakapoweza kukusanya watoe asilimia tano kwa wanawake, asilimia tano kwa vijana na wakimaliza watoe asilimia 60 ili kupeleka kwenye miradi ya maendeleo ambayo inaweza kuwasaidia katika Halmashauri zao. Hii yote tulifanya hivyo kwa sababu tuliona Hazina hawapeleki fedha inayostahiki katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, Hazina hawana mtiririko kabisa wa kupeleka hizi fedha na hatujajua kipaumbele cha Serikali ni nini. Kwa sababu tunapoisema TAMISEMI, tunasema ndiyo Tanganyika iliyopo kwa sababu mambo yote unayapata TAMISEMI. Ukitaka kilimo, dawati la kilimo TAMISEMI lipo, hasa huko kwenye Halmashauri zetu, ukitaka afya, zipo kwenye Halmashauri zetu lakini tunashangaa kabisa pale ambapo Hazina haipeleki fedha TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa mwaka wa fedha uliopita, fedha ya maendeleo ya ndani iliyokwenda ni asilimia 28 tu. Tunajiuliza, hivi kweli kuna maendeleo? Ndipo tunapona, wananchi wanajitolea nguvu zao, wanachanga kama Serikali ilivyoagiza wajenge maboma Serikali itaezeka lakini baada ya wananchi kujenga maboma mpaka leo kuna baadhi ya maboma yameoza kwa sababu maboma yale ya shule hayajaezeka, maboma ya zahanati hayajaezeka, Halmashauri wanasubiri fedha za maendeleo kutoka Hazina, fedha hizi haziendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama hiyo haitoshi, katika ushauri tuliowashauri Halmashauri waweze kutenga fedha za ndani asilimia 60 ili waweze kufanya shughuli zao za maendeleo, pia imekuwa kizungumkuti. Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula nikichukulia *sample* tu ya Mkoa mmoja wa Rukwa, wanadaiwa na Mkoa Sh.2,588,389,000 na fedha zingine kidogo. Tunajiuliza, ile asilimia 60 ya Halmashauri kujendesha, Serikali haitaki kulipa, japokuwa Waziri Mkuu kasema, wameongeza hifadhi ya maghala, tatizo siyo maghala, tatizo ni wananchi walipwe fedha zao, hilo ndiyo tatizo, ili waweze kujikwamua kiuchumi, waweze kujikwamua kimaendeleo na waweze kuendesha Halmashauri zao kama jinsi ambavyo Kamati imeagiza. Kwa hiyo, tunachoomba, kupanua maghala tu peke yake haitoshi, sasa tunataka muwalipe fedha zao, hii ni *sample* ya Mkoa mmoja tu wa Rukwa lakini kuna Njombe na Mikoa yote inayolima mahindi kwa wastani wanaidai Serikali, ukizijumlisha unapata fedha za kutosha. Kwa hiyo, Serikali tunataka mijifunge kwa sababu mmesema hamjachoka, mlipe fedha za watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunasema tunapeleka madaraka Mikoani Hazina inawapelekea asilimia 17, sijui ni madaraka gani hayo tunayoyapeleka Mikoani. Kama walivyoongea wengine, hakuna madaraka tuliyopeleka Mikoani, ni kwamba tunawaongezea Wakuu wa Mikoa matatizo yasiyoweza kutatulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mtandao wa barabara nchini, tunaomba sheria hii Mheshimiwa Waziri Mkuu ibadilike, huwezi ukamwambia paka amgawie panya chakula, akamgawia chakula kinacholingana, haiwezekani! Sasa tunataka Mheshimiwa Waziri Mkuu sheria hii ibadilike na Wizara ya Ujenzi wapate asilimia 60, TAMISEMI wapate asilimia 40 ili waweze kuendana na matatizo mnayoongeza, utawala wa Halmashauri na utawala wa vijiji kukarabati barabara hizi. Kwa sababu sheria hii ilipita, TAMISEMI walikuwa wanahudumia kilomita 58,000 sasa wanahudumia kilomita 108,000. Sheria ile inayosema kwamba

tunaunganisha barabara Mikoa kwa Mikoa, haisaidii kama ndani hatuwezi tukafanya kazi ya msingi, kama watu watalima mazao yakatae kutoka kijijini. Wale wanaosema CCM imefanya, tunawaambia bado haijafanya vya kutosha kwa sababu waliposimama kuomba kura kura kuingoza nchi hii hawakusema watafanya wachoke, tunaomba wasichoke, wafanye na kubwa zaidi wawe na nidhamu ya bajeti. Siyo bajeti imepangwa kwa suala lingine unakwenda kufanya suala lingine kwa kutumia bajeti ile. Watu wamepanga mambo yao ya msingi Halmashauri, unawaambia wajenge maabara, maabara ni sawa, lakini tungeweza tukachukua utaratibu wa *Road Fund*, angalau zile fedha zikaweza kujenga maabara taratibu na kwamba mambo mengine yasingesimama kwenye Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda nigusie kidogo Mfuko wa Wanawake na Vijana, wengi wameugusia lakini mimi kama mwanamke ni vyema nikaugusia. Tunafahamu wazi kabisa, asilimia 30 ya wanawake wanaoongoza kaya ni wanawake wasiokuwa na wanaume na wanaongoza familia kubwa. Kama Mfuko huu ukitoka kiuhalali, wanawake wakapata fedha za mikopo zisizokuwa na riba, ni ukweli usiopingika, hatutakuwa na kaya masikini, lakini Mfuko huu umefanywa shamba la bibi. Halmashauri zingine wanapeleka kwenye Mwenge, Halmashauri zingine wanapeleka kwenye uchaguzi yaani Halmashauri wanaona huu Mfuko kama upo tu umeelea hauna mwenyewe na pale ndiyo kila mtu anaamua ajichotee na afanye kazi anayotaka. Kama vijana mmesema vijana ni bomu linalokuja lakini anayetengeneza bomu hili ni mwakamke, kwa sababu wanawake tunajifungua kila mwaka na tunaojifungua ni vijana hawa. Kwa maana hiyo, kama hatutaweza kuwalea vijana hawa kwa uadilifu, ndiyo watazidi kuwa bomu kubwa kuliko inavyotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kidogo nigusie suala ambalo Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa leo ameliongea hapa ndani. Amesema wananchi wanaingilia mipaka ya Jeshi, sasa mimi nakwambia Wanajeshi mnaingilia mipaka ya wananchi. Hili nalisema siyo kwa kulibuni, ninalifahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, afahamu kwamba mitaa ya Nyanguku na Lukobe, mmeweka *beacons* zenu na mmeweka *ma-go down* ya silaha. Msije mkatusababishia katika mitaa hii ya Nyanguku na Lukobe ikaja ikawa kama Gongo la Mboto, kwa sababu wananchi wamechanganyikana na silaha zenu, tena silaha za kivita. Kwa maana hiyo tunasema, mmekubali kabisa kwamba zile *beacons* mmeziweka na zimewakuta wananchi, mji ule unakua, watu wanaendelea kuzaana na sisi Watanzania tuna heshima, baba, mama na mtoto kuanzia miaka mitano hawawezi kulala chumba kimoja. Mvua inanyesha, nyumba zinabomoka, mwananchi akijaribu hata kupanda muhogo anakuja kufyekewa muhogo wake.

Mheshimiwa Spika, nakuomba kupitia kwako, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tarehe 6 nilifika ofisini kwake na wakaahidi baada ya wiki mbili watakuja kuangalia na kufanya tathmini na kuangalia zile *beacons* zenu mlizoweka, ilikuwa iwe tarehe 14 Machi lakini mpaka leo, sasa hamjachoka kweli? Mchokeje kama hapo hamjachoka? Kama kuja kuangalia ilikuwa ni wiki mbili tarehe 14 lakini mpaka leo hamjaja kuangalia, hamjui wale wananchi wanaishije, watoto wanachukuliwa fisi, hivi kama mtoto wako angechukuliwa fisi wewe ungekubali? Kwa hiyo, tunawaomba, ninyi mnaoishi Masaki na hawa wanaoishi kwenye maeneo mnayoyachukua mnayaona ni mali, mje muwathamanishie waondoke, wananchi ni waungwana na wanahitaji kuondoka, wala hawahitaji kuendelea kukaa karibu na silaha za moto kama zile.

Mheshimiwa Spika, pia ningeomba kitu kimoja, tunapokaa vikao vya *road board*, nafikiri vyama vyote vya siasa hasa vyenye Madiwani vinakuwepo ndani ya vikao vile. Nafikiri katika Mkoa wa Mwanza tunapokaa tunakuwa na Mwenyekiti, Mheshimiwa Diallo - Mwenyekiti wa

Chama cha Mapinduzi na haya maamuzi tunayoyafanya na yeye anayaunga mkono. Tumekaa vikao visivyopungua vitatu, Halmashauri imeamua kusogeza huduma karibu na wananchi, nafikiri mnapoanzisha Serikali mpya, Halmashauri mpya, mnasogeza huduma karibu ya wananchi na Mkoa ndiyo unajua, barabara gani ikifunguliwa Mkoa utapata unafuu. Kwa Mkoa wa Mwanza imekuwa ndivyo siyo, tunapoomba barabara ya Sabasaba – Kiseke - Busweru ifunguliwe, ina maana hiyo ni njia ya mkato kwenda Halmashauri. Mtu haheitaji kwenda Wilaya jirani halafu ndiyo arudi Halmashauri, ina maana utakuwa bado hujamsogezea huduma bali umemwongezea gharama. Barabara hii tumeshampa Mheshimiwa Magufuli aishughulikia kwa sababu Halmashauri hawana uwezo wa kuishughulikia. Kitu cha ajabu, mpaka leo Mheshimiwa Magufuli hana habari na barabara hii. Kwa hiyo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante mama. Tuendeleo Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse!

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Spika, -nashukuru na mimi kupata nafasi ya kuchangia bajeti hii muhimu ya Taifa, Ofisi ya Waziri Mkuu. Naomba anijikite katika maeneo machache tuna eneo la kwanza ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha na kushangaza kwa Viongozi Wakuu wa nchi kuwa na kauli mbili tofauti kwa jambo moja. Kambi ya Upinzani hapa Bungeni ionekana kama kioo kwa Serikali na kwa chama tawala na faida ya kioo ni wewe kujiangalia wapi hapajakaa sawasawa ili usonge mbele. Maana hili Taifa ni letu sisi wote, siyo la Chama cha Mapinduzi, ni letu sisi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tulisema na kulalamika sana haiwezekani kuwa na Kura ya Maoni, kwa mfumo ulioko hapa wa kura ya ndiyoo, ndiyoo, ikaonekana tumeshindwa lakini Viongozi Wakuu waliendelea kulieleza Taifa kwamba inawezekana *by 30th April*, Kura ya Maoni itakuwepo, kitu ambacho hakikuwezekana. Kwa waumini wa Kikristo hata na Waislam, Mungu alipoagiza wana wa Israel waende nchi ya ahadi, Farao alifanya moyo wake kuwa mgumu. Sasa hii Serikali ya CCM inaonekana kama Farao yaani moyo mgumu. Watanzania tunawaambia haiwezekani, wameendelea kusema inawezekana, kwa aibu mwisho wa siku wakasema kweli haiwezekani Kura ya Maoni tarehe 30 Aprili. Leo tukizungumza hapa, bado Serikali hii inazungumza kwamba Uchaguzi Mkuu Oktoba wakati huohuo pia Kura ya Maoni itapigwa, ni aibu kwa Serikali hii. Kwa sababu, ni wazi kwamba haiwezekani kupiga Kura ya Maoni kwa sababu ni lazima Sheria ya Kura ya Maoni irekebishwe kwanza na Bunge hili ndiyo la mwisho, litavunjwa, *this is shame to this government*, kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu akihitimisha, awaambie Watanzania kwa wazi bila kigugumizi kwamba hakuna Kura ya Maoni mwaka huu, tusimame kwenye Uchaguzi Mkuu na tutie nguvu kwenye huo. Tukizungumzia Uchaguzi Mkuu maana yake, turudi kwenye uandikishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, nguvu kubwa iwekwe hapo, kila Mtanzania mwenye sifa ya kupiga kura awe ameandikishwa. Mnaona jinsi mwenendo wa uandikishaji unavyosuasua na tumbakiwa na muda mfupi, hatuna fedha kama Serikali, kama nchi lakini bado tunabandika vitu vingi bila kuwaambia Watanzania ukweli wa jambo halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali hii ambayo mimi nimeibatiza ina moyo mgumu, hata wakipigwa namna gani hawaelewi na hwataki lakini mwisho wa siku Watanzania

wanaenda Kaanani. Niwaombe Watanzania mnaonisikia sasa, suala la kujiandikisha tuliweke kwa *priority* kubwa sana, kila mmoja ajiandikishe. Hakuna namna nyingine ya kuiondoa CCM madarakani isipokuwa kwa kura yako wewe Mtanzania, mwezi wa kumi mwaka huu. Maana yake kajiandikishe, kapige kura na kalinde kura yako. Tarehe 26 tujue CCM imeondoka, UKAWA unaingia madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uandikishaji kwa wanavyuo, picha inatuambia katika chaguzi zilizopita, wanaandikishwa wakiwa vyuoni wakati wa kupiga kura wako makwao. Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali, hii nchi ni yetu, hao ndiyo wasomi wetu, vijana wetu, wana haki ya kupiga kura. Kama wakati wa Katiba iliwezekana kupiga kura watu wakiwa wagonjwa, wakiwa *Muscat*, wakiwa *Jihad*, leo inakuwaje? Kwa hiyo, niombe Serikali ije na majibu ya wazi kwamba kila Mtanzania, mwanachuo, raia, mwezi wa kumi apige kura *wherever he or she is*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye eneo moja kulingana na Hotuba ya Waziri Mkuu la vita dhidi ya rushwa. Ni kweli kwa nchi yetu sasa rushwa imekuwa tabia au labda sehemu ya maisha. Tukisema kwa Serikali iliyoko madarakani yaani ya CCM kwamba imechoka, maana yake haiwezi kuleta kitu kipya tena katika kupambana na rushwa ambayo kimsingi imeozesha nchi hii. Niombe Serikali ije na majibu na mipango mikakati ya wazi, ni kwa vipi tutapambana na rushwa nchi hii. TAKUKURU wapo lakini hawana meno, tunaona Waziri Mkuu aliahidi kwamba tutawaongezea meno kidogo, siyo kuwaongezea tu, tuwapeni meno *full* na ndiyo namna pekee ya kuachana na tabia ya rushwa iliyoenea nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulisemea ni suala la usafiri wa anga. Waziri Mkuu ameeleza namna ya kukarabati viwanja na kadhalika lakini kwa nchi hii kubwa, sisi tunawaandalia tu watu viwanja wengine waje, tuna mpango gani wa kimkakati wa kuwa na usafiri wa anga Tanzania. Ukienda Kenya wanazo ndege nyingi tu mpaka nchi ndogo kama Rwanda wanazo ndege nyingi tu, Tanzania tunabaki kukarabati viwanja tu hatuna mpango na usafiri wa anga. Ni lazima tuondoke hapa tulipo sasa kama nchi ili tuweze kuwahudumia na kuwatumikia hawa Watanzania waone Serikali yao ikiwafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Mheshimiwa Lusinde alisaidia pamoja na kujikanyagakanyaga sana, alisaidia kusema Serikali hii imechoka inatakiwa Serikali nyingine lakini baadaye akaendelea kueleza huo uchovu ukoje, ni kweli imechoka, haiwezi kuwaza zaidi tena. Kwa hiyo, niwaambie Watanzania mnaotusikiliza mwaka huu mwezi wa kumi ni mwaka wa maamuzi mazito. Ni wakati pekee nchi hii ije kwenye mabadiliko ya kweli na uhuru wa kweli kwa kuiondoa CCM kwa kura yako, kura yako ni muhimu sana. Wanajifariji, wanajifariji lakini hiyo faraja mwezi wa kumi ndiyo kitaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kusema, wakati ikifahamika wazi kwamba katika bajeti hii hakuna fungu lililotengwa kwa ajili ya Kura ya Maoni bado Rais anasisitiza kwamba itakuwepo mwezi wa kumi, Waziri Mkuu anasema itakuwepo mwezi wa kumi, Serikali inasema itakuwepo mwezi wa kumi, itafanyikaje bila fedha, Serikali haijatenga fedha kwa ajili hiyo. Kwa hiyo, ni kweli Serikali ikija ije na majibu ya kuwaambia Watanzania wazi bila kigugumizi kwamba haiwezekani tubaki na uandikishaji wa Daftari la Kudumu na kupiga kura mwezi wa kumi.

Mheshimiwa Spika ahsante sana kwa nafasi hiyo. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Peter Serukamba atafuatiwa na Mheshimiwa Assumpter Mshama na Mheshimiwa Selemani Zedi.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze kwa mradi wa maji Kigoma. Mradi huu wa maji ulitakiwa uwe umekabidhiwa mwezi wa sita mwaka huu. Mradi huu fedha zipo, mkandarasi amelipwa, tatizo ni usimamizi wa Wizara. Nataka wakati wanatujibu watuambie wana mkakati gani maana mpaka sasa mradi ambao fedha zipo wamefanya *only* asilimia 40, fedha zipo kwa miaka mitatu yote ambayo wamekuwa pale.

Mheshimiwa Spika, la pili ni suala la kahawa. Moja ya zao linaloleta fedha za kigeni ni kahawa. Naomba Serikali ije na majawabu tunafanya nini kwenye bei ya kahawa, uwazi katika kupanga bei lakini pia na ruzuku. Kwa sababu hili ndilo zao ambalo linaleta fedha za kigeni, nilitarajia zao hili lingepewa kipaumbele kikubwa kwenye suala la ruzuku.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni tatizo la wakimbizi. Wakimbizi wamekuja wengi sana Kigoma kutoka Burundi wako pale Kagunga, Serikali inasubiri UNHCR ikawachukue. Sasa Kagunga kutaanza kutokea mauaji kwa maana ya magonjwa ya mlipuko, watakaoumia siyo wakimbizi peke yake, ni Watanzania wetu ambao hawana hatia. Ni matarajio yangu kwenye fedha za maafa haraka haraka waende wakasaidie ili wakimbizi wale waende kwenye makambi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la nne ni madeni. Madeni ni makubwa sana na Serikali hapa wala haijibu tunafanya kama mambo ni mazuri tu. Nchi hii Wizara ya Ujenzi peke yake wanadai shilingi trilioni moja, tunaulizana hapa hamna anayetaka kujibu fedha zitatoka wapi lakini watu wanaokufa ni wakandarasi wadogo, mabenki yanauza nyumba zao watu wao wanakufa, haiwezekani tunyamaze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tano, Wizara ya Ulinzi wamekuja pale Kigoma wamekaa kwenye nyumba za watu, hawalipi kodi zaidi ya miaka mitatu. Yule mtu aliyejenga nyumba yake kwa shida mnakaa hamumlipi maana yake nini? Mimi ningeomba tupate majawabu ya mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, sita ni kuhusu Jiji la Dar es Salaam. Mimi nadhani umefika wakati, kwenye Kamati ya Miundombinu tulisema toka tumeanza tuandae bajeti maalum kwa ajili ya miundombinu ya Jiji la Dar es Salaam. Yanayoendelea Jiji la Dar es Salaam hayawezi kuvumilika hata kidogo. Watu wanakufa kila mwaka tunaona ni kawaida tu, mafuriko kila mwaka tunaona ni kawaida tu, haiwezekani, ni kwa sababu hatutaki kuwekeza. Waziri amekuja anajibu anasema tuna mradi wa *World Bank*, hivi kweli *World Bank* ndiyo wajali maisha ya watu wetu kabla ya sisi wenyewe? Hapana! Nadhani umefika wakati tuhangaikie na suala hili. Watu wanakaa masaa mengi sana barabarani, watu wanateseka, watu wanakufa Dar es Salaam, lazima kama Serikali sikivu ya CCM tufanye juhudi kuhakikisha tunatatua tatizo la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, saba ni suala la *ESCROW*. Juzi Katibu Mkuu, nampongeza sana kiongozi, ametoa ripoti, anasema suala la *ESCROW* lilishughulikiwa na Wizara ya Madini na Nishati na Wizara ya Madini na Nishati wanasema Katibu Mkuu wake, Waziri Mkuu wake ni safi, maana yake muamala ule ni safi. Kama muamala ule ni safi, Katibu Mkuu ni safi, Waziri ni safi, Chenge anakuwaje mchafu, Tibaijuka anakuwaje mchafu, Ngeleja anakuwaje mchafu, mliowapeleka Mahakamani wanakuwaje wachafu? Haiwezekani, tuache, hizi ni *style* za kizamani, hatuwezi kufanya mambo ya namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninatarajia kesho umteue Chenge arudi kwenye Uenyekiti wake, maana Serikali wanasema muamala ule ni safi, pamoja na kwamba watu hawakulipa kodi, watu wamedanganya, watu wameleta *fake* kila kitu, wanasema ni safi. Kama ni safi, hawa tunawahukumu kwa nini? Tibaijuka tunamuhukumu kwa nini, ama kuna *citizens* wazuri

nchi hii wengine wabaya kwa Serikali hii, tuambieni, nataka Waziri Mkuu aje atuambie usafi wa hawa watu ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nane ni suala la Tokomeza. Mmefanya vizuri sana. Tuliomba ripoti ya tokomeza ije hapa na kama watu wa Tokomeza mmesema ni safi, naombeni Serikali hii muwateue kesho warudi kwenye nafasi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule Kenya wakati wanauza *Grand Regency Hotel* ya Kenya, Waziri wa Fedha alituhumiwa kwamba amekula rushwa aka-resign. Mwai Kibaki akaunda Tume ya *Judicial Inquiry* kama walivyounda kwenye Tokomeza, ripoti ilipotoka kwamba Amos Kimunya aliyekuwa Waziri wa Fedha hajakosa lolote *then the next day* Rais alimteua kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Mnapoamua kwenda kwenye hizi *High-tech democracy* za *good governance* msiishie nusu, haiwezekani mkaishia nusu. Mkishaamua kusema tunachunguza kama kweli hawa walikosea, mkagundua hawakukosea mnawarudisha kwenye nafasi zao, ndiyo matakwa ya *good governance*. Tuache usanii kwenye jambo hili. Kuna watu hapa, akina Maige, Maige alituhumiwa hapa kwamba amesafirisha wale wanyama kwenda nje, muundieni Tume na yeye tuone kama kweli ndiye aliyekwenda kwenye ndege kuwaingiza pundamilia ili na yeye mumsafishe mbona mnasafisha watu nusu? Hii ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, akina Ngeleja hapa, akina Mkulo waundieni Tume wote tujue kama walikosea, haiwezekani muumize wachache. Mimi hili hapana, kama kuna jambo linaniumiza ni *injustice*, haiwezekani tuwe na Serikali ya *double standard*. Wali-resign akina Karamagi hapa, akina Msabaha, Waziri Mkuu, kwa nini hamkuunda *Judicial Inquiry*, kwa nini hamkuunda? Maana kama mmeamua na kweli hizi ndizo njia nzuri za *good governance* kwamba mtu ame-resign aundiwe *Judicial Inquiry* tujue kama kweli alikosea, mkigundua hajakosea m-come out, m-restate nafasi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nakuomba kwa suala hili la *ESCROW* lazima tukubaliane hapa akina Chenge nao muwasafishe, *unless* mniambie na hao mliowasafisha ni wachafu. Mimi sipingi kuwasafisha lakini mnaishia nusu, ama mna ajenda nao, ndiyo tuambieni kwamba kuna ajenda hapa. Akina Mwambalasa wamesimamishwa pale Uenyekiti wao na wenyewe semeni hawakukosea, kwa nini muishie nusu? *It can not be*, vitu vingine tunaweza tukanyamaza lakini tuache uonevu kwa watu. Haiwezekani kuna watu ni wema, kuna watu ni wabaya, haiwezekani, hiki si chama tunachokijua wote. Werema aliondoka kwa sababu gani, maana kama muamala huu mnasema ni safi, waliosimamia wote mnasema ni safi, mwingine yeyote si mchafu. Maana kuna watu wa Ikulu wametuhumiwa lakini bado wako ofisini, sasa Werema anafanya nini, mlimuondolea nini u-*Attorney General* wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kweli kama tumeamua kwenda kwenye routes hiyo ya kusema hawa wali-resign jambo jema, tunakwenda kwenye *Judicial Inquiry* jambo jema, nakubali, lakini tusiishie hapo, tusiishie kwa Maswi, tusiishie kwa Muhongo, twende na kwa wote waliohusika na muamala huu. Leo Tibaijuka amekosea nini? Maana kama muamala ni safi maana yake fedha zile zilikuwa safi na fedha zikiwa safi za kwangu nagawa navyotaka, kwa nini iwe dhambi kwa niliowagawia? Maana haiwezekani wengine wote ni wachafu wasafi ni Maswi na Muhongo, haiwezekani, *there is no way*, hii haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mlichofanya mimi nawashangaa sana, wale mliowapeleka Mahakamani wote kesho kutwa wanakwenda kushinda na wao *defence* yao ni moja tu, jamani yes, *PCCB* ametuleta Mahakamani lakini muamala huu ni safi, ndiyo maana Serikali imewasafisha waliohusika na muamala huu. Maana waliosaini kila kitu ni Wizara, sasa walisaini jambo jema na mmesema wengine wanakuwaje wachafu, hapana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge lako hili naomba tu-demand Serikali hii ituambie na itangaze hawa wengine wote ni watu safi. Mnamwambiaje Chenge kwenye Jimbo lake, mnamwambiaje

Ngeleja kwenye Jimbo lake, mnamwambiaje Tibaijuka kwenye Jimbo lake, ama hawa hata wakiondoka mnaona sawa? Haiwezekani, mambo gani haya? Anakuja Katibu Mkuu anasema hawa safi, *fine*, Tokomeza tumeomba ripoti haijaletwa, anasema ripoti ya Tokomeza siwezi kuileta ni siri ya nani sasa? Unatusomea nusu nusu unapotaka tuone. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, huku unakiri watu wamekufa, huku unasema watu safi, *fine*, watu safi warudishieni Wizara zao maana ndiyo sababu ya kufanya *Judicial Inquiry* na duniani kote ndivyo wanavyofanya. Mkiamua kwenda kwenye hizi nchi zenye *democracy* kubwa na mambo ya utawala bora mkishafika huko msiishie nusu, fanyeni *all the way* mtapata *credibility* lakini mnasema hawa watu ni safi halafu mmekaa kimya ili iweje, msingesema tu. Halafu hawa tunawa-clear hawa hapana, hii ni nini, huu ubaguzi unatoka wapi? Huu ni ubaguzi tu *nothing else*. Nyerere alisema huu ni ubaguzi tu, hakuna dhambi mbaya kama ya kubagua watu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Assumpter Mshama atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Zedi.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia leo katika jambo lililoko mbele yetu.-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninayo shukrani mbele za Mungu na mbele ya Bunge lako Tukufu kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Spika, la pili, nakupongeza wewe Mwenyewe Mheshimiwa Spika kwa kipindi chote ambacho mimi nimekuwepo Bungeni umenithibitishia kwamba kwa kweli mwanamke anaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine napenda kumpongeza Waziri Mkuu pamoja na TAMISEMI kwa namna ya pekee ambavyo wameweza kufanya kazi na katika kazi zote walizofanya matunda yanaonekana.

Mheshimiwa Spika, hii ni awamu yangu ya kwanza kuwa Bungeni, napenda niwashukuru wana Misenyi kwa namna ya tofauti walivyoamua kunipa nafasi nikawawakilisha Bungeni na kwa kweli naamini mabadiliko wameyaona na mimi niseme ahsante kwa kuniwezesha kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze moja kwa moja na suala la elimu. Kwa nini nawapongeza wana Misenyi, wakati naingia katika Bunge hili, suala la ufaulu katika kidato cha nne katika Mkoa wa Kagera, Wilaya yetu ilikuwa ya nane. Hivi tunavyoongea kwa ushirikiano wao katika Wilaya nane Misenyi tuko namba tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, katika ufaulu wa sekondari kitaifa wakati nakuwa Mbunge nilikuta tuko nafasi ya mia moja kumi na tatu. Leo hii tunavyoongea kwa ushirikiano wao na kwa kushikamana pamoja tuko nafasi ya ishirini na moja kati ya Halmashauri 164. Kwa hiyo, ni kwa nini nawapongeza linaeleweka kazi tumeifanya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote lakini bado tunaiomba Wizara ya Elimu itusaidie. Katika elimu ya msingi tunapungukiwa Walimu 228 na katika elimu ya sekondari upande wa masomo ya sayansi tunapungukiwa Walimu 88. Kwa kazi hii ya kushika nafasi ya 21, je, tungekuwa tumepata Walimu wa kutosha tungekuwa labda wa kwanza au wa pili kitaifa. Kwa hiyo, naamini kwa upungufu huu tukiumaliza tutakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, wana Misenyi wamenituma tena katika suala la ardhi. Napenda kuishikiri Wizara ya Ardhi, Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi wanavyoendesha kwa sasa kwa *speed* hii ambayo tunakwenda nayo. Naamini kama itaongezewa na kuboreshwa vizuri tunaweza tukafanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo? Wakati fulani au Bunge lile lililopita, wewe mwenyewe uliunda Kamati ya kwenda kuchunguza nini kinaendelea katika vurugu iliyokuwa imetokea katika masuala ya ardhi. Napenda niseme kwamba hiyo taarifa ilivyokuja ilionyesha kwamba kuna kitu kimeonekana na tatizo linakwenda kutatuliwa. Ukisoma ukurasa wa 50 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameeleza mambo yanayoleta tatizo la migogori ya ardhi lakini katika maelezo yake ameeleza mambo mawili tu ambayo ni ugomvi na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, sisi Misenyi tuna zaidi ya ugomvi na uharibifu wa mazingira. Katika jambo hilo kuna watu wamekufa, katika tatizo hilo kuna watu wameporwa mali zao, katika tatizo hilo kuna watu wamefukuzwa katika maeneo yao, wamenyang'anywa sehemu zao za kuishi na watu wameharibiwa mazao yao. Kwa hiyo, kama tutarudi kwenye ile ripoti ambayo Kamati yako uliyoiteua walituletea nina uhakika haya mambo yatakwishwa.

Mheshimiwa Spika, hebu nisome tu kidogo katika ile hotuba iliyokuwa imetolewa au katika yale ambayo walibaini. Ukienda katika kile kitabu cha Kamati yako Teule, ukurasa wa 107 walisema hivi, tatizo kubwa lilikuwa ubinafsishaji usiozingatia mipaka ya vijiji. Kamati imetusaidia kutueleza la kufanya. Niende moja kwa moja kwenye ushauri. Inashauri kwamba kutozingatia mipaka ya vijiji vinavyozunguka mashamba na *ranch* wakati wa zoezi la ubinafsishaji kumesababisha wananchi wa vijiji vilivyo jirani kukosa maeneo ya kufanyia shughuli zao na hivyo kuvamia mashamba hayo na ya *ranch* kwa ajili ya kuendesha shughuli zao hali inayochangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro baina ya wawekezaji na wananchi wa vijiji husika. Suluhisho, Kamati inapendekeza kuwa Bunge litatake Serikali itoe maeneo yaliyolalamikiwa na wananchi kwamba yamebinafsishwa bila kuzingatia mipaka halisi ya vijiji na kuirejesha ardhi hiyo kwa wananchi baada ya kulipa fidia za wananchi. Hili likifanyika hatutakuwa na mgogoro wa ardhi tena, mgogoro ni watu kuwaporwa mali zao, kuchukua ardhi kuwapa wawekezaji wakati hawajawekeza kitu chochote. Kwa hiyo, nashauri wale watu wa Kakunyu wasiondolewe kwenye maeneo yao maana hili ni tamko tayari. Kuna haja gani ya kusumbua watu wakati tumeshapata suluhisho la jambo hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la umeme. Napenda kuishukuru Wizara ya Nishati kwa kazi njema wanayoifanya. Kazi ambayo kwa kweli katika Jimbo langu ni vijiji vyote vimepata umeme lakini naona nguzo na sehemu nyingine wameshapeleka hata nyaya. Naomba Wizara hii hasa maeneo ya Ishozi, Minziro, Mshasha na Bulembo ambapo tayari nyaya zimewekwa, Serikali inisaidie kupeleka umeme ili watu wafaidi matunda hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Hawa Ghasia kwa kazi kubwa aliyotufanyia wana Misenyi. La kwanza, ametusaidia kupata daraja la Kabingo ambalo limejengwa 2012 na kumalizika 2014, kwa kweli wana Misenyi tunakushukuru. Umetusaidia barabara kama nne ambazo sina haja ya kuzitaja lakini jambo ambalo tunakuomba sasa ambalo naomba kwa suala la barabara, tutengenezewe barabara inayotoka Kanazi kuelekea Minziro, barabara hii haipitiki kabisa. Naomba barabara ya kutoka Bugandika kuelekea Luzinga itengenezwe, wakati huu wa mvua watu wanashindwa kupita. Pia naomba barabara inayotoka Katoma kuelekea Kashenye itengenezwe ili watu waweze kupita. Kwa kweli kama hizi barabara zitategenezwa, watu watafanya kazi zao na uchumi wao utaongezeka na utakua vizuri kama tutasaidiwa hizi barabara. Kama alivyokuwa ametuahidi Mheshimiwa Magufuli kwamba zitategenezwa, tunaomba sasa zitengenezwe ili wananchi waweze kupita vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kuchangia ni suala la Wenyeviti wa Vijiji na wa Vitongoji. Kwa kweli hili limekuwa ni tatizo. Huwezi kumpigia mtu kura akachaguliwa ukampa nafasi asiyepata posho hata senti kumi lakini umemwekea mzigo mkubwa ukilinganisha na ile kazi ambayo watu wengine tunafanya. Kwa mfano, ili tupate amani tunaanza na Mwenyekiti wa Kitongoji, ili tuone kama ile miradi tuliyoipeleka kwa wananchi imefika tunaanza na Mwenyekiti wa Kitongoji. Hivi kwa nini wasitengewe kiasi kidogo ili na wao wafurahi kuona kwamba Serikali yao inawajali?

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba niseme jambo moja, kuna jambo hapa linachezewa bila kulifikiri. Mtu unapoanza kugusa mpaka Usalama wa Taifa kwa kusema ume-*paralyze* lazima wewe mwenyewe uwe ume- *paralyze*. Huwezi kutamka Usalama wa Taifa kwamba ume-*paralyze* wakati nchi ina amani namna hii, huwezi kusema Usalama wa Taifa umelala wakati Tanzania nzima na Afrika nzima tunasifiwa kwamba ni nchi ya amani, kazi hiyo inafanywa na Usalama wa Taifa. Haya matusi wanayotukana leo na huko mitaani wanakoandamana ni kwa sababu tuna chombo cha Usalama wa Taifa kinachofanya kazi vizuri. Mimi naweza kusema kwamba usalama na amani ya Taifa lolote inategemeana na Usalama wa Taifa. Hapa Bungeni tumekaa kwa amani namna hii Usalama wa Taifa umeshajua kwamba leo tutatoka, unawezaje kudhalilisha chombo kikubwa namna hiyo? Kwa hiyo, wao wenyewe wanakwenda wanasema eti wanataka kuingia Ikulu, hivi wewe Ikulu na mtu hata usiyeelewa maana ya Usalama wa Taifa unakwenda Ikulu kufanya kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwaulize jambo moja ambalo nilikuwa nalishangaa. Mimi nilishawahi kukutana na mtu anasema mimi nitakupiga, lakini wanapotaka kupigana anamwita mtu anamwambia mshike huyu usipomshika mimi nitampiga. Ni sawasawa na CHADEMA, nitaitoa CCM lakini wakati wa kuttoa anasema tunajiumba na UKAWA na vyama vingine ambavyo hata majina siyajui....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Sasa nitamwita Mheshimiwa Selemani Zedi, Mheshimiwa Meshack Opolukwa, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa wajiandae.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene nitoe mchango wangu katika hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na Mawaziri wote walio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa namna ambavyo wanajituma, wanafanya kazi na kupata matokeo ambayo kwa kweli kwa macho yanaonekana kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa na kwa nafasi hii nimezunguka katika Halmashauri zaidi ya 100 kufanya ukaguzi wa hesabu na kuangalia miradi ya maendeleo. Naomba niseme, pamoja na kwamba bado kuna mambo ambayo yanahitaji kurekebishwa lakini kwa kweli kuna mambo mengi sana katika maeneo mengi ambayo yameboreka na kwa macho inaonekana kabisa jitihada zimefanyika. Kwa hiyo, kwa kila hali napenda niwapongeze sana Waziri Mkuu na Mawaziri wote ambao wapo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakwenda moja kwa moja katika mambo ambayo yanahusu Jimbo langu la Bukene. Kama mwakilishi wa wananchi wa Bukene bila woga wowote na kwa ujasiri

kabisa, kwa niaba yao, naomba niishukuru Serikali kwa mambo ambayo yamefanyika na kwa kweli yameongeza tija na hali ya maisha kwa wananchi wa Jimbo la Bukene.

Mheshimiwa Spika, naanza na suala la umeme. Kwa mara ya kwanza Jimbo la Bukene limefanikiwa kupata umeme. Hivi tunavyoongea awamu ya kwanza ilikamilika, vijiji vya Kagongwa, Busasi, Itobo, Bukene, Uduka na Kabanga vyote sasa hivi vinanufaika kwa nishati muhimu ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo nasisitiza hapa ni kwamba baada ya nishati hii muhimu kupatikana mahitaji yamekuwa makubwa mno yaani mwitikio ni mkubwa sana.

Mimi niwapongeza wananchi wa Bukene na maeneo ya Itobo kwa kuona umuhimu wa umeme na kuja na mwitikio na mahitaji makubwa sana. Wananchi wako tayari kulipia na sasa hivi ninavyoongea kuna mahitaji makubwa mno ya umeme ambapo TANESCO ina kazi kubwa ya kuyatimiza. Nimpongeze Meneja wa TANESCO wa Mkoa wa Tabora anajitahidi, ananipa ushirikiano lakini nitumie fursa hii kuiomba Wizara na hasa TANESCO Mkoa wa Tabora wafanye kila jitahada ili angalau tupate nguzo kama 200 kwa Bukene Mjini lakini nguzo kama 100 kwa Mji wa Itobo ili tuweze kukidhi mahitaji makubwa sana ya wananchi wa maeneo hayo ambao wako tayari kulipia, wanahitaji huduma hii lakini shida ni upatikanaji wa vifaa hasa nguzo na vifaa vingine vya kuunganishia.

Mheshimiwa Spika, lakini katika suala hilo hilo la umeme, nimpongeze sana Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Charles Mwijage, tarehe 8/4 alifanya ziara katika Jimbo langu na alitembelea maeneo ambayo awamu ya pili ya REA inatekelezwa. Alifanya mikutano na kuongea na wananchi katika vijiji vya Mwagoye, Mogwa, Mbutu na Mambali. Kwa kweli aliwapa matumaini wananchi na aliangalia kwa macho utekelezaji wa miradi ile na kwa kweli wananchi wamepata matumizi na sasa wako wamekaa mkaa wa kula na kusubiri kuanza kutumia huduma hii muhimu ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo langu wanafahamu kabisa kwamba bila nishati muhimu ya umeme maendeleo yatakwenda kwa kasi ndogo mno. Kwa maana hiyo, tuna kila sababu ya kuipongeza Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini kwa kutupatia umeme katika vijiji hivyo zaidi ya 20 ambavyo kwa kweli sasa vitaongeza kasi ya maendeleo ya kiuchumi na jambo ambalo ndio wananchi wanalitajaraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika eneo la maji, kwa niaba ya wananchi wa Bukene, naipongeza tena Serikali kwa kupitia Wizara ya Maji kwa kufanikisha miradi zaidi ya sita ya visima virefu na hivyo kuwapatia maji zaidi ya wananchi 20,000 ndani ya Jimbo la Bukene ambao walikuwa hawana uhakika wa vyanzo vya maji safi na salama. Kwa kipindi hiki cha miaka mitano, jitihada kubwa zimefanyika, wananchi wa vijiji vya Buhondo, Nawa, Mahene, Ikindwa, Itobo na Sigili kwa ujumla wao ambao ni zaidi ya 20,000 ambao walikuwa hawana uhakika wa vyanzo vya maji safi na salama, sasa wanapata maji hayo. Kwa hiyo, jitihada za kuwapatia wananchi zaidi ya 20,000 maji safi na salama siyo jambo dogo ni jambo kubwa ambalo linahitaji kupongezwa. Mimi mwakilishi wao, kwa niaba yao kwa kweli naipongeza Serikali kwa kufanya waweze kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado kuna changamoto katika maeneo ya miundombinu ya barabara na hili hasa linasababishwa na upatikanaji mdogo wa fedha katika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega hasa katika Mfuko wa Barabara. Kuna baadhi ya barabara ambazo tumekuwa tukizitengea fedha kila mwaka lakini mwaka unakwisha barabara hizo hazijapata fedha kwa hiyo hazipitiki. Naiomba Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi kwa kupitia Mfuko wa Barabara na Halmashauri ya Nzega ifanye kila jitihada kwa kadri itakavyowezekana ili vijiji vya

Semembela na Isagenhe ambavyo kwa kweli havifikiki kutokana na kukosa miundombinu ya barabara vipate huduma hiyo muhimu.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukitenga fedha miaka yote hii mitatu lakini kwa bahati mbaya kila mwaka unakwisha fedha hazijaja. Naiomba Serikali tunapokwenda kumaliza sasa zipatikane fedha. Nina taarifa kwamba kiasi fulani cha fedha kimepatikana, taratibu za kutafuta Mkandarasi zimeanza ili ujenzi wa barabara ambao utawezesha vijiji vya Semembela na Isagenhe vifikike. Naomba jitihada hizi zikamilike ili kwa kweli wananchi wa vijiji hivi waweze kupata huduma muhimu itakayowezesha kufikisha mazao yao sokoni na kuyauza kwa bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu kwa kupitia Serikali, kupitia Wizara ya Afya, sasa hivi ujenzi wa vyumba viwili vya upasuaji unakamilika. Chumba kimoja cha upasuaji kiko katika Kituo cha Afya cha Bukene na kingine katika Kituo cha Afya cha Itobo. Hizi ni jitihada kubwa sana ambazo zitapunguza vifo vya akina mama na watoto na jambo Serikali siku zote imekuwa ikiweka jitihada ili kuhakikisha vifo vya akina mama na watoto vinapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, rai yangu hapa, nilishaongea na Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Kebwe kwamba ujenzi umekamilika na jitihada zinazofanyika sasa kupitia Wizara ya Afya Makao Makuu ni kukamilisha upatikanaji wa vifaa na upatikanaji wa wataalam ili haraka iwezekanavyo na kwa mujibu wa mazungumzo yangu na Mheshimiwa Dkt. Kebwe ikiwezekana ndani ya mwezi wa saba ili tuweze kwenda kufungua vyumba hivyo vya upasuaji. Vyumba hivi kwa kweli ni muhimu sana kwani akina mama na watoto wa maeneo ya Bukene watafanyiwa *operation* maeneo ya karibu na wanapoishi na jambo hili litapunguza vifo vya akina mama na watoto na tutakuwa tumeongeza tija na afya kwa wananchi wa maeneo hayo. Kwa hiyo, rai yangu kubwa ni kwamba kama itawezekana kabla ya Bunge hili kumalizika basi vyumba hivi vya upasuaji katika hivi Vituo vya Afya viwili cha Bukene na Itobo huduma zizinduliwe na wananchi waanze kupata huduma hizo muhimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Bukene ambao siku zote wananipa ushirikiano na nawaahidi kwamba nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu na jitihada zote. Nina uhakika kabisa katika uchaguzi ujao Chama changu cha Mapinduzi na mimi mwenyewe nitaendelea kushinda ili niweze kuwawakilisha na kuwapa huduma wananchi wangu kwa kadri ambavyo wanahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naomba Serikali iendeele kufanya jitihada kama ambavyo inafanya ili wananchi wainue hali zao za maisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Meshack Opolukwa.

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii muhimu sana kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, leo nitazungumzia masuala ya Walimu tu na hususani Halmashauri ya Meatu. Matatizo ya Walimu na kwa bahati mbaya sana mwaka jana tulikubaliana na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa kwamba Walimu wana matatizo mengi na wanahitaji Naibu Waziri mwenyewe aende kungea nao kwa sababu maji yamefika shingoni. Tukakubaliana na Naibu Waziri kwamba tunakwenda, tukapanga ratiba lakini akaingia mitini. Sasa yanayoongelewa hapa kwamba Serikali imechoka ni kweli imechoka na inajidhihirisha kwa viongozi wetu Mawaziri nao wamechoka kwani wanashindwa hata kwenda kuwaona watu ambao wanawaongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi nimekuwa na kikao na Walimu kwenye Jimbo la Meatu, nimemuita Mkurugenzi ameahidi atakuwepo, ameingia mitini. Tunaposema wamechoka ina maana wamechoka kuanzia Waziri mpaka watendaji wa chini. Sasa Walimu wa Meatu wana madai yao mengi ambayo wanataka yatatuliwe na Mheshimiwa Naibu Waziri nakuomba sana pamoja na kwamba uliingia mitini mwaka jana Walimu hawa bado wanakuhitaji uende kuwasilikiliza mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kuna madai ambapo Walimu wanataka yatatuliwe mapema zaidi. Walimu wa Meatu siyo wa Tanzania wana madai ya mishahara zaidi ya shilingi milioni 197 lakini ambazo zimeshalipwa mpaka sasa ni shilingi milioni 6.6 ambazo ni sawa na 3.3%. Haya madai ya Walimu wanaomba yalipwe vinginevyo wanasema kazi haitafanyika madarasani. Bahati mbaya sana Mkoa wa Simiyu na Shinyanga imekuwa ikiongoza kwa wanafunzi kufanya vibaya, ni kwa sababu kuna matatizo lukuki ambayo hayajapata ufumbuzi na hususani ya madai ya mishahara na maslahi ya Walimu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia suala la uhamisho, Walimu wa Meatu wanadai shilingi milioni 104.7 lakini fedha ambayo imeshalipwa mpaka sasa ni shilingi milioni 15.8 sawa na 15%. Walimu wanadai hizi fedha ni kwa nini hazilipwi? Ni matatizo yapi yanayosababisha fedha za Walimu zisilipwe? Ndiyo maana sasa hivi wanafanya kazi wakiwa wamekata tamaa sana. Kuna fedha za likizo wanadai shilingi milioni 4.3 ambazo mpaka sasa haijalipwa hata shilingi moja ambayo ni 0%. Wanadai fedha ya masomo shilingi milioni 3.5 lakini mpaka sasa hata shilingi moja haijalipwa ni 0% ambayo imelipwa. Wanadai posho ya kujikimu shilingi 315,000/= imelipwa fedha 0%. Wanadai fedha ya matibabu shilingi milioni 2.7, Walimu wa Meatu hawa, lakini mpaka sasa imelipwa shilingi milioni 1.5.

Kwa hiyo, madai yote ya Walimu wa Halmashauri ya Meatu ni shilingi 308,265,879/= lakini fedha ambayo imelipwa mpaka sasa ni shilingi 23,645,980/=. Walimu hawa wanaomba walipwe fedha zao.

Mheshimiwa Spika, kada ya Ualimu inaonekana sasa imekuwa ni kichaka. Watumishi wengine wa Serikali wanalipwa fedha zao, kwa nini Walimu? Ni kwa nini Walimu wa Meatu wanaodai shilingi milioni 308 ambazo hazijalipwa mpaka sasa ni milioni 284, iliyolipwa ni 7.6% tu ya madai ya Walimu wa Meatu. Waoneeni huruma hawa watu, ioneeni huruma hii kada ili Walimu walipwe fedha zao na kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo lingine linaloendana na madai ya Walimu. Kuna Mwalimu mmoja anaitwa Debora Nkinde, tarehe 17 Aprili, 2009 alipata ajali ya kuvunjika nyonga na alikuwa kwenye kituo cha Esanga Itinje akaletwa pale kwenye hospitali ya Wilaya. Mwalimu huyu akapata matibabu lakini baadaye akapata rufaa kwenda Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga. Ikaonekana kwamba matibabu yake yanahitaji *attention* kubwa, akapelekwa Bugando na baadaye Muhimbili. Mwalimu huyu amekuwa akipata matatizo hata ya fedha ya kujikimu wakati anatibiwa, imekuwa ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa ameshatoka Muhimbili maana aliambiwa na wataalam wa Muhimbili kwamba aje akae karibu na hospitali (Hospitali ya Wilaya) asikae mahali ambapo ni mbali na huduma hii. Matokeo yake baada ya kurudi amepelekwa kwenye Kata inaitwa Mwandoya ambako ni zaidi ya kilomita 50 kuja kwenye hospitali ya Wilaya. Ameomba ahamishiwe karibu na Hospitali ya Wilaya ili aweze kuwa anapata *attention* ya Madaktari lakini imeshindikana. Naomba Mwalimu huyu asaidiwe kwa kurudishwa kwenye kituo ambacho kitakuwa karibu na hospitali, aendeleo kupata matibabu kama ambavyo Madaktari Bingwa wameshauri.

Mheshimiwa Spika, kuna Mwalimu alipoteza maisha mwaka jana na naomba Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. Huyu Mwalimu aliyepoteza maisha anaitwa

Beatrice Ingereza alipoteza maisha wakati akiwa mikononi mwa Madaktari katika harakati za kujifungua. Bahati mbaya ilikuwa mwaka jana wakati wa mwaka mpya, tarehe 01 Januari, 2015, alifikishwa pale kwenye hospitali yetu ya Halmashauri, Nesi hakuwepo alikuwa anasherehekea mwaka mpya nyumbani, Daktari hakuwepo alikuwa anasherehekea mwaka mpya nyumbani. Mama huyu alipoteza maisha chini ya uangalizi wa Madaktari kwa bahati mbaya sana kwa uzembe wa Madaktari.

Mheshimiwa Spika, iliundwa Tume na wakati ule tulikuwa na DC ambaye ni Mheshimiwa Kirigini ambaye amehamishiwa Maswa, Tume hii iliundwa kwa kuhusisha DC mwenyewe, DED, DAS na Madaktari wengine. Wakasema kwamba wanaunda Tume kwa ajili ya kuchunguza suala hili. Uchunguzi ulifanyikwa kwa siku saba, wakaongezewa siku saba nyingine lakini mpaka leo ripoti hii haijatoka na hawa watu bado wanaendelea kudunda wakifanya kazi za Serikali. Naomba wakati Waziri anahitimisha anieleze hii Tume iliyoundwa inaleta majibu gani kwa Walimu hawa pamoja na familia ya mwathirika wa mauti ambayo yamesababishwa na uzembe wa Madaktari pamoja na Nesi.

Mheshimiwa Spika, kuna *issue* nyingine hapa kuhusu Walimu ambayo ni suala la ruhusa ambapo Mwalimu anaomba wakati wa dharura. Mwalimu anaweza akawa amefiwa labda na mtoto wake, Baba yake au Mke wake, lakini ili aweze kupata hiyo ruhusa kwenda anakotaka, anaambiwa ni mpaka akabidhi vipindi kwa Mwalimu mwingine. Hebu tujaribu kufikiria, umepata msiba leo usiku, unatakiwa uondoke asubuhi kwa ajili ya kuwahi taratibu za mazishi na mambo mengine, unaambiwa ni lazima upate Mwalimu wa kubadilishana naye vipindi ndiyo uweze kuondoka. Suala hili linasikitisha na linakatisha tamaa. Naomba kama kweli ni maelekezo ya Wizara basi liweze kurekebisha. Kama ni maelekezo ya Halmashauri basi naomba Wizara ipeleke maelekezo chini ili yaweze kufanyiwa kazi. Walimu hawa wanapopata dharura, wanapotaka kwenda maeneo mengine kwa ajili ya kwenda kuwazika wapendwa wao, familia zao, wasipewe mikwara na vikwazo kwamba mpaka apate Mwalimu mwingine wa kushika vipindi vyake ndiyo aweze kuondoka.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la uhamisho kwa Walimu wanapotaka kuhama kwenda kufanya kazi maeneo mengine. Meatu ni Wilaya ambayo iko katika mazingira magumu, haiwezekani Mwalimu anataka kuhama baada ya kufanya kazi miaka 10 Meatu na anataka aka-enjoy masuala mengine ya Miji mikubwa, abadilishane na Mwalimu wa wa Kinondoni Dar es Salaam au wa Mwanza Mjini, Ilemela aende Meatu, haiwezekani. Kwa hiyo, utaratibu wa Wizara ufanyike ikifikia mtu anataka kuhamishwa basi ahamishwe na wale walio kwenye mazingira mazuri au walioko mijini wapelekwe Meatu wakafanye kazi, wote hawa ni watumishi wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini inapofikia Mwalimu wa Meatu anataka kuhama, amefanya kazi miaka mitano, sita, saba, anataka angalau na yeye ahamie sehemu nyingine nzuri anaambiwa kamlete mtu wa kubadilishana naye ndiyo tukuhamishe. Lakini kuna watu wengine pamoja na kwamba wamechoka na wanaamua kuhamia maeneo mengine, akitaka kuhama bado anaambiwa hatuwezi kukupa fedha na maslahi ya uhamisho kwa sababu umejiombea uhamisho mwenyewe. Huu ndiyo utaratibu wa Wizara? Ninaamini mtumishi wa Serikali kuhama ni masuala yake ya msingi. Sasa Walimu hawa wanapotaka kuhama kwenda maeneo mengine wasiwekewe vipangamizi kwamba eti ni lazima alete mtu wa kubadilishana naye.

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. MESHACK M. OPULUKWA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja inaongelewa hapa ya ma-MEK. Kumekuwa na tatizo Meatu, nimekuwa na kikao na Walimu juzi wanasema wanashangaa hawa ma-MEK kwa Meatu wamekuwa ni wengi mno. Kata moja inakuwa na MEK wawili. Kata ya Mwahnuzi peke yake kuna MEK watatu.

MBUNGE FULANI: MEK ni nini?

MHE. MESHACK M. OPULUKWA: Walimu wanafahamu vizuri sana, ni Mratibu wa Elimu Kata. Sasa imefikia kiasi hawa ma-MEK wanasababisha upungufu wa Walimu wa kufundisha madarasani kwa sababu hawa ufundishaji kidogo unakuwa haupo. Sasa imefikia mahali kwa sababu kuna maslahi kwa mfano ya *EQUIP* ambapo wafadhili wametoa fedha kuweza kusaidia Walimu hawa kwenye masuala ya watoto wa madarasa ya chini kuweza kusoma na kuandika. Kwa sababu kuna fedha kiasi kidogo inatolewa na wafadhili kama *DFID* na kwa sababu kuna maslahi ambayo yanawasaidia Walimu kuongeza kipato chao, kuna Afisa Elimu wa Wilaya Shule za Msingi akaamua kumteua mke wake kuwa MEK ili kuweza kupata fedha za *EQUIP*. Sasa tunakwenda wapi? Yaani wewe mwenyewe unajiteulia mke wako akafanye kazi hizo badala ya angalau kuwateua watu wengine waweze kufanya kazi zile.

Mheshimiwa Spika, bado nazidi kusesitiza kwamba Walimu hawa bado wanahitaji kuongea na Mheshimiwa Waziri ili aweze kutatua matatizo yao.

SPIKA: Ahsante, kengele imegonga.

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Kigirini!

MBUNGE FULANI: Anatoa taarifa gani?

TAARIFA

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Nilitaka nimpatie taarifa Mheshimiwa Opolukwa, Mbunge wa Jimbo la Meatu kwamba ni kweli taarifa za kifo cha Mwalimu aliyemtaja zilifikishwa kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na ni kweli kama alivyosema Ofisi ya Mkuu wa Wilaya iliunda Tume na Tume ile inayo mamlaka ya kuripoti Mkoani.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nimuombe Mheshimiwa Mbunge awe mvumilivu, ofisi ya Wilaya haiwezi kutoa taarifa au majibu ya kitaalam kwa Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, niombe awe mvumilivu, taarifa ile iko Mkoani inafanyiwa kazi na majibu yale yatakapokuwa tayari yatarudi kwa ajili ya utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

SPIKA: Naomba tuendeleee. Nilikuwa na wasiwasi kwamba ni nani aliunda Tume na anatakiwa kuwajibika wapi, nilikuwa na maswali hayo lakini nadhani nimepata ufafanuzi.

Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, kama hayupo Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau.

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote, nachukua nafasi hii kumshukuru kwanza Mwenyezi Mungu, Muumba Mbingu na Ardhi na vilivyomo ndani yake.

Mheshimiwa Spika, vilevile nakushukuru sana wewe binafsi na nikupongeze kwa kazi ya miaka mitano ambayo umeifanya na kwa kweli umekuwa kioo kwetu. Mimi niliyesimama hapa hili ni Bunge la lala salama, nikitoka hapa naenda Jimboni Pangani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu wameanza propaganda huko wanapita wanasema kuwa mtamchaguaje mwanamke ninyi? Nashukuru Watanzania siku hizi wana akili! Wakawaambia kuwa hao Wabunge wenyewe tuliowachagua wanaongozwa na Spika mwanamke Bungeni na amefanya vizuri kwa miaka mitano. Kwa hiyo, angalau tuna majibu ambayo hatuna haja ya kupapasapapasa, yako wazi kabisa. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Ahsante Mbunge. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Spika, nielekee kwenye hotuba ya Waziri Mkuu. Kwa kweli Serikali yoyote ambayo iko makini kabisa, ni wajibu wao wa msingi kutoa huduma za jamii kwa wananchi na siyo lazima wananchi kushukuru. Kushukuru lile ni suala la kiungwana tu, lakini siyo lazima wawe wanyenyekevu na kusema, afadhali tumefanyiwa hiki, ni wajibu wa msingi kabisa wa Serikali yoyote ile iliyo makini kuhakikisha kuwa wananchi wake wanapata huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, naanza kwenye maji. Nimeona kwenye hotuba ya Waziri hapo ameelezea kwanza iko kwenye *BRN* na angalau kuna juhudi zinafanyika, lakini nimwambie tu Mheshimiwa Waziri kwamba bado na kwa kweli hiyo *speed* ni ndogo kutokana na hali halisi ilivyo kwa wananchi. Nikichukulia tu kwa ndugu zangu Pangani, hali kwa kweli ni mbaya sana kwenye suala la maji, maji ni uhai, tunahitaji maji safi na salama. Ule Mradi wa Vijiji Kumi tu wa *World Bank* bado haujatekelezeka, umefeli. Nina mfano mmoja tu wa kijiji cha Mzambarauni ambacho kwenye mradi huo wametumia shilingi milioni 209 ukitoa VAT, kisima hicho kimetoa maji kwa mwezi mmoja tu, sasa hivi hakuna maji tena. Sijui Wizara husika itakapokuja itasema nini kuhusu suala kama hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna vijiji vingine ambavyo hii leo mtu anapata maji ndoo tatu tu kwa siku mbili kwa sababu siku ya pili huruhusiwi kuchota kuna foleni, mpaka siku inayofuata. Kwa hiyo, hali ni mbaya sana. Tunaomba kama kweli iko kwenye *BRN* hiyo *speed* ya kwenye *BRN* iende na uhalisia kwa wananchi ili waone. Hakuna watu wanaoichukia Serikali ila wanachotaka ni huduma ziweze kuwafikia, basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naenda kwenye afya. Kwa kweli tumeona kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri humu kuna mengi yanafanyika na kuna ule Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Jamii lakini mpango ule bado haujatekelezeka katika baadhi ya maeneo. Ni kweli *speed* ipo, Zahanati zimeongezeka na kadhalika lakini ukiangalia uhalisia bado kuna vijiji ambavyo ni mbali sana na huduma za afya. Mpaka leo kila kijiji kuwa na Zahanati na Kituo cha Afya kwa kila Kata haijafikiwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, nikichukulia mfano wa maeneo ambayo nimetembelea kama Pangani bado kuna vijiji ambavyo mpaka leo wanawake wanakufa, hakuna kabisa Zahanati na hicho Kituo cha Afya chenye kipo kimoja tu Mwera na hakina vifaa kabisa. Kwa Pangani tunashukuru Madaktari wapo lakini hakuna vifaa ambavyo vinaweza vikasaidia mtu akaweza kupata tiba mpaka kuweza kufika Pangani bila kudhurika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hakuna *ambulance*. Jana nilimsikia Mheshimiwa Rage akichangia na kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba Tabora wamepata *ambulances* 16 na yeye anasema kwake alikuwa nazo tatu, kwa hiyo na zile mbili sasa amekuwa na tano. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Pangani nao pia ni Watanzania. Kama kweli hao wamepata hizo,

Pangani hakuna *ambulance* hata moja, zote mbili ziko juu ya mawe na gari zote za pale hospitali ni mbovu na barabara hakuna. Kwa hiyo, mtu yeyote akiwa hoi bin taaban au kwenye hali mbaya, wanaomba gari kutoka kwa mtu binafsi ili aweze kupelekwa Tanga Mjini, Hospitali ya Rufaa, lakini barabara yenyewe ni balaa, na hilo ni suala lingine.

Mheshimiwa Spika, naelekea kwenye elimu. Nimeangalia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, nashukuru kuna baadhi ya vitabu sasa hivi vipo mashuleni. Nilifanya ziara kwa shule za msingi zote angalau ukifika kuna vitabu. Suala la Walimu nimeona Mheshimiwa Hawa Ghasia amegusia pia kuwa wamepata kibali cha kuweza kuajiri na wengine wameishaajiriwa ili kuweza kuongeza idadi ya Walimu. Bado nasisitiza tusiwasahau Walimu kwenye marupurupu na waweze kupata malimbikizo yao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, vilevile Walimu wanafundisha vipindi vingi zaidi, labda kama hao Walimu wakiongezeka itawasaidia kuweza kupunguza idadi ya vipindi. Kwa wiki Mwalimu anatakiwa angalau afundishe vipindi 35 lakini utakuta Mwalimu mmoja anafundisha vipindi vingi sana kwa siku. Kama hakuna utoshelevu wa Walimu basi wapewe angalau *bonus* (motisha) fulani ambao itawafanya waweze kufundisha kwa sababu wana moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile nimeona Mheshimiwa Waziri kwenye kitabu chake ameelezea ongezeko la nyumba za Walimu, kuna nyumba ambazo zimejengwa mwaka 2006/2007, zile ni fedha za Serikali lakini mpaka leo hazijamaliziwa na ziko zile mbili kwa moja na moja, nyumba tano hazijawahi kukaliwa au kuhamiwa, zimeshaanza kuvunjika, ile ni fedha ya Serikali inapotea. Zile nyumba zimaliziwe ili Walimu wasiteseke kwa kukaa mbali na shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naelekea kwenye suala la ajira kwa vijana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, humu na yeye imemgusa kuwa kweli hili ni tatizo ukizingatia kwamba vijana ni milioni 16 yambao ni asilimia 35 ya Watanzania. Hii ni balaa kwa sababu ni asilimia moja ya walioajiriwa kwenye sekta ya umma, lakini asilimia sita wameajiriwa kwenye sekta binafsi. Asilimia 93 hawana ajira, tukisema wameajiriwa kwenye kilimo, uvuvi, mifugo na biashara ndogo ndogo, nguvu kubwa sana inapotea ambayo ni nguvu kazi ya Taifa. Vijana wengi wanauza *big-G* na wanakimbia kutoka vijijini wana sababu, vijijini hawana maeneo ya kulima. Mfano halisi ninao, Pangani tumeathirika sana na Mashamba ya Mkonge. Nimemuandikia Waziri wa Ardhi hapa kwamba kuna tatizo la mashamba pori ya mkonge mengi ambayo Serikali inatakiwa ifanye maamuzi haraka, wawagawie vijana maeneo ili waweze kujajiri. Vijana wawekewe miundombinu ambayo ina uhakika na maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tumesikia hapa suala la Tokomeza. Hili limewagusa sana ndugu zangu kule, kuna vijana ambao walijajiriwa kwenye Mashamba ya Mkonge walikuwa na magobole. Operesheni Tokomeza ilipopita kule iliwanyang'anya silaha nyingine na magobole na wote walionyanyang'anywa wanamiliki kihalali, mpaka leo Serikali iko kimya. Wale vijana hawana ajira kwani bila lile gobore huajiriwa kwenye Mashamba ya Mkonge.

Sasa tunaiomba Serikali isikae kimya, iseme vijana wale hatima yao ni nini? Wawaambie kama watawarudishia au hawatawarudishii ili wajue. Nchi hii inaongozwa kwa mujibu wa sheria na taratibu tulizojiwekea, wawaambie kwani wanachohitaji ni kauli tu kwamba watarudishiwa au hawarudishiwi silaha zao, hawarudishiwi kwa nini, basi, Serikali isiwe bubu, iseme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naelekea kwenye suala la mifugo. Kuna tatizo la mifugo na naweza kusema ni tatizo kwa sababu ni mgogoro mkubwa kwa wakulima na wafugaji. Kwa kweli mifugo imeongezeka sana kwenye maeneo yetu. Pwani zamani tulikuwa hatujazoea kuona wafugaji lakini sasa hivi wafugaji wamekuwa wengi kutokana na hitaji la malisho na maji.

Kwa kweli hili ni tatizo. Nimeona kwenye suala la ardhi kwamba kuna mpango ambao unakuja wa kuweka mipaka na kupanga matumizi bora ya ardhi. Naomba lifanyiwe uharaka wa hali ya juu. Ni muhimu sana kwa sababu wanaona Watanzania wa maeneo mengine jinsi wakulima na wafugaji wanavyopigana.

Mheshimiwa Spika, jana nimeona yaliyotokea Morogoro, wafugaji wamechinjiwa ng'ombe wao 30, mfugaji hawawezi kukubali na mkulima hawezi kukubali hata kidogo mifugo ikaingia kula mimea yake, kwani amelima kwa shida. Kwa hiyo, ni kitu ambacho naomba hiyo speed iongezeke na masuala ya hifadhi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nitamuita Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla halafu atafuatia Mheshimiwa Victor Mwambalasa.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kwa mara nyingine tena kukutana hapa siku hii ya leo kutekeleza majukumu yetu lakini pia kutufikisha hapa kwenye kilele cha shughuli hii ya Ubunge ambayo tulipewa na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2010.

Nichukue fursa hii kwa namna ya pekee kukupongeza Mheshimiwa Spika na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote pamoja na Wabunge wenzangu. Kwa sisi ambao tulikuwa Wabunge wapya mwaka 2010, tulitumia fursa hii kujifunza na ninaamini tusingepata watu wazoefu kama ninyi tusingeweza kuwa bora kama tulivyofikia leo hii.

Mheshimiwa Spika, jana kwa nafasi yangu kama Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, niliwasilisha Taarifa ya Kamati yangu kuhusiana na Wizara yetu ya Kisekta. Taarifa ile kwa kiasi kikubwa ilielezea mambo yaliyo katika changamoto kwenye Serikali. Tungeweza kueleza mambo mengi ya fursa zilizopo, mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji kwa kipindi kilichopita, lakini tulionelea kwa sababu muda ni mdogo, basi angalau tu-focus kwenye changamoto ili zifanyiwe kazi. Tungetaka kuelezea mambo yaliyofanyika ni mengi sana, Taarifa ile ingekuwa kubwa kweli; kwa sababu tungeanza kwenye mambo ya barabara tungeeleza kilomita zaidi ya 13,000 za lami zilizoengwa katika kipindi cha miaka kumi ya Utawala wa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete.

Nitumie fursa hii kumpongeza kwa jitihada hizo. Naipongeza pia Serikali nzima kwa kufanya kazi kubwa ya kumsaidia Rais kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Nimegusia barabara, lakini pia umeme, Nzega kuna vijiji vilikuwa havina umeme, leo hii zaidi ya vijiji 40 vinawaka taa. Hayo yote ni mafanikio. Mimi ningekuwa sina cha kueleza kama Serikali hii ingekuwa imechoka na haifanyi mambo kama ambavyo ilisemwa hapa jana. Naomba niseme kwamba, kitu chochote kile hata kikiwa kizuri namna gani, hakiwezi kukosa kasoro, kitakuwa na upungufu wake na sisi kwenye taarifa yetu kwa jana tuliambia kuelezea changamoto zilizopo, kubwa ikiwa ni mapato na namna ya kubana matumizi kwenye Serikali. *(Makofi)*

Haimaanishi kwamba tuli-dismiss na kutupilia mbali kwamba Serikali yote haifanyi kazi au imechoka ama vipi. Ninaomba niliweke sawa hilo ili watu wasiendelee kuninukuu vibaya, kwa

sababu tulichokifanya sisi kwenye Taarifa yetu ni ku-address changamoto chache ambazo tuliamua kuziweka wazi mbele ya Bunge na Jamhuri watu watusikie kama mfano.

Bila kusahau ninaomba nielezee na niwashukuru kwa dhati kwa niaba ya Kamati yangu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri wa Mkuu (TAMISEMI) na Naibu Mawaziri wake, pamoja na Waziri Mkuu mwenyewe Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI, wamekuwa wakitupa ushirikiano wa hali ya juu. Bila wao tusingeweza kufanya kazi nzuri tuliyoifanya ya kuisimamia Serikali na pengine tusingekuwa na mambo mazuri ya kueleza hapa Bungeni kama tulivyoeleza jana. (Makofi)

Ninaomba tuwape heshima yao na sifa zinazostahiki. Wanasema *give the devil his credit where it is due*. Ninawapongeza sana Waheshimiwa. (Makofi)

Wabunge wengi hapa wamekuwa wakinifuata mimi kama Mwenyekiti wa TAMISEMI, kuniomba nitumie *influence* yangu kidogo niliyonayo, kushawishi baadhi ya mambo yafanyike kwenye Majimbo yao. Sasa kama Waziri Mkuu ambaye ndiye mwenye dhamana na Mawaziri wake hao wangukuwa siyo wasikivu, wangukuwa siyo waelewa, wangukuwa wamechoka kama ilivyokuwa inaelezwa hapa jana, nisingeweza kutatua migogoro ambayo ilikuwepo kwenye Majimbo ya Waheshimiwa ambao walikuwa wananiletea mimi kama Mwenyekiti wa TAMISEMI ambaye ni Mbunge mwenza.

Mheshimiwa Spika, ninaomba tujadili upungufu kwenye Serikali kama upungufu, lakini tusijaribu hata kidogo kutumia changamoto ambazo sisi tumezieleza kwenye Taarifa yetu kama kigezo kwamba, basi na mimi nina-endorse huo upupu ambao umekuwa ukisemwa hapa kuwa Serikali imechoka; ni mambo ambayo siwezi kukubaliana nayo.

Mimi kama Mwenyekiti, nimesoma Maoni ya Kamati na kwenye Kamati kulikuwa kuna Wabunge wengi zaidi wa CCM kuliko Wabunge wa upande wa pili; hivyo, tuliyoaandika yale tulikubaliana sisi kama Wajumbe wa Kamati na hivyo, mimi nililazimika tu kusoma maoni ya Wajumbe wenzangu. Kwa mfano, Wabunge wa *Opposition* ndiyo waliokuwa wengi zaidi ambao mimi katika miaka hii ya Utumishi kwenye Kamati, waliokuja kunifikishia matatizo ya kwenye Majimbo yao na tukayashughulikia. Sasa mimi ningeyashughulikiaje maana sipo kwenye Serikali mimi na Kamati yangu?

Mheshimiwa Spika, ni lazima aidha nimwone Waziri wa Nchi au nimwone Waziri Mkuu na wao washawishike na ushawishi ambao mimi kama Mwenyekiti wa Kamati ninaupeleka kwao. Mgogoro wa Ilemela, Mheshimiwa Kiwia angekuwepo ange-*testify*. Mgogoro wa Arusha kote huko kuna Wabunge wa *Opposition* na migogoro yote tumeishughulikia kwenye Kamati yetu kwa weledi wa hali ya juu na bila kuangalia vyama. Tumeishughulikia kwa masilahi ya Umma na Mawaziri hawa wakiongozwa na Waziri Mkuu, wameipatia ufumbuzi migogoro hiyo, leo hii hakuna migogoro tena. (Makofi)

Juzi tumetatua mgogoro wa Diwani wa CUF kule Urambo Kaliua. Diwani yule ni wa CUF, Mbunge aliyelalamika kwetu ni Mbunge wa CUF, lakini tumeusikiliza na sisi tumeshauriana na Mawaziri wametusikia na wameutatua. Sasa leo Bungeni hapa mnakuja mnawasema tena mnasema Mawaziri hawa ni wachovu, sijui Serikali imechoka, hapana hiyo siyo haki, tuwape haki yao pale ambapo wamefanya mazuri. Kwa sababu changamoto zipo tu hata kama ninyi mkipata fursa mkaingia kwenye Serikali mtaendelea kupopolewa mawe tu. Ninajua hilo jambo liko mbali sana kutokea lakini linaweza kutokea. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa kama linaweza kutokea na ninyi mkawa kule, hata ninyi hamtakuwa *perfect* mtakuwa na upungufu vilevile na huo upungufu utasemwa na watu. Sasa

tuseme ule upungufu, lakini pia tusingahau mazuri tuliyofanyiwa kwenye Utumishi wetu. Kwa sababu wewe Mbunge wa CUF au wa CHADEMA, kwenye Jimbo lako kuna tatizo unalitatuaje wewe haupo kwenye Serikali? Wanatatua matatizo hayo ni wale wenye dhamana, sasa hao hao wenye dhamana unasema wamechoka, wakati miaka mitano yote ya Ubunge wako umekuwa ukipeleka matatizo ya Jimbo lako kwa hao hao na wameyatatua! (Makofi)

Ninataka tutumie lugha yenye staha tunapotaka ku-*point out* upungufu kwenye Serikali yetu. Hilo nimeliweka sawa.

Nilitaka kuweka sawa jambo lingine kwamba, Taarifa ile siyo ya Kigwangalla na wala sikulenga kuitoa kwa sababu ya harakati zangu za kutafuta Urais, hapana. Wajumbe wa Kamati wasingekubali, Taarifa sijaiandika mimi, Taarifa imepitishwa na Kamati, imekubaliwa na Kamati. Maana tume-*pinpoint* mambo ya muhimu na tuliangalia zaidi upande wa changamoto hususan kwenye ukusanyaji wa mapato na kwenye kubana matumizi; na ndiyo maana ikaleta mambo yale ya kupunguza *size* ya Serikali, kwa sababu kama una Serikali kubwa ni jambo la wazi tu kuwa ni lazima utafute namna ya kupunguza *size* ya Serikali ili upunguze matumizi na mwisho wa siku u-*direct* pesa nyingi zaidi kwenye Miradi ya Maendeleo. Hiyo ndiyo kazi tuliyofanya kwenye Kamati yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hata kwenye Halmashauri tumeshawishi sisi na Serikali imekubali, imetoa *circular* kwenye Halmashauri zote nchini kwamba, zile pesa zinazopatikana kwenye makusanyo ya ndani pale *locally* kwenye Halmashauri, badala ya zote kutumika kwenye *other charges* kama ilivyokuwa zamani na kubakisha 21% tu kwenye Miradi ya Maendeleo, tumepindua shilingi tumesema 60% ya pesa zinazokusanywa kutoka kwenye mapato ya ndani ndiyo ielekezwe kwenye Miradi ya Maendeleo, 10% kwenye Mfuko wa Vijana na Wanawake na 30% inayobaki ndiyo ielekezwe kwenye matumizi mengine ambayo siyo matumizi ya Miradi ya Maendeleo. Tumetaka kila mwaka walete taarifa kwanza kwenye Wizara yenyewe, lakini pia kwetu sisi kwenye Kamati tunapokuja kufanya uchambuzi wa Taarifa zao au bajeti zao. Vilevile kila siku tumekuwa tukikagua kwa miaka yote miwili na nusu iliyopita.

Sasa utaona hapo tulichokuwa tunakifanya sisi katika miaka hii miwili na nusu ni ku-*address* tatizo kwamba, tunapata wapi pesa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kwa mfano, Mradi mdogo mdogo pale kwenye Jimbo labda wa kuchonga barabara tu kwenye eneo ambalo halina barabara hauhitaji mabilioni ya fedha, hauhitaji tusingu ruzuku kutoka Serikali Kuu, Halmashauri yenyewe inaweza kutekeleza. Mradi wa Kuchimba Kisima, Mradi wa Kujenga Zahanati, unahitaji labda milioni 20 tu ujenge maabara, pesa zile zinapatikana kwenye *collection* za ndani pale pale kwenye Halmashauri.

Kwa hiyo, sisi tulichokifanya ni kuwasaidia kwamba, wa-*block* 60% ya pesa zao kwenye *collections* zao palepale kwenye Miradi ya Maendeleo ili hizo fedha zitumike kwenda kutekeleza mambo madogo madogo ambayo yanawagusa wananchi moja kwa moja na siyo mambo *complicated* sana. Kwa hiyo, ukiona tulivyokuwa tunafanya kazi ndiyo tumefanya kazi katika misingi hiyo.

Nitumie fursa hii kuwashukuru sana Wananchi wa Jimbo la Nzega, juzi nilikuwa kule nimewahutubia kwa hiyo nimewaeleza tuliyoyafanya, sina haja ya kuyasema hapa Bungeni. Tumefanya mambo mengi, tumejenga barabara ya lami kutoka Nzega kwenda Tabora, umeme kupeleka mpaka Ndala, zaidi ya kilomita 80 zina umeme sasa hivi, vijiji zaidi ya 40 vinapata umeme, tumechimba visima zaidi ya 70. Mambo mengi tumeyafanya katika kipindi hiki cha miaka mitano. Hayo mambo sikufanya mimi Mbunge imefanya Serikali. Mimi kazi

yangu ni ushawishi tu, mtu atawadanganya Mbunge kajenga kisima, Mbunge unachimbaje kisima, unajengaje barabara? *(Makofi)*

Mbunge huna pesa, Mbunge unashawishi ndiyo kazi unayofanya. Kwa hiyo, ukiona mambo yanafanyika kule Jimboni kwenye Halmashauri, ujue Mbunge yule ana ushawishi mkubwa kwa watu wa Serikali. Hii ndiyo maana mimi siwezi kuiita Serikali imechoka, kwa sababu kesho ninaenda kuwashawishi hao hao waniongezee umeme kwenye vijiji vingine, waniongezee kilomita za lami pale mjini maana sasa hivi tumekuwa Halmashauri ya Mji.

Mheshimiwa Spika, leo hii kuna Wabunge wengi wamekuja hapa wana maombi wapate Wilaya, wapate Majimbo, wapate Halmashauri ya Mji na mimi huyu huyu nimeyapeleka kwa hao hao Serikali na wamesaidiwa. Wengine mwezi wa saba zinaanza. Sasa hatuwezi kusema Serikali imechoka katika misingi hii. Serikali hii ina Viongozi ambao wanasikiliza na wanafanyia kazi mambo wanayopelekewa. Isingekuwa hivyo, haya mambo yote ambayo tumekuwa tukiyafanya yasingetokea, kwa sababu mimi kama Mbunge ningeweza vipi kufanya mambo yote?

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Sasa namwita Mheshimiwa Victor Mwambalaswa!

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa wasaa huu na mimi niweze kuchangia kwenye hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza, ninataka kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi; mimi niliugua bega liliharibika, ofisi yako imenitibu. Mimi toka nizaliwe kulala hospitali ilikuwa ni mara ya pili, lakini wanasema hujafa hujaumbika, bega limewekwa vitu vya ajabu lakini nimepona niko tayari kuitumikia nchi. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Pili, ninamshukuru sana Waziri Mkuu, Mawaziri wote na Wabunge wenzangu, tume-survive as a Bunge miaka mitano, siyo jambo dogo hili ni jambo kubwa sana, lazima tumshukuru Mungu kwa hili. Vijembe vyote tunavyopigana lakini tumeishi kama Bunge kuishauri Serikali kwa miaka mitano, ni lazima tumshukuru Mungu sana ametuwezeshwa.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Wabunge ni kuishauri na kuisimamia Serikali. Mimi sipendi sana Wabunge kujibizana Bungeni, lakini kwa hili ambalo limenikuta mimi jina langu limesemwa ninaomba niliseme. Mbunge mwenzangu wa Chama changu ametamka jina langu kwamba, kwa nini Mwambalaswa aliondolewa kuwa Mwenyekiti? Mimi siwezi kupingana na Azimio la Bunge, wala sihitaji kutetewa na wala sijitetei.

Ninarudia, sipingani na Azimio la Bunge, sihitaji kutetewa na wala sijitetei. Niliwajibika kikawaida kisiasa kwa sababu mimi nilikuwa Mjumbe wa Bodi ya TANESCO. Siku Bodi ilipokaa mimi sikuwepo, lakini walisema nilikuwepo mimi nimenyamaza; kwa hiyo, sijitetei na sihitaji kusafishwa kwa sababu sina tope, sijapelekwa kwenye Tume yoyote na wala kwenye Kamati yoyote, nimewajibika kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unajua bahati mbaya tu nilikuwa Mjumbe wa Bodi ya TANESCO, Bodi ya TRA na Bodi ya Ununuzi. Sasa wanadamu wanasema aah, Bodi zote zina akili! Mimi ndiyo nilikuwa mlengwa, hawa Wenyeviti wenzangu wawili niliwaponza mimi.

Mheshimiwa Spika, nimeliweka sawa hilo.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii niishukuru timu ya Jimbo langu la Lupa, Timu ya Maendeleo, Mwenyekiti wa Wilaya - Bwana Deusdedit Kinawiro, Mkurugenzi wa Wilaya na Madiwani wenzangu wote, tumeishi miaka mitano hii tukipeperusha Ilani ya CCM kuwaletea wananchi maendeleo. Ninawashukuru sana, tumekuwa timu nzuri sana ya ushindi na tumefanya makubwa mengi sana, tumeisimamia Serikali imejenga barabara ya lami kutoka Mbeya mpaka Chunya na itaelekea Makongolosi, tumeisimamia Serikali ya CCM.

Ninawasihi Wananchi wa Chunya hasa Vijiji vya Chalangwa, Isenyela na Mbugani hata Chunya Mjini, nilipokuwa ninaomba barabara niliwaambia jamani neema zinakuja na tabu; sasa barabara imekuja ya lami, magari yanateleza hatuyasikii, tuna vifo vingi sana. Niliwaambia Wananchi wa Chunya ninaomba tuwe waangalifu sana, tumepata neema sasa hivi tunakwenda Mbeya kwa shilingi 3,000 badala ya shilingi 10,000, tunasafirisha mazao yetu yanakwenda sokoni kwa bei rahisi, lakini vifo ni vingi, naomba tujiangalie sana Wananchi wa Wilaya ya Chunya.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa barabara imefika Chunya, ninaiomba Serikali sasa itoke Chunya kwenda Makongorosi na baadaye itoke Makongorosi kwenda Singida kama ilivyo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Tumefanya kazi na Madiwani wangu pamoja na Mkurugenzi, tumepeleka fedha za ukarabati kwenye shule za msingi zote kwenye Jimbo, aidha kutoka kwenye Mfuko wa Jimbo au mfukoni mwa Mbunge mwenyewe, ninyi Madiwani mmesimamia, ninawashukuru sana.

Tumepeleka umeme kwenye sekondari zote Jimboni kwangu. Kwa fedha za Mbunge mwenyewe tumeamua watoto wetu wa sekondari wafanye *prepo* jioni, tumepeleka umeme kwenye shule zote za sekondari. Shule za sekondari sita zimepata umeme, zimebaki mbili ambazo ziko nje ya gridi, nako tutapeleka. Ninawashukuru sana Madiwani, mmefanya kazi kubwa sana.

Tumechimba visima vya maji vingi kwa fedha za Serikali, fedha za Mfuko wa Jimbo au fedha za Mbunge mwenyewe. Tumechimba visima vingi sana, ninawashukuru sana Madiwani wenzangu, tumefanya kazi kubwa sana. Ninaomba msife moyo, tuendelee kuchapa kazi hii.

Serikali imetusaidia kupitia Wakala wa Umeme Vijijini, umeme umefika Lupa na mwaka huu utafika mpaka Matwiga kupitia Isangawana na vijiji vyote vya Kata ya Mtanila vitapata umeme. Umeme utakwenda Mapogoro mwaka huu, Serikali hii ya CCM, umeme utatoka Sangambi kwenda Igundu na Godima, umeme utatoka Mlima Njiwa kwenda Ifumbo, Serikali hii ya CCM tunayoisema na ninyi Madiwani wenzangu tumechapa kazi kubwa sana, ninawashukuru sana. Tujipange vizuri, tuwaambie wananchi wetu CCM imefanya haya na inaomba ridhaa tena iendelee kutenda hayo ambayo imeyatenda. *(Makofi)*

Kiongozi wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alionyesha nia ya kutaka kuugawa Mkoa wa Mbeya uwe Mikoa miwili. Mheshimiwa Waziri Mkuu nawe umekuja ziarani, pamoja na kwamba nilikuwa nina maumivu bega lilikuwa linauma lakini nilikuja kuunga mkono na wewe ukaonyesha hiyo nia unayo. Kwamba, salama ya kuugawa Mkoa wa Mbeya kwanza ni lazima uigawe Wilaya ya Chunya. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba suala hili utakapokuwa unahitimisha utuambie kama Wananchi wa Chunya tutapata Wilaya mbili kama ulivyosema. Vilevile Waziri Mkuu utuambie Bajeti ya Wilaya hizo mpya mbili tayari ziko katika Bajeti ya TAMISEMI. Nitaomba ulete majibu hayo Mheshimiwa Waziri Mkuu, samahani sana.

Mheshimiwa Spika, Bunge hili mwaka 2013 lilibadilisha Sheria ya Ushirika na mabadiliko hayo yalilenga sana kuwasaidia Wakulima wa Tumbaku, wakulima ambao wako kwenye Ushirika wa Tumbaku. Katika kufanya hivyo, Bunge liliondoa ushiriki wa Appex kwenye

mchakato wa Tumbaku. Waliiondoa Appex Watu wa Morogoro kwamba, Ushirika wa Wilaya na Ushirika wa Vijijini uwe ndiyo unatosha.

Nia ya Bunge ilikuwa ni kutoa mzigo huu ambao walikuwa nao watu wa Appex. Fedha hizo au asilimia hizo ambazo zilikuwa zinakatwa wapelekewe wakulima, sasa huu ni mwaka wa pili mimi sijaona kama Wakulima wa Tumbaku kama hayo makato waliyokuwa wanakatwa na watu wa Appex wamerudishiwa wakulima. Ninaomba Mheshimiwa nipewe majibu hiyo fedha itakwenda lini kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kupitia Wizara ya Nishati na Madini, pamoja na kupeleka umeme Chunya kwenye vijiji vyote ambavyo nimevisema, imegawa maeneo ya uchimbaji ya wachimbaji wadogo wadogo sehemu za Itumbi na sehemu za Saza, toka mwaka juzi imetangaza nia ya kugawa, imetenga, lakini bado haijagawa. Ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja hapa Waziri wa Nishati, atuambie wachimbaji wadogo wadogo wa Chunya, maeneo ya Itumbi na maeneo ya Saza watapata lini?

Ninaomba niongelee Uwanja wa Ndege wa Songwe Mbeya. Uwanja ule ni wa muhimu sana kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na nchi za jirani.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefanya kazi nzuri, wengi wamechangia na muda umetumika vizuri, sasa nina tangazo dogo tu hapa. Katibu wa Wabunge wa Upinzani anaitwa David Silinde, anaomba niwatangazie Wabunge wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa, kutakuwa na kikao leo tarehe 13 Mei, 2015 kwenye Ukumbi wa Msekwa, baada ya kuahirishwa kwa Bunge mchana huu, maana yake sasa hivi, ninadhani taarifa itakwenda kwa wote.

Ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi jioni.

(Saa 8.00 mchana Bunge lilifungwa hadi saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Kidawa Hamid Saleh) Alikali Kiti

MWENYEKITI: Tunaendelea na mjadala. Mchangiaji wangu wa kwanza jioni hii atakuwa Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, atafuatiwa na Mheshimiwa Murtaza Ali Mangungu na Mheshimiwa Betty Machangu ajiandae.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii adimu ambayo nimepewa ili niweze kuchangia machache kuhusu hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *nina-declare interest*, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI na kwamba, tumekuwa tukipitia Mipango ya Ofisi ya Waziri Mkuu na pia Wizara ya TAMISEMI, Tawala za Mikoa na hata Halmashauri na Majiji mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa sasa tunatimiza miaka mitano na kwamba, ule Mpango tuliouanza mwaka 2011, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, tunatimiza kwenye kikao hiki, ningependa sana niishukuru Serikali na kuipongeza kwa kazi kubwa sana ambayo imeweza kuifanya juu ya maendeleo katika nchi hii.

Hakuna asiyeona kilichofanyika, kila mtu anaona, kwa hiyo basi ni budi kila mmoja aweze kushukuru. Kwa kuwa haiwezekani kila kilichopangwa kikatekelezwa, hata majumbani mwetu tunapanga mambo mengi, lakini ni machache tunayatekeleza, yale mengine yanayokuwa yanashindikana tuna-*carry forward* kuyapangia tena. Haiwezekani hata siku moja mtu kapanga mambo kumi na yote ukayatekeleza hata kama ungekuwa tajiri kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo kwa Waziri Mkuu, Manaibu wote, Katibu Mkuu na Watendaji wote katika Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, ningependa kuchangia machache katika kutoa ushauri.

Ushauri wangu ni kwamba, Mipango tunayokuwa tunaipanga, kwanza, najua *process* ya kupanga Mipango ni nzito sana, ambayo inajumuisha utumiaji wa akili sana katika kutambua matatizo na kuyawekea vipaumbele. Vipaumbele hivyo ambavyo ni *burning issues* ukilinganisha na pesa chache tunazozipata, kwa hiyo basi katika Mipango inayopangwa na Halmashauri na Serikali za Mikoa na hata Majiji, ni vizuri vinapokuwa vimewekea bajeti, basi pesa zinapokuwa zimetolewa na Hazina, utekelezaji ufanyike kulingana na vipaumbele kadiri vilivyopangwa.

Mara nyingi Halmashauri zimekuwa baada ya bajeti kupitishwa sasa kunaingia kazi nyingine ya kuhamisha mafungu kutoka vipaumbele hivi kwenda kutekeleza vipaumbele vingine ambavyo pengine vinakuwa havijapangiwa. Tunapoambiwa nidhamu ya matumizi, nidhamu ya matumizi pamoja na mengine ni pamoja na kuheshimu jinsi tulivyopanga pesa zikatumika kadiri ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mipango hiyo na baada ya Bunge kuidhinisha bajeti, tatizo linalofuatia ambalo pia limeonekana ni changamoto katika Halmashauri karibuni zote za nchi hii, hata Mikoa na hata Ofisi yenyewe ya Waziri Mkuu; changamoto zinazojitokeza ya kwanza ni ucheleweshaji wa fedha, mtiririko wa fedha kutoka Hazina kwenda kwenye Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa Mipango.

Tumeona hata Ofisi ya Waziri Mkuu nao wanalalamika kwamba, pesa hazitolewi au hazifikishwi kunakohusika mapema, wakati mwingine pesa zinazoombwa siyo zote zinazopelekwa, zinapelekwa kidogo na wakati mwingine pesa hazitolewi kabisa. Kwa mfano, Mkoa wa Rukwa tumewasikia wakisema kwamba, kuna wakati mwingine pesa wanazozomba zinakuwa hazifiki. Sasa kama pesa hazifiki, tunategemea ule Mpango au vile vipaumbele vitatekelezwa namna gani?

Ninatoa ushauri Serikali izingatie mtiririko wa utoaji wa fedha kulingana na Mipango. Tunaamini kuwa Mipango hii ni ya wananchi, sasa pesa zinapokuwa hazijatolewa ni kwamba, tunawanyima wananchi haki zao na hasa pale ambapo tunakuwa tumewashirikisha katika kutambua matatizo na katika kupanga Mipango yao, Mipango Shirikishi na kuwekea bajeti. Tusipowapelekea pesa, tunawanyima haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu kucheleweshwa kwa fedha kwenda kwenye Halmashauri, kunasababisha madeni ya aina mbalimbali. Wazabuni ndiyo wanaathirika sana kwa kutopelekwa fedha huko. Wazabuni wanakuwa hawana fedha, kwa hiyo, utakuta shughuli za kifisi na hata katika sekondari zetu masuala ya chakula na hata katika vituo vya afya na hospitali vyakula vinakuwa havipatikani. Wazabuni wanakuwa hawajapata pesa na kwa hiyo inaleta matatizo sana kwa walimu wanaoangalia wanafunzi katika shule za bwani.

Kuna sekondari moja nimewahi kwenda nikakuta walimu wanajichangisha mifukoni mwao. Uki-*imagine* walimu wanapata mishahara midogo sana, lakini hawawezi kuvumilia kukaa na wanafunzi ambao wamekaa na njaa. Kwa hiyo, wanafika wanaanza kuhamasishana wenyewe kwa wenyewe wanachangishana, kwenda kununua pengine kiroba kimoja au kilo kumi za maharage ili shule nzima iweze kula. Ninatoa ushauri, Serikali tunapopanga hapa basi nayo itiririshe fedha kwenye Halmashauri na kwenye Mikoa kulingana na muda ulivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri za Mkoa wa Rukwa kipato chake kinategemea sana mauzo ya mahindi. Tuna vyanzo vingine lakini zaidi sana tunategemea mahindi. Sasa nilikuwa najaribu kumkumbusha Waziri wa Kilimo kwamba, msimu wa mavuno kwetu Rukwa unafahamika kabisa, kwa hiyo, ingekuwa bora wakala anaye-*supply* magunia kwa ajili ya kuweka mahindi tayari kwa kuuzwa, awe anaharakisha asicheleweshe.

Magunia yanapokuwa yamekwenda, wananchi au wakulima wakaweka mahindi hayo kwenye yale magunia, basi *NFRA* wajitahidi kwenda kununua hayo mahindi haraka ili wananchi waweze kupata pesa za kuweza kutumia majumbani mwao, waweze kulipia ada za watoto wao mashuleni na waweze kusafirisha watoto wao kwenda mashuleni haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NFRA* inapokuwa imenunua mahindi haipeleki ushuru kwa Halmashauri kama inavyotakiwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa kengele ya pili.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Murtaza Mangungu. Mheshimiwa Betty Machangu ajiandae na Mheshimiwa Clara Mwatuka. Namwita Mheshimiwa Betty Machangu!

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri ya kusimamia shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na Dar es Salaam. Naongea kwa uchungu mkubwa kwa sababu Dar es Salaam limekuwa kama Jiji la mateso hasa kipindi hiki cha mvua. Ukitoka Mjini saa kumi unafika nyumbani kwako tuseme pale Mbezi Beach saa nne usiku na maji yameingia kwenye makazi ya watu kwa sababu mitaro haizibuliwi.

Ninasikitika 2012 au 2013 barabara wanayoita ya Mwai Kibaki, walimkabidhi Rais wa Mkenya wakati huo na Mwai Kibaki akasema lolote la hii barabara basi niambieni. Kama kweli

haitakuwa ni aibu kwao basi wamdai hela ya kuzibua mitaro. Kwa sababu ni kitu cha ajabu, wangoje mpaka Mheshimiwa Rais aende kwenye maeneo akaseme zibueni mitaro ni mambo ya aibu. Kwa nini mitaro haizibuliwi halafu unaona Mameya wanapeana zawadi? Inasikitisha sana, kweli tunahitaji tufanye kazi zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee kuhusu vyama vya upande wa pili. Nilikuwa nafuatilia sana uchaguzi wa Uingereza juzi hapa. Chama cha Labor ambacho ni cha Upinzani, yule Miliband chama kilishindwa na haraka sana akajiuzulu. Chama cha Liberal Democrats hivyo hivyo, haraka sana wale viongozi wakajiuzulu. Huku kwetu vyama vinashindwa lakini ni wao wao kila wakati. Naomba *Chief Whip* wetu atufafanulie pengine siasa sijui, inakuwaje huku kwetu vyama vinashindwa lakini watu hao hao wanaendelea miaka nenda miaka rudi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikichangia sasa Hotuba ya Bajeti, naomba nianze na ulinzi na usalama. Zipo ajali zimetokea 8,072 katika mwaka 2014/15. Ajali hizi zimeleta vifo 2,882 na majeruhi 9,570. Hizi ni roho za watu na inavyoelekea ni kweli ndiyo Serikali inajitahidi, lakini ninaomba nishauri mambo madhubuti ambayo naona kama yatasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, wakati *accidents* nyingi zimetokea, Chuo cha Usafirishaji kimesema katika wale madereva wote hakuna hata anayeonekana anaweza kupeleka mabasi masafa marefu. Maana yake ni kwamba, hiki Chuo tunaweza kuwafanya wao ndiyo watahini madereva watakaokuwa wanaendesha mabasi yanayokwenda safari za mbali. Kwa hiyo, SUMATRA au Serikali niseme wawape nafasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa madereva wapimwe macho kila mwaka, inawezekana wengine hawaoni vizuri. Namba za simu za SUMATRA na za Ofisi za Usalama Barabarani ziadikwe kwenye mabasi kwa herufi kubwa, kiasi mtu akikaa kwenye kiti aweze kusoma na ampigie *traffic* yeyote aliyeko njiani. Waweke kule mbele na waweke ubavuni abiria wasome. Abiria wengine wanaogopa kusema, kwa hiyo, naomba zikiwekwa vizuri wataandika meseji au watapiga na haya mabasi yataenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba kondakta atakapokuwa anatangaza sasa tunaondoka, atangaze fungeni mkanda na atangaze namba hizi za hao Maofisa ziko ubavuni na kule mbele. Kubwa kabisa, hawa madereva wapewe Mikataba ya Kudumu. Serikali isimamie wapewe Mikataba ya Kudumu. Hawa wanaofanya biashara za mabasi ni biashara nzuri, biashara kubwa, zina pesa nyingi; kwa nini wasiwape mikataba ya kudumu hawa madereva na wao wakaweza kujikimu na familia zao? Kwa hiyo, Serikali isimamie wapate Mikataba ya Kudumu na isimamiwe na Wanasheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Vitambulisho vya Taifa. Inaonekana kama sasa hivi Vitambulisho vya Taifa siyo *priority* sana. Mimi nasema pengine vingekuwepo Vitambulisho vya Taifa hata hii BVR tunayohangaika nayo sasa hivi isingekuwa ya moto moto namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ione umuhimu wa kuendelea na ajenda ya Vitambulisho vya Taifa. Kule Kigoma sasa hivi ninavyoongea, wakimbizi wameshafika 50,000. Tunavyoendelea wataongezeka zaidi na sisi tunaenda kwenye uchaguzi, hakuna Vitambulisho vya Taifa, mwisho wa siku watajiandikisha wapige kura. Naomba Serikali ilianganalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye maendeleo ya sekta binafsi. Sekta binafsi inalalamika kwamba Serikali haiwatunzi ipasavyo. Ukiangalia tuna viwanda 51 hapa nchini, lakini *impact* ya vile viwanda huioni, kwa sababu mali nyingi zinaletwa kutoka nje ya nchi ambazo hata *quality* yake ni mbaya zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa kama sukari, sementi, nguo na mafuta ya kula, zinaagizwa nje zinashindana na viwanda vyetu vya ndani. Tunahitaji kulinda viwanda vyetu vya ndani.

Viwanda vyetu vya ndani watozwe kodi kidogo. Zile mali zinazotoka nje kodi iwe kubwa la sivyo hatuwezi kuwa na ajira. Tuisahau kwamba, tunataka kulinda viwanda hivi kwa sababu ya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye uzalishaji mali. Sera ya Taifa ya Kilimo ya 2013 ya Azimio la KILIMO KWANZA, Programu ya Kuendeleza Umwagiliaji na BRN zote zimeleta matunda mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuisahau mabadiliko ya tabia nchi yanakuja kwa spidi. Kuna mtaalamu mmoja anasema yanakuja kwa spidi kuliko UKIMWI. Sasa kilimo bila umwagiliaji tutakuwa tunajidanganya. Je, Serikali inafanya nini kutengeneza mikakati ya kuweka kilimo cha umwagiliaji?

Ipo miundombinu kama kule Kilimanjaro kuna mradi unaitwa Lower Moshi, ulitengenezwa mwaka 1984, wenye hekta 23,000, ukiwa unalisha watu 3,700. Ninavyoongea ni hekta 700 zinatumiwa zinazolisha watu 1,500, kwa sababu miundombinu ile imechakaa. Je, Programu kama hizi mahali pengine popote Serikali inafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee elimu. Naishukuru Serikali kwa kufanya vizuri kwenye elimu ya awali, msingi na sekondari. Tunajenga maabara takribani elfu kumi, maabara haya lazima yawe na *re-agency* kwa ajili ya kufanya *practicals* za *chemistry*, biolojia na fizikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri Mkuu afafanue, je, fedha itakayokuwa inatumika kununulia vifaa vya maabara ni ileile ya *capitation* au ni bajeti nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko ya shule za bweni kutokuwa na chakula. Watu wa hali ya hewa wametangaza kutakuwa na ukame hasa Mikoa ya Kati. Serikali imejipangaje kuhakikisha kunapatikana chakula cha kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa watumishi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Serikali imetoa kibali Halmashauri za Wilaya ziajiri Watendaji wa Vijiji, wa kumbukumbu na wengine. Hata Watendaji wa Kata ni kada ndogo. Unamtoa Mtendaji wa Kata kule Tunduru unampeleka Arusha, gharama yote hiyo ya nini? Wapewe Halmashauri ya Wilaya waajiri na Watendaji wa Kata, *then* ile *level* ya Wilaya ndiyo Serikali iandae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Huvisa, Mheshimiwa Clara Mwatuka ajiandae na Mheshimiwa Paresso ajiandae.

MHE. DKT. TEREZYA P. L. HUVISA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kukushukuru binafsi kwa kunipa nafasi hii. Namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya na kuniwezesha kusimama mahali hapa ili niweze kuchangia bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa uongozi mzuri, pamoja na Mawaziri wote ambao wako chini yake, kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mimi nianze moja kwa moja na Sekta ya Kilimo. Pamoja na Sera nzuri ya Serikali kuanzisha Mpango wa KILIMO KWANZA na wakulima wengi wameitikia Mpango huu, lakini suala la pembejeo bado ni tatizo. Unakuta wakulima wengi wa Vijijini wanahangaika kutafuta mbolea, mbegu na pembejeo nyingine zinazohusika na wakulima hao. Kwa hiyo, naomba Serikali iendelee kuboresha na kuweka mikakati mizuri ili wakulima waweze kupata pembejeo kwa wakati na za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za mabadiliko ya tabia nchi sasa hivi zinajidhihirisha. Matatizo yote yanayotokana na kukosekana na mvua, lakini pia mvua zinazokuja zinakuwa na athari kubwa, mafuriko pia na maradhi. Naomba bajeti hii itenge fedha kwa ajili ya kuelimisha wananchi athari hizo ili waweze kuelewa na wajue njia gani wanaweza kuzitumia kujikinga na athari hizo. Vilevile naomba Serikali iwaelimishe wananchi wapande mazao yanayoweza kukomaa mapema ili tusipate matatizo ya njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu hifadhi ya chakula. Naipongeza Serikali kwa kuiongeza uwezo NFRA, kwa kununua mazao ya chakula. Kutokana na mwitikio wa KILIMO KWANZA, msimu uliopita mazao ya chakula yalikuwa mengi sana kule Songea, Mbozi na maeneo mengine, hivyo, NFRA haikuweza kununua mazao yote hayo, lakini hata yale ambayo yamechukuliwa, bado wakulima wengi hawajalipwa. Nichukue fursa hii kuiomba Serikali ilipe fedha hizo, lakini pia bajeti hii iweze kutenga hela za kutosha kuweza kununua mazao mengi zaidi msimu ujao ili tuwe na akiba ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue fursa hii pia kuipongeza Serikali kwa kuendeleza ujenzi wa maghala pamoja na vihenge vya kisasa. Kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu imesema kabisa kuna maghala yanajengwa huko Mbozi na Songea. Maghala haya yakikamilika na hivi vihenge, vitaweza kuhifadhi mazao ya chakula mengi zaidi. Ninaomba bajeti hii ya Serikali iweze kutenga fedha za kutosha ili kujenga hivyo vihenge pamoja na maghala haya na kuwezesha kuweka chakula cha kutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uwezeshaji, pamoja na kwamba, Serikali imeweka mpango mzuri, lakini bado wananchi wengi hawana habari na mambo ya uwezeshaji. Wengi hawajui wapi wataweza kupata hiyo mikopo nafuu, kwa hiyo, ninaiomba pia Serikali itoe elimu kwa wananchi hususan vijana. Kwa upande wa Vyuo Vikuu, ningeomba kabla wanafunzi hawajamaliza muda wao wa masomo, waweze kuipata hiyo elimu wakiwa kule kusudi wanapotoka tu badala ya kuzagaa mitaani, wapate fursa ya kujiunga katika vikundi na kupata hizi pesa za mkopo nafuu kwa ajili ya kujiwezesha wenyewe na kufanya Miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sekta ya Elimu, ninaishukuru Serikali kwa kuongeza Vyuo Vikuu toka Vyuo 23 mpaka 49. Kuwepo kwa Vyuo hivi maana yake kudahili wanafunzi wengi zaidi, tatizo kubwa linakuwa kwenye mikopo. Mimi ninaiomba Serikali kupitia bajeti hii, itenge fedha za kutosha ili wanafunzi hawa wasipate matatizo mengi wakati wa masomo, kwa sababu unakuta migomo mingi inaanzishwa hasa wanafunzi wanapokosa mikopo. Kwa hiyo, ninaomba bajeti hii izingatie, iweke fedha za kutosha kwa ajili ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu ili waweze kupata pesa na waweze kusoma bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamezungumzwa na kwa sababu nimeona sina haja ya kurudia, naomba niishie hapa na ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nimemwita Mheshimiwa Clara Mwatuka, Mheshimiwa Cecilia Paresso ajiandae na Mheshimiwa Ezekiel Maige ajiandae!

MHE. CLARA D. MWATUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia walau kidogo katika zoezi lililopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko napenda niseme kwamba, hali iliyopo hapa ndani ukweli hairidhishi, kwa sababu inaonekana tunafanya *debate*. Mashuleni zamani wanafunzi walikuwa wanaweka kitu wanashindanisha hiki na hiki kipi bora, hawa wanasema hiki bora na hawa wanasema hiki bora na kurudishiana maneno na nini, ndivyo tunavyofanya hapa! Hapa tunapeana vijembe badala ya kwenda kwenye mambo ambayo yameletwa mbele yetu tuyafanyie kazi. Kuna hali ya mtu kujaminisha Bunge lijalo nitarudi, hayo tumwachie Mungu, Mungu ndiye anayepanga mambo yote. Hivi sasa watu wanapishana vibega, wanapigana vikumbo, wale ambao wanategemea kugombea Jimbo moja, sivyo! Mimi niachie mambo kama yalivyo na ninawaomba wenzangu tuachane na hayo, twende kwenye njia ambayo ipo wazi na siyo za michepuko, tukiacha ile michepuko ya bwana nani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi juu ya suala la marekebisho ya Katiba, kwa sababu ilisemwa kwamba uchaguzi utafanyika kwa kutumia Katiba iliyopo, lakini Bunge litafanyia marekebisho. Mpaka hivi sasa naona uchaguzi unakaribia, marekebisho sijui yatafanyika lini na Bunge ndiyo hivi karibu mwezi wa sita linamaliza muda wake tunaondoka. Bunge hilo litakalofanya marekebisho ni lipi na ni lini?

Nilitaka nifahamu hilo kwa nia njema tu, maana hivi sasa Katiba ndiyo hiyo ambayo watu tunapigiana vikumbo, hii lazima itapita, mwingine haipiti, itapita inayopendekezwa; jamani siyo kazi yetu sisi ni kazi ya Mungu, tumwachie yeye ndiye mpangaji wa mambo yote. Wengine tunafikia kukasirikiana, wengine tunacharurana kupita mpaka, siyo kazi yetu! Kwa hiyo, ningepomba hivi sasa tujue kwamba, mambo ya Katiba tuyaache kama yalivyo, yatapelekwa kadiri Mungu alivyopanga na anavyotaka, ni yeye hakuna wa kumbishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika Mipango ya Serikali. Serikali yetu kwa kawaida inajua kubuni Mipango mingi na mizuri, lakini tunakosea kitu kimoja kwamba, inatakiwa kuwa na Mipango shirikishi, lile linakosekana. Kwamba, hatushirikishi wanaohusika kwenye Mipango ambayo inapangwa. Kwa mfano, ulipotolewa Mpango wa Stakabadhi Ghalani, wananchi waliambiwa tu, uliitishwa mkutano vijijini, kule viongozi walika wakapanga kutakuwa na Mpango wa Stakabadhi Ghalani, itakuwa hivi na hivi, wakapewa watu kazi ya kwenda kuwaelimisha wananchi, kuwaambia siyo kuwaelimisha.

Walipofika kule waliambiwa kama amri, walipojaribu kukataa mfumo huo hautapendeza wakaambiwa mtake msitake hilo litakuwa. Matokeo yake ndiyo haya ambayo tumekwenda mpaka hivi sasa mambo hayaendi sawa, zimekuja kuzaliwa tozo nyingi ambazo zinawakamua wananchi na kuwadhulumu na kufanya mali ambazo zinafanyiwa tozo siyo za kwao. Ulikosekana nini? Ushirikishwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna Mradi wa Maabara ambao Rais ameuleta, ni mpango mzuri. Utaratibu wa maabara mashuleni, kwa kweli unapendeza kwa sababu wanafunzi wanapata mambo yote, wanajifunza kwa nadharia na kwa vitendo hasa masomo ya sayansi. Yeye alikurupuka na kutangaza kuwaambia Wakurugenzi kwamba, ni lazima wajenge maabara kila shule sijui mbili, tatu, lakini nyenzo hakuwapa. Sasa kutokana na hali ile, Mkurugenzi anajua yupo chini ya Rais na inabidi atekeleze lile ambalo ameambiwa, matokeo yake wengine wamekwenda kuchangisha wananchi kwa ajili ya ujenzi ule na wengine wakaogopa kuwachangisha wananchi, wakaamua kuchukua pesa za Halmashauri ambazo walishapangia Miradi yao tayari na kufanya Miradi yao mingine ife ili watekeleze kutimiza amri ya Mkuu.

Nitolee mfano kwangu Masasi, kijiji changu au vijiji vingi vilikuwa na Miradi ya Maji, lilipokuja suala hili sehemu zingine kama Kijiji cha Nanganga au Kata ya Nanganga walishaandaa, mabomba walishaweka tayari yalikamilika, lakini maji hayawezi kupatikana kwa sababu pesa hakuna, zimekwenda wapi, zimekwenda kwenye maabara! Sehemu zingine wameshindwa hata pa kupata pesa za kuendeleza Mradi wa Maabara, wamekwenda kuchukua madarasa ambayo hayatumiki yaliwekwa akiba kwa madarasa yajayo yamekuwa ndiyo maabara. Sasa hali kama hii pangukuwa na ushirikiano kule mwanzo, wangeshirikishwa wananchi, lingekwenda polepole lingepita vizuri tu, lakini sasa limekwenda limekuwa kero. Kwa hiyo, kuwashirikisha watendaji ni vizuri zaidi kuliko kuingia tu ghafla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie masuala ya afya au matibabu. Wabunge tumepata utaratibu wa Jubilee ambao tunatibiwa, Serikali au Bunge linalipa, lakini mpango huu haujakamilika. Kutokamilika kwake ni hivi; wengine mikoani tuliko huko, hospitali zilizopo kule ni zile za hali ya chini, hata Bima ya Afya imepokelewa hivi karibuni tu, sasa tunapowapelekea kadi hizi za Jubilee hawazijui, kwa hiyo tunakosa kupata matibabu kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimekwenda pale Muhimbili ambapo wanashughulikia meno na matibabu mengine, wakasema sisi hatuna hiyo, hatujui na hatupokei. Nimepata hasara nikatibiwa na wakati huo huo nikitibiwa nikileta risiti hapa Jubilee sirejeshewi, tunapewa tu *blah blah!* Sasa mipango mingine hii naona iangaliwe na nina imani kwamba, kama utaratibu huu ulishapangwa, kuna kiwango maalum ambacho Mbunge amepangiwa kwamba atibiwe kwa kiasi fulani. Inawezekana mwingine haumwi mpaka anamaliza muda wake na zile pesa zimeshakwenda, badala ya kurudishiwa mwenyewe kwamba pamoja hukuumwa hela zako ulizokadiriwa upewe kwa matibabu ni hizi hatupewi, linapata tu shirika lile au sijui kampuni; ni hivyo! Kwa hiyo, mambo haya yarekebishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mambo ya mirathi kwa watumishi ni mtihani. Watumishi wanatambulika tu wakiwa kazini, wakishakufa kama hawana ndugu wa kusimamia kufuatilia mirathi zao wanakosa. Mimi hapa nilizungumzia siku za nyuma juu ya marehemu fulani ambao walikosa msaada wakakimbilia kwangu kama Mbunge wao, nikafikisha kwa Naibu Waziri hapa Mheshimiwa Majaliwa, akaniambia niletee kumbukumbu zake, nikamletea fomu zake ambazo zilijazwa vizuri nikamkabidhi, ooh nitazishughulikia kimya! Nikamkumbusha tena, nitashughulikia kimya mpaka mtoto aliyeachwa akiwa darasa la kwanza hivi sasa yupo *form four*, kwa tabu tu. Sasa kitu kama hiki jamani, tunawadhulumu waliotumikia nchi hii halafu mafao yao yasipatikane. Serikali iliingalie hilo, wajaliwe hawa, haiwezekani kwamba kumbukumbu zao hatuna, jamaa zao hawajulikani, siyo kweli! Naomba liangaliwe sana hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kuna suala la Walimu ambao wengi wanalilia, ukweli bado hawa watu wanastahili kupewa haki zao wanazohitaji. Usipomtimizia mtu yale anayoyataka au ambayo ni haki yake, hafanyi kazi ile kwa moyo. Tunalalamika watoto hawafaulu mitihani na nini, Mwalimu anakwenda kufundisha wengine hawafundishi wanasema hatupewi.

Nitatoa mfano mmoja Masasi kuna shule moja inaitwa Sabasaba, nimetembelea siku mbili ninakuta Walimu wamekaa tu. Mwalimu Mkuu amekwenda kusoma, wale wa chini wamekaa tu wanajua hakuna wa kuwapigia kelele. Kulingana na hali ilivyo, hawaipendi hiyo kazi, wanafanya kama lazima kwa sababu imebidi. Tujaribu kuwatimizia hawa waipende kazi yao ili pawepo na ufanisi, maana hata sisi hapa tunalalamika tusipopata, jamani bado kule, jamani hawajaingiza na hawa vilevile wanataka wapate haki zao. Wengine wanakaa mbali na Mji, sasa yale marupurupu ya kuwafanya wasahau kule kukaa maporini hawapati, hali inakuwa ngumu, wanafikia mahali wakitoka basi wanajongomea. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Nimemwita Mheshimiwa Paresso, atafuatiwa na Mheshimiwa Maige, Mheshimiwa Innocent Kalogeris na Mheshimiwa Dunstan Mkapa wajiandae.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Awali ya yote, nimpongeze na kuunga mkono Hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na niseme kwamba, tunajadili Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, bajeti ya mwisho kwa Serikali ya Awamu ya Nne. Mara zote katika hii miaka mitano ambayo tunamaliza kama Kambi ya Upinzani kupitia Msemaji wetu Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mbowe, tumetimiza wajibu wetu wa kuishauri Serikali kupitia Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshauri mambo mengi kuhusiana na huduma zote za kijamii ikiwemo elimu, afya, maji, masuala ya barabara, masuala ya kilimo, mifugo, ardhi na kadhalika. Mara nyingi tumetoa ushauri na hatujawahi kuona ushauri wetu ukichukuliwa na Serikali na kutekelezwa. Matokeo yake, yale yote ambayo tumekuwa tukiyashauri ama tunapuuzwa, yanabezwa au tunapewa kejeli eti tu kwa sababu ni Wapinzani, eti tu kwa sababu ninyi mnajiita ni Serikali sikivu mnaongoza nchi hii kwa sasa miaka 53 baada ya Uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshauri, tumetimiza wajibu wetu ndani ya Bunge na nje ya Bunge. Tumewaambia Watanzania ni kwa nini leo wapo hapo walipo, ni kwa nini leo Watanzania wakienda hospitalini hakuna dawa, ni kwa nini Watanzania leo hawana uhakika wa kupata maji safi, ni kwa nini Watanzania leo baadhi ya maeneo barabara hazipitiki. Tumewaambia Watanzania pia ni kwa nini wanakumbana na migogoro mbalimbali ya ardhi katika maeneo yao. Tumewaeleza na kuwaambia Watanzania hayo wanayokutana nayo kama changamoto ni kwa sababu ya Serikali inayojiita sikivu imeshindwa kutimiza wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali yoyote ni lazima ikusanye kodi kupitia vyanzo mbalimbali ili iweze kutimiza mambo ya msingi ambayo yanamgusa mwananchi. Mmekusanya kodi kwa miaka yote toka tumepata Uhuru nchi hii, mmeiongoza Serikali hii, lakini hatujaona kinachofanyika. Hatujaona kwa maana ya kodi mnazozikusanya kupitia vyanzo mbalimbali haviendani na maendeleo tuliyonayo leo. Mtakataa lakini huo ndiyo ukweli. Mtakataa mtabeza kama ambavyo mmefanya miaka yote mitano, leo tunamaliza uongozi wenu wa Serikali wa Awamu ya Nne inaisha, mtabeza na kukejeli na kukataa lakini ndiyo ukweli. Mnapokea kodi, mnakusanya kodi, kwa sababu ndiyo wajibu wa Serikali lakini maendeleo hayaendani na kasi iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge hili na Watanzania ambao wanatusikiliza, tunawaambia Watanzania kwa makundi yote, vijana ambao wanateseka kwa namna moja ama nyingine kwa kukosa ajira, akina mama ambao hawajui masuala yao ya kiuchumi, masuala ya huduma za afya, wakienda zahanati wanajifungua kwenye mazingira mabovu, kuna vifo vingi vya akina mama kutokana na uzazi, tunawaambia wazee wa nchi hii ambao walipaswa wapate pesheni lakini hawaipati, wazee hao ni hazina ya nchi hii ambao walipaswa wahudumiwe na Serikali hii, tunawaambia makundi mbalimbali ya kijamii kwamba, wakati wa kuondokana na adha walizozipata miaka yote ni mwaka huu na wanaondokana na hayo ikifika wakati wa kwenda kupiga kura. *(Makofi)*

Tumezoea tukisema na tukiwaambia ukweli huwa mnabeza na kukejeli, lakini tunaamini Watanzania wanatusikia kwamba, kama mnaona changamoto zote hizi sasa ifike wakati wa

kwenda kuondokana na changamoto zilizopo, kwenda kutumia haki yako ya kikatiba ya kuchagua viongozi wengine wa kuunda Serikali nyingine, tujumzishe Serikali ambayo imetuongoza kwa miaka 53 tujaribu na Serikali nyingine nayo iongoze nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewashauri kuhusu mambo kadha wa kadha ikiwemo suala la matumizi makubwa ya kodi ambazo zinalipwa na wananchi, matumizi mabaya, tumeshuhudia ufisadi, wizi, kutokuwajibika kwa Watumishi wa Serikali na Viongozi wa Kiasia na tumeshuhudia mambo kadha wa kadha. Tumewashauri mara nyingi ifike wakati kama mmeshindwa mlishaambiwa mmechoka kaeni pembeni ipisheni Serikali nyingine nayo ijaribu kuiongoza nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la uwajibikaji, kupitia Bunge hilihili kulikuwa kuna Azimio kuhusiana na sakata la Escrow. Baadhi ya Viongozi wa Kiasia wakawajibika na Watendaji wengine wakawajibika, lakini leo baadhi ya Watendaji na Viongozi wa Kiasia wanasafishwa na wengine wanaachwa! Ameongea vizuri sana Mheshimiwa Serukamba asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kufikiri zaidi ya hapa, Bunge ni chombo ambacho kinaisimamia na kuishauri Serikali. Bunge lilipofikia Azimio lile la suala la sakata la Escrow, lilifikia kutokana na ushauri mbalimbali ikiwemo Taasisi ya Serikali kupitia Ofisi ya CAG kwamba, fedha kweli zimeibiwa, kuna watu wanapaswa kuwajibika na mambo chungu nzima ambayo CAG alitushauri na Bunge ndiyo tukafikia uamuzi huu.

Leo unaona Bunge limeazimia, Serikali inaenda kuwasafisha watu...

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza!

MWENYEKITI: Mheshimiwa ya pili.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza!

WABUNGE FULANI: Ya kwanza!

MWENYEKITI: Ooh, endelea!

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tumeshuhudia leo baadhi ya watu wanasafishwa na Serikali! Maana yake ni kwamba, tunakoenda maamuzi ya Bunge yatakuwa hayana maana yoyote, kwa sababu inaonekana kuna kushindana kati ya Mhimili wa Serikali na Mhimili wa Bunge. Bunge limeazimia, limetoa mapendekezo, Serikali inaenda kuwasafisha watu wengine; maana yake Maazimio yaliyotolewa na Bunge hayaheshimiwi, yanadharauliwa! Tunakoenda Bunge litakosa maana, Bunge litakuwa siyo chombo tena cha kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana kama Viongozi wa Bunge hili mkasimamia haya na Serikali mkaionya, kama Bunge limeazimia ni kutoa Maazimio kwa nia ya kuishauri na kuisimamia Serikali, Maazimio yale yaheshimiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala lingine kuhusiana na matumizi makubwa ya Serikali. Ukichukulia suala moja tu la Sherehe za Kitaifa; tumeshuhudia Sherehe za Kitaifa ni nyingi sana na kila Sherehe lazima iadhimishwe. Tumeona juzi, mfano mmojawapo labda ije Sherehe ya Muungano, sijui mambo mengi ya Wafanyakazi, lakini tunaona gharama hizo za kuendesha hizo Sherehe za Kitaifa ni nyingi sana. *T-Shirts* zinaprintiwa, kofia, miamvuli, unaona Taasisi za Serikali eti zinampongeza Rais, Waziri Mkuu, Makamu wa Rais, kupitia matangazo mbalimbali kwenye gazeti; huu utamaduni utakwisha lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaona Taasisi moja inatumia labda nusu *page* na nusu *page* kutangaza kwenye gazeti moja ni kati ya shilingi 1,180,000 mpaka 1,470,000. Inaonekana ni hela ndogo, lakini hiyo ni Taasisi moja. Tuna Taasisi nyingi sana na Taasisi zote ikifika kama ni Sherehe ya Muungano wote wanampongeza Rais, ikifika Siku ya Wafanyakazi wote wanampongeza Rais; kwa nini huu utamaduni usikome? Wanampongeza Rais ili kiwe nini wakati ni wajibu wake? *(Makofi)*

Kwa nini hata siku moja isitokee basi Ofisi ya Rais kwa maana ya Taasisi ya Rais, yenyewe ndiyo itoe labda tangazo kwa niaba ya Wafanyakazi wote? Kwa nini hizi Tasisi zote zinatumia fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike wakati huu utamaduni ufe. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Nimekwita Mheshimiwa Maige, anafuatiwa na Mheshimiwa Kalogeris!

MHE. EZEKIEL G. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza, naomba niipongeze sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo imefanya katika kipindi cha miaka mitano hii tunayoimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ambayo tumeyafanya katika kipindi hiki yanaonekana kila mahali. Maeneo ambayo yalikuwa nyuma sana kama Jimbo la Msalala, kwa dhahiri kabisa watu wanaweza wakashuhudia kuna kazi kubwa imefanyika. Yako maeneo ambayo hatukuwa na barabara, sasa hivi barabara zipo. Yako maeneo ambayo tulikuwa hatujawahi kuota tutakuja kuona nguzo za umeme leo tunashuhudia. Yapo maeneo ambayo tulikuwa tunasikia tu kwenye vyombo vya habari kwamba, wanakunywa maji ya bomba leo kuna maeneo hayo huko kwetu wanakunywa maji. Yako maeneo ambayo wananchi wengi walikuwa wanasikia tu kwamba, kuna vituo vya afya watu wanakwenda wanafanyiwa huduma za upasuaji, leo huduma hiyo inapatikana. Yako maeneo ambayo tulikuwa tunawabeba wagonjwa kwenye machela kuwapeleka hospitali, leo *ambulance* zipo. Kwa ujumla, kazi kubwa sana imefanyika na ninaipongeza sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, niseme kwamba, kwa maoni yangu, nadhani tunakuwa *too ambitious* katika kuweka Mipango yetu. Kwa sababu, kuna baadhi ya maeneo ambayo inaonekana dhahiri kabisa kwamba, uwezo wa kifedha wa Serikali siyo mkubwa kihivyo na hivyo tunajikuta tunapata shida kuyatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kama ambavyo taarifa za Serikali zinaonesha, fedha ambazo zimetoka Hazina kwenda kwenye Halmashauri na Mikoa, fedha kwa ajili ya Miradi ni chini ya 30% na fedha kwa ajili ya matumizi (OC) haizidi 70%. Kwa hiyo, ukiangalia wastani ni kama 60% hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama bajeti ya Serikali kwa mfano ya huu mwaka tunaoumaliza, ilikuwa ni kama trilioni 20 na fedha zilizotoka ni kama 60%, maana yake fedha zilizokusanywa na kutumika kiuhalisia ni kama trilioni 16. Sasa bajeti ambayo tunategemea mwaka huu tunaouanza imependekezwa na Serikali, nilisikia kwenye semina pale Ukumbi wa *Julius Nyerere International Conference Centre* kwamba, tunategemea kuwa na bajeti ya trilioni kama 22. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, uwezo halisi wa Serikali ni kukusanya trilioni 16. Kwa hiyo, tunapoweka lengo la trilioni 22, tunakwenda kuahidi Miradi fulani fulani itatekelezwa na mwisho wa yote inakuja kushindikana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kuishauri Serikali, katika mazingira ya namna hii inapotokea, basi walau tuwe na uwazi. Kwa mfano, Wananchi wa Kagongwa Isaka, tuliwaahidi watapatiwa maji ya bomba kwa kuunganisha na Mradi mkubwa wa kutoka Ziwa Viktoria hadi Kahama. Kwenye Bajeti ya Serikali hii tunayoimaliza, tulitenga shilingi bilioni nane kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huo na baada ya bajeti hiyo kupitishwa, Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja akafanya mkutano Isaka, akawahakikishia wananchi kwamba, mara moja fedha zikitoka utekelezaji utaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ni mwezi Mei, bado mwezi mmoja tu wa fedha, fedha ambazo Mamlaka ya Maji Safi na Salama ya Shinyanga (*KASHUWASA*) wamepelekewa, hazizidi milioni 400 kwa ajili ya Mradi huo. Ina maana katika bilioni nane, bado zaidi ya bilioni 7,600,000,000 hazijatoka na sidhani kama zinaweza kutoka katika kipindi cha mwezi mmoja uliobaki. Kwa hiyo, dhahiri kabisa unaona Mradi huu unaweza usitekelezwe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingefaa sana zingetoka taarifa za wazi kwamba, kuna tatizo gani lililotokea, ili tuwaeleze wananchi kwamba, imeshindikana kutekelezwa kwa kipindi hiki, kwa sababu moja, mbili, tatu, ili baadaye tuweze kuwatekelezea. Juzi nilipokuwa Isaka nilipokuwa naongea nao waliniambia kwamba, Maige tunakupenda na unafanya kazi nzuri na tunafikiria namna gani tuweze kuchukua hatua kwa wale waliotudanganya. Aliyetudanganya tumeshuhudia ni Waziri mwenyewe, kwa sababu Mheshimiwa Makalla ndiyo aliyekuja hapa! Sasa hebu tusaidie tutamwadhhibuje Mheshimiwa Makalla au Mheshimiwa Profesa Maghembe?

Nikasema cha muhimu tunahitaji sisi wenyewe tuelewe hali ilivyo na ikiwezekana tutake majibu kutoka kwa Waziri.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana kwamba, Mradi huu Serikali wakati inakuja kujumuisha, kwa maana ya Waziri wa Maji, atueleze ni tatizo gani hasa ambalo lipo? Najua ni fedha, lakini fedha kwa maana gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa Mradi mwingine, mwaka juzi tulikataa Bajeti ya Wizara ya Maji na Serikali ilipokwenda kufanya marekebisho iliongeza bilioni 84 na tukaongeza idadi ya vijiji ambavyo vingeanishwa na bomba kuu la kutoka Mwanza au kutoka Ziwa Viktoria kuja Kahama. Jimbo la Msalala likawa na Vijiji 22 ambavyo vingepata maji. Pamoja na kurekebisha bajeti hiyo na kuongezwa bilioni 84, hadi hivi sasa Vijiji katika vile 22 vya Jimbo la Msalala ni Vijiji vitatu tu ambavyo vimeunganishwa, ina maana bado Vijiji 19 na muda unakwisha! Ukiuliza, unaambiwa uongee na Katibu Mkuu, uongee na Waziri mwenyewe, inafika mahali mpaka Mawaziri wanasema bwana tunaomba utusaidie au mtusaidie ninyi kama Wabunge kusema jamani fedha Hazina hazitoki! Kwa hiyo, naomba sana Miradi hii inayochelewa kwa sababu hizi za fedha ambazo wananchi hawaelezwi vizuri, ni vizuri sababu zikatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ahadi za Rais; mara nyingi Mheshimiwa Rais amekuwa akitoa ahadi, lakini utekelezaji wake umekuwa ukichelewa sana. Kipekee sana, nianze kwa kushukuru sana hatua ambazo zilichukuliwa na Serikali na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, mama yangu Mama Mhagama, tulipopata matatizo pale Mwakata, Mheshimiwa Rais na Serikali ilikuja na hatua ambazo zilichukuliwa za dharura, zimewapa matumaini sana wananchi. Hivi tunavyoongea, toka tatizo lilivyotokea, hapajatokea tatizo la uhaba wa chakula. Leo nimeongea na Mkuu wa Wilaya anasema chakula ambacho amewapa wananchi wale kinawapeleka hadi tarehe 15 mwezi Juni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo la kuanza utekelezaji wa ahadi ya Rais ya kujenga zile nyumba 403 ambazo ziliharibiwa na mvua. Kwa bahati mbaya wananchi hawa wamekuwa wakiishi kwenye mahema toka wakati huo na mahema kama unavyojua, kwa sisi ambao hatujawahi kuwa wakimbizi, kwa taarifa ambazo wananchi wale wanasema ni kwamba, yana ubaridi sana nyakati za usiku na wakati wa mchana yanakuwa na joto sana. Kimsingi, siyo maeneo au siyo vifaa ambavyo vimetengenezwa kwa ajili ya matumizi ya kudumu ya wananchi. Kwa hiyo, naomba utekelezaji wa ahadi ya Rais ya kwamba, Jeshi la Wananchi au JKT watafika Mwakata kwa ajili ya kujenga hizi nyumba, uanze mara moja. Ahadi hii ilitoka katika mazingira ya dharura, tunategemea utekelezaji wake utafanyika katika mazingira yaleyale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ahadi ya kujenga Chuo cha Ufundi kwenye eneo la Bugarama. Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye kampeni mwaka 2010 kwenye Uwanja wa Halmashauri pale Kahama mwezi Oktoba, aliahidi kwamba, Serikali itasaidia au itatekeleza ahadi hii ya kujenga Chuo cha Ufundi VETA kwenye eneo ambalo wananchi walikuwa wamekwisha kutenga. Mpaka hivi sasa hatua ambazo zimechukuliwa na Serikali kwa wananchi wa kawaida hawaoni. Kwa hiyo, naomba sana hii ahadi nayo iweze kukamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la matumizi au usimamizi mbaya wa Miradi. Kuna Miradi ambayo imetengelezwa, lakini usimamizi wake umekuwa mbaya. Kuna Mradi wa Umwagiliaji wa Kahanga pamoja na Skimu ya Umwagiliaji ya Chela, Miradi hii imetengelezwa na ninaambiwa zaidi ya milioni 700 zimetumika, lakini ukiangalia hali halisi kwenye *ground* hakuna kilichofanyika!

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliongea na Naibu Waziri Zamboni muda fulani mchana huu akasema atafuatilia. Naomba kumkumbusha na atoe majibu hadharani, amechukua hatua gani kwa wasimamizi wa Miradi hiyo, ili kuweza kuona Miradi hiyo inakamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna Mradi wa Maji wa eneo la Kagongwa pamoja na Chela, ambao ni Mradi wa vile Vijiji 10 vya kila Halmashauri au kila Wilaya. Mradi huu wa Kagongwa baada ya kuwa umetengenezwa na maji yamepatikana, baada ya muda mfupi kisima kikakauka, kwa sasahivi yamebaki matenki na mabomba yasiyo na maji. Tunaomba Waziri wa Maji ajaribu kufuatilia na kuchukua hatua zinazostahili, ili kuona wananchi wanapata maji kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ninalotaka kuzungumzia, kuna mvutano unaotaka kujitokeza baina ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala na Halmashauri ya Nyang'hwale kuhusu ushuru wa huduma kutoka Mgodini wa Bulyanhulu. Mgodini wa Bulyanhulu uko katika Wilaya ya Kahama, lakini uchimbaji wake kwa mujibu wa leseni yao unagusa sehemu ya Wilaya ya Nyang'hwale. Wenzetu wa Nyang'hwale wamekuwa wakidai walipwe ushuru wa huduma, jambo ambalo wamelianza hivi majuzi baada ya kuomba na kuibana Serikali ikawabana wakarekebisha Mkataba. Miaka yote walikuwa wanalipa dola laki mbili na

hatukupata mzozo kutoka kwa wenzetu wa Geita, lakini baada ya kuwa tumerekebishiwa Mkataba na sasa wanalipa Service Levy, kumeanza kujitokeza kwamba, tugawane jambo hili, ambalo kimsingi sisi hatuna tatizo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoomba kama Wananchi wa Kahama ni kwamba, Serikali ije kwenye *ground* waweze kuangalia mipaka halisi na uchimbaji ambapo umefikia, ili kujiridhisha kama kweli sasa hivi uchimbaji unafanyika kwenye eneo la Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Nimekwita Mheshimiwa Kalogeris, Mheshimiwa Dunstan Mkapa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Haji Kombo!

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kubwa zaidi na mimi nitoe pongezi kwa Serikali kwa kazi nzuri ambayo imefanyika katika kipindi cha miaka mitano. Vilevile nitumie nafasi hii kutoa pongezi kwa Mwenyekiti wangu wa Halmashauri ya Morogoro Vijijini na Baraza zima la Madiwani la Wilaya ya Morogoro pamoja na Watendaji, kwa kazi kubwa ambayo tumeifanya wote katika kipindi cha miaka mitano katika kuleta maendeleo kwa watu wa Wilaya ya Morogoro na hususan Jimbo la Morogoro Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuwapongeza Wanajimbo wote wa Morogoro Kusini, kwa ushirikiano mkubwa ambao wamenipa katika kipindi cha miaka mitano katika kusaidiana kuleta maendeleo. Najua tumejenga nyumba za Walimu, tumejenga barabara, tumejenga maabara, tumejenga zahanati na mambo kadha wa kadha. Kubwa zaidi, haya yote yamepatikana katika ushirikiano ambao tulikuwa tumeuleta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, nitumie nafasi hii na mimi kuipongeza TAMISEMI na Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kutuleta hoja ambayo iko mbele yetu. Ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake nzima, umesikia kilio cha Wabunge, wengi wamepiga kelele hapa wakilia; ni ukweli usiofichika, yako mambo ambayo Serikali inatakiwa kuyafanyia kazi. Ombi langu kwako; la kwanza, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kweli Bunge tulipitisha bajeti katika Bunge lililopita na tulitarajia hicho tulichopitisha kitoke na kiende kwenye Mawizara na kwenye Halmashauri, kikafanye kazi ya kuleta maendeleo. Hadi tunaingia katika kipindi hiki cha bajeti, kinachoonekana ni 60% tu ndiyo imefika. Hiki ni kielelezo tosha kwamba, tunachokipitisha kama hakifiki kinatuvunja Wabunge, kinawavunja wananchi, kiasi ambacho tunaona wenzetu wengine humu wanapiga kelele humu eti CCM na Serikali yake imechoka iende nje. *(Makofi)*

Nataka nikwambie kwamba, Serikali ya CCM hajichoka. Mimi ningependa tu Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe ukiwa kama Mtendaji Mkuu wa Serikali Bungeni, wakati unakuja na majibu yako hebu tueleze Wabunge, waeleze wananchi, ni sababu zipi ambazo zimefikia au zimefanya Serikali ishindwe kutimiza majukumu yake wakati tunaelekea katika kipindi hiki cha bajeti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama mzazi, kama Serikali, ukiwaeleza wananchi, lakini kubwa zaidi ukitueleza sisi Wabunge, ninaamini hata katika bajeti za Wizara nyingine zinazokuja, kutakuwa na uhalisia au kutakuwa na hali ambayo itawafanya Wabunge wakajua wasichachamae zaidi, upo uwezekano wa Serikali ilikwama kwa sababu moja au sababu nyingine. Kwa hiyo, utaweka utaratibu ambao utatufanya tuendeleo kuamini Serikali yetu.

Baada ya pongezi, naomba na mimi niunge mkono hoja ambayo iko mbele yetu. Kubwa zaidi, niambie Serikali yangu, kwa sababu hii bajeti inakwisha, tunaunda bajeti nyingine na katika kipindi hiki ndiyo tunapoandaa maandalizi ya kufanikisha mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la elimu Serikali imefanya vizuri sana na katika Halmashauri yangu imefanya vizuri zaidi. Tumefanya mambo makubwa kama nilivyosema, ujenzi wa madarasa, ujenzi wa nyumba za Walimu na kadha wa kadha. Serikali iliendelea kutupa Walimu wa Msingi na Sekondari, ambalo ndiyo lilikuwa tatizo kubwa katika Halmashauri zetu katika upande wa Elimu. Kwenye Halmashauri yangu, katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo tulipata Walimu, lakini katika mwaka huu hatukupata Walimu! Katika orodha na mahitaji halisi ya Walimu katika Wilaya ya Morogoro Vijijini, tulitakiwa tuwe na Walimu 1,806, hadi sasa hivi tuna Walimu 1,324, tuna upungufu wa Walimu 535. Nikuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, nikuombe kupitia Wizara ya Elimu, tunaomba Walimu waje Morogoro Vijijini. Kwa sababu ndani ya Morogoro Vijijini kuna shule ina Mwalimu mmoja, kuna shule ina Walimu wawili, kiasi ambacho tunadororesha masomo na elimu kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande huo wa elimu tuna tatizo kubwa la malipo ya likizo ya Walimu, malipo kwa ajili ya *transfer* ya Walimu na Wastaafu. Ndani ya Halmashauri yetu tuna deni la zaidi ya milioni 120, ambalo limefikia hapa Watumishi hawa wa Idara mbalimbali wanataka kuishitaki Halmashauri yetu Mahakamani. Kwa hiyo, niombe tu Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunawaomba mtusaidie jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye upande wa afya tumefanya mambo makubwa. Kwenye Halmashauri yangu sasa hivi Hospitali zote na Vituo vyote vya Afya, vina majengo ya *Theatre Room*. Kwa hiyo, akina mama na watoto, tunaamini vifo vyao vitakuwa vimepungua. Tunachokuomba kitu kimoja Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna jambo ambalo linatusumbua sisi Wananchi wa Wilaya ya Morogoro Vijijini; kuna *tendency* ya kuwahamisha Watendaji, tena bahati mbaya Watendaji wazuri ambao wanatusaidia Halmashauri mnawaondoa! Juzi ameondolewa Mganga Mkuu wa Wilaya ambaye anafanya kazi nzuri ya kutusaidia. Anaondolewa analetwa Daktari mwingine ambaye hatumjui, kiasi ambacho mnatuvunja nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili linaenda sambamba, tuliondolewa juzi tu Afisa Mipango mzuri ameondoka. Tumeletewa mwingine, kuna misigano isiyo na kichwa wala mguu, kiasi ambacho nikuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu utusaidie.

Halmashauri yetu ya Morogoro Vijijini, tulikuwa na Hati Chafu mfululizo ndani ya kipindi cha miaka minne, lakini baada ya kupata Watendaji na sisi wenyewe kusimama imara kama Madiwani, Halmashauri yetu imepata Hati Safi. Leo hii kutuondolea Watumishi ni kutufanya turudi kulekule tulikotoka. Nikuombe katika hili, najua tunakwenda kwenye kuvunja Bunge, tunakwenda kwenye kuvunja Baraza la Madiwani, lakini nataka nikuthibitishie kwa baraka za Mwenyezi Mungu tutarudi. Tungependa Halmashauri yetu wasihamishwe Watendaji na kutuletea Watendaji wabovu. Tubakie na watendaji wale wale ambao tunaamini watatuvusha katika kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, kwenye maji naipongeza Serikali, muda mwingi nilikuwa napiga kelele fidia kwa wananchi wa Bwawa la Kidunda, wananchi wangu wamelipwa. Sambamba hilo kulikuwepo na matatizo madogo madogo, niliomba Serikali na Serikali imeleta watu kutathmini upya au kuhakiki. Sambamba na hili, naomba baada ya uhakiki wananchi watakaonekana fidia yao ilikuwa siyo stahiki, waletewe fedha na wapewe.

Nawaomba watu wa DAWASA ambao ndiyo wenye Mradi, Halmashauri tumewakabidhi watujenge majengo ya kijamii, basi majengo haya yakamilike kwa haraka ambayo ni shule, zahanati na nyumba za Ibada. Wananchi wako tayari kwenda kule na wameshakabidhiwa viwanja, tungependa waende kule na waweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili katika maji kupitia Mradi wa Vijiji Kumi wa World Bank, tunaomba fedha ikamilike au iwepo kwa ajili ya kuwalipa wakandarasi waweze kumaliza.

Siwezi kuzungumza bila kutaja migogoro ya wakulima na wafugaji. Mkoa wa Morogoro umeendelea kuwa kimbilio la wafugaji na kuondokana na dhana ya Mkoa wa Morogoro kuwa Ghala la Taifa la Chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Serikali itakapokuja kutoa majibu yake, itupe majibu imejiandaa vipi kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji na vilevile kuondoa vifo visivyo vya lazima vya makundi yote haya mawili.

Ndani ya Bunge hili tumeunda Tume mbili; ya Tokomeza ninaamini imekuja na majibu na tuliunda Tume ambayo iliongozwa na kaka yangu Ole-Sendeka, ilikuja na majibu ya kuishauri Serikali katika maeneo ya mashamba pori, katika maeneo ambayo kulikuwa na mapori ya akiba. Serikali iamue sasa iyatoe mapori ya akiba ambayo hayaendelezwi na mashamba pori ambayo hayaendelezwi, ili wakulima waende wakalime na wafugaji waende wakafuge tuondokane na migogoro isiyo na kichwa wala mguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Serikali kwa upande wa umeme, Morogoro Vijijini ilikuwa ni hadithi kwa wananchi kuona umeme, lakini ndani ya kipindi cha miaka mitano kama Mbunge umeme umewaka na sasa hivi nguzo kupitia REA zimeshafika mpaka Kisaki, zinakwenda mpaka Singisa na zinakwenda mpaka Bwakila Juu. Kinachonipa mashaka kama Mbunge wao, sioni kuvutwa waya. Mimi ni fundi umeme, ndani ya mkataba tumeambiwa tarehe 30 Juni umeme utawaka, ningepomba Serikali inapokuja inithibitishie na Wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini, kuona kwamba kweli umeme utawaka kama mkataba wa mkandarasi unavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la Halmashauri kuhamia Mvuha. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilikuja mimi, DC, Mwenyekiti wangu wa Halmashauri na Mkurugenzi, tulikwambia ili tuweze kuleta maendeleo ya haraka kwa Wananchi wa Morogoro Kusini na Wilaya ya Morogoro lazima tuhamie Mvuha. Kuendelea kubaki Morogoro Mjini wakati sisi Halmashauri yetu inatakiwa tuwepo vijijini, tunaendelea kupoteza pesa nyingi kwenye vikao bila sababu za msingi. Ulituahidi na ulimwambia Mkurugenzi wako, twende tukaangalie na tufanye tathmini, tumekwenda tumeangalia kuna maeneo Mvuha yako majengo makubwa, ambayo tunaweza kuyageuza kuwa ofisi ya muda ya wilaya wakati tunajenga ofisi kubwa. Katika tathmini kinachoonekana tunahitaji hadi ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante, kengele ya pili.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Tunaomba tu Mheshimiwa tupate hiyo. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante sana. Nimekuita Mheshimiwa Dunstan Mkapa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Haji, Mheshimiwa Mangungu ajiandae, Mheshimiwa Mfutakamba ajiandae na Mheshimiwa Amina Amour ajiandae.

MHE. DUNSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza, naomba nitamke wazi kwamba, naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nanyumbu ina changamoto nyingi sana, lakini niishukuru Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kuweza kupunguza baadhi ya kero na matatizo mbalimbali ambayo yalikuwa yanaisibu Wilaya hii pamoja na wananchi wake.

Moja ya changamoto tuliyonayo ndani ya Wilaya ya Nanyumbu ni matatizo ya maji. Nashukuru Mradi wa Benki ya Dunia wa Vijiji Kumi umekamilika. Vilevile kulikuwa na ujenzi wa bwawa pale Sengenya, limeweza kupunguza baadhi ya kero za maji kwa Wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu. Kulikuwa kuna Mradi pale Nandembo umekamilika, nao pia umeweza kusaidia kupunguza kero hii ya maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipokuja Rais mwaka jana mwezi wa saba, nilimwomba anisaidie kupunguza kero ya maji katika Wilaya ya Nanyumbu. Nashukuru wito wangu umeitikiwa na sasa hivi Wizara ya Maji imeshatuma Wataalam kule, kuweza kuona ni jinsi gani wanaweza kutoa maji kutoka Mto Ruvuma. Mradi huu ulishapelekewa pesa za kuanzia, nadhani baada ya muda si mrefu, kwa sababu mhisani wa kutoa hizo pesa amepatikana, shughuli hii itaanza ndani ya muda mfupi ujao. Vijiji vingi vitanufaika katika Mradi huu wa Maji tokea pale Mtambaswala, Lukula, Masugulu, Chungu, Nanyumbu, Namasogo na Mangaka yenyewe Mjini, wataweza kunufaika na Mradi huu mkubwa wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tatizo la maji limebaki kwa baadhi ya vijiji; kwa mfano, Mkwajuni, Mnaratani, Nanderu, Makanya, Maneme, Mhinawe, Likokona, Michiga na Nangomba. Maeneo haya yana matatizo makubwa ya maji. Kwa hiyo, naomba Wizara husika pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, ione ni jinsi gani inaweza kutatua kero hii ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo kubwa kwa sababu tuna vituo vitatu tu vya afya na zahanati kumi na mbili. Ninaiomba Serikali ituongeze uwezo wa kuweza kujenga tena zahanati zingine ili kuweza kukidhi mahitaji ya Wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu. Ikumbukwe kwamba, Wilaya ya Nanyumbu ilikuwa ni uwanja wa vita wakati wa ukombozi Kusini mwa Afrika, kwa hiyo, miundombinu yake bado ni duni na wananchi bado wanateseka kupata huduma ya afya. Vilevile kuna uhaba wa madawa na uhaba wa watumishi. Wazee wa Wilaya ya Nanyumbu bado hawapati huduma kama maagizo yalivyotolewa kuhusu wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu, tumejitahidi kujenga sekondari, madarasa ya shule za msingi, nyumba za walimu na matundu ya choo, lakini bado kuna changamoto ambazo Wilaya ya Nanyumbu inazikabili kuhusiana na Sekta hii ya Elimu. Uhaba wa walimu, mgao huu wa juzi nategemea tutapunguza kero hii ya uhaba wa walimu.

Kuna shule kwa mfano za Chihuve, Nyangaramo pale na maeneo mengine ambayo walimu wake ni wachache sana, naomba mgao huu unaokuja maeneo haya yapate walimu wa kutosha. Kuna tatizo bado la madarasa na matundu ya choo ambayo yanawakabili wanafunzi wetu hasa shule za msingi. Kwa upande wa kilimo, sisi zao letu kubwa ni korosho, lakini kutokana na usumbufu wanaopata wakulima hasa bei kubwa ya pembejeo, tunalanguliwa sana kule pembejeo, bei ya *sulphur* ni kubwa sana, kwa hiyo, wakulima hawa

sasa hivi wamejikita kwenye mazao mengine mathalani ufuta, choroko, karanga na mbaazi. Changamoto kubwa ni kwamba, bado bei ya mazao haya ipo chini kiasi cha kumfanya mkulima asipate haki yake ambayo inatokana na jasho alilolitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ujenzi, hapa naomba niishukuru Serikali kwa sababu sasa hivi Wilaya ya Nanyumbu karibu itakuwa na mtandao mkubwa wa barabara za lami kuliko Wilaya nyingine yoyote ndani ya Mkoa wa Mtwara. Kuna barabara ya kutoka Masasi mpaka Mangaka, kuna barabara inajengwa kutoka Mtambaswala kuja Makanga na kuna barabara inajengwa kutoka Makanga kwenda Tunduru na nadhani hivi karibuni itanza kujengwa barabara ya kutoka Nangomba kwenda Nanyumbu. Kwa hiyo, hivi vyote kama vitakamilika, Wilaya ya Nanyumbu tutakuwa tumeendelea mbali sana. Bado kuna ukamilishaji wa Daraja la Mpombe kwenye Mto Mkwamba na tatizo lingine ni kulipa fidia, bado kuna watu wanadai fidia hawajalipwa ambao wamepisha ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme umeshafika Mangaka Makao Mkuu ya Wilaya. Vilevile Serikali imeweza kutupelekea umeme mpaka Mtambaswala pamoja na vijiji vyote vinavyopitiwa na umeme huo. Hata hivyo, Wizara haijakamilisha ahadi yake ya kutupatia vijiji 24 umeme katika Wilaya yetu ya Nanyumbu. Labda nimalizie kwa kutoa pongezi zangu kwa Mkuu wa Mkoa mpya, Mheshimiwa Halima Dendego, ambaye amehamishiwa hivi karibuni, ameanza vizuri na tunategemea atatusaidia sana kuinua hali ya uchumi katika Mkoa wetu wa Mtwara. Nakupa hongera sana Mheshimiwa Dendego. *(Makofi)*

Napenda kumkaribisha Mkuu wangu wa Wilaya, amekuja siku chache zilizopita, anaitwa Sauda Mtindoo, tunashirikiana naye vizuri na nadhani tutakutana baada ya Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za mwisho ni kwa Wapiga Kura wangu wa Wilaya ya Nanyumbu, nimeshirikiana nao vizuri, wamenilea nimewalea na nafikiri hawatanisahau tena awamu ijayo. Kuna watu wanajipitisha pitisha kule, lakini wao wasijali. Watu wana hela zao chafu wanazigawa kama pipi lakini wao wasijali, wajue mimi tumeleana kwa muda wa miaka kumi na nitaendelea kuwa nao mpaka pale watakaponiambia basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mkapa. Nilimwita Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, ajiandae Mheshimiwa Mangungu, Mheshimiwa Mfutakamba, Mheshimiwa Amina, Mheshimiwa Matiko na Mheshimiwa Zuberi!

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa sababu hii inawezekana ikawa nafasi yangu ya mwisho baada ya miaka mitano ndani ya Bunge, haitakuwa kitu cha busara kama kwanza sitawashukuru wale ambao walionileta hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Wananchi wa Jimbo la Chake Chake kwa imani yao kwangu. Namshukuru sana mke wangu ambaye alinisaidia sana mpaka nikawa Mbunge katika Jimbo la Chake Chake. Wale wengine wanaosema wake zangu walikuwa wanapiga dumba tu, tututu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mkuu wa Wilaya ambaye sasa amekuwa Mkuu wa Mkoa, Mkoa wa Kusini Pemba. Yeye ni M-CCM kweli kweli na akakutana na CUF kweli kweli, lakini bahati nzuri sana akatoa ushirikiano mkubwa sana na kwa sababu yeye ofisi yake iko katika Jimbo langu. Namshukuru kwa ushirikiano wake na kupeleka maendeleo katika Mji Mkuu wa Chake Chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri Mkuu nimwoneshe kidogo kwa nini tulisema tuwe na Serikali Tatu. Hotuba hii ya Waziri Mkuu yote inazungumzia ile nchi ambayo wamekubali wenyewe kuifuta iliyokuwa ikiitwa Tanganyika, sasa haipo tena. Kuna mambo mazuri tu ambayo Waziri Mkuu katika Taarifa yake kuanzia ukurasa 57 mpaka ukurasa wa 64, ambao unazungumzia sana maendeleo ya kiuchumi katika nchi hii ya Tanganyika. Kuna gesi asilia, kuna nishati, kuna huduma za mawasiliano na kuna huduma za mawasiliano. La kusitisha ni kwamba, hakutueleza sote tukafahamu waliipata vipi gesi asilia; ni kwamba, ulifanywa utafiti ndiyo ikaonekana na ndiyo tarajio kubwa la Tanganyika kwamba itasaidia sana kiuchumi. Ningelifurahi sana kwa sababu ni Waziri Mkuu wa Tanzania, angelieleza nini tatizo ambalo mpaka sasa wamelipata kutokufanya utafiti Zanzibar tukajua tuna kitu gani, hata Taarifa hii ya Miaka Mitano maskini ambayo tunaagana naye akatueleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiomba hilo kidogo Waziri Mkuu akirudi atueleze, ni Mjumbe wa Kamati nafurahi amefika atajua. Ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, natoa shukrani za dhati kabisa kwa Meneja au Mkuu wa Viwanja vya Ndege vya Tanzania, Engineer Selemani, kwa juhudi zake ambazo anafanya katika viwanja hivi. Tukiangalia Terminal III inayojengwa sasa, alipokuja kwenye Kamati yetu tukamshauri aiombe Serikali aweze kupata nafasi ya kuchukua mkopo CRDB na akafanya hivyo, anaendelea vizuri. Naomba sana Serikali iyasaidie haya mashirika ambayo yana matatizo, kuingia kwenye mikopo ili waweze kulipa baadaye lakini maendeleo yaonekane.

Naiomba sana Serikali kwa sababu sisi tunatembea sana kwenda kusoma nje nini wenzetu wanafanya, tuingie kwenye *privatization*, tusifikirie Serikali kila itajenga njia, barabara ya kutoka hapa mpaka Kilombero, ndiyo haya sasa matatizo tuliyonayo. Wizara ya Ujenzi inadauwa trilioni moja, lakini Serikali ingeliamua barabara zile zijengwe na watu wa binafsi, wakijenga watapewa nafasi ya kutoza *road toll* ya kulipa madeni yao kisha wanakabidhi nchi. Nchi zote Duniani hivi sasa ndiyo zinavyokwenda. Nchi zote tunazozitembelea maelekezo yake ni hayo. Sasa kama bado tunataka tupate *ten percent* tutakosa, ni kweli tutapata matatizo ya muda mrefu.

Leo *six percent* ndiyo iliyotolewa kwa bajeti iliyopita, sasa *forty percent* haipo na tunakwenda na 22 trilioni, badala ya kutafuta mahali ambapo tunahitaji Serikali ifanye kazi, tunajichukulia sisi majukumu tufanye kazi hizo. Kuna watu wana pesa hawajui watafanya nini badala ya kuwaambia wakakubali masharti yetu tukawakabidhi hizo kazi, ndiyo kitu rahisi kitakachofanyika. Kama bado tunaona ni Sera ya Chama cha Mapinduzi katika Ilani ya Uchaguzi, tutakuwa hatuwezi kusema tumetimiza Ilani ya Uchaguzi.

Suala la pili, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu akija anieleze faida kuu za TASAF III kwa Visiwa vya Zanzibar na Pemba. Inafanyika vipi kazi hii mpaka kupata maendeleo Zanzibar?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, naomba Waziri Mkuu akija atuambie msaada wa MIVAFU umefikia wapi Zanzibar; nani anayesimamia na unaendelea vipi?

Kwa kumaliza, Mheshimiwa Waziri Mkuu hili suala kidogo ni la kusikitisha sana, Bunge na Serikali ilikubali kutoa fidia kwa waathirika wa vifo vya 2001 Zanzibar na Pemba, vilivyotokea tarehe 26 na 27, watu wasiopungua sitini walikufa. Serikali ilikubali kulipa fidia kwa familia zilizobakia. Mheshimiwa Rais anamaliza kipindi chake cha miaka kumi, Mheshimiwa Waziri Mkuu anamaliza kipindi chake cha miaka kumi, agizo hili bado halijatekelezwa, manung'uniko mengi yanatokea. (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante sana.

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Hiyo ya kwanza mama hiyo!

MWENYEKITI: Ya pili.

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Ya kwanza hiyo.

MWENYEKITI: Ulikuwa unaongea kwa utaratibu mno.

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Sasa naomba anieleze malipo haya yatapatikana lini?
(Makofi)

MWENYEKITI: Nimemwita Mheshimiwa Mangungu, Mheshimiwa Mfutakamba, Mheshimiwa Amina Amour, Mheshimiwa Zubeir na Mheshimiwa Matiko mjiandae!

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na Mwenye Kurehemu, leo inakuwa ni mara yangu ya tano kuchangia kwenye Bunge hili na kuichangia Hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote mtu mwenye akili timamu na fikra timamu, huwa anafagia kuanzia aliposimama. Jana tumesikia Hotuba ya Waziri Mkuu pamoja na Hotuba ya Waziri wa TAMISEMI, lakini yapo maneno ambayo yalikuwa yakisemwa na siku zote ukiuacha uongo uendeleo kusemwa vile unavyosemwa, unaweza ukafika wakati ukaaminika kuwa ni ukweli. Hayo yalikuwa ni maneno ya Lenin, Mwasisi wa Taifa la Urusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, CCM haiwezi kuchoka kwa sababu kila baada ya miaka kumi inafanya mabadiliko ya Viongozi wake, inaweka wagombea wengine na ndiyo ambao wanashinda uchaguzi. Tofauti na hivyo vyama vyao vya kisultani ambavyo Mwenyekiti, Mgombea, wanakuwa hao hao miaka nenda miaka rudi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kaka yangu msomi, Lissu alisema, hatujawahi kuahirisha uchaguzi tangu mwaka 1960. Inaweza ikawa ni bahati mbaya kusema hivyo, lakini awe ana kumbukumbu pengine hata hiyo CHADEMA yenyewe ni mgeni, mwaka 2005 tuliahirisha uchaguzi baada ya kufa Mgombea Mwenza wa CHADEMA aliyekuwa anagombea na Mbowe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha miaka 20 tangu kuingia Vyama Vingi, ndipo ambapo CCM tunasema tunafanya kazi kwa jitihada kubwa baada ya wao kufukuzwa na wengine kutoka. Hatuhesabii miaka hamsini, tunahesabu miaka 20, maana hao ambao wanapiga kelele huko walikuwepo huku tukawafukuza. Bado tunayo mabaki mabaki huku tumewaacha kama mbegu lakini nao tutawafukuza vilevile. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lawama kubwa iliyokuwepo hapa kwamba, Miradi haitekelezeki, haitekelezwi, lakini wanasahau wao ndiyo wa kwanza kukimbilia kwa wahisani kuwaambia msipeleke pesa. Sasa Miradi ya Maendeleo inapatikanaje na ninyi kutwa mnashinda kwenye ofisi hizo kuwaambia wahisani wasichangie Miradi ya Maendeleo? (Makofi)

Tunapokuja humu kwenye bajeti siku zote wanasema hapana, kesho wanauliza barabara mbona haijengwi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya ya kusema mwaka huu tutashinda tumeshazowea kila mwaka wanayasema na wala hatuyahofii. Walisema hivyo mwaka jana na tukawashinda kwenye Uchaguzi wa Serikali za Vijiji. Kwa ukurasa wao nimalizie kwa kusema, hata Quran imesema katika *Surat Baqarah* kuwa: “*Summun bukmun umyun fahum laa yarji'uuna.*” Kwa maana kwamba, wale ambao ni vipofu, viziwi na wala hawatorejea. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukirudi kwenye bajeti iliyowasilishwa jana, Mheshimiwa Waziri wa Maji na Naibu wake, tunawashukuru walifika katika eneo la Jimbo la Kilwa Kaskazini. Tuwaambie tu pesa ambazo wametupangia kasma yake, inahitaji kuongezwa, kwa maana kwamba, Mradi ule wa Maji kutoka Mingumbi, Tingi kwenda Miteja, sasa tumeshaanza kuufanyia kazi. Kwa hiyo, tunaomba pesa hizo zipatikane ili tuweze kuwamalizia. Eneo la Kipatimu na Chumo kuna tatizo kubwa la maji, visima vilishachimbwa, lakini hivi sasa tunahitaji fedha kwa ajili ya kusimamia utengenezaji wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo ambalo limejitokeza na hili Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba alitolee tamko haraka iwezekanavyo; zimetangazwa ajira mpya za walimu, walimu wameshaajiriwa na iliwekwa tarehe ya mwisho ni tarehe 10 Mei, wengine wametoka Kilwa, Lindi, Mtwara na maeneo mbalimbali ya nchi. Wakati wanafika Dar es Salaam ili kwenda katika maeneo yao, kulikuwa na tatizo la mgomo wa madereva, mabasi hayakufanya kazi na vyombo vya usafiri vilikuwa vina ugumu. Sasa tunaomba muwape muda zaidi ili hawa watu ajira yao iweze kuendelea, tumewasomesha kwa fedha za umma, kwa hiyo, ni haki sasa waendeleo kupata hiyo ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo kwenye madai ya walimu, ahadi ya Serikali tunakubaliana nayo, fanyeni haraka. Agizo la Rais hakikisheni yanakokotolewa na tunamaliza madeni haya kwa kipindi hicho, tunajua madeni mengine yatakuja huko baadaye lakini kwa sasa lazima tumalize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la miundombinu ya barabara. Wakati tukiwa kwenye Kamati wiki iliyopita, nilitoka eneo la Garden Avenue na kufika Mtaa wa Libya kwa kutumia zaidi ya saa nane. Hili ni jambo la ajabu sana, kwa hiyo, tunaiomba Serikali iongeze kasma na hasa uboreshaji wa miundombinu kwenye Jiji la Dar es Salaam. Maeneo ya mjini yamekuwa na shida na mnawapa kazi askari askari polisi, walikuwa barabarani mpaka saa nane, saa kumi za usiku na wale wanaingia *shift* kuanzia saa kumi na mbili mpaka muda huo wote. Kwa hiyo, *almost* wamefanya kazi saa 24 kwa kipindi hiki, lazima muwape unafuu kwa kuhakikisha viraka vinawekwa na barabara zile zinafanyiwa matengenezo ili kuweza kuboresha miundombinu ya Dar es Salaam. Vilevile uhakiki wa ubora wa barabara zinazojengwa, barabara zinajengwa lakini kiwango chake kinakuwa cha chini. Nimesikia kwenye kituo cha Radio Clouds FM walikuwa wana majadiliano wakasema hata mtu akikojolea ile barabara inaweza ikabomoka! Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo inabidi myaangalie na tuweze kurekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu ndani ya Bunge hili ameshawahi kutoa agizo kwamba, Machinga wasibuguzwe na wala wasihangaishwe. Nimemwona Waziri Mkuu zaidi ya mara mbili na nimesikia tamko la Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam anasema, Machinga wasibuguziwe na wala wasinyang'anywe mali zao, lakini watendaji bado wanaendelea kuruhusu Machinga wananyang'anywa mali zao. Kuna mfano mzuri eneo la Mtaa wa Zanaki, wauza mbonga pale wananyang'anywa mboga, wanapigwa, wanateswa; sasa haya ndiyo mambo ambayo watu waliyakataa wakataka uhuru ili tuweze kujitawala. Hili lazima lisimamiwe na ihakikishwe linafanyika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, tunayo Miradi mingi sana ambayo tumewaahidi wananchi kuitekeleza. Hatusemi kwamba, ifike mwisho isitekelezwe, tunataka katika kasma ya bajeti ya mwaka huu, tuhakikishe Miradi ile yote ambayo tumewaahidi wananchi, tunaitekeleza na iweze kuboresha miuondombinu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Amina Amour, anafuatiwa na Mheshimiwa Mfutakamba!

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uzima na kuweza kusimama leo hapa nikaweza kuchangia kidogo.

Naanza na suala la amani, amani ni kitu muhimu. Kwa nini nazungumzia sasa hivi? Sasa hivi tunaeeleka kwenye uchaguzi na ukitazama amani huwa inatoweka wakati wa maandalizi wa uchaguzi, wakati wa uchaguzi na wakati wa kutoka matokeo. Tayari Sheria za Uchaguzi zipo, wanaotaka kuandikishwa wanajulikana, wasiokuwa na haki ya kuandikishwa wanajulikana. Mimi natoa wito tu kwa Vyama vyote, tunadi Sera zetu vizuri, tushindane kwa hoja na atakayeshinda apewe bila kupigana. Haya mambo ya kuuwana kila siku, sote ni ndugu hapa, CCM kaa kwa CHADEMA, CHADEMA kaolewana CCM. Kwa hiyo, mambo ya kupigana hayana haja, tujikite kunako Sera, atakayeshinda apewe na atakayeshindwa apokee matokeo na akubali matokeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vuzuri na mimi nikatumia wakati huu kuagana na Wabunge wenzangu, nimeshatumikia Bunge kwa miaka mitano na kipindi kinachokuja sitagombea. Ninaheshimu sana maamuzi ya Chama change, baada ya kuniona nimechoka, nakubali kuwa nimechoka na wengine watagombea. Nawapongeza pia Mwenyekiti wa Chama change na Katibu wa Chama change, kwa kunipa miaka mitano iliyopita na mwaka huu akaona si vizuri kugombea tena. Kwa hiyo, ninaheshimu maamuzi ya Chama changu na ninawaambia hawajafanya makosa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitazungumzia suala la bajeti tegemezi. Kila siku tunapiga kelele tuachane na bajeti tegemezi na mwaka huu pia tumeenda na bajeti tegemezi. Matokeo yake, imefika wakati pesa hazijatolewa na wafadhili kwa vizingizio vyao vya Escrow na mwaka jana ilikuwa vizingizio vingine. Hakuna mwaka hata mmoja ambapo wafadhili walitimiza zile fedha walizotuhidi. Naiomba Serikali itakayokuwa madarakani, ikiwa ni CCM ama UKAWA, walione jambo hili na waachane na bajeti tegemezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukuaji uchumi. Kila siku tunaambiwa uchumi unakua, lakini mimi nashangaa uchumi huu kukua mbona umaskini unazidi! Namwomba Mheshimiwa Waziri aniambie ni lini itafika uchumi utakua na umaskini utapungua? Naomba kukua kwa uchumi kuendane na umaskini kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija matumizi ya fedha za Serikali, bado Serikali inaendelea kuwa na matumizi mabaya ya fedha. Sisi wenyewe fedha tunangojea tukusanye tutumie, tunayo *cash budget*. Sasa zile pesa tukishazipata tena Serikali mara kuna sherehe hii, mara kuna sherehe ile, tunashereheka kila siku. Sasa ifike wakati mtu anaambiwa ajipime kwa kile anachokipata. Tusitake kuiga nchi za wenzetu kwa sababu wanasherehekea uhuru, sijui kafa nani tarehe hiyo wanashereheka, sijui kafanya nini, tutumie kile tunachopata. Ukitazama

tunachokipata kila mwaka huwa kinatumika kingi kwa matumizi ya Serikali. Hebu mwaka huu tuachane na matumizi mabaya ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti imenishitua sana, kutoka trilioni 19.8 hadi 23 na naamini Wabunge wengi imewashitua. Sasa ni bajeti ya 19 hatujaweza kufikia mapato ya kupata trilioni 19.8; kuna miujiza gani itatokea hata tuweze kupata trilioni 23?

Namwomba Waziri wa Fedha wakae tena waizingatie hii bajeti angalau ifikie trilioni 21, lakini siyo 23. Kwanza, ukitazama wanaokusanya kodi TRA bado hawajabadilika, wako kwenye mfumo uleule, nusu zinaingia mfukoni na nusu ndiyo zinakwenda. Wafanyabiashara bado hawajataka kutumia mashine za EFD wanazozana. Tukitumia mashine hizi tunaweza kupata mapato ya kutosha. Kwa hiyo, hili tuliangalie pia. Ukimtazama mwananchi, anatozwa kodi kubwa sana, kiwango cha kodi kimepandishwa kimekuwa kikubwa sana. Wafanyabiashara wadogo wadogo wengi wanashindwa kuzilipa hizi kodi. Kwa hiyo, hili nalo tulitazame ndiyo tujue tunaamua kwenda na bajeti gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nidhamu ya matumizi inakuja. Pesa nyingi huwa zinatumiwa ambazo hazijakuwa budgeted na hili tunalisema kila mwaka. Pesa ambazo hazijawa budgeted zisitumike. Kuna Mfuko wa Maafa sijui wa nini ule, pesa zitakuwa zinatengwa. Sasa nauliza kwa mwaka huu pesa zile zimetumiwa, zikaja kutumiwa nje ya bajeti; maafa gani makubwa yaliyotokea nchi hii hata zile pesa zikaisha na nyingine zikatumiwa nje ya bajeti? Naomba Mheshimiwa Waziri akija hapa anielezee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kuhusu wawekezaji. Wawekezaji wanakuja hapa na suala la Waziri kusema wawekezaji wanakuja kidogo, hili siyo sawa, wawekezaji wanakuja wa kutosha, lakini tuna urasimu wa maamuzi. Mwekezaji atakuja mwaka huu aambiwe mimi ofisi yangu haihusiki nenda kwa Waziri Mkuu. Akitoka Ofisi ya Waziri Mkuu anaambiwa haihusiki nenda Wizara wa Mambo ya Ndani, anahangaishwa yule mwekezaji mpaka anaamua kwenda zake. Kweli mmejipanga tayari kuna sehemu ambapo wanaweza kuja wawekezaji wakapewa, lakini huo urasimu wa maamuzi, kwa nini hamuweki kitengo fulani wakija tu wale wawekezaji wakapewa zile nafasi wakawekeza na kuweza kupata mapato ya kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, nazungumzia suala la misamaha ya kodi. Pamoja na Mheshimiwa Waziri amesema misamaha ya kodi mingi imepunguzwa lakini bado inaendelea. Ukitazama tuseme mashirika ya dini, wengine hutumia tu mashirika ya dini wakasema hili shirika la dini na ambapo wataagizia magari kama hamsini na yote hawalipii ushuru. Sasa ukitazama yale magari yanafanya kazi gani, matokeo yake wanauza magari hayo wanatumia. Namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri au Waziri, afuatilie jambo hili ili lisiweze kuendelea. Ahsanteni. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Amina. Tumemwita Mheshimiwa Mfutakamba, Mheshimiwa Zubeir na Mheshimiwa Matiko mjiandae!

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema. Niwashukuru pia Wanaigalula, kwa kuniamini kwa miaka mitano. Namshukuru Mungu, nimewatumikia kadiri ya uwezo wangu na taarifa zote za yale niliyoyafanya nimewaandalia kitabu wanasoma mpaka vijiwani, aliyofanya Engineer Mfutakamba kwenye Jimbo la Igalula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na utaratibu mdogo wa mchango wa Mheshimiwa Mbowe, namheshimu sana Mwenyekiti wa Upinzani. Kitabu hiki nimekisoma, kurasa zimezungumzia uchumi, siasa ni uchumi na uchumi ni ule unaosimamiwa na sayansi na

teknolojia. Mheshimiwa Mbowe, hakugusa kabisa, ana kurasa nne tu ndiyo amezungumzia kidogo suala la uchumi. Nimeangalia taarifa iliyosheheni, hii Taarifa ya Upinzani nilikuwa nategemea itatoa Mpango Mbadala wa Taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini imekuwa tofauti kabisa. Nafikiri waendeleo na kuangalia sana mchango wa sayansi na teknolojia katika Hotuba ambayo ni Mbadala kutoka Upinzani. (Makofi)

Taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na ya Mheshimiwa Hawa Ghasia, nazipongeza sana, zimesheheni yote ambayo hata sisi TAMISEMI tumefarijika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitaarifa tu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende mchango wangu wa kwanza. Tunayo DART, tumeeleza kwenye Taarifa yetu, nilikuwa nasoma magazeti hasa Gazeti la *Citizen*, zilisema *World Bank* haikuwa inataka wale Umoja wa UDA RT, wasipewe ule Mkataba wa kuendeleza muda mrefu. Niiipongeze TAMISEMI, nimpongeze *Attorney General*, niiipongeze pia Kamati ya TAMISEMI, kwa kusimama kidete na kuhakikisha kwamba, shughuli hizi tunawapa Watanzania wanaweza, kampuni hizi za nje zishughulikie masuala makubwa mawili tu, ambayo ni utoaji wa tiketi kwa njia ya kielektroniki (*automatic fair collection system*), pamoja na utaratibu wa kufuatilia yale mabasi (*real time fleet tracking management*). Masuala hayo huwa ni asilimia kumi au tano kwenye Mkataba mzima huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependekiza, kama *World Bank* watasuasua, tuangalie uwezekano wa *SINO Insurer*, hii ni *Insurance Credit System* ya China, inaweza kutoa mkopo zile dola milioni 60, wasitusumbue ndugu zetu China wanaweza kuzileta hizi zikamaliza *Phase II* mpaka *Phase VI* ya DART.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hilo naomba litazamwe na TAMISEMI na pia Ofisi ya Waziri Mkuu na *Attorney General* ili tupate Mkataba mzuri, usi umiza kwa utaratibu wa PPP.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la biashara. Tufanye tafakari na tafakuri kwenye biashara ya AGOA. AGOA ni *Africa Growth and Opportunity Act*, hii ilianza mwaka 2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna bidhaa 6,400 ambazo ziko kwenye Skimu hii, Wamarekani wanatusaidia. Kule Igalula tuna asali ya asili, *organic honey*, tuna viazi vitamu, tuna kiwanda cha nguo pale Tabora, lakini kinahitaji kufufuliwa ili kutengeneza zile *aperals*, vitambaa tunaweza kwenda kuuzwa Marekani. Ukiangalia kwenye takwimu, uuzaji huu sisi umekuwa unashuka tangu mwaka 2000, AGOA ilipoanza.

Mwaka 2000 tulianza na asilimia kama 18, tukaja asilimia nane, sasa tuko asilimia nne. Serikali itueleze kwa nini mporomoko huu, ukilinganisha na jirani zetu wa Kenya, wao walianza na asilimia 56, wamekwenda asilimia 75, sasa wako asilimia 95; iweje sisi tunashuka?

Naomba Mheshimiwa Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na Wizara mtambuka, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, tujifunze kutoka kwa wenzetu Kenya wanafanyaje ili na sisi tuweze kwenda kibiashara na tuweze kufaidika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Igalula sasa hivi tunaweza kutoa mihogo, mihogo inaweza kuuzwa huko Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la gesi na mafuta. Sasa hivi kwenye Mwambao wa Pwani; Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara, pia Rukwa, Kigoma, Katavi, pamoja na Ruvuma, iko miamba ya mawe aina ya Karoo, hii ina aina ya gesi inaitwa gesi ya *shale*, pamoja na mafuta. Teknolojia yake ukitumia na utaratibu wa *satellite* inakwambia mafuta yako wapi kwa gharama *one fifth* ya gharama ya kuchimba kwenye miamba iliyoko kwenye sakafu ya bahari, ndani, *deep sea* kule. Tunaweza kuchimba kwa gharama nafuu. Halmashauri zishauriwe ziingie ubia na makampuni mbalimbali ili tuweze kupata pato la haraka tuchimbe mafuta na sisi tuna utajiri mkubwa ule, ni wakati mwafaka sasa hivi kuutumia kitaalam ni *Hydraulic Horizontal Fracturing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkongo wa Taifa, suala la *ICT* ni la msingi sana. Sasa hivi asilimia 75 ya wanafunzi wanaotoka katika Vyuo vya Marekani, wanajijaji wenyewe. Asilimia 50 ya nchi za Umoja wa Ulaya, *EU*, wanafunzi wanao-graduate wanajijaji wenyewe.

Tuweke utaratibu wa vyuo vyetu vikuu, kutengeneza mitaala ambayo mwanafunzi atatoka ajijaji mwenyewe, tusitegemee kuajiriwa. Haya Mataifa yote yamekuwa kwa kuendeleza sayansi na teknolojia. Mkongo wa Taifa utatusaidiaje? Uko Mkongo wa Kimataifa, ambao unapita pale Dar es Salaam, iko mikongo miwili na sisi Serikali tumeshajenga Mkongo wa Taifa, zipo nchi ambazo hazina bahari, wanatutegemea sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kila Halmashauri iweze kutengeneza utaratibu wa kuanzisha *centers* hizi za *technology*, kufundisha vijana mambo ya *TEHAMA*, wanaweza kujijaji kule kule kwenye wilaya na inaweza kufika sasa hivi hata ngazi ya vijiji baadhi ya maeneo. Tutumie fursa hiyo kwa sababu itatusaidia sana kujenga ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kidogo suala la *NAFTA*, *NFRA*, pamoja na pamba na ardhi. Serikali Kuu ipeleke hizi fedha kwa wahusika, kwa sababu kwenye Kamati yetu tuligundua ile 60% ya mapato ya ndani, wanashindwa kutekeleza Miradi kwa sababu hizi fedha hazikupelekwa na Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hilo lisimamiwe ili maeneo yote haya yaweze kupata mikopo hasa ya akina mama na vijana. Asilimia tano tano zile zitapatikana tu kama hii michango inarejeshwa sehemu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze sana Miradi ya Barabara, kilomita 85 Chaya – Nyahua. Hii ni Barabara Kuu kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma, hiyo sehemu ni ya Igalula. Naomba lami iwekwe na Mheshimiwa Rais amenithibitishia, lami inakuja na Wakuwait wamekwishaanza. Mheshimiwa Naibu Waziri, Engineer Gerson Lwenge, alinitaarifu hapa kwamba, tayari utaratibu unafanywa. Naomba iwekwe lami haraka sana na sisi tuje haraka sana Dar es Salaam na kwenda Kigoma kwa ndugu zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mto Ng'wala kule Loya, hii ni kati ya Igunga na Igalula, tunaomba daraja pale haraka iwezekanavyo, kwa sababu kuna wananchi wanapata adha nyingi; akina mama lazima wavuke ule Mto kwenda upande wa pili, watoto hawaendi shuleni kwa sababu Mto Ng'wala ukijaa usafiri unakuwa mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kusahau umeme, mimi naishukuru sana Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kufanya kazi kubwa. Igalula niliingia pale mwaka 2010, hatukuwa na grupu hata moja, sasa Mheshimiwa ngoja nikupe uhondo hapa, umeme *Mini-Grid* Kata za Loya, Lutende, Tura, tayari umeme unawaka, makofi. (*Makofi*)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Ndugu zangu TANESCO, REA umeme nguzo na nyaya zinasambazwa Kigwa, Igalula, Goweke na Nsololo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante.

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Tunakwenda na Tura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuruni. Halmashauri ya Igalula tutashukuru kama tutapatiwa fedha na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Said Zubeir, Mheshimiwa Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Ignas Malocha!

MHE. SAID MUSSA ZUBEIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na Mwenye Kurehemu, kwa kutupa afya njema. Baada ya hapo na mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, kwa kusimama muda mrefu pale, akionekana ana afya, hajachoka na ana uwezo wa kuendelea. *(Makofi)*

Niipongeze Serikali kwa kazi nzuri iliyofanya kwa kipindi chote hiki cha miaka mitano na sasa inahitimisha. Naipongeze kwa sababu zifuatazo:-

Hali ya kiuchumi, kiukweli tulikotoka nyuma na sasa hivi hali ya kiuchumi imeboreka zaidi. Sasa hivi tumeweza kufikia angalau asilimia saba tofauti na asilimia 4.7 miaka mitano iliyopita. Kwa hiyo, hii inaonesha dhahiri kwamba, tumetoka wapi na sasa tuko wapi. Changamoto zipo, lakini hali inaonekana kuwa nzuri.

Tukija kwenye suala la elimu na hili ni suala la msingi sana, Serikali hii imejitahidi sana kuweka hali nzuri, kuongeza walimu, kujenga mabweni, kujenga madarasa na hatimaye wanafunzi wanaoingia kila mwaka wanaongezeka. Hii ni ishara tosha ya kuonyesha kwamba, Serikali haijachoka na inakijua inachofanya. Kwa haya inaonekana dhahiri kwamba, bado CCM iteaendelea kuongoza pengine miaka 15 mpaka 20 mbele; kwa hili mimi sina wasiwasi nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sishangai kuona upande wa pili wanabeza haya, ni mambo ya kawaida tu, kwa sababu ningelishangaa kuona na wao wanapigia chapuo na huku wakisema wanahitaji kuingia Ikulu, hii ingelikuwa ni tofauti. Kinachotakiwa sisi tuliohisi kwamba CCM imefanya vizuri, tueleze yale yaliyoyafanywa, kama wao wanavyokaa na kuzungumza mabaya. Kwa sababu kwenye mambo haya unatakiwa ulinganishe kwenye kizuri na kibaya halafu utazame faida ziko wapi.

Hakuna jambo lolote utakalolifanya likawa liko *hundred percent*, ila unatakiwa uangalie una asilimia ngapi za mafanikio kwenye jambo fulani. Sasa ukiona una asilimia kuanzia 75 kuendelea mbele za mafanikio, hilo jambo ina maana limeleta faida. *(Makofi)*

Siyo kwamba litakuwa halina changamoto, sasa kwa upande wa pili mimi huona Wapinzani pengine wanazungumzia zile asilimia 25, sema wanaziboresha kwa kuzitia uongo mwingi na kuwatia hofu watu mimi linakuwa halinishughulishi. Ninachotazama mimi ni kwamba, tulikuwa wapi, tuko wapi na wapi tunataka kuelekea. Mungu amejalia kwa hili, hata Watanzania ni watu wenye akili sana, wanakijua wanachokifanya, ni watazamaji wazuri, wasikilizaji wazuri, lakini ni waamuzi wazuri na ndiyo maana muda unapofika na mimi hata hofu sina, tukifika Oktoba 25, nina hakika Watanzania walio wengi, watakwenda watachukua wataweka waaa kwa upande wa CCM. Hili sina wasiwasi nalo, kwa sababu wanajua nini kinafanywa na wanaelewa kwamba, debe tupu kawaida yake kupiga kelele, lakini lililojaa huwezi ukalisikia linafanya zogo, kwa sababu tayari limeshasheheni lina kazi nyingi za kufanya, lakini lililokuwa tupu kupiga kelele ni jambo la kawaida. *(Makofi)*

Tukija kwenye masuala ya afya, tumetoka na watu 5,000 mwaka 2015, hadi sasa hivi tumefikia 7,000, hawa wote wameajiriwa. Tunapozungumzia afya, unatakiwa uangalie na *demand*. Unaposema bajeti haikamiliki vizuri, mambo yamekuwa mengi, mikopo imekuwa mingi, tulipoongeza walimu, tukaongeza na maabara, tunahitaji na matumizi zaidi. Kwa hiyo, unatakiwa hiki nacho ukifikirie. Unapoongeza madaktari, ukaongeza na hivi vituo vingi vya afya, tunahitaji matumizi mengi zaidi, kwa hiyo, ni lazima huu mzigo utakuwa unapanda. *(Makofi)*

Hapa kwa upande wa Serikali tu, niwaambie kwamba, *wa-pull up their socks* kuhakikisha tunatafuta mambo mengine mbadala ya kuhakikisha tunaongeza mapato yetu katika kukua uchumi wetu.

Pato la Mtanzania la mtu mmoja mmoja, lilikuwa liko kwenye 360,805 mwaka 2005. Hivi sasa tunazungumzia 1,725,290, inaonekana tumepiga hatua na maisha yenyewe yanapanda. Sasa hapa mtu anatakiwa apige hesabu jinsi maisha yanavyopanda na hili pato linavyoongezeka; je, linakidhi haja? Labda hii ilikuwa ndiyo *challenge* ya kuizungumzia, lakini siyo kwamba tuko chini, tumepanda tunatakiwa tutazame tu kasi ya upandaji wa hili pato kwa mtu mmoja mmoja pamoja na hali halisi ya maisha na siyo Tanzania tu bali ulimwengu mzima ikoje. Je, tunakwenda sambamba, tumeongeza *speed* ama tuko chini hata kama tumepanda? Hapa ndiyo unaweza ukasema inaonekana pato la mtu mmoja mmoja linapanda, lakini bado hali pengine ni nzito.

Ukilinganisha na uchumi pamoja na kilimo na mambo mengine tuliyoyafanya huko nyuma, utapata jibu sahihi kwamba, hata hali yenyewe nayo imepanda. Tumetoka tulikotoka, tulifikia mwaka jana hapa tulikuwa tunapiga kelele mazao hatuna pa kuyapeleka, inaonekana hata watu wamefanya kazi, ina maana hizi fedha bado zimeendelea kuwa na thamani. Hii milioni moja na laki saba kwa pato la mwaka la mwananchi, limeendelea kuwa na thamani kwa sababu huku chini tuna hali nzuri ya uzalishaji.

Tungelikuwa tuna hali mbaya na fedha yetu ikawa haina thamani kupindukia, ndiyo hapo tungesema tuko pahala pabaya. Nawaomba Watanzania, watafakari vizuri walikotoka na walipo, wasihangaishwe na maneno ya watu ambao lengo lao ni kutafuta Serikali kwa njia yoyote. Maana yake hili limekuwa kama genge la watu ambao wanakaa na kufikiri watachukua Serikali kwa njia gani, ndiyo maana mara walete maandamano!

Watazame walikotoka na walipo, nina hakika maamuzi yao yatakuwa ni sahihi na yenye masilahi kwa taifa letu hususan kukisaidia Chama cha Mapinduzi. Hili mimi sina wasiwasi nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuje kwenye suala la wawekezaji. Tunawapigia debe sana wawekezaji, lakini mimi niko tofauti sana. Mimi napendelea wawekezaji wa ndani kuliko wawekezaji wa nje, kwa sababu wawekezaji wa nje wanapokuja hapa, shabaha yao ni moja tu, kuhakikisha wanapata faida na kuondoka na fedha.

Tukiwasaidia wawekezaji wa ndani na kama tutaendelea na Mipango yetu kama hivi tunavyokwenda, MKUKUTA na mambo mengine kusaidia wananchi wa ndani, Watanzania wenyewe, tunaweza tukapiga hatua kubwa na kupunguza kuagiza, badala yake tutaongeza sisi kusafirisha. Vizuri tuwe na viwanda vyenye uhakika tunaposafirisha kitu ambacho kinakuwa tayari tumemaliza kukitia thamani sisi wenyewe, ndipo tutakapoweza kupiga hatua.

Ukweli mimi sipendelei sana ninapokaa nikasikia wawekezaji wanakuja wanahangaishwa, wakati mwingine kila wakihangaishwa huwa naona ni vizuri zaidi, ili sisi wenyewe tuweze kujipanga. Tusikae tukasubiri wao wakaja wakavuna kutoka kwenye migongo yetu halafu baadaye wakatuacha sisi hatuna kitu na kuondoka. Hili ndiyo Taifa ambalo linaweza likienda pahala pabaya. Tukitaka twende vizuri kama tulikotoka na hapa tulipo, basi ni lazima tuwafikirie sana wawekezaji wa ndani, tuwafikirie hawa waliokopa humu ndani kama ni makandarasi au watu wengine, tunapofikia hatua ya kusema wanahitaji watu kulipwa, basi hawa ndiyo walipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Nimemwita Mheshimiwa Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa John Chiligati na Mheshimiwa Likokola ajiandae!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nianze kwa kushangaa ni kwa nini Radio Tanzania inarusha matangazo wakati wa maswali na majibu tu na ikikumbukwa mwaka jana wakati wa bajeti, niliuliza kitu hiki na Naibu Waziri, Mheshimiwa Nkamia, akasema atalirekebisha. Itambuliwe kwamba, zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania hawana *television*, hawana umeme na wale wenye *television* majumbani kwao wanakuwa wapo makazini; sasa kama kweli tuna nia ya dhati ya kuwaeleza Watanzania kinachojiri Bungeni; ni kwa nini Radio Tanzania inakatisha matangazo baada ya maswali na majibu ila TBC inaendelea wakati ikijua ni asilimia tano tu au kumi ya Watanzania ndiyo wanaoweza kushuhudia kinachoendelea Bungeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi, jana wamerusha kipindi cha Maswali na Majibu, hotuba yote ya Waziri Mkuu imerushwa, alivyoanza Mwenyekiti wa Katiba na Sheria, matangazo yakakatwa, akafuata Mheshimiwa Mbowe, yamekatwa; wachangiaji wengine wote yamekatwa na ndiyo maana humu ndani Wawakilishi wa wananchi, kwa maana ya Waheshimiwa Wabunge wanaongea wanachokipenda wakijua zaidi asilimia 90 ya Watanzania hawafuatilii.

Kwa hiyo, nataka kujua ile haja ya Mheshimiwa Nkamia kwamba Redio Tanzania itaenda kutangaza matangazo yote ya Bunge, imeishia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bora *TBC* isitangaze, Redio Tanzania itangaze maana Watanzania masikini wanachunga ng'ombe wanasikiliza redio kwa simu zao, wanakwenda mashambani, makazini wanasikiliza kwa *computer*, wakiwa kwenye foleni kwa sababu barabara zenu ni mbovu, tunakaa kwenye foleni zaidi ya masaa nane, Watanzania wanaendelea kufuatilia Bunge. Ni kwa nini Redio Tanzania isitangaze? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nikiunganisha hapo hapo kwenye barabara, wakati Waziri Mkuu anaongea, amesema kabisa Serikali ya Chama cha Mapinduzi miaka kumi imejitahidi sana kwenye barabara ya lami na changarawe. Lakini kiuhalisia, sisi tunaotoka huko Wilayani na hata juzi tulipokuwa Dar es Salaam, miundombinu ya barabara sijui kwenye lami na changarawe yote ime-*paralyze*. Barabara zimekatika, hakuna mawasiliano kabisa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi natoka Bunge, nimetoka saa 8.00 kuja kufika hapo ninapokaa, Aghakan, zaidi ya masaa nane. Uchumi una-*paralyze*, halafu leo mnakaa mnajisifu kabisa mnajipigia makofi kwamba mmeboresha miundombinu. Barabara inajengwa baada ya miaka miwili imeharibika. Barabara ya Kachube ukiiona leo, siyo barabara, utafikiri haikuwekewa lami. Hakuna thamani ya pesa. Fedha za Watanzania zinapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajali nyingi zinatokea ingawaje mningizia ni madereva, chanzo ni barabara mbovu. Ilitokea Mbeya, ikatokea kwenye daraja ya Pida Musoma kule, ndugu zetu zaidi ya 70 wakafariki. Lakini kwa sababu Tanzania ajali zikitokea Serikali inaendelea kupeta, Watanzania wanaendelea kupotea kama vile siyo binadamu, ndiyo maana mnakaa mnaandika hotuba, mnakuja mnawachanganya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wa leo siyo wa jana, siyo wa 2010 siyo wa 2005. Mwaka huu watakwenda kudhihirisha kwamba ndugu zao waliowazika kwa madhila yote ya ajali za barabarani, afya na madhira mengine, majanga yote yanayosababishwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, sanduku la kura linakwenda kuonyesha mwaka huu. Msifikiri kwamba wanazika leo ndugu zao halafu bado waende kuwapigia kura wakati wakijua mmesababisha nyie kupoteza ndugu zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye huduma ya afya, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza kabisa kwa kina wamejitahidi, zahanati nyingi kwenye kila Kijiji, vituo vya afya vingi, yaani nikawa najjuliza, labda huko Tanzania kwingine ni tofauti na Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninavyojua, vijiji vingi havina hata hizo Zahanati. Mfano, niseme Kata ya Susuni ina vijiji zaidi ya vitano, kuna zahanati moja tu ya Kiongera tangu nikiwa na miaka mitano mpaka leo na inahudumia na Kata nyingine zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa Tarime juzi, nimehudhuria misiba zaidi ya kumi ya wamama wajawazito wanafariki wakati wakijifungua, kwa sababu zahanati zile haziwezi kutoa huduma yenyewe, hakuna vifaa tiba, hakuna Waganga! Wanajitahidi kuwakimbiza hospitalini, barabara za CCM mbovu, halafu hawana *ambulance*. Mileta vibajaji ambavyo sijui mlipiga hela tu havijafanya kazi, mnazidi kuua Watanzania halafu mnakaa huku mnasema ooh, Serikali inafanya mambo mazuri, itaendelea! Nani amewadanganya? Hivi mnafikiri hawa wakina mama kumi tumewazika Tarime ndugu zao watakwenda kuwachagua ninyi kwa uzembe wenu? Amkeni! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo, kwenye suala la mgogoro wa ardhi. Leo msikilize kabisa na ninajua mkitoka hapa mtakwenda kuyatafakari ingawa hapa mtacheka kwa kubeza,

lakini yatawaingia. Migogoro ya ardhi! Tangu nimekuwa Mbunge hapa, kulikuwa kuna mgogoro kati ya Jeshi la Wananchi na wananchi wa Lonsoti na Msati, na tukaeleza kwa kinagaubaga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wanajeshi baada ya kuwa hakuna miundombinu ya daraja, ikabidi wahamie kwa wananchi huku Msati na Lonsoti tukawakaribisha. Baadaye mkaamua kwamba Jeshi lichukue lile eneo. Kuwalipa imekuwa kitendawili, mmezuia wasifanye shughuli zao za maendeleo kuanzia 2007 mpaka leo, mnawadhaliisha, lakini zaidi mashamba yale nyie mnakodisha kwa watu wengine. Halafu tena, yaani mnanishangaza kwa kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa Nyamongo, juzi DC amekwenda na Naibu Waziri; niliuliza swali hapa Naibu Waziri akasema tutakwenda wote Mheshimiwa Matiko, tukaangalie kule hao wananchi wanaosema wamefanyiwa fidia kuanzia 2012 hawajalipwa; ndani ya mita 200 kinyume na sheria Mgodji unaendelea ku-operate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri amekwenda na DC eti mnawaambia watu kwamba watakwenda kufanya uchunguzi vizuri kwa waliofanyiwa tathmini, kama sio mzaliwa wa pale, halipwi. Hivi Naibu Waziri mwenyewe hapo alipo, Dar es Salaam amejenga, kwa hiyo, aondolewe Dar es Salaam! DC hapo alipo, nyumba yake aliyojenga, siyo ya kule Songea.

Fanyeni tathmini muwalipe wale watu wote wanaoishi pale, msiseme kwamba mnakwenda kuwalipa sijui Wanyamongo, sijui wale wa pale tu! Kuna watu wengine ni Wasukuma wanaishi pale, kwa nini muwanyanyapae?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mgogoro mwingine kati ya JKT na iliyokuwa Kata ya Mwema na Kata ya Legicheli, muwalipe fidia zao, vinginevyo mtakuwa wapinzani tena wenye Wabunge kumi tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu, sasa hapa ndiyo majanga kabisa! Mnajinafasi! Elimu inazidi kuzorota siku hadi siku, halafu bila aibu mnakwenda mnafunga Shule za Msingi, eti zimekosa choo. Nimefanya ziara Tarime, Walimu wanakuonyesha nyumba zao, mvua ikinyesha wanahamisha godoro wanaweka pembeni, wanajisaidia ndani. Jamani, *are we serious?* Wakati tunapata fedha kibao! Fedha kibao, lakini mnazipeleka kwingine kabisa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitabu cha Maendeleo kinaonesha Mkoa wa Mara mmetupa asilimia 10 hadi Machi, halafu leo mnategemea elimu itapanda! Hao Walimu ambao hamuwajali waje kuwafundishieni watoto wafaulu! Au ni kwa sababu watoto wetu hawasomi kwenye hizo shule za watoto masikini, ndiyo maana ukienda unakuta shule inakaribia kuanguka, unajjuliza, hivi kuna Wakaguzi wanapita hapa? Mnaenda kabisa mnafunga shule eti hamna choo! Vyoo vingine ni vya ajabu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali; siyo TAMISEMI, siyo Serikali kuu, hampeleki mkono wowote ku-support na mnajua wale wananchi wa vijijini ni masikini. Kilimo mnachosema Kilimo Kwanza, chenyewe hamuwawezeshi. Kilimo chenyewe siyo Kilimo Kwanza! Wanapata wapi hela? Wakilima tumbaku, wanauza Sh. 500/=, watalima kiasi gani waweze kupata fedha wajenge madarasa? Tuwe tunaongea uhalisia! Tuwe tunajivisha uhalisia wa yale tunayoyaongea na kuyatenda kama kweli tunalipenda Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye maji. Kuna mradi kule Gibaso umetumia zaidi ya Shilingi milioni 350 kuanzia mwaka 2012, mpaka leo hautoi maji wala nini. Kuna mradi mwingine umeanzishwa zaidi ya Shilingi milioni 200, wananchi wanateseka, wanatembea kilometa nyingi hawana sehemu ya kupata maji. Ndoa zinahatarishwa! Kwenye vitabu mnaandika kwamba tumetekeleza ndani ya mita 300 watu wanapata maji, kinyume kabisa na mnayoyaongea na mnayoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa nyumba za Magereza, Tarime kwa sababu kengele imegongwa. Ukienda kwenye nyumba za Magereza, wale watu jamani, hata ukisema una mifugo ya kuku na sungura kule, Bwana Mifugo anakufukuza. Mwendu mtembelee, nina picha hapa naweza nikatoa CD. Huwezi ukajua kama binadamu wanaishi mle! Zile nyumba zimejengwa tangu miaka ya 1960. Jamani, hivi ninyi mnavyokuwa mnakaa kwenye maghorofa yana AC, mnawatembelea hao wengine huko mkaona wanaishi vipi ili mwaonee huruma mwajengee nyumba? Halafu leo mnategemea kwamba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Nimemwita Mheshimiwa Malocha, Mheshimiwa Kayombo, atafuatia na Mheshimiwa Chiligati. Mheshimiwa Malocha

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuungana na wenzangu katika kuchangia hotuba ya Serikali, Ofisi ya Waziri Mkuu. Naungana na wenzangu kupongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa namna ambavyo alitoa hotuba yenye ufafanuzi ambayo ime-*quote* maeneo yote kwa miaka mitano, mafanikio na matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, palipo na mafanikio, matatizo hayakosi! Hakuna mtu ambaye anaweza akasema anafanya mambo asilimia 100. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakupongeza umefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, wapo watu wachache ambao wako Serikali wanaotuchafua. Wanafanya maovu makusudi na wananchi wanadhani ni Serikali nzima. Nami nataka nieleze jambo moja ambalo linanisikitisha, ambalo liko Maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi wa Nne nilipokea maandamano ya watu 108 kutoka kwenye ukanda wa Reserve wa Uwanda Game Reserve wakiwa wanalalamika kwamba Maliasili wamewapiga, wanawanyanganya mazao wanayauza. Nikasema kwa nini mlilima kwenye reserve ya Serikali? Wakasema tuliruhusiwa na wao wenyewe kwa sababu ni reserve jina tu, walituruhusu tukalima. Tumelima maekari na maekari. Sasa hawakutuzuia wakati tunalima, lakini tumekomaza mazao, tumeivisha, wanatupiga, wanatunyang'anya na wanakwenda kuuza mazao yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichukua hatua ya kumwona Mkuu wa Wilaya. Mkuu wa Wilaya alimwita Mkuu wa Reserve, akamwambia, ndugu yangu, unashindwa kukataza watu wakati wanaanza kulima, unaacha wanalima, mazao yanakomaa, inafikia hatua ya kuvuna ndiyo unawasambaza halafu unachukua mazao unauza? Hii unatuletea uchafu kwenye Serikali. Nakuomba kuanzia leo uache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikubali machoni pake, baada ya siku mbili akachukua gari akanunua *sulphate* akashuka, ameenda kupiga wananchi, kunyang'anya mazao na kuuza na pesa yenyewe haiingii Serikalini, wanagawana wenyewe. Nimeshindwa kuvumilia! Nimemwambia Mkuu wa Mkoa leo. Amepiga simu akamwambia nataka uache! Siyo kwamba tunaunga mkono watu kulima reserve, lakini kwa nini hamkuchukua hatua awali za kuwazuia? Mmeacha wamelima, mipunga yao mnaiuza. Akamwambia, acha!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hivi leo, wale watu ni wa ajabu sana! Sijui kiburi wanakipata wapi! Sasa hivi wanaendelea kuwanyang'anya wananchi mazao; mipunga,

mahindi, wanauza na wanaingiza fedha mfukoni. Sasa nasema, Waziri huyu wa Maliasili, nawaomba na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kama suala hili halijapatiwa ufumbuzi, hii Wizara, bajeti yake isipite hapa. Hakuna! Haiwezekani watu wachache mnaichafua Serikali halafu Serikali ndiyo inaambiwa inafanya maovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami namwomba Waziri Mkuu, jambo hili kama nasema uongo, hata sasa hivi piga simu kule utakuta wananchi wanateseka. Kuna maandamano wananchi wananyang'anywa mazao, watu wanauza tu! Huu ni uchafu mkubwa sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niliseme hili kwa sababu linaitia doa Serikali!

MBUNGE FULANI: Kabisa!

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linaitia Serikali doa kubwa sana!

MBUNGE FULANI: Kweli kabisa!

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ichukue hatua juu ya jambo hili. Mkitaka kuhakikisha, hata leo ondokeni mtakuta wananchi wanateseka kule. Hivi tumefikia hatua hiyo kweli katika nchi hii?

MBUNGE FULANI: Dah!

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niliseme hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kuzungumzia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amefafanua vizuri sana suala la miundombinu ya barabara. Lazima tukubali jamani, Serikali imefanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikachukulia mfano wa Jimbo langu; Jimbo langu nimelikuta lina hali mbaya! Magari hayapi! Hata pikipiki wakati mwingine zilikuwa hazipiti na Waziri Mkuu ni shahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipindi amepita na gari, amepotea, akafuata kondo la ng'ombe, akashtukia ametokea ziwani, hasa barabara ya kutoka Kasansa kwenda Kijamatundu. Lakini sasa hivi barabara hiyo inapitika japokuwa kuna changamoto, hiyo ni kawaida kwa sababu mvua za kwetu ni nyingi; madaraja yanabomoka, lakini nina imani Serikali inafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri, kukomesha tatizo la barabara hiyo, Serikali iweke mpango wa kuiweka lami. Ni barabara yenye changamoto kubwa, ni ndefu na ina uchumi mkubwa.

MBUNGE FULANI: Sawa! *(Makofi)*

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, naishukuru Serikali, tulikuwa na tatizo la barabara ya Kalamazita – Ilemba...

MBUNGE FULANI: Ndiyo!

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Ni barabara sugu! Nimeomba hela mara kadhaa hapa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini nashukuru leo hii TANROAD wameichukua hiyo barabara, nina imani itatengenezwa vizuri kwa kiwango kinachotakiwa. Haya yote ni mafanikio ya Serikali ya CCM. Anayesema Serikali haijafanya kitu, ana lake jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nililotaka kuzungumzia ni barabara ya Mawenzuzi – Msia. Halmashauri iliomba hela, tulipewa hela. Bajeti ilikuwa ya Shilingi bilioni 1,500, tumepewa tumepewa kama Shilingi milioni 200, tulishaanza kuitengeneza, tunaomba Serikali itumalizie pesa ili barabara ile iweze kupitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilitaka kuzungumzia daraja la mto Momba. Bajeti ya 2013/2014 mlitupa Shilingi bilioni mbili, mwaka 2014/2015 mkatupa Shilingi bilioni mbili; lakini cha ajabu lile daraja halijaanza kujengwa. Ni maneno tu, upembuzi yakinifu, *feasibility study*, michoro! Tunataka daraja lianze kujengwa!

MBUNGE FULANI: *Yes! (Makofi)*

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, lianze kujengwa! Nataka Mheshimiwa Waziri wakati anakuja hapa, atoe maelezo ni lini daraja litaanza kujengwa? Wananchi wamechoka na maneno haya! Nilitaka hilo wakati anakuja kutoa ufafanuzi aweze kulitolea majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni daraja la kwenda Kaengesa Seminari. Daraja lile lilijengwa na Waseminari. Bahati mbaya kwa mvua za mwaka huu daraja lile limebomoka na linahitaji fedha nyingi. Halmashauri imeshaomba maombi maalum Shilingi milioni 150, tunaomba mwasaidie. Ninyi ni mashahidi, watu wengi mmesoma Seminari, mna vyeo vikubwa; saidieni watu hawa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wetu wanasoma pale, wasaidieni Shilingi milioni 150. Ite Seminari imesomesha viongozi wengi katika nchi hii. Naomba msaidie lile daraja mtoe pesa liweze kujengwa. Ni aibu kubwa! Kwanza walijenga wenyewe, limebomoka. Sasa hivi wanaomba msaada, Serikali tujenge. Hawatumii wao tu, hata wananchi wa kule Itete na maeneo mengine wanatumia lile daraja. Kwa hiyo, nami natoa wito, nadhani Mheshimiwa Waziri Mkuu umeshasikia, unafahamu mazingira ya kule kwetu, naomba mtie mkazo hawa watu waweze kupata pesa, daraja lile liweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Wizara ya Nishati na Madini. Mimi napongeza. Katika jambo ambalo kwa kweli Serikali mmeweka nguvu kubwa ni kwenye umeme. Mimi nawashukuru sana japokuwa maeneo mengine hamjafikia, lakini kule kwangu kwenye Jimbo langu umeme kutoka Sumbawanga nguzo zinajengwa kuelekea Laela. Ila upande wa ukanda wa Ziwa Rukwa, Kata 13, Vijiji zaidi ya 70 sijaona dalili yoyote ya kupeleka umeme kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea na Mheshimiwa Waziri, nashukuru amesema atatafuta namna ya kwenda. Naomba uende ukajione jinsi eneo lile lilivyo na uchumi mkubwa; na kama mkipeleka umeme mwone jinsi linavyoweza kutoa mchango katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kuzungumza ni suala la maji. Nashukuru katika suala la maji kwa kweli kwa fedha ambazo mlitupa Halmashauri, tumeweza kujenga miradi mizuri kwa ufanisi mkubwa. Kijiji cha Mpui, Ikozi, Kilyamatundu, Nankhanga, Solola, Kinambo, Mfinga, tunalo tatizo la kutokamilika kwa mradi wa maji katika mji mdogo wa Laela na vitongoji vyake na vijiji vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi ule ni mkubwa, unahitaji pesa zaidi ya Shilingi bilioni mbili. Mkandarasi amejitahidi, amejenga, amesambaza mabomba, lakini ameishiwa pesa, kwa sababu Serikali haijapeleka pesa. Kwa hiyo, nami natoa wito, Serikali ipeleke pesa!

MBUNGE FULANI: Yes!

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimwuliza Waziri wa Fedha, hebu toa pesa, toa pesa! Unajua wakati mwingine sisi Wabunge wa Majimbo mnatutesa sana. Tunaamini kwamba inawezekana hampati misukosuko kama tunayopata sisi kwenye Majimbo yetu. Tunaomba upeleke pesa miradi hii iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kuzungumzia ni Wizara ya Mawasiliano. Naishukuru Serikali, nilikuwa na tatizo kubwa la kukosa mawasiliano kwenye baadhi ya maeneo kwenye Jimbo langu, lakini nashukuru maeneo yote yaliyokuwa na matatizo ya mawasiliano, minara imejengwa. Mfinga mnara umejengwa Mtapenda; Milepa mnara umejengwa Kisa Kinambo; Kaengesa Mnara umejengwa Seminari; na Kaoze Mnara umejengwa Chombe na Kaoze. Hizo zote ni shughuli ambazo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeahidi na inazitekeleza. Napongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Wizara ya Ardhi na Nyumba. Kwa kweli napenda nichukue fursa hii kwa kweli kumpongeza Waziri wa Ardhi wa sasa. Mnyonge mnyongeni, lakini haki zake mpeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mfupi, Mheshimiwa Waziri huyu ametembea maeneo mengi yenye migogoro; na wananchi wanafurahi sana wanapomwona Kiongozi, wanazungumza naye, wanatoa matatizo yao, anawasikiliza, anatoa ufumbuzi, wanafurahi. Ndiyo kazi inayotakiwa kwa Kiongozi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu Waziri amefanya kazi kubwa sana. Hata kwenye Jimbo langu kwenye mgogoro wa Malonje, amefika, wananchi wametoa maelezo, amewasikiliza, ametoa ufafanuzi, ametoa majibu kwamba wavute subira. Wananchi wameelewa na wametulia, wanasubiri majibu ya Serikali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba madaraka haya, ukienda kwa watu inatoshwa kabisa ukienda kwa watu ukizungumza nao. Sasa jambo limechukua miaka nenda rudi. Mzee wa watu nakuombea kwenye Jimbo lako huko wasikuangushe. Ni mchapakazi mzuri sana. Nawaambia watu wa Jimbo hilo kwamba mna mchapakazi wa kweli kweli! Mkimwachia huyu mtu, sisi wote tutawalaumu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Kengele ya kwanza!

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Nimemwita Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Chiligati, atafuatiwa na Mheshimiwa Likokola. Mheshimiwa Kayombo hayupo.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kabla sijaenda kwenye bajeti, naomba nitoe maangalizo mawili.

La kwanza, ni kwamba wananchi wanasikiliza sana shughuli za Bunge, wanafuatilia sana shughuli za Bunge. Sana! Kinachowasikitisha ni baadhi ya lugha zinazotumika humu ndani. Kwa sababu hii ni sehemu takatifu, ina heshima yake. Lugha inatakiwa vilevile ifanane na mahali hapa. Lakini baadhi yetu kwa kweli tunawaudhi wananchi kwa kutumia lugha za kuudhi na kejeli. Hili wananchi hawalipendi na hawalitaki. Naomba sana hilo tulijue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kazi yetu sisi Wabunge ni kuikosoa Serikali, sawa, ni haki yetu kikatiba. Lakini hata unapokosoa, basi kosoa kwa lugha ya staha tu, wananchi watakuelewa. Lakini kukosoa kwa lugha ambazo zinaudhi, kwa kweli wananchi hawatuelewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu, wale ambao wanadhani wataiangusha Serikali ya CCM kwa kutumia lugha ambazo hazina heshima, hazina adabu mahali pa heshima na wanadhani watafanikiwa, nawatakia kila la kheri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalizo la pili, Tume ya Uchaguzi imeanza kuandikisha wapiga kura; angalizo langu ni kwamba sisi Wanasiasa hebu tuwape nafasi Tume ya Uchaguzi wafanye kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi Wanasiasa kila asubuhi, jioni, mchana tunaisema Tume hii na nini, tuache! Ile ni kazi ya kitaalamu! Tuache ifanye kazi! Kama watapata matatizo, watarudi kutuambia, tumefanya kazi hii, tuna matatizo haya, tusaidieni twende mbele. Lakini sisi wanasiasa kila siku tu ni kuizogoa ile Tume, kuichokonoa, mara sijui uchaguzi umeahirishwa; nani amesema uchaguzi umeahirishwa? Tunapeleka hofu kwa Watanzania, hofu ya bure kabisa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba sana Wanasiasa kwamba haya mambo nimesema ni angalizo kwa sababu wananchi tunawapa hofu ya bure na hawapendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye bajeti. Napenda kumshukuru sana Waziri Mkuu na timu yake yote, bajeti walivyotusomea jana ni nzuri, kwenye matatizo wameyasema matatizo, kwenye mafanikio wameyasema mafanikio; na mafanikio ni mengi na makubwa katika kila sekta. Kwa mfano, kule kwetu kwenye Mkoa wangu wa Singida; miaka kama 10 iliyopita tulikuwa hatufikiki! Ilikuwa ni mahali *not reachable*; siyo kwa barabara, siyo kwa ndege wala kwa lolote. Lakini naweza kusema kwamba kwa sababu kazi iliyofanywa na Serikali ya awamu ya nne, sasa hivi Singida pale panafikika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeunganishwa na Mikoa yote kwa lami. Ukitaka kwenda kwa jirani zetu wa Tabora kuna lami; jirani zetu wa Dodoma, kuna lami; majirani zetu wa Mkoa wa Manyara Babati kule, kuna lami. Shida iliyopo na naomba Serikali iendelee kutusaidia ni kuunganisha Mkoa wetu na Mkoa wa Mbeya. Najua barabara ya lami kazi imeanza kutoka Mbeya mpaka Chunya, sasa wanakaribia Makongorosi. Sasa hiyo barabara ndiyo inayotuunganisha sisi na Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaiomba Serikali, ikishatoka Makongorosi, basi iingie Wilaya ya Manyoni, Rungwa, Itigi na Mkiwa, inakuja kukutana na barabara ya Dodoma - Mwanza. Naamini kabisa kama kote huko Serikali imefanya, sidhani kama itakuwa ni tatizo sasa kutuunganisha Singida na Mbeya.

Pili, nizungumzie habari ya hali ya chakula. Msimu uliopita ulikuwa ni mzuri kwa Mikoa yote, hata sisi wa Mikoa ya Kati, yaani Mikoa kame, mwaka 2014 tulipata mvua nyingi na tulivuna vizuri. Kule Manyoni tulivuna mpaka na ziada na baadhi ya wapiga kura wangu

wakaiuzia Wakala wa Chakula cha Akiba. Ninachosisitiza ni kwamba mpaka sasa hawajalipwa, wanadai.

Mheshimiwa Waziri Mkuu uliwahi kutoa ahadi kwamba kufika mwezi wa Tatu, yale madeni watalipwa, sasa tumeshafika mwezi wa Tano. Tunaomba utakapofanya majumuisho utoe kauli ni lini wananchi watalipwa ili watulie. Sasa kila siku huwa napata simu, message, hata leo nimepata karibu message tatu kutoka kwa watu wangu wa Manyoni wakiongozwa na Mwenyekiti wa Wafanyabiashara pale Sokoni anaitwa Bwana Jumanne, nadhani ananisikiliza saa hizi kwamba mbona hamzungumzi? Madeni yetu, Wabunge hamzungumzi? Bwana Jumanne, Wabunge tunazungumza, nadhani huko Manyoni unasikia na Waziri Mkuu amesikia ili madeni hayo ya mahindi ambayo tuliiza msimu uliopita yalipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu ni kinyume chake, mvua haikunyesha kabisa na siyo Manyoni tu, nadhani ni Mkoa mzima wa Singida na majirani zetu wa Dodoma ni hivyo hivyo, Tabora, Shinyanga na Simiyu, tupo wengi.

Sasa ombi letu wa Mikoa hiyo ambayo tumekamatwa na njaa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ulitoa hotuba kwamba chakula kipo cha kutosha; watu wasiwe na wasiwasi na sisi ule ujumbe tukaufikisha kwamba Serikali imesema kuna chakula cha kutosha wasiwe na wasiwasi. Sasa mlisema kwamba takwimu zije ili kuonyesha ukubwa wa tatizo lenyewe ni nani hao, wangapi? Takwimu zimeshakuja, tunaomba sasa mharakishe kuleta chakula cha msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufumbuzi wa kudumu kwa sisi wa Mikoa ambayo ni kame, ni kuvuna maji ya mvua. Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na ukame wetu, hiyo mvua ndogo ambayo inanyesha, yale maji yanapita tu. Tunachoomba kwa Serikali ni kwamba muwe na *program* maalum kwa Mikoa ambayo ni kame. Programu za maji msituchanganye na Mikoa ambayo ina mito, maziwa na mvua nyingi. Sisi tupo katika eneo maalum, tunataka programu maalum au mpango maalum. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naiomba Serikali watuweke katika *programu* maalum, tuvune maji ya mvua, hiyo mito ambayo inapitisha maji, tukiiziba tutapata mabwawa na mabwawa yatatupa maji ya kunywa, kwa mifugo yetu na tutamwagilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwangu Manyoni tumebuni mradi mkubwa wa bwawa la Mbwasia; bahati nzuri Serikali imekuja kufanya upembuzi yakinifu na umeshakamilika vizuri, tunangoja tu fedha zije, mradi uanze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba, kwenye bajeti inayokuja, nitafurahi sana na wanamanyoni watafurahi sana kama hili bwawa la Mbwasia litapata fedha ili tulime kilimo cha umwagiliaji. Tunazo skimu saba za umwagiliaji ambazo zina mifereji na miundombinu, lakini bwawa la kupeleka maji kwenye hizo skimu halipo. Tukipata bwawa hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, hutamwona tena Mbunge wa Manyoni anakuja kwako kuomba chakula kwa sababu nina uhakika kabisa hili tatizo litakuwa limekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kengele imeshalia, nizungumzie mawili ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru katika miaka hii miwili wenzetu wa Wizara ya Maji wametusaidea, tumemaliza miradi ya maji katika maeneo ya Kilimatinde, Solya, Majili na Ilondoni, tunashukuru sana. Lakini bado tuna tatizo kubwa sana katika Vijiji vya Bonde la Ufa. Tunao mradi wa kuchukua maji Mbwasia kupeleka Kintinkhu, mradi ambao utahudumia vijiji 10 katika Bonde la Ufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshazungumza mara nyingi hapa Bungeni na juzi juzi nashukuru mmeleta Shilingi milioni 280 ili waanze kuchimba visima. Lakini mpaka sasa ninavyozungumza, Mkandarasi hajaanza kufanya hiyo kazi. Tunaomba Wizara tusaaidiane ili Mkandarasi huko aliko aanze kufanya kazi. Fedha zilizobaki, kwa sababu ule mradi unagharimu karibu Shilingi milioni 800, mmeleta Shilingi milioni 200, bado Shilingi milioni 600; zilizobaki nazo zije ili wananchi wangu wa Bonde la Ufa ambao mwaka huu watakuwa na njaa mbili; njaa ya maji na njaa ya chakula ili angalau hili la maji tulishughulikie haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni umeme. Naishukuru Wizara ya Nishati kupitia REA awamu ya kwanza tulipata umeme karibu vijiji 14, tunashukuru sana. Sasa awamu ya pili ambayo inakwenda kwenye Tarafa nzima ya Nkonko yenye vijiji zaidi ya 20, mradi ulianza vizuri, tukaona nguzo zinawekwa kwa haraka na waya. Wamefika kilomita 70, usingizi kabisa! Hawaonekani! Nashukuru Kamati ya Nishati na Madini ilifika mwezi uliopita kukagua ule mradi, wakatoa amri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Nimekuita Mheshimiwa Likokola, atafuatiwa na Mheshimiwa Malole, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Antony Mbassa ajiandae.

MHE. DEVOTA M. LIKOLOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami niungane na Wabunge wenzangu kwanza kabisa kushukuru kwa ajili ya hotuba ya Waziri Mkuu na niungane na Wabunge wote ambao tunaendelea kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa iliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri Mkuu, pamoja na kazi zote zilizofanyika, napongeza hotuba yenyewe. Hotuba hii imesheheni kila sekta. Inaonekana kwamba Mawaziri walipo kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, wamemsaidia kwa kiasi cha kutosha Waziri Mkuu katika kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia katika maeneo matatu; eneo la kwanza ni la kuwawezesha wananchi kiuchumi; eneo la pili, nitachangia katika Sekta ya Nishati na Madini; na eneo la tatu, nitachangia katika maendeleo ya Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na eneo la kuwawezesha wananchi kiuchumi. Serikali imefanya kazi kubwa na imefanya mambo mengi; na wakati tulionao sasa ni wa wananchi kufanya mambo makubwa. Lakini wananchi hawataweza kufanya mambo makubwa bila kuwezesha. Ni lazima mkakati wa kuwawezesha upewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni tatizo la Serikali kuangalia zaidi Baraza la Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi. Kwa nini? Kama wananchi watawezesha kiuchumi, maana yake, wataiwezesha Serikali kwa kulipa kodi, ajira na kwa shughuli mbalimbali. Kwa hiyo, ni lazima wananchi wawezeshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda wa miaka saba tangu Baraza la Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi liundwe, halijapata pesa za kutosha. Kwa maana hiyo, kama Baraza halina pesa, haliwezi kuwawezesha wananchi. Hapa kila Mbunge analalamika kwamba vijana, wanawake na wazee hawajawezeshwa. Suluhisho pekee ni kuliwezesha Baraza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia, wananchi wa Tanzania kisiasa tupo vizuri sana. Kijamii, tumekaa vizuri, lakini kiuchumi bado hasa kwa wananchi wa kipato cha chini, uchumi ni mdogo sana. Kwa hiyo, naomba Baraza lipate fedha za kutosha. Hilo ndiyo ombi langu kubwa.

La pili, Baraza lenyewe lishuke mpaka ngazi ya familia. Hili Baraza limekaa kitaifa tu! Kwa hiyo, naomba Waziri anayeshughulikia uwezeshaji wa wananchi ahakikishe kwamba Baraza linaunda Kamati za kuwawezesha wananchi kiuchumi tangu ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya, Kata, Kijiji, Mtaa na ngazi ya Familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ngazi ya Familia Baba ndio awe Mwenyekiti wa kuwawezesha wananchi kiuchumi. Lazima tuwawezeshe watoto wetu na familia zetu na mama awe Katibu ili kila mmoja akiwezeshwa, maendeleo Tanzania yatakuwa makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda katika hotuba ya Waziri Mkuu kwenye suala la kuwawezesha wananchi kiuchumi, ambapo amezungumzia pia ukurasa wa 28, kwamba Serikali imesaidia sana katika kuanzisha SACCOS na VICOBA. Pia Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema, mtaji wa VICOBA sasa hivi ni Shilingi bilioni 86. Mimi nashindwa kuelewa, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa nini asiwape kazi maalum Wizara ya Fedha? Kama mtaji wa VICOBA ni Shilingi bilioni 86, kwa nini Wizara ya Fedha wasianzishe Benki ya VICOBA? Wakati kuanzia Benki ya VICOBA ni Shilingi bilioni tano tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya Fedha wahakikishe kwamba mtaji wa VICOBA ni mkubwa, *unless otherwise* waseme kwamba hizi Shilingi bilioni 86 hazipo kwa wana VICOBA. Lakini kama wameshafikisha mtaji mkubwa hivi, waanzishiwe benki yao. Wizara ya Fedha hakuna mtaalamu wa kuwasaidia wana VICOBA wakaanzisha benki? Mbona ni mambo ya ajabu! Wasaidieni waanzishe benki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika napenda kuwasifu sana Wabunge wa Bunge hili kwani wamekuwa ndio wawezeshaji wa wananchi kiuchumi. Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiziwezesha SACCOS, VICOBA na vikundi mbalimbali. Hakika Waheshimiwa Wabunge wamefanya kazi ya kuwawezesha watu na popote tunapokwenda sifa hii hamtaipoteza; na wale mliowawezesha nanyi watawakumbuka katika ufalme ujao. Siyo mbali sana! Nami naomba kabisa wale wote, vikundi mbalimbali msiwasahau Waheshimiwa Wabunge waliowawezesha na wenyewe wanakuja kwenu sasa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Sekta ya Nishati. Hakuna anayebisha! Umeme umekwenda vijiji mbalimbali, Wilaya zote za Tanzania na maeneo mbalimbali, lakini kazi hii kubwa iliyofanywa na REA sasa hivi inataka kukwama. REA bajeti yao imekuwa ndogo sana. Kwa maana hiyo tukikwamisha hii bajeti ya REA, tukiwapa pesa ndogo hawataweza kuendelea kupeleka umeme maeneo yote ya Vijijini. Nani asiyetaka umeme hapa? Mimi naomba tukubaliane kimsingi kwamba kipaumbele kiwe ni kupeleka fedha REA, wapate fedha ili umeme uende kila mahali. Umeme ndiyo utakaofungua maendeleo ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala zima la miradi mbalimbali lakini pia Waheshimiwa Mawaziri jaribuni kutumia PPP. Watu wengi wanataka kuwekeza nchini; wakiwekeza kupitia PPP miradi mingi itajengwa. Kwa nini hatuwapi fursa? Tujaribu kuwapa fursa na wenyewe watusaidie. Vile sisi hatuna pesa, watu wenye pesa wanataka kujenga miradi, wapeni fursa ili nchi isonge mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia Mkoa wa Ruvuma. Kwanza kabisa naisifu Serikali hii kwa kufungua milango mbalimbali ya kuwezesha wananchi wa Ruvuma. Tunavyozungumzia Mkoa wa Ruvuma sasa hivi ni Mkoa ambao Serikali imefanya mambo makubwa sana.

Tumefungua barabara za Songea - Mbinga, Songea - Namtumbo na Songea - Tunduru. Lakini siyo suala la barabara tu, umeme umekwenda kwenye Wilaya zote. Vilevile tuna mradi mkubwa wa Makaa ya Mawe Ngaka. Kwa maana hiyo, kutakuwa na raslimali kubwa ya Makaa ya Mawe na tumeanza kusafirisha Makaa ya Mawe kwenda nchi za Malawi na Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kazi iliyobakia ni moja tu Mkoa wa Ruvuma, viwanda! Nami nasikitika hapa, Mawaziri maadam mpo, mpelekeeni salamu Mheshimiwa Kigoda. Mkoa wa Ruvuma sasa tunataka viwanda ili tufungue ajira kwa vijana, tufungue mapato ya kodi na uchumi. Sasa hivi Mkoa wa Ruvuma tunataka kwenda kwenye uchumi wa viwanda, hatutaki uchumi mdogo mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru pia Mheshimiwa Kigoda kwa kulipa fidia ya eneo la viwanda la EPZ, Shilingi bilioni 2.6. Umfanya kazi nzuri sana! Sasa pale kama umelipa fidia, lazima uhakikishe kwamba Wizara ya Viwanda inasaidia kutafuta wawekezaji wa viwanda vikubwa na hapa lazima nieleweke, sizungumzii viwanda vidogo vidogo, nazungumzia viwanda mama. Leo Mkoa wa Ruvuma mahindi yamejaa; hakuna kiwanda mama cha kusindika mahindi; kwa nini kisijengwe kiwanda? Wananchi wanahangaika kubembelezana na Serikali kuhusu kununuliwa mahindi yao, lakini kama kungekuwa na kiwanda, leo mahindi yangeweza kuuzika kwa wenye viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Ruvuma sasa hivi tunataka utalii upambe moto kwa sababu mambo yote yanayowezesha utalii yako Mkoa wa Ruvuma. Napenda sasa hivi Mawaziri mtambue kwamba Mkoa wa Ruvuma ndiyo wenyewe ambao mkiwekeza hakika maendeleo Tanzania yatafumka kama mvua. Maendeleo ya Tanzania yatategemea sana Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kwamba tayari kuna mpango wa reli kutoka Mtwara mpaka Mbamba Bay. Pia reli hiyo itafungua mambo ya uchumi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa umemaliza muda wako!

MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, namwita Mheshimiwa Mallole, atafuatiwa na Mheshimiwa Chilolo na Mheshimiwa Mbassa ajiandae.

MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru sana kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hasa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa wananchi wangu na Serikali, lakini pia nitamalizia na suala la upimaji wa ardhi ya Mji wa Dodoma. Ntoa shukrani sana kwa wananchi wote kwa jinsi tulivyoweza kushirikiana nao kwa kipindi chote cha miaka mitano kutoka mwaka 2010 hadi leo 2015. Nashukuru wamekubali kwamba kazi niliyoifanya ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba pande mbalimbali za Mji huu watu wameandamana sana. Upande wa Mashariki watu wameandamana kwenda kunisimika hasa

katika ile Kata za Iyumbu na Nzuguni, kuwa kiongozi wao wa jadi. Pia wameandamana upande wa Kaskazini katika Kata ya Chang'ombe ambayo mara nyingi inajulikana kama ni Wilaya ndogo katika Jimbo la Dodoma Mjini kwa sababu ya watu ambao wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru pia maandamano makubwa yaliyofanyika kunipokea katika Kata ya Kusini, kule Kikuyu ambako pia walinisimika kuwa kiongozi wao wa jadi. Jambo hili linaonesha wazi kabisa kwamba, nakubalika na wala hatuwezi kuwa na siasa za uongo na kweli za watu ambao wanaweza kuunda maneno yao yasiyo na msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya sasa nitumie pia nafasi kuishukuru sana Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika Jimbo la Dodoma Mjini. Nawashukuru sana kwamba Serikali imeweza kutuletea barabara. Mtu ambaye hakuwepo hapa Dodoma hasa kutoka mwaka 2010 mpaka siku ya leo 2015, akija anaweza akashangaa kama kweli ni Dodoma hii aliyoiacha au vipi. Barabara nyingi zimeshaweka lami, urefu wa kilomita 47.7 na hata zile za vijijini zimetengenezwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwamba Serikali pia ina mpango wa kuweza kuhakikisha kwamba kilomita nyingine 55 za barabara nzuri zinatengenezwa hapa mjini. Namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa sababu amefanya kazi nzuri sana ya kunisaidia. Kila nilipomwona alikuwa tayari kunisaidia. Bado tuna changamoto ndogo tu hasa katika hizi barabara kubwa, kutoka hapa kwenda kule kwenye Chuo cha Mipango na kupitiliza kidogo hadi Msalato na kutoka pale Ihumwa kwenda Chuo cha Hombolo. Barabara hizo nimezipigia kelele muda mrefu, naomba Serikali iangalie ili iweze kuzitengeneza kwa sababu haziko katika hali nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa maji. Namshukuru sana Mheshimiwa Prof. Maghembe ambaye pia amekuwa msikivu kwa kunisikiliza kwa karibu. Maji sasa Dodoma ni mengi japo ninapozungumza sasa hivi inawezekana baadhi ya maeneo maji yakawa hayatoki vizuri, lakini hii ni kwa sababu ya mabomba makubwa ambayo sasa yanafunikwa katika ardhi na wengi mliyaona. Tunaondoa mabomba ya zamani ambayo yalikuwa membamba kidogo, tena yalikuwa yamechakaa na kuweka mabomba mapya. Kazi hiyo itakapokuwa imeisha, maji hapa yatakuwa mengi kwa sababu bado tunayo matenki makubwa katika milima ya Itega na Image na yameshazinduliwa yote na Rais wetu. Baada ya muda siyo mrefu, maji yatakuwa ni mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa mradi mzuri ambao unaandaliwa kutoka katika Bwawa la Farqwa ambapo hatimaye maji yatakuwa ni mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo naomba sana Serikali iongeze nguvu kwa kutoa fedha za kutosha katika Halmashauri zetu ili kusaidia hali ya maji hasa kwa upande wa maeneo ya vijijini. Mabomba mengi yameharibika na wananchi wanapata taabu sana ya maji. Mabomba yale yanahitaji kufufuliwa na kuwekewa mashine ili kusudi na wananchi walioko upande wa vijijini waweze kupata maji mengi na ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo makubwa sana hasa katika Vijiji vya Mapinduzi, Ng'ong'ona, Matumbulu, Mkonze na Bihawana. Makorongo yote ambayo yako pale, wamechimba kupita kiasi na karibu yote wameshayachakaza, hawapati maji. Lakini kwenye baadhi ya vijiji hivyo, kuna visima vingi sana ambavyo vimeshachimbwa na mashine zilishakufa. Naomba mashine hizo zifufuliwe ili hata wananchi wa vijijini kule waweze kupata maji ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa sewerage system ambayo pia inasaidia sana kuweka Mji wetu uwe safi. Tunaomba gharama za sewerage system zipunguzwe ili ikiwezekana wakazi wote wa Mji wa Dodoma waweze kuvuta sewerage systems zipite kwenye maeneo yao kwa ajili ya kurahisisha usafirishaji wa majitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengi sana makubwa na ambayo nadhani nikiendelea kuyasilimulia hapa, naweza nikachukua muda mrefu na nisyamalize ambayo Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi imefanya, ni lazima tukubali kwamba bado yako matatizo makubwa sana hasa kwa upande wetu wa shirika letu la CDA ambalo bado liko hapa.

(Hapa kengele ya kwanza ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE: Kengele!

MBUNGE FULANI: Ndiyo!

MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE: Eeh! He!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa CDA tulishakubaliana na hii iko kwenye ukurasa wa 78. Kwenye ule ukurasa wa 78 Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe amekiri kwamba Serikali imekubali kuboresha na kuhalalisha maeneo yaliyojengwa kiholela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona huu ni uamuzi wa hekima na busara ya kutosha kwa sababu watu wametumia miaka mingi kudunduliza kujenga nyumba zao. Kuwabomolea nyumba zao ni kuwaletea ufukara usio wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashangaa kwamba pamoja na maamuzi hayo, bado baadhi ya maeneo CDA haikubali hata kidogo kwamba yapimwe, mojawapo likiwa ni eneo la Mbuyuni kule Nzuguni ambako wako zaidi ya watu 6000, wao wanataka wabomoe eti kwa kujenga viwanda. Tuliishaamua kabisa kwamba ardhi ya Dodoma ni kubwa sana, watafute maeneo mengine, lakini bado wameng'ang'anika.

Pia bado kuna maeneo ya Chaduru pamoja na Swaswa, wamekataa kutoa viwanja ili wananchi wa maeneo hayo waweze kuhama. Wamewawekea "X" wanawaambia wasijenge wala kukarabati. Kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa kama mvua mbili kubwa zitanyesha tena, nyumba zaidi ya 500 zitaanguka hapa Dodoma. Tunashindwa kuelewa ni kwanini wanazuia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo eneo ambalo lilijulikana kama ni eneo la kijani, lakini baadaye limefutwa na kwamba linatakiwa lipimwe. Eneo hilo liko katika Kata ya Nzuguni na tulishakubaliana kabisa kwamba Halmashauri ya Manispaa ndiyo ipime. Lakini sasa wamekataliwa kwamba wasipime, watapima CDA, lakini hawapimi. Kwa hiyo, wanaendelea kuwatesa wananchi na mpaka dakika hii, watu hawaridhiki hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie tu kwa kusema kabisa kwamba, juu ya matatizo ambayo yanajitokeza, Waheshimiwa Mawaziri, tumewasikiliza CDA vya kutosha, turudi nako kule kwa Wananchi tukawasikilize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya CDA kwamba mkienda kuwasikiliza wananchi eti watawapiga mawe, au watawazomea, siyo ya kweli. Waache mikwala ambayo wanaweka

wao kwamba kuingia kwenye Ofisi zao ni lazima uingie na kadi. Ile kadi unatumbukiza pale kwenye mlango, halafu baadaye unaulizwa kwamba wewe ni nani? Wakiona kwamba wewe ni mtu ambaye unadaidai ardhi, unaambiwa toka hapa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, CDA wamegonganisha wananchi maeneo ya lhumwa, ardhi ile sasa wamewapatia Wanajeshi ili wananchi wapigane nao. Wamewanyang'anya ile ardhi ambayo iko kule maeneo ya Msalato wamewapatia Polisi ili wananchi waweze kupambana nao. Tunaomba tabia hii ife.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanadai fidia ya zaidi ya Shilingi bilioni tatu hasa katika yale maeneo ya Msalato yaliyochukuliwa kwa ajili ya kujenga uwanja wa ndege, hawajalipwa mpaka leo. Bado wale wa maeneo ya Iyumbu wanadai Shilingi bilioni 1.6 hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie suala hili. Nataka nilete ujumbe hapa ambao nimetumwa kwamba mara nyingi wananchi wa Dodoma wamekuwa wakidanganywa hasa kutokana na matatizo ya CDA kwamba tutayatatua, lakini uchaguzi ukishapita, bado hakuna kitu ambacho kimetendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamejifunza hili katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa zilizopita. Walidanganywa, safari hii wamesema hawako tayari kupigia kura Katiba Inayopendekezwa na wala hawako tayari kupiga kura kwenye Uchaguzi wa Oktoba, 2015 mpaka maeneo yote haya wahakikishe kabisa kwamba Serikali inasema nini na inatoa kauli gani hapa katika hitimisho la Waziri Mkuu, kama yale maeneo mengine nayo yatapimwa. Vinginevyo, watajua kwamba wanadanganywa na kwa vyovyote vile moja kwa moja hawatakuwa tayari tena kupigia kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hili *seriously*, naomba nipate majibu, ndipo nitatoa majibu kama naunga mkono bajeti hii au la. Vinginevyo, sitaweza kueleweka na wananchi wangu. Nawashukuruni sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Diana Chilolo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbassa na Mhashimiwa Sylevester Mabumba ajiandae.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu. Kwanza kabisa nataka nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nawapongeza Mawaziri wote ambao wako chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu; Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Hawa Ghasia na Manaibu Mawaziri, kwa kweli wanafanya kazi nzuri. Baada ya pongezi hizo, niwapongeze pia Watendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI chini ya Dkt. Fatuma Mrisho pamoja na Kamishna wa Uratibu wa Dawa za Kulevya mpya ambaye ameteuliwa kwa kazi nzuri anazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafsi hii kuishukuru Serikali kwa namna ya pekee sana kwa kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa UKIMWI, Shilingi bilioni tatu, ambazo nimeziona ndani ya bajeti. Naiomba Serikali, kwa kuwa imeonesha nia thabiti ya kupambana na UKIMWI, fedha hizi ambazo zimeanishwa hapa Shilingi bilioni tatu zije zionekane na zifanye kazi isije ikawa kitendawili, tunaandika maandishi mazuri lakini utekelezaji unakuwa mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano mmoja mdogo; Tume ya Dawa za Kulevya, bajeti hii ambayo imebakia mwezi mmoja imalizike, ilikuwa imetengewa Shilingi bilioni nne, lakini mpaka sasa hivi fedha ambazo wamepata ni Shilingi bilioni 1.5; Shilingi bilioni 2.5 hazijapelekwa

na umebakia mwezi mmoja tu. Naiomba Serikali tunapoamua kufanya jambo, tufanye kiukweli. Hii habari ya kuainisha tu maandishi halafu utekelezaji unakuwa mdogo, haipendezi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia katika vita dhidi ya dawa za kulevya, watu tunaopambana nao ni matajiri, sasa kama Watendaji hawatakuwa na fedha ujue, upambanaji huo ni mgumu sana. Naomba chonde chonde, kazi iliyoonyeshwa ya kutenga fedha hizi za kupambana na UKIMWI ni nzuri na mfuko huu sasa umeonyesha sasa unaanzishwa, ninaomba sana fedha zije zitengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naiomba Serikali, pia ile kanuni watakayoitengeneza kwa ajili ya kusimamia mfuko huu wa UKIMWI, basi iwe na meno. Kanuni hiyo iainishe namna bora ya vyanzo vya mapato vya kuingiza fedha kwenye UKIMWI. Leo tumetengewa bila kujua zimetoka kwenye eneo gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tumefanya ziara Botswana, tumekuta wenzetu wana vyanzo kabisa vya mapato vinavyoingia kwenye Mfuko wa UKIMWI. Unakuta kodi za wafanyakazi nchi nzima zinapokusanya, kabla hazijaingia Hazina, wanakata 3% zinaingia kwenye Mfuko wa UKIMWI. Nasi kwenye Kanuni yetu, tuainishe vyanzo vya mapato vitakuwa ni nini ambavyo vitatunisha huo Mfuko wa UKIMWI.

Vilevile ioneshe namna bora ya kugawanya zile fedha, tusipeleke tu fedha kiholela. Tutakapoonesha namna bora ya kutumia hizo fedha, tutakuwa tumesaidia sana suala la UKIMWI kupata matumizi mazuri.

Kwa mfano, mpaka sasa hivi tunawapa dawa wagonjwa wenye CD4 mwisho 350, tufike mahali tutoe dawa kwa wenye CD4 500. Tukishapeleka hizi fedha, ninaamini wataanza kupata dawa mpaka kwa wenye CD4 500. Ni vizuri kumtibu mtu bado ana nguvu kuliko kusubiri mpaka wadhooifike. Hiyo hatuwasaidii, tunapunguza nguvu kazi ya Taifa. Naishukuru sana Serikali kwa kazi hiyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kuhusu hizi *sober houses*. *Sober houses* zilianzishwa na wenzetu walioathirika na madawa ya kulevya na baadaye wakapona. Naiomba Serikali iingilie kati, ipeleke wataalam kwenye nyumba hizi ili huduma inayotolewa kwenye nyumba hizo iwe ya kitaalam. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumesaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Jenista, hili jambo alilichukua kwenye Kamati yetu vizuri sana na ninaamini atalifanyia kazi na litatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hilo, nataka niongelee kuhusu Mfuko wa Vijana na akina Mama. Mfuko huu kwa kweli ni mzuri sana, lakini hautoshelezi. Vijana wanahitaji kujijiri, watajijiri vipi wakati wanakopeshwa kwa fedha ndogo? Naiomba Serikali iangalie namna bora ya kusaidia vijana wetu ili waweze kujijiri pamoja na akina mama kuondokana na umasikini; kwa sababu Serikali imekuwa na malengo mazuri sana, imeamua kuanzisha vyuo vya ufundi kila Wilaya ili vijana wapate elimu waweze kujijiri. Sasa tukubali kwamba, tupeleke pia fungu la fedha kwenye Vyuo hivi vya VETA ili vijana wanapomaliza mafunzo wapewe vifaa vya kujijiri. Kijana kama atatoka na elimu yake, lakini hana mtaji wala vifaa, unafikiria atajijiri vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie namna bora ya kupeleka fedha kwenye vyuo hivi vya VETA na fedha hizo basi ziainishwe kwamba kila mwanachuo anapohitimu, apewe vifaa vya kuondoka navyo ili awe na uhakika wa kujijiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile namwombe Mheshimiwa Jenista, alitembelea pale Manyoni kuona yale majengo ambayo tumepewa na Wakandarasi wa barabara ambayo

tunategemea majengo hayo yafunguliwe Chuo cha VETA. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri aliishayaona majengo hayo na yanafaa, hebu aniambie humu ndani, mbona sioni fedha alizozitenga kwa ajili ya kuanzisha Chuo hicho? (Makofi)

Naomba watakapokuwa wana-*wind up* hebu aoneshe *seriousness* kwamba, majengo yale aliyoyaona yametengewa fedha na Chuo hicho kinaanza mara moja kwa ajili ya vijana wetu kuweza kufika mahali wapate elimu na waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongelee kuhusu Halmashauri zetu za Wilaya na Miji. Halmashauri hizi zilizo nyingi Wakuu wa Idara hawapo, wanaofanya kazi ni Makaimu. Hivi ni kwanini tunafanya kazi na Makaimu wakati tuna wasomi wazuri? Kama watu mmeshawaona wanafaa, hebu mwathibitisha wafanye kazi ili wajiamini. Hatutategemea ufanisi wa kazi ndani ya Halmashauri kama zitaendeshwa na Makaimu Wakuu wa Idara. Naomba sana suala hili lipate ufumbuzi wa kutosha kwa sababu wasomi wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kuhusu ujenzi wa Uwanja wa Ndege Singida. Ndugu yangu leo ni miaka 15 niko hapa tunaongelea Uwanja wa Ndege wa Singida. Serikali imeahidi lakini mpaka leo hapajatekelezwa. Nnaomba kiwanja hicho hebu kiongezwe upana mdogo tu ili angalau hata ndege za abiria zianze kutua kule. Hata sisi tunahitaji kupanda ndege! Watu wameishaondokana na umaskini wana hela za kusafiri katika usafiri salama. Naomba sana suala hilo wakati Waziri Mkuu ana- *wind up* napo tupate majibu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niongelee kuhusu ujenzi wa Mahakama Kuu Singida. Naiomba sana Serikali tuliishaahidiwa mara nyingi, naiomba sana Mahakama Kuu sasa fedha zionekane kwenye bajeti hii tunayoijadili ili ujenzi uanze kwa sababu tayari chini ya uongozi wa Mkuu wa Mkoa tuliishaanisha, kiwanja kizuri kipo, tuanze kujenga Mahakama Kuu ili azma ya Serikali ikamilike. Hamwezi kuwa mnatuhidi tu, hamtekelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni Hospitali ya Rufaa ya Singida. Serikali mmekuja wote! Mheshimiwa Rais kaja, Makamu wa Rais kaja, Waziri Mkuu kaja, sijui mkuu gani kaja; mmeona hospitali ile ilivyo nzuri, hata Muhimbili haitaikuta Hospitali ile. Hivi mnapata kigugumizi gani kutenga fedha kidogo tu pale ili tumalize hospitali hiyo? Vifaa viko pale vimeletwa, Mkuu wa Mkoa anachukua likizo kwa nauli yake mpaka Amerika anatafuta fedha, analeta, anafanya kazi nzuri. Kwanini Serikali isionyeshe kumuunga mkono huyu Mkuu wa Mkoa kwa kuongeza fedha? Badala ya kutupa Shilingi bilioni mbili, hebu tupeni hata Shilingi Shilingi bilioni nne ili tumalize hospitali hiyo.

Mheshimiwa Spika, hospitali hiyo ikifanya kazi, watu wa Tabora watatibiwa, watu wa Manyara, Singida na Shinyanga watatibiwa. Jamani kazi nzuri hiyo iliyofanywa, mnataka kweli tuwe tunatazama majengo tu, mpaka vifaa na dawa vifike mahali viweze ku-*expire*! Mpaka madawa ya-*expire*! Naomba sana tufanye kazi kwa malengo. Naomba mtafakari, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anajibu hapa mtwambie fedha za kukamilisha Hospitali ya Rufaa ya Singida ni Shilingi ngapi mmezitenga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nataka nifike mahali nihitamishe kwamba mtenge fedha za kupima viwanja. Wanawake wanashindwa kukopa mikopo benki kwa sababu wanakosa dhamana. Viwanja ni dhamana! Hii kazi ya kupima viwanja kwenye vijiji, tuongeze kasi na tutenge hela ya kutosha ili viwanja vipimwe watu waweze kupata dhamana. Unapoenda benki unaulizwa, haya hati ya kiwanja iko wapi? Hati ya nyumba iko wapi? Lakini hii yote inatokana na kwamba *seriousness* ya Serikali ya kupima hivi viwanja kwenye vijiji vyetu ni ndogo. Tuongeze kasi, viwanja vipimwe ili watu waweze kupata dhamana ya kukopa fedha kwenye benki zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja iliyo mbele yetu. Kwa kweli kazi inayofanywa na Serikali, naomba Wabunge wenzangu wakubaliane na Serikali. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Chilolo, namwita Mheshimiwa Anthony Mbassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mabumba na Mheshimiwa Elizabeth Batenga.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia pumzi na afya njema ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu nami kutoa mchango wangu katika hoja inayoendelea hususan hotuba ya Waziri Mkuu inayohusiana na Bajeti inayoendelea.

Pili, nawashukuru zaidi wananchi wa Jimbo la Biharamulo Magharibi kwa ushirikiano mkubwa na mzuri wanaonipa kwa kazi tunazozifanya za maendeleo katika Jimbo letu. Ninalotaka kuwaambai ni moja tu, uzi ni ule ule na kamba ni ile ile, ni lazima Biharamulo tuivushe. CHADEMA mtindo mmoja na ukawa ndiyo tumaini letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru zaidi familia yangu kwa jinsi wanavyonivumilia na usumbufu wanaoupata. Hakika niko katika majukumu ya kutimiza kazi za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Kiongozi Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni aliyotoa hapa ambayo ilikuwa imejaa mambo mazuri ya msingi ambayo kimsingi naomba ndugu zangu tusibeze, tuyasome na tutafakari ili tuweze kuvuka salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuongelea kwa fedha za maendeleo kuchelewa na kutotolewa kwa wakati. Nikiangalia Mkoa wangu wa Kagera, mpaka leo hii tunavyoongea hapa umeletewa asilimia 26 tu ya fedha za maendeleo na ukiangalia bakaa iliyobaki kwa muda uliobaki, fedha hii itakuja lini? Naomba wanapokuja kuhitimisha hapa, nipate hilo jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Jimbo langu la Biharamulo kwa kazi tuliyoifanya japo kwa makusanyo yaliyopatikana yametumika vizuri na ninawapongeza sana wasimamizi wote, lakini bado kuna tatizo kubwa sana, ukiangalia fedha iliyokuwa imetengwa ya Sh. 2,813,068,000/= zimepatikana Sh. 756,179,960/=, sawasawa na asilimia 27.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi za maendeleo kama haziletwi, tunategemea nini kitakachoendelea ndani ya Halmashauri zetu? Nalisema hili, Serikali imeshindwa kuleta fedha za maendeleo, lakini huko vijijini kuna michango tele! Wananchi wanalambishwa bakora, ndiyo zawadi zao, wakati Serikali hata halleti fedha. Tutakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike basi mahali basi hata huyu mwananchi tunayemchangisha wa bakora naye tumhurumie, kama Serikali haiwezi kutimiza wajibu wake. Jambo hili linasikitisha sana na tunaomba mamlaka zinazohusika basi, kwasababu kodi inakusanywa, lakini inarudije kwa mwananchi? Hatuioni! Tafadhali fedha hizi za maendeleo ziletwe ili miradi iliyoazimiwa iweze kutimizwa kwa muda muafaka tuweze kuendana na bajeti yetu ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirejea kwenye kitabu cha hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 71 kuna huduma kwa wazee na watu wenye ulemavu. Mimi ni Mjumbe wa Kamati za Huduma za Jamii, sehemu nyingi tumezungukia, hizi nyumba za wazee hazihudumiwi. Hali ni mbaya, mazingira ni mabovu, wazee Mungu wangu wamekata tamaa kana kwamba wao siyo raia wa

nchi hii. Hili jamani huwa naliongelea hapa kila leo, kuwa mzee ni dhambi? Au ni makosa? Naomba tafadhali Serikali itimize wajibu wake kwa kuwapelekea wazee huduma stahili mahali pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na suala hili, naongelea kuhusu wastaafu; naona Mheshimiwa Waziri Mkuu kawasahau wazee na wastaafu humu ndani. Wastaafu wanaishi maisha magumu sana, pensheni yao haitoshi, haitoki kwa muda. Leo hii viwango vinabadilika, gharama za maisha zinapanda, lakini wastaafu hawa wamesahaulika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Waziri Mkuu atakapokuja, aje na majibu kutuambia wazee hawa wanasaidiwa? Pensheni zao zitarekebishwa? Pamoja na mafao wanayoyapata kutoka katika Mashirika au Hifadhi za Jamii! Watu sasa hivi wanalia na NSSF. NSSF inatoa mafao kidiogo sana ukilinganisha na mashirika mengine ya mafao. Sasa tunajiuliza, kuna tatizo gani? Watu hawa walikuwa wanafanya kazi ya ajira ya aina moja, mshahara ni ule ule lakini wenzao wakistaafu wanalipwa pesa nzuri; hawa mafao yanayotoka NSSF yanakuwa kidogo sana! Naomba wanapokuja na majibu ku-*wind up* watueleze juu ya suala hilo, linafanyiwa kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hilo linaenda sambamba na wajane. Kuna wajane wanaohangaika na masuala ya mirathi, wamehangaika na kupitia hatua zote, lakini mpaka leo hii hawajaambulia hata tone la senti kama mafao ya wenzao ambao wamepoteza maisha. Njiuliza, kuna nini hapa? Ni taratibu gani zinazokosewa? Mbona kila kitu kinafanyika na *documents* zinaletwa? Wanapofuatilia, itabaki njoo kesho, njoo keshokutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natokea pembezoni huko Mkoa wa Kagera, Wilaya ya Biharamulo, wapo wajane waume zao wamefariki katika majukumu mbalimbali ya Kiserikali lakini mpaka leo hii hawajapatiwa mafao yao. Naomba tafadhali mnapokuja na majibu, mtuambie, hao watu watalipwa fedha zao za mirathi lini ili waweze kutunza familia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye ukurasa wa 77, kuna uanzishwaji wa maeneo mapya ya kiutawala. Tumepeleka sisi kama Wabunge wanne, Mheshimiwa Ntukamazina, Jimbo la Ngara; Mheshimiwa Eng. Chiza, Buyungu; Mheshimiwa Felix Mkosamali, Muhambwe; nami Mbassa, Biharamulo; kuomba kupata eneo jipya la Mkoa. Tumepeleka *document* yetu, tumeifanyia kazi, imepita katika hatua zote, lakini mpaka sasa hatuoni angalau katika mapendekezo wala hajui ni nini kinachoendelea. Tunaomba tupate angalau jibu ni nini kinachoendelea, kwasababu tulishapitisha katika vikao vyote na hatua zote muhimu zimepitiwa. Tunaomba tupate jibu juu ya hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kulikuwa na suala la uanzishwaji wa Mji mdogo wa Biharamulo ambao tulishapitia hatua zote na Mheshimiwa Aggrey Mwanri hapa nilimsumbua sana, akasema kuna kitu ambacho hakijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli tulikwenda kwenye Kikao cha RCC, ikaonekana Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya kilikuwa hakijakaa. Tumekaa kikao kile, kimebariki mambo yale na tumepeleka muhtasari, lakini mpaka sasa hatuoni kinachoendelea, kitu ambacho kinatuathiri katika uandaji wa Bajeti yetu ya Wilaya ya Biharamulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wanapokuja kujibu, basi waje na majibu ya nini kinachoendelea ili tuweze kujipanga vizuri. Tumesema Jimbo la Biharamulo ni maendeleo kwa kwenda mbele, masuala ya uzembe hatutaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala zima zima la Tokomeza. Suala hili limeleta ukakasi mkubwa sana. Tumeona Serikali ilivyowasafisha baadhi ya watumishi na

kuwaacha wengine ilhali haijawazungumzia kabisa wale wafugaji ambao wamepokwa mifuko yao na wengine wamepoteza maisha. Hili linaelewekaje? Juzi kimekaa kikao pale Lamadi, wakaitwa baadhi ya watu wachache, lakini hata kilichojadiliwa kilikuwa bado ni ukakasi. Tunaomba tupate majibu kwa wale wafugaji waliopokwa mifuko yao, waliopoteza mifugo yao na wale waliopoteza maisha, fidia yao ikoje? Tunaomba sasa tupate majibu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la Walimu. Nimekuwa nikiongelea hapa suala zima la Walimu kwamba wanakwenda kuripoti, wanarudishwa kwamba wamechelewa kufika kwenye vituo vyao. Hilo linaweza lisiwe sahihi sana kwasababu kulikuwa na athari ya mgomo wa madereva lakini bado wengine walikwenda kuripoti vituo mbalimbali. Lakini kuna Walimu wengine waliokwenda kuripoti, mimi baada ya kufuatilia nimekuta kwamba hawakuwa na vyeti na wameandikiwa waende wakalete vyeti ili kusudi waripoti wakiwa na vyeti halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali tafadhali pale inapoona kwamba kuna hili tatizo, watoe majibu ya haraka na waeleweke kwamba wanachokihitaji ni nini? Tuna shida ya Walimu kule pembezoni; Mwalimu anapofika tena akafukuzwa na huna uhakika wa kupata Mwalimu mwingine, ni shida kweli kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali hili ilifanyie kazi vizuri, wale watu ambao wameripoti katika muda huo, kama wameripoti na vyeti vyao safi na nini, wapokelewe na waanze kazi mara moja. Tuna uhitaji mkubwa sana Walimu. Tusije tukawakatisha tamaa vijana hawa ambao wanasota kupata elimu na bado wanasota kupata ajira ilhali tuna uhitaji mkubwa wa Walimu katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuongelea suala zima la mawasiliano. Nina shida ya mawasiliano katika Kata zangu mbili; Kata ya Nemba na Kata ya Nyakahula. Lakini mawasiliano haya, nilijaribu kuleta taarifa hapa na nikaahidiwa kwamba linafanyiwa kazi. Mpaka sasa yako maeneo kwa kweli upatikaji wa mawasiliano ni tatizo. Naomba ndugu zangu wa mawasiliano, mliangalie kwa makini suala hili ndani ya Jimbo langu la Biharamulo ili tuweze kuwa na mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika ni ya mwisho, nakushukuru, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, nimemwita Mheshimiwa Sylvester, atafuatiwa na Mheshimiwa Batenga, Mheshimiwa Herbert Mtangi, Mheshimiwa Teu na kama tutawahi na Mheshimiwa Kiwelu.

MHE. SYLVESTER MASELE MABUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Awali ya yote, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kupongeza hotuba ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi; na pia niwapongeze Wasaidizi wote katika Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa nmana ambavyo wameteteleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kusema kwamba Chama cha Mapinduzi ni Chama ambacho kina heshima kubwa sana ndani na nje ya Tanzania. Sasa anayebeza CCM, nadhani anabeza hata yeye uwepo wake hapa kwa sababu mwaka 1992 CCM yenyewe iliruhusu kuanzishwa kwa mageuzi ya Vyama vingi. Wale ambao walikuwa waasi, wakapata nafasi sasa ya kujiunga na kuwa na Vyama ambavyo sasa wanavyo. CCM isingefanya hivyo, naamini wasingekuwepo hapa. Kwa hiyo, ni lazima waipongeze sana CCM.

Mheshimiwa Spika, sifa ya CCM ni kwasababu ya kuwa na viongozi wazuri mahiri tokea Baba wa Taifa hadi Rais wa sasa Mheshimiwa Kikwete. Mheshimiwa Kikwete amefanya mambo makubwa sana. Ili nchi iendelee, ni lazima wanawake na wanaume wafanye kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Rais Kikwete ame-promote sana akina mama, ndiyo maana hata Katiba pendekezwa inaangiza kuwa na 50 kwa 50. Haya ni mambo ambayo ni lazima Watanzania tujivunie. Sasa kama kuna wengine wanabeza, inatia ukakasi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa nianze kutoa mchango wangu. Napenda sana Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja kujumuisha michango hii, atuambie; Serikali imejipanga vipi kulipa madeni ambayo Walimu wa kada mbalimbali wanaidai Serikali? Ili Taifa letu ili liweze kufankiwa ni lazima Walimu wetu wafanye kazi katika mazingira mazuri sana. Walimu wana stahiki nyingi ambazo wanadai. Naomba sana Serikali iangalie madeni haya, iweze kuwalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nipendekeze hapa, kuna Benki ya Walimu imeanzishwa, napenda kuishauri Serikali yangu kwamba kama upo uwezekano, ielekeze Halmashauri zote nchini kutenga asilimia fulani ya mapato ya ndani kuchangia kwenye Benki hii ili walimu waweze kupata mikopo yenye masharti nafuu na hivyo kuwaondolea shida na kero ambazo zinawasumbua Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili, napenda pia kada nyingine kama Wauguzi na Askari Polisi wetu, wana madeni makubwa; madeni ya likizo hawajapewa na tunajua kabisa watu hawa tunawatumia kwa ajili ya kulinda amani na utulivu katika nchi hii. Sasa hawawezi kuendelea na mambo haya kama wao roho zao zitakuwa zimenyongeka. Kwa mujibu wa kazi zao, watafanya kazi, lakini naiomba Serikali iangalie kulipa stahiki za Askari Polisi hawa, Wauguzi ambao pia wanalinda maisha yetu na pia kada nyingine ambazo zinaidai Serikali, basi Serikali itimize wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kupitia Wakala wa Umeme Vijijini, (REA), Tanzania sasa sehemu kubwa inang'ara kupitia Wakala huu. Lakini naomba sasa iongeze fungu lake kwa REA ili REA iweze kutimiza majukumu yake. Vijiji vingi bado havijapata umeme na ninaamini katika Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa, tumejipanga kuonyesha kwamba Tanzania inaangazwa kupitia Wizara ya Nishati. Sasa Serikali ipeleke fedha nyingi za kutosha kwa ajili ya Wakala huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nipongeze Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia TAMISEMI kwa mradi wa Usafiri wa mabasi yaendayo kasi Dar es Salaam. Lakini tunapofanya kazi hii ya kubadilisha Dar es Salaam kutokana na shida ya usafiri, naishauri Serikali ijipange katika Miji Mikuu mingine sasa. Tumejifunza adha na dhiki ya Dar es Salaam, lakini adha na dhiki hii haiko Dar es Salaam peke yake; ukienda Mwanza, Arusha, Mbeya, Tanga na Miji mingine mikubwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni wakati Serikali iwe na mpango mkakati kuonyesha kwamba Miji hii inaondolewa kero. Kwasababu muda tunaotumia kwenye foleni za magari katika Miji hii, inapoteza pia ari na kasi ya uzalishaji katika nchi yetu na hivyo tunakwenda kinyume kidogo na mikakati ambayo iko katika malengo ya milenia, katika MKUKUTA na pia katika maelekezo mbalimbali ya Mheshimiwa Rais kuonyesha kwamba Watanzania wanahudumiwa vizuri.

Kwa hiyo, naiomba Serikali iwe na mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba mbali ya Dar es Salaam, lakini Miji mingine mikubwa hapa nchini wanaweka utaratibu sasa wa kuwa na usafiri mzuri na wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila aliyechangia hapa ameonyesha namna ambavyo Halmashauri na Mikoa hapa nchini, fedha ambazo tuliidhinisha, zimepelekwa kiduchu sana, matokeo yake Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wameshindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo kama ambavyo tungewapelekea fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua, atakapokuja kujumuisha Waziri Mkuu atuambie tatizo liko wapi? Kwasababu Mkurugenzi Mkuu wa TRA siku zote anahutubia kwamba Taasisi yake inakusanya kwa 100% au zaidi. Sasa fedha zinakwenda wapi kiasi kwamba fedha ambazo Bunge lako Tukufu linaidhinisha hazipelekwi kwa wakati na zikipelekwa, zinakuwa hazitoshelezi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tuambiwe hapa, tatizo liko wapi? Fedha hizi zinatafunwa wapi? Hata Halmashauri zinashindwa kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi, Wakuu wa Mikoa wanapata taabu, Mikoa yao inashindwa kuhudumia wananchi, matokeo yake wananchi wanaanza kulalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, nilikuwa napendekeza kwamba kutokana na ufinyu wa fedha ambazo tunazo lakini pia nadhani hata vipaumbele vyetu ni kwamba tunakuwa na bajeti kubwa ambayo hela yake nyingi inaelekezwa kwenye matumizi ya kawaida, lakini fedha za maendeleo zinakuwa kidogo. Ni kwa nini tusiwe na vipaumbele vichache ambavyo tunaweza kutekeleza kwa ufanisi zaidi na baadaye tukaanza na vipaumbele vingine ambavyo pia vitatutua kero za wananchi? Mfano, Waziri wa Fedha alipowasilisha mpango wake na Bajeti yake ya mwaka 2015/2016 ni kama Shilingi trilioni 22 hivi, lakini Shilingi trilioni tano tu inakwenda kwenye maendeleo.

Sasa tunaposema tuna Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa, nashindwa kuelewa ni kwa namna gani mpango huu tunaweza kuufikia. Pia tunapoteketeleza MKUKUTA ambao unatutaka ifikapo mwaka 2025, nchi hii iwe na kiwango cha uchumi wa kati, huku eneo kubwa la bajeti yetu inakwenda katika matumizi mengineyo; na hata ile ya maendeleo unakuta tunategemea wahisani. Napenda kujua, vipaumbele vyetu hasa ni vipi, hata tunakwenda kuwa na bajeti kubwa kwa upande wa matumizi ya kawaida?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukiangalia kwenye Fungu 25, sehemu ya mshahara ni ndogo sana kuliko matumizi mengineyo. Kuna Shilingi bilioni 1.6 Ofisi Kuu; lakini kuna matumizi mengineyo ya 4.09 billion ambayo yanakwenda karibu mara tatu au mara nne ya stahiki za Watumishi katika Ofisi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua, hali hii inakuwaje? Kwamba unakuwa na wafanyakazi kidogo, lakini matumizi ya wafanyakazi hao yale ya kawaida ni makubwa sana na huku tunatekeleza Mpango wa MKUKUTA?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka nishauri kwamba tunazo programu nzuri. Tunayo Programu ya Kilimo Kwanza, tuna programu sasa ya Matokeo Makubwa Sasa, lakini nilikuwa napenda kushauri, kabla ya kuingia programu nyingine, Serikali itupe tathmini. Mfano, namwomba Waziri Mkuu atakapokuja kujumuisha atupe tathmini ya Programu ya Kilimo Kwanza, imefanikiwa kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unawakuta Waheshimiwa Wabunge ambao Mikoa yao ndiyo magwiji katika uzalishaji wa mazao, mazao yao yanaoza mashambani, wakulima wananyongeka. Ni kwa namna gani tutawatia moyo wakulima hao wazalishe wakati walichoza lisha hakikununuliwa, kimeoza mashambani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ije tathmini kabla ya kuingia programu nyingine. Hii itawatia moyo wananchi wetu na kuweza kuangalia changamoto ni zipi? Tumefanikiwa wapi? Tumeshindwa kufanikiwa sehemu gani? Kwa nini tulishindwa? Tufanye nini? Hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nizungumzie suala zima la amani ya nchi yetu. Nampongeza sana Msajili wa Vyama Vingi kwa maelekezo yake kwamba ili tuwe na utulivu, Vyama Vya Siasa viache kuwa na vikundi vya ulinzi; vikundi ambavyo bahati mbaya vingine vinapewa mafunzo ya kivita ya kijeshi. Nilikuwa napendekeza, mapendekezo ya Msajili wa Vyama Vingi Vya Siasa, Vyama hivi vya Siasa viyaheshimu; naye asisite kuchukua hatua kali kwa Vyama ambavyo vina vikundi ambavyo kwa kweli vinatishia amani ya nchi yetu. Kwa kufanya hivyo nchi yetu itakuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
Kwa muda wa Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, ni kengele ya pili!

MHE. SYLVESTER MASELE MABUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Batenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mntangi na Mheshimiwa Gregory Teu, ajiandae.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie machache katika hotuba ya Waziri Mkuu na Waziri wa Nchi, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake; naipongeza Serikali kwa ujumla kwa kazi kubwa na nzuri, kwa kuleta maendeleo makubwa ambayo yanaonekana kwa macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wale wasioona, basi waendeleo kutoona labda itawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupongeza, kweli barabara zimejengwa, lakini zinaharibika upesi kwa sababu ya kubeba mizigo mizito. Mizigo mizito yote inapita juu ya barabara! Sasa sijui Serikali haijaona umuhimu wa kuweza kushughulikia reli ili ipunguze mizigo hii mizito inayopita juu ya barabara na barabara zikaharibika upesi! Pia kuwajali wananchi wa Mikoa ya Ziwa na humu katikati kwa sababu wanaadhibika sana kununua bidhaa kwa bei kubwa sana kwa sababu zinasafirishwa kwa njia ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuiuliza Serikali, hivi haioni umuhimu wa kujenga reli? Iwe ni reli ya kati, reli inayokwenda Arusha, Singida na kwingineko. Naomba, kama inaona umuhimu, basi Serikali iunde mfuko wa reli ambao utaitwa *Tanrailways* kama ilivyo *Tanroads*, ili tujue kwamba na yenyewe itakuwa na mfuko wake wa kuimarisha hizi reli. Bila reli baadhi ya maeneo ya nchi yanajisikia kana kwamba hayako Tanzania. Mkoa wa Kagera tunajisikia kama vile hatuko Tanzania, kwa sababu vitu tunanunua kwa ghali sana, kwa sababu zinasafirishwa kwa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kuunda Mfuko wa *Tanrailways*, basi tukumbuke kwamba Mheshimiwa Rais aliahidi watu wa Mkoa wa Kagera, Mwanza na Mikoa yote ya Kanda ya Ziwa kwamba tungepatiwa meli mpya ambayo ingefanya kazi katika Ziwa Victoria badala ya MV. Victoria ambayo sasa hivi haifanyi kazi. Kwa hiyo, Mkoa wa Kagera sasa

hivi kwa kweli ni mateso makubwa sana tunayopata kwa usafiri wa abiria, pia hata kusafirisha mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika mwezi huu mmoja na nusu uliobaki, sijui atatuhakikishia kwamba hiyo meli itapatikana! Tunaisubiri kwa hamu na tunauliza na tutaendelea kuuliza hiyo meli. Lakini napenda tusiendeleo kuuliza, meli hiyo tuletewe, tupate kupunguza matatizo yanayotukabili sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa kufikiria na kuamua kukarabati viwanja mbalimbali vya ndege kama alivyoeleza katika hotuba yake, kimojawapo kikiwa Bukoba. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kukarabati hivi viwanja na upungufu wa fedha uliopo, bado Serikali imeendelea kushika maeneo mbalimbali. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, tumetembea sehemu mbalimbali. Musoma kuna eneo kubwa ambalo lilishikwa kwamba kutajengwa kiwanja cha ndege miaka mingi, wananchi wamezuiwa kulima, wamezuiwa kufanya kitu chochote katika ardhi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie zaidi eneo la Mkajunguti Bukoba, Wilaya ya Misenyi. Eneo hilo limekamatwa, wakasema kitajengwa kiwanja kikubwa cha ndege kikubwa cha Kimataifa. Kwa hali ninayoiona, kuna miaka mingi ya kusubiri kujenga uwanja huo. Sasa kwa vile wananchi hawa hawajapewa fidia, tunajua ardhi ni mali ya Serikali, lakini wananchi kama wanaitumia, Serikali inapoamua kuichukua, ni lazima iwafidie.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, niseme moja kwa moja kwako wewe, watu hawa wa Mkajunguti wamehangaika sana kuuliza hatma yao. Wameandika barua nyingi ambazo hazijajibiwa na Wizara inayohusika. Wakaamua kuja kwako kana kwamba wanakwenda kupata jibu la uhakika. Walikuja na barua mkononi. Uliwakaribisha, ukawapa soda, ukawapa juisi, chai na keki, kwakweli wakafurahi sana, wakaondoka wanashangilia. Wakasema sasa tumemaliza tatizo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa masikitiko, hata ile kuwajibu tu kwamba Serikali ina mpango huu, kwamba mtarajie lini mtapewa fidia, kwakweli inashindikana! Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu nilikuwa naomba, hii utanieleza wakati wa kujumuisha; yaani itaingia sasa kwenye *handing over notes* zako unapofunga Ofisi yako hiyo kwamba kipindi chako kimekwisha, utaiandika kwenye *handing over notes*, au utatuambia katika kujumuisha kwamba watu wa Mkangujuti mtalipwa lini na mtalipa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, kumwambia mtu ukweli ni kumheshimu. Lakini kama huwezi kumjibu, ukamwambia ukweli wako, unacho ama huna, akajua, kwakweli ni kumdharau, tena ni kumnyanyasa Mtanzania ndani ya nchi yake. Nakuomba radhi kwa kusema haya, lakini yanauma sana. Kwa hiyo, nadhani tutajibiwa wakati wa majumuisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine imeelezwa kwenye hotuba kwamba Serikali ina mpango wa kujenga, kuimarisha bandari mbalimbali, Mtwara, Tanga na nyinginezo, lakini pia kujenga bandari ya Bagamoyo; na wenyewe ni mpango mzuri. Lakini kabla ya kujenga Bagamoyo, kwanini tusiimarisha, tukapanua Bandari ya Dar es Salaam, tukaiunganisha na reli ili mabehewa yaweze kuchukuliwa na reli kutoka bandarini na kusafirishwa huko yanakokwenda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba gati namba saba na namba nane; gati namba 11 mpaka 13, zijengwe ili kazi za bandari zifanyike kwa ufanisi zaidi, meli kubwa ziingie na kuleta mizigo na kupakuliwa kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
Kwa muda wa Mzungumzaji)*

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naunga mkono hoja pamoja na hayo yote. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Mntangi, Mheshimiwa Teu simwoni, atafuatiwa na Mheshimiwa Kiwelu.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia. Napongeza sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo Ofisi inayosimamia Wizara zote, ndiyo maana ukitazama kwa makini hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, imegusa sekta zote; kuanzia Kilimo, Maji, Ufugaji; zote zimeguswa. Ni mambo makubwa ambayo yamefanyika! Wote tunajua Kiswahili na taarifa hii imeandikwa kwa lugha ya Kiswahili, nina imani wote tutaielewa vizuri na tutampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Hata hivyo, niwapongeze ndugu zangu wa TAMISEMI kwa kazi nzuri ambayo wanaoifanya ya kusimamia Halmashauri zetu. Kazi wanayoifanya ni nzito, ni kubwa, lakini wanajitahidi. Naomba tu wafanye jitihada za kuhakikisha utaratibu wa kufikisha fedha kwenye Halmashauri hauna matatizo makubwa. Fedha ziwe zinakwenda kwa urahisi na kuzifikia Halmashauri zetu kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muheza jambo letu moja kubwa kwanza kwa Waziri Mkuu, ni kwamba Muheza ni Mji mdogo na tumekwishaomba kuwa Mji kamili. Muheza ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ya Muheza.

Kwa hiyo, tunastahili kwa kweli kuwa Mji. Vigezo vyote vya kuwezesha Muheza kuwa Mji tumevikamilisha. Mpaka hatua za kuweza kupitisha maombi rasmi kwenye Halmashauri Kuu ya Mkoa; RCC Mkoa wa Tanga, tumefanya hivyo na maombi hayo yameshafika TAMISEMI. Nina imani kabisa yamefika katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Tunachosubiri ni kuhakikishiwa Muheza na sisi tunakuwa Mji kama ambavyo wenzetu wengine wamefanikiwa kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, manufaa makubwa ni Muheza vilevile tukishakuwa Mji tutaweza kuwa na Halmashauri ya Mji na tutakuwa na Halmashauri ya Muheza. Sasa sijui wataita Muheza Vijijini au vipi, lakini uamuzi utafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine kubwa Muheza ni ahadi za Mheshimiwa Rais. Nimetoa mapendekezo mara kwa mara na nikasema, ni vizuri kumsaidia Mheshimiwa Rais. Anapotoa ahadi siyo rahisi kuzikumbuka zote. Kwa hiyo, kuwe na kitengo maalum cha Serikali kitachokuwa kinasimamia na kuona kwamba ahadi hizo zinatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nakuja tena na ushauri kwamba kitengo hicho sasa kwa ushauri wangu kiwe ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwakuwa yeye ndiye anayesimamia Wizara zote. Ahadi yoyote Mheshimiwa Rais atakayokuwa ameiweka, huyu aliyepo sasa na hata huyu atakayekuja baadaye, itagusa mojawapo ya hizo Sekta, kwa maana hiyo itakuwa inasimamiwa na mojawapo ya Wizara katika utekelezaji.

Kwa hiyo, chombo hicho kikiwepo, kitakuwa kinajaribu kufuatilia kila bajeti ya Wizara, sekta ile inayosimamia ahadi ya Mheshimiwa Rais, itakuwa pia inatoa mawazo kwa Wizara zinazohusika kukumbushia ahadi hizo za Mheshimiwa Rais ili utekelezaji uweze kufanyika kwa wakati. Naomba hilo lifanyiwe kazi kwa kuheshimu kabisa ahadi za Mheshimiwa Rais. Anayekuja naye atapita kwenye kampeni, atatoa ahadi vilevile. Jambo kubwa ni utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya hizo ahadi kwa Muheza ya kwanza ni ya maji. Nafahamu kwamba yupo Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba naye atoe kauli kuhusu mpango wa maji Muheza Mjini ili kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais. Nafahamu kinachoendelea, nimeshawaambia wananchi wangu, lakini wananchi wangu wanataka kusikia sasa kauli kutoka kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini na kauli kutoka kwa Waziri mwenyewe wa Sekta ya Maji. Wahisani wamejitolea, wamekuja, wamekutana na wenzetu kutoka Wizara ya Fedha na Wizara ya Maji, nnaamini jibu sahihi litatokea.

Pamoja na hayo, nachukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa jitihada ambazo ameonyesha kuisaidia Muheza katika Sekta ya Maji. Namshukuru sana na nina imani ataendelea kutusaidia. Naomba pia nimshuruku Naibu Waziri wa Fedha ambapo alikuja Muheza na katika suala la maji akaweka pia uwezekano wa kuweka ahadi ya kupata fedha kupitia kwenye bajeti. Laiti kama fedha kutoka kwa Wahisani zitakuwa hazijapatikana, naamini kabisa hili litafanikiwa aidha kwa Wahisani au kupitia bajeti kuu kama Naibu Waziri wa Fedha alivyotuahidi.

Jambo lingine kubwa sana Muheza ni barabara ambayo pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Lami kilomita 34 kutoka Muheza kwenda Amani. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu na Ujenzi, Mheshimiwa Magufuli. Katika kipindi ambacho lami bado haijawekwa, jitihada ambazo mimi na yeye tumekuwa tukishirikiana ni kuhakikisha tumefanikisha kuweka zege katika kona zote hatari zaidi ya kona tisa zilizoko katika mteremko wa hiyo barabara inayotoka Amani kuja Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kona hizo sasa zimewekwa zege na zinapitika wakati wote. Magari hata madogo leo ninavyozungumza yanapeleka watalii huko Amani katika eneo ambalo ni kivutio kikubwa pia cha utalii unaoingizia nchi hii fedha nyingi za kigeni. Jitihada za kuweka lami, ahadi ya Mheshimiwa Rais najua inaendelea vizuri, tathmini imeshakamilika. Mara ya mwisho Mheshimiwa Rais alipokuja Muheza mwaka 2014 mwezi April alirudia tena ahadi hiyo na akawahakikishia wananchi wa Muheza kwamba Mkandarasi atakuwepo kuweka lami, kabla ya mwisho wa kipindi chake cha Urais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Sekta ya Kilimo tuna mradi mkubwa wa umwagiliaji. Namshukuru sana *Engineer* alifika, aliyekuwa Waziri wa Kilimo wakati huo. Bwawa ambalo limejengwa ni kubwa kweli kweli na Serikali imetumia zaidi ya Shilingi bilioni moja kwa kufanya kazi hiyo. Kazi ambayo ipo mpaka sasa hivi ni ujenzi wa Mifereji na hatimaye kuweka maeneo maalum kwa ajili ya wakulima hao. Wachama wapo zaidi ya 100. Mfereji mkubwa wa kwanza umekamilika, huu wa pili unakwamakwama kwa sababu fedha hazijafika. Ndugu yangu Mheshimiwa Chiza ulikuja pale, nimeahidiwa pia na Mheshimiwa Naibu Waziri aliyepo sasa hivi, atakuja kuangalia ili kuweka kasi ya kukamilisha hiyo mifereji na wakulima waweze kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tuwashukuru sana wenzetu wa Kampuni za Simu. Katika suala la ajira hapa Tanzania wametusaidia sana. Kila utakapokwenda, wapo Mawakala ndani na nje na wanafanya kazi. Bila Kampuni hizo kuwepo, Mawakala hao na ndugu zetu na huduma ambazo tunapata, tusingezipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine moja kubwa, nilishukuru Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kukubali kupitisha sheria iliyoruhusu bodaboda, yaani pikipiki kuwa chombo cha usafiri. Wengine tulipotoka nje ya nchi ya Tanzania, tuliyaona hayo, hasa kule Afrika Magharibi. Kwa hiyo, tulipoleta mawazo na mapendekezo, Serikali imeyakubali. Leo bodaboda kila mahali na ajira imekuwa kubwa. Ukifanya tathmini kwa nchi nzima, siyo chini ya milioni moja waajiriwa wa bodaboda hapa nchini. Katika Mkoa wa Tanga, Wilaya ya Muheza tunashukuru, tuna bodaboda nyingi kuliko mahali pengine popote ndani ya Mkoa wa Tanga. Kwa hiyo, vilevile nitoe shukrani kwa viongozi wangu; Mkuu wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya aliyekuwepo Mheshimiwa Subira na huyu aliyekuwa sasa hivi, wote wanafanya kazi vizuri ya kuwaelimisha wananchi na kujenga msingi mzuri wa kuweza kuwaletea wananchi maisha bora. Nawapongeza sana viongozi hao na ninawaomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki, waendeleo kuwasaidia wananchi wetu wa Wilaya ya Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo. Nashukuru sana kwa haya machache niliyosema, kwa nyongeza nikipata nafasi kwa Wizara zinazohusika nitayaongezea vizuri zaidi. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mntangi. Namwita sasa Mheshimiwa Kiwelu!

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nami niweze kutoa mchango wangu mdogo kwa hotuba hii ya Waziri Mkuu. Nianze kwa kuipongeza hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani pamoja na Mawaziri Vivuli waliofuatia, ni hotuba nzuri na ukiona CCM wameisoma, basi ujue dozi imewafika na imewatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wa Chama cha Mapinduzi wamesema kwamba Wapinzani hatuna macho, napenda kuchukua nafasi hii kuwaambia kwamba tuna macho, tuna midomo na tuna masikio na ndiyo maana tunayasema hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiishauri sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa miaka mitano, lakini sasa ni zamu ya UKAWA kuongoza nchi hii. Tumewashauri, hamtaki kuchukua ushauri wetu, ndiyo maana leo mambo mengi hayatekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoka kupitisha bajeti mwaka 2014, lakini Wizara nyingi, Mikoa na Halmashauri zetu bajeti haikwenda kama tulivyopitisha hapa. Tumekuwa *rubber stamp*, tunapitisha bajeti, bajeti haipelekwi tunakuja kupiga maneno tu hapa. Sasa muda wa maneno umekwisha, tunawaambia Watanzania sasa ndiyo muda wao wa kuibadilisha Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la afya, tulipitisha hapa kwamba akina mama wanapokwenda hospitalini wapate vile vifaa vya kujifungulia bure. Chama hiki cha Mapinduzi ambacho kinasema ni Serikali sikivu, lakini leo tunaona akina mama wanapofika kule mahospitalini, wanadaiwa vifaa hivi na wakishindwa kuvipata, akina mama wanapoteza maisha wao au watoto wao. Tukisema, mnasema hatuna macho. Tunayaona ndiyo maana tunayasema leo tena kwa mara nyingine, kwa miaka mitano, sasa imetoshia! Hatuwezi kuona akina mama wanakufa kwa sababu ya ahadi zisizotekelezeka za Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme suala la ajira kwa vijana. Tumewapa matumaini makubwa sana kwamba watapata ajira; ajira haijapatikana mpaka leo na kama imepatikana ni kidogo sana na inapatikana kwa wale watoto wa vigogo. Kwa watoto wa wananchi masikini ambao hawana watu wa kuwapigania, ajira hizi hazipatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliona Uhamiaji, sisemi uwongo, tumeyaona, tumesoma. Ndiyo maana nasema tuna macho, tuna mdomo, ndiyo maana tunayasema leo. Kwa hiyo, niwaambie Watanzania, mkitegemea ajira kwa Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, haiwezekani! Kama zitapatikana, basi zitapatikana kwa wale wale ambao wamo humo Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewasikia Waheshimiwa Wabunge hapa wakiipongeza Serikali, najiuliza, hivi hawa wanatokea wapi? Wanatoka Tanzania hii na vijiji hivi ninavyovifahamu vya Tanzania ambako hakuna maji? Tunaona Watanzania leo wanakunywa maji na mifugo, maji ambayo ukiyaona utafikiri ni chai ya maziwa iliyoongozwa majani; ina viluilui! Wananchi wetu hawapati maji safi na salama, leo tunasimama hapa tunapongeza. Ndiyo maana Mheshimiwa Esther amesema hapa, tuhakikishe Redio Tanzania inafanya kazi ili Watanzania wasie Wabunge wao waliowatuma humu ndani kuwatetea mambo wanayoyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatia huruma sana ukiwaona Watanzania wanavyohangaika. Wakulima leo tuliwaambia walime; wamelima, hawana mahali pa kuuza mazao yao. Wamekwenda kukopa...

MBUNGE FULANI: Si mnunue nyie!

MHE. GRACE S. KIWELU: Tunanunua wapi wakati ninyi ndiyo Serikali tuliowapa madaraka? Mnashindwa kutimiza wajibu wenu, mnasema sisi tununue! Tununue kwa pesa zipi? Ninyi ndio mnaokusanya kodi. Serikali makini ni lazima ihakikishe wananchi wake wanapata huduma zote muhimu; kuwatafutia masoko wananchi wao, kuhakikisha wanapata huduma zote muhimu za kijamii ikiwemo afya, maji na elimu. Lakini mkituambia leo kwamba nyie mfanye, mmetupa nafasi? Ndiyo maana nawaambia Watanzania leo kwamba umefika wakati sasa wa kuachana na Serikali ya Chama cha Mapinduzi na kuichagua UKAWA. *(Makofi)*

Mnasema kwamba hatuna nguvu ndiyo maana tumekimbia kujiunganisha; kilio kikubwa sasa hivi kwa Watanzania ni Vyama vya Upinzani vyenye dhamira ya kweli tuunganishe nguvu tuweze kuwakomboa Watanzania. Tumetimiza kilio cha Watanzania cha kuunganisha nguvu ili tuweze kukiondoa Chama cha Mapinduzi madarakani. Watanzania wamewaamini, wamewapa nafasi, lakini bado leo maisha yao yanaendelea kuwa duni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifo vya akina mama kama nilivyosema, vinaendelea kuongezeka; watoto wadogo chini ya miaka mitano mliambiwa wakienda hospitalini watapata huduma bure, lakini leo wakienda hospitalini hakuna dawa. Hivyo hivyo na wazee wetu ambao walilitumikia Taifa hili bila kuchukua rushwa na walifanya kazi zao kwa uaminifu; leo wanakwenda hospitalini, hakuna dawa; pensheni zao bado ni ndogo. Mnataka wazee hawa wakimbilie wapi? Wamekimbilie kwenu, mmeshindwa kuwatekelezea. Kwa hiyo, niwaombe Watanzania, umefika wakati sasa tubadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la ardhi. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Tatizo hili ni kubwa sana katika nchi yetu. Kamati yetu imezunguka katika nchi hii, tatizo kubwa liko katika Mkoa wa Morogoro. Kibaya, ardhi hizi zimeshikwa na watu wakubwa, watu wenye nafasi Serikalini na wengine wamesafishwa juzi, wana mashamba makubwa, hawayaendelezi wala hawayalipii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaona Watanzania masikini hawa wanauana wakulima na wafugaji; tunaiomba hii Serikali inayokwenda kumaliza muda wake, hebu waokoeni masikini

hawa! Watanzania hawa wanakufa bila sababu; mnajisikia raha gani wafugaji wanapouana na wakulima? Damu zinamwagika kila siku, tunaona kwenye vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Wizara ya Ardhi, tunamwomba Mheshimiwa Lukuvi, tumemwona anapita, tunaomba afuatilie wenye mashamba haya ambayo hayaendelezwi, yarudi mikononi mwa wananchi. Tumechoka kuona Watanzania wasio na hatia wakifa. Wanaojilimbikizia ardhi, hawalimi; Halmashauri zenyewe hazinufaiki na mapato au kodi inayotokana na mashamba hayo. Kwa hiyo, umefika sasa wakati wa kurejeshewa wananchi mashamba haya ili waweze kwenda kuyalima kwa amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisemea suala la amani na utulivu. Amesema ndugu yangu pale aliyemaliza kuchangia kwamba Vyama vivunje vikundi vya ulinzi ambavyo wanavianzisha. Tumeona Viongozi wanapigwa, tena Viongozi wa Vyama vya Upinzani. Nasema hivi, Mheshimiwa Rose Kamili yupo India kwa mwezi wa pili sasa, amefanyiwa operesheni mara ya tatu. Alipigwa na *green guard* ndani ya Ofisi ya Chama cha Mapinduzi, mpaka leo hatujui kesi imeishia wapi, mama yule amekuwa kilema na yupo hospitali mpaka leo; na Chini ya usimamizi wa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaambia Serikali ya CCM, hatuwezi kuyavunja makundi haya. Polisi wameshindwa kutulinda, tutatumia vijana wetu kutulinda. Tumechoka kupigwa na tumechoka kulalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine, nisemea suala la hospitali ya Mkoa ya Mawenzi. Kila ninapopata nafasi nalisemea hili, hospitali ya Mawenzi Wodi ya Wazazi. Nasema kwa miaka mitano sasa mpaka Mheshimiwa Spika aliomba wodi ikikamilika pale iitwe Kiwelu. Lakini Mheshimiwa Spika huko uliko, jengo lile linakwenda kuoza na mvua za masika zinazoendelea, jengo lipo pale pale, hakuna kinachoendelea. Kaka yangu Mheshimiwa Mwanri, tunatoka wote Mkoa wa Kilimanjaro, ile ni hospitali yetu ya Mkoa; akina mama wanaotoka Jimboni kwako wanapata huduma pale. Wodi ya wazazi sasa wanalala akina mama watatu kwenye kitanda kimoja. Tunawaambukiza watoto maradhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi inayojiita sikivu lakini haisikii, mwaonee huruma wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro, pelekeni fedha mkamalize jengo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana! Waheshimiwa Wabunge, muda uliobakia hautoshi kumpa mchangiaji kwa sababu kuna matangazo ambayo inabidi tuyatoe.

Tangazo la kwanza ni la kuainisha wachangiaji wa kesho asubuhi. Mchangiaji wetu wa Kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mchangiaji wa Pili atakuwa Mheshimiwa Gregory Teu, Mchangiaji wa Tatu atakuwa Mheshimiwa Ishengoma na mwingine wa nne Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo nina matangazo mengine mawili. Moja ni kwamba mnatangaziwa kwamba ratiba ya Mkutano wa bajeti imefanyiwa marekebisho kidogo ambapo Wizara mbili zimebadilishana tarehe za uwasilishaji wa hotuba za bajeti zao kama ifuatavyo:-

Moja, hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika iliyokuwa imepangwa kuwasilishwa tarehe 20 Mei, 2015, sasa itawasilishwa tarehe 23 Mei, 2015.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Pili, hotuba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliyokuwa imepangwa kuwasilishwa tarehe 23 Mei sasa itawasilishwa tarehe 20 Mei. Nadhani tumeelewana kwa hilo. Wamebadilishana zile tarehe.

Tangazo la pili ni kwamba, kutokana na mjadala wa hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu unaoendelea, kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu hakitakuwepo kesho Alhamisi tarehe 14 Mei, 2015 ili kumpa fursa Mheshimiwa Waziri Mkuu kufuatilia mjadala huo na kujiandaa kujibu hoja za Wabunge. Kwa maana hiyo kesho Maswali kwa Waziri Mkuu hayatakuwepo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana kwa siku ya leo na ninaomba kuahirisha kikao hadi kesho saa Tatu asubuhi.

(Saa 1.51 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamis, Tarehe 14 Mei, 2015 Saa Tatu Asubuhi)